

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 4 Juni, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatuh Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tilia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

#### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**NAIBU SPIKA:** Hati za Kuwasilisha Mezani, Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa niaba yake Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa niaba yake Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 367

**Tatizo la Ajira kwa Vijana Nchini**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wanapomaliza vyuo vikuu?

(b) Je, ni kwa nini vijana hao wasitumie vyeti vyao kama dhamana kupata mikopo ili wajishughulishe na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Nderiananga, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu Swalii la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wanapomaliza Vyuo Vikuu, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Fursa za Ajira ambao unatoa maelekezo kwa sekta zote za kiuchumi ya namna ya sekta hizo zinavyopaswa kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji ili wawekeze na kuzalisha fursa za ajira za kutosha. Mikakati mingine ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu (*internship program*). Katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya wahitimu 5,975 wamewezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi katika taasisi mbalimbali za Umma na binafsi ikiwa ni mkakati wa kuondoa kikwazo cha uzoefu kwa vijana wanapotafuta kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya ufundi na stadi katika fani mbalimbali kwa vijana wakiwemo wahitimu wa elimu ya juu ambapo katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya vijana 28,941 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kujitilia mafunzo ya uanagenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo usio rasmi wa mafunzo kwa lengo la kuwawezesha vijana kuajiriwa na kujiajiri; na pia kuijendeleza kiujuizi katika taasisi mbalimbali za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeanzisha na kutekeleza Programu ya Mafunzo ya Kilimo cha Kisasa kwa vijana wakiwemo wahitimu wa elimu ya juu kujitilia teknolojia ya kitalu nyumba (*greenhouse*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vile vile imeanzisha na kutekeleza programu ya vijana kufanya mafunzo katika nchi ambazo zimepiga hatua katika kilimo ambapo takribani vijana 136 wameweza kuhudhuria mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israeli. Pia, Serikali imeendelea na mkakati wa pamoja wa ajira kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Utumishi

na Wizara nyingine na hasa kupitia Miradi ya Maendeleo. Vilevile Serikali imeanza kufanya utafiti kuhusu Hali ya Rasilimali watu Nchini (*Manpower Survey*) na utafiti wa Hali ya Ajira Nchini (*Labour Force Survey*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapokea ushauri Mheshimiwa Mbunge wa kutumia vyeti vyaa uhitimu mafunzo kama dhamana ya mikopo kwa vijana na kwenda kufanya kazi. Aidha, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya utoaji mikopo kwa vijana kupitia mifuko na programu mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia hapo Mheshimiwa Naibu Waziri ameweza kuonesha programu mbalimbali na nyingi ambazo Serikali inaendelea kuzifanya kwa ajili ya kuwasaidia vijana. Sasa wanasema wakati mwingine kuona ni kuamini. Hebu anieleze sasa: Ni lini Serikali walau itaaniszha hata programu moja katika Jimbo langu ili vijana wangu nao waweze kuona haya mengi ambayo Serikali imeweza kuyazungumza? (*Makofii*)

Swali la pili; kwa kuwa vijana wanaopata umri wa miaka 18 kwenda juu wapo wengi; na mojawapo ya jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha kwamba vijana wanapata ajira: Je, ni kwa nini sasa Serikali isiwe na ule utaratibu kama iliyokuwa nao wa JKT wa *crash programme* ya miaka miwili au mitatu huko huko wanajifunza ukakamavu, kilimo, ufungaji wa samaki na mafunzo mbalimbali ili baada ya hapo Serikali iwape mitaji waweze kuendelea na maisha yao? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Vedastus Mathayo Manyinyi kwa namna anavyojitolea katika kuhakikisha vijana katika Jimbo lake na nchi yetu wananaufaika na programu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kumhakikishia na kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kuititia bajeti ambayo mmetupitishia ambayo itaenda kutekelezwa kuanzia mwezi wa Saba mwaka huu tutapeleka programu ya *greenhouse* katika mikoa tisa iliyobakia ikiwemo Mkoa wa Mara na tutajenga *greenhouse* hizi katika kila Halmashauri. Kwa hiyo na Musoma Mjini ambapo anatoka kaka yangu Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi itapata *greenhouse* hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile programu hizo za uanagenzi tutafanya na vyuo mbalimbali vilivyopo Mkoa wa Mara ikiwemo Chuo kile cha Lake Victoria na vyuo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii lake la pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu sana na wenzetu wa JKT. Utakumbuka pia katika wasilisho la bajeti la Wizara ambayo inahusika na masuala haya ya JKT, Waheshimiwa Wabunge tulipokea ushauri wenu kwa kuona namna ambavyo JKT inaweza ikatusaidia katika kuwajenga vijana na kuwaandaa kikamilifu ili waweze kujiajiri na kuajiriwa na hata kuajiri wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu fasaha kabisa. Niwakumbushe tena

Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi na yawe moja kwa moja.

Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

Na. 368

**Mpango wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mtwara**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO K.n.y. MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi Mei, 2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Hospitali hiyo inajengwa katika Kituo cha Afya Nanguruwe ambacho kitapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Halmashauri baada ya kuongeza miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Mei, 2021 ujenzi wa majengo matano umekamilika. Ujenzi wa wodi tatu za kulaza wagonjwa unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi

Septemba, 2021. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika Hospitali ya Halmashauri. Vilevile katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa changamoto iliyopo Jimbo la Mtwara Mjini la kukosa Hospitali ya Wilaya linafanana sana na changamoto ya Jimbo la Kilindi: Je, ni lini sasa Serikali itapeleka pesa kujenga Hospitali ya Wilaya ya Kilindi ili kuokoa maisha ya akina mama wa Kilindi na Mkoa wa Tanga kwa ujumla? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunajenga Hospitali za Wilaya na Halmashauri katika Halmashauri zote ambazo hazina Hospitali hizo nchini kote. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya Halmashauri zote ambazo hazina Hospitali za Halmashauri na fedha hizo zitapelekwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali hizo. Kwa hiyo, pamoja na Jimbo hili la Kilindi kwa maana ya Halmashauri ya Kilindi itatengewa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi huo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa sisi Mkoa wa

Ruvuma tuna changamoto; hatuna hospitali kubwa ya kisasa ya Mkoa wa Ruvuma; sehemu iliyopo ni ndogo sana; sasa hivi ukitaka kuongeza jengo lazima ubomoe jengo linguine:-

Je, Serikali ipo tayari kutupangia na kutujengea Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Serikali ni kuhakikisha kila Mkoa unajengewa Hospitali ya kisasa ya Rufaa ya Mkoa na Hospitali za Rufaa za Mkoa ambazo zimeendelea kujengwa katika mikoa mipyä zipo hatua za mwisho kabisa za ukamillishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mkoa wa Ruvuma una Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, lakini hii ni ya siku nyingi nae neo ni dogo. Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tutakwenda kufanya tathmini na kuona kama kuna uwezekano wa kuboresha hospitali iliyopo au kama kuna uwezekano wa kujenga hospitali nyingine mpya, tutapeleka taarifa katika Mkoa wa Ruvuma baada ya kufanya tathmini hiyo. Nakushukuru. (Makofî)

**NAIBU SPIKA:** mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi.

Katika Mkoa wa Arusha, Jimbo ambalo lina jiografia ngumu sana, ni Jimbo la Ngorongoro; na ukisema uweke tu Hospitali ya Wilaya pale Loliondo Mjini, Kata nyingine zenye umbali mkubwa hawawezi kupata hii huduma:-

Je, Serikali inalitizamaje Jimbo hili ili wale wananchi waweweze kupata huduma nzuri za afya na zinazotakiwa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba Jimbo la Ngorongoro ni kubwa na jiografia yake ina changamoto, lakini Serikali imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba kwanza kuitia Sera ya Mpango wa Maendeleo ya Afya Msingi kila Kijiji kinakuwa na zahanati, lakini pia kila Kata inakuwa na kituo cha afya na Halmashauri kuwa na Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuitia mpango huo ambao utakwenda kujenga zahanati katika kila Kijiji, lakini pia kujenga vituo vya afya katika kila Kata, tutakwenda kutatua changamoto ya ukubwa na jiografia ya Jimbo la Ngorongoro na hivyo tutahakikisha kwamba huduma za afya zinawafikia ipasavyo wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 369

### **Ujenzi wa Shule za Sekondari Bombo na Ndungu – Same Mashariki**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa maboma ya Shule za Sekondari Bombo na Ndungu ili Kidato cha Tano kianze baada ya mabweni ya wasichana kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari Bombo na Ndungu zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Same ni shule za kutwa zinazopokea wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne. Serikali ina mpango wa kuzipandisha hadhi shule hizi ili ziweze kuchukua wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita. Katika kutekeleza mpango huo katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Same shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Bombo na shilingi milioni 75 kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja katika Shule ya Sekondari Ndungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bweni moja katika Shule ya Sekondari Bombo umekamilika na ujenzi wa bweni moja unaendelea; na ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari Ndungu umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Same shilingi milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari Bombo na shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula katika Shule ya Sekondari Ndungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa kushirikiana na wananchi inaendelea na ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ndungu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 120 kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja na maktaba ya TEHAMA katika Shule ya Sekondari Ndungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, mwaka 2022 hivyo kuwezesha Shule hizo kuanza kuchukua wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, shule hizi ziliahidiwa tangu 2019/2020 kwamba zingeanza *high school*; na madarasa yalishakamilika Shule ya Bombo na bweni lilikuwa ni moja tu ambalo lilikuwa ljengewe ili wawulana nao wapate nafasi. Cha kusikitisha ni kwamba sasa yamepelekwa tena mpaka Septemba 2022. Swali langu ni kwamba: Kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuona kwamba *high school* ni muhimu sana katika shule zetu ili wanafunzi wetu waweze kuendelea na masomo ambayo yatawapa ujuzi zaidi katika maisha yao? (*Makofii*)

Swali la pili ni kwamba, kwa kuwa somo la Stadi za Kazi mashulenii linafanywa zaidi kinadharia: Je, Serikali ina mpango gani kuongeza nguvu katika kufanya masomo ya vitendo kusudi wanafunzi wanapomaliza shule wakaweze kujiajiri kwa kuzingatia kwamba Serikali haiwezi kuajiri wanafunzi wote wanaomaliza shule? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa amejaribu kuainisha, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kufungua shule hizo kama ambavyo ilikuwa imeahidi katika mwaka wa fedha 2019/2020? Nimweleze tu kabisa kwamba Serikali inafahamu umuhimu wa kuanzisha Kidato cha Tano na Sita katika shule hizo na ndiyo maana tumekuwa tukipeleka fedha kila mwaka ili kuhakikisha kwamba shule hizo zinakidhi vigezo vyote vinavyotakiwa. Kwa sasa kuna upungufu wa miundombinu ya msingi; madarasa bado hayajajitosheleza, hakuna maabara na hakuna maktaba katika maeneo hayo. Kwa hiyo, tunataka tukamilishe ili tuweze kuzifungua shule hizo zikiwa na vigezo vyote vilivyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu stadi za kazi mashulenii kwamba wanafunzi kwa sasa wanasoma nadharia, nieleze tu kwamba Sera ya Serikali ni kuhakikisha kwamba stadi zote za kazi mashulenii wanafunzi wanafanya kwa vitendo. Ndiyo maana unaona katika mwaka uliopita 2020 kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, watoto waliomaliza Kidato cha Nne kwa mfano kwenye masomo ya sayansi hawakufanya ile *alternative to practical*, walifanya ile *real practical* kwenye mitihani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii inaonesha tu kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaondoa hii dhana ya nadharia na ndiyo maana katika bajeti zetu unaona tumejenga maabara karibu katika shule zote nchini na tutahakikisha tutazikamilisha kwa wakati ikiwemo kuzipelekea vifaa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, sasa aulize swalilake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Ng'enda.

Na. 370

**Tatizo la Wakazi wa Kigoma Kuitwa Wakimbizi**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA K.n.y. MHE. ASSA N. MAKANIKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi wa Kigoma ambao wamekuwa wakikamatwa mara kwa mara kwa kuitwa wakimbizi nchini mwao:-

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalil

Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupita Idara ya Uhamiaji imepewa jukumu la kudhibiti, kusimamia na kufuatilia uingiaji, ukaaji na utokaji wa wageni hapa nchini kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 12 (1) cha Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 rejeo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza jukumu hilo, Idara ya Uhamiaji imekuwa ikifanya operesheni, doria na misako mbalimbali kwa lengo la kuwabaini wageni wanaoingia na kuishi nchini kinyume cha sheria na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya mahojiano na uchunguzi wa kina ili kujiridhisha juu ya uraia wa watuhumiwa wanaokamatwa wakati wa operesheni husika na kwamba Idara ya Uhamiaji katika kushughulikia masuala ya uraia huzingatia matakwa ya Sheria ya Uraia Sura ya 357 rejeo la mwaka 2002. Operesheni, doria na misako hufanyika kwa mikoa yote na siyo Mkao wa Kigoma pekee. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Kilumbe Ng'enda, swalii la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza na nitaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ni ukweli kwamba tunajua umuhimu wa kazi ya Idara ya Uhamiaji katika kusimamia masuala aliyoyasema Mheshimiwa Waziri ya uingiaji wa wageni ukaaji wao. Hata hivyo, kiwango cha usumbufu wa wananchi unaotokana na doria za uhamiaji kimepita kiasi ambacho sisi tunakifahamu katika historia ya Mkao wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri aniambie kuna jambo lipi jipya ambalo limejitokeza linalosababisha kwa sasa kuwe na misako inayosumbua hata raia halali waliokaa katika mkao wetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; msingi wa kukua kwa tatizo hili ni kuchelewa kwa Wizara yake kutoa vitambulisho vya *NIDA* kwa wananchi halali wa Mkoa wa Kigoma, jambo ambalo lingekuwa limekamilishwa, haya yote yasingekuwepo. Anieleze ni lini Serikali itakamilisha kazi hii ya kutoa vitambulisho vya *NIDA* ili kuondokana na usumbufu huu; na kama inawezekana misako hiyo isimame mpaka hapo mtakapokamilisha vitambulisho vya *NIDA?* (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha usumbufu katika kusimamia Sheria ya Uhamiaji, Kifungu cha 12 kama ilivyorejewa mwaka 2016 ambapo Jeshi la Uhamiaji limepewa jukumu la kufanya misako, doria na hata ikibidi kufanya upukuzi ili kubaini nani ni raia na nani sio raia; zoezi hili kama tulivyojibu katika jibu letu la msingi, linafanyika kwa nchi nzima. Usumbufu huu unatokana na mkoa ulivyo na mipaka na majirani zetu ambapo mara nyingi kumekuwa kuna shida katika nchi zao na kwa hiyo wana msukumo mkubwa sana wa kuja katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli kwa muda wa miezi mitatu tumekamata wahamiaji haramu zaidi ya 1,000. Kiwango hiki ni kikubwa na siyo rahisi tusifanye doria, lakini tunafanya hivyo kwa mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anauliza vitambulisho vya *NIDA* vingetotewa basi usumbufu usingekuwepo. Ni kweli, lakini nataka niseme, kupewa kitambulisho cha *NIDA* cha uraia wa Tanzania siyo mwarobaini kwamba wewe sasa huwezi ukaulizwa kuhusu uhalisia na uhalali wa uraia wako. Sheria hizi ni mbili tofauti; kuna Sheria ya Uraia, Sheria ya Uingiaji Nchini na Sheria ya Vitambulisho vya Taifa na zote hizi zinashughulikia mambo mawili tofauti. Vitambulisho hivi hata wakazi wasio raia wanapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna madaraja tofauti tofauti ya kutoa vitambulisho. Siyo kwamba ukipewa kitaambulisho hiki, basi wewe hutaulizwa tena. Tutaulizwa, hata mimi naweza nikaulizwa uraia wangu hata kama nina kitambulisho na hata kama natoka Dodoma; nitaulizwa uraia wangu na uhalsia endapo utajitokeza wasiwasi wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo majibu yetu ya Serikali na tunaomba Mkoa wa Kigoma watuelewe hatufanyi kwa Mkoa wa Kigoma peke yake, tunafanya kwa mikoa yote. Hivi sasa kuna oparesheni imeanza tarehe mosi itaisha tarehe 15 ya mwezi huu kwa mikoa yote ya Tanzania. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 371

#### **Ujenzi wa Barabara ya Handeni - Turiani**

**MHE. REUBEN N. KWAGILWA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Handeni, Mziha hadi Turiani, Morogoro?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Handeni – Mziha – Turiani yenye urefu wa kilometra 109.36, inahudumiwa

na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Handeni – Mziha – Turiani umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetengwa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mkandarasi wa barabara ya Magole – Turiani yenyе urefu wa kilometra 45.2 na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Turiani – Mziha – Handeni yenyе urefu wa kilometra 104.0 kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Kwagwilwa, swalı la nyongeza.

**MHE. REUBEN N. KWAGILWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swalı langu la msingi lilikuwa: Ni lini, Serikali kwa kiasi kikubwa inatoa maelezo ya kipande cha barabara cha Magole – Turiani badala ya Handeni – Mziha – Turiani. Naomba kurudia: Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kipande hiki cha Handeni – Mziha – Turiani? La kwanza. (*Makofı*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; tunayo barabara inayofanana na hiyo ya kutoka Handeni – Kibilashi – Kiteto – Kondoa – Singida, mikoa minne inaunganisha barabara ile; Na bomba la mafuta linalotoka Hoima mpaka Tanga linapita kwenye barabara hiyo: Ni lini Serikali pia itaanza ujenzi wa barabara hiyo muhimu? (*Makofı*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri subiri kidogo. Mheshimiwa Mbunge swalı lako la kwanza limejibiwa kwenye majibu ya msingi niliyonayo mimi hapa. Wamesema bajeti ijayo ya 2021/2022 wanaanza maandalizi ya huo ujenzi na hapa imendikwa hiyo barabara unayoitaja Turiani – Mziha – Handeni kilometra 104. Mwishoni mwa lile jibu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swalı la pili la nyongeza. (*Makofı*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA**

**M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati njema sana, kwenye bajeti ya Wizara hii tarehe 27, 28 mwezi uliopita Mheshimiwa Waziri alisimama hapa kwenye Bunge Tukufu akataja kwamba tumepata kibali cha barabara 16 kati ya barabara 29 na barabara hii ya Handeni – Kibilashi – Kiteto – Kondoa – Singida imetengewa kuanza ujenzi wa kilometra 25 na wakati wote kuanzia sasa itatangazwa, ipo kwenye mchakato mbalimbali wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Wabunge wa maeneo ya Mkoa wa Tanga, Dodoma, Manyara na Singida ni kwa sababu tumepata *activation* kubwa, bomba la mafuta linapita hapa na mmeshuhudia Mheshimiwa Rais Museveni amekuja hapa na Mheshimiwa Mama Samia wallkuwa pamoja wameweka sahihi ya ujenzi wa bomba hili la mafuta. Maana yake ni kwamba barabara hii ni lazima ijengwe ikamilike ili huduma hii iweze kufanya vizuri. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi ujenzi wa barabara hiyo utakamilika mapema sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 372

**Kufanya Marekebisho ya Mtaala wa Elimu ya  
Msingi na Sekondari**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ya malengo ya Mtaala wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini ili kuendana na uhitaji wa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

## **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kufanya marekebisho mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ili kuwawezesha wanafunzi kupata stadi mbalimbali zinazoendana na mahitaji ya wakati. Kwa sababu hiyo, Serikali imekuwa ikiboresha mitaala hiyo kila kunapokuwa na hitaji la kisayansi, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imepanga kufanya mjadala mpana kuhusu mfumo wa Elimu nchini ambao utahusisha Sera ya Elimu na Mitaala kwa ujumla ili iendane na wakati na ikidhi mahitaji ya sasa na baadaye. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi lilikuwa linalenga kwenye malengo ya mtaala; na malengo ya mtaala kwa mujibu wa sera ni kumwandaa mwanafunzi ili aweze kuendelea na ngazi zinazofuata za masomo. Hii imesababisha wimbi kubwa la wanafunzi wanaoshindwa kupata hiyo nafasi ya kuendelea kuachwa na mfumo wa elimu.

Je, Wizara sasa ina mpango gani wa kuboresha mtaala kwa kuongeza malengo ya kumwandaa mwanafunzi kujajiri kwenye mazingira yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni lini sasa au ni kwa namna gani Serikali inakwenda kutoa elimu ya lazima hadi Kidato cha Nne. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba tunakwenda kuwa na mjadala mpana ambao utakwenda kuhakikisha kwamba taaluma yetu na nchi yetu wapi tunapotaka kuelekea. Katika mjadala huo mpana tunaamini hayo malengo Mheshimiwa Mbunge anayoyazungumza, tutaweza kuyadadavua, kuyafafanua na kuyaweka kwa namna tunavyotaka yawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza awali, kwamba mitaala yetu hii imekuwa ikifanyiwa maboresho na maboresho haya mara nydingi sana huwa yanalenga katika maeneo ambayo yamekuwa na changamoto. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mjadala wetu mpana huu, malengo haya ambayo anayozungumza yatakwenda kuzingatiwa na vilevile maboresho ya mitaala yetu ili sasa vijana wetu wanapohitimu waweze kujajiri nayo vilevile yanaweza kuzingatiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maji, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, sasa aulize swalilake.

Na. 373

**Mradi wa Kuyatoa Maji Ziwa Tanganyika Mpaka Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza mradi wa kuyatoa maji toka Ziwa Tanganyika na kuyapeleka katika Manispaa ya Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mpanda ni miongoni mwa miji itakayonufaika na mradi wa miji 28 kupitia mkopo wa Dola za Kimarekani 500 kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa Mji wa Mpanda utahusisha matumizi ya chanzo cha maji cha bwawa la Milala liliopo katika Manispaa ya Mpanda kwa kujenga chujio na miundombinu mingine. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali ina mpango wa kutumia Ziwa Tanganyika ili kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Mpanda na maeneo mengine ambayo itakuwa rahisi kutumia ziwa hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu tusaidie. Jibu la msingi ni dola za Kimarekani milioni 500 au dola za Kimarekani 500?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni milioni 500.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha maeneo mengine duniani ikiwemo China kwa kutumia vyanzo vya kudumu imeweza kuiunganisha nchi yake kutoka kaskazini kwenda kusini kwa vyanzo vya maji. Tanzania tuna Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika; ni lini Serikali itatumia vyanzo hivi muhimu kuiunganisha nchi? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maziwa makuu ni moja ya mikakati ya Serikali kuweza kutumika na kuwa suluhisho la tatizo la maji katika nchi yetu. Hivyo, napenda kukuhakikisha Mheshimiwa Mbunge, Ziwa Tanganyika katika eneo lako litatumika kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI M. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wakati tunasubiri mradi wa kuyatoa maji Ziwa Tanganyika kupeleka Mpanda Mjini, Serikali illahidi kutupatia shilingi milioni 240 kwa ajili ya kukarabati vyanzo vya maji na kuhakikisha vijiji vile ambavyo vilitakiwa vipate maji, vinapatiwa maji:-

Je, Serikali inatupatia majibu yapi kupeleka hizo fedha shilingi milioni 240?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara tuliahidi hizi fedha ziweze kwenda kusaidia kukarabati miundombinu muhimu ili vite vijiji viweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mbunge hizi fedha mapema tunavyoanza mwaka wa fedha 2021/2022 zote zinatumwa katika Wilaya yako, lengo ni kuona kwamba ule mradi unakarabatiwa na wananchi wanapata maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 374

### **Ujenzi wa Mradi wa Maji Kutoka Nzega Hadi Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika mradi wa kutoa maji kutoka Nzega Mjini, tenki la Ushirika hadi Bukene ambapo vijiji 20 na vitongoji zaidi ya 100 vitanufaika?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tuko swalii namba 374 la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nibadilishe jibu la swalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imekamilisha kazi ya usanifu wa mradi wa kutoa maji katika tenki la Ushirika Mjini Nzega kwa ajili ya kuhudumia watu zaidi ya 79,485 katika vijiji 20 na vitongoji vyake. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha fedha shilingi bilioni mbili kimetengwa na utekelezaji wa mradi huu utaanza, ambapo utahusisha kulaza mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilometra 176, kujenga matenki matano ya kuhifadhi maji ya ujazo wa lita 100,000, lita 150,000, lita 250,000 na lita 300,000 na kujenga vituo vya kuchotea maji 83.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, yanayoleta matumaini kwa wananchi zaidi ya 80,000 katika vijiji 20 vya Jimbo la Bukene ambao sasa wanakwenda kupata majisafi na salama kutoka Ziwa Viktoria: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari baada ya Bunge hili la bajeti tuongozane kwenda Bukene ili apeleke hizi taarifa njema na kuwaandaa wananchi kupokea mradi huu muhimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, jana Mheshimiwa Spika alisema inabidi mumwombe kibali. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo. Upo tayari kuambatana na Mheshimiwa Selemani Zedi kwenda Bukene? (*Kicheko/Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru sana kwa kupigilia msumari ruhusa ile ya Spika aliyoiongea jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi napenda tu kukuhakikishia, kwenda kwenye majimbo yenu Waheshimiwa Wabunge ni moja ya majukumu yangu. Hivyo, baada ya Bunge hili Bukene nitafika, tutafanya kazi vizuri kwa pamoja, lengo ni kuona majisafi na salama yanapatikana bombani kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa fedha za ujenzi wa mradi wa maji ya Ziwa Viktoria kutoka Ziba, Nkinga zipo: Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huu wa kupeleka maji maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji,  
*Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mradi huu alioutaja wa maji kutoka Ziwa Viktoria kuelekea maeneo yote ambayo ameyataja, tunatarajia kuutekeleza mwaka ujao wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Isack Kamwelwe swalii la nyongeza.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Namuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwenye jibu lake la msingi la swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mjini Mpanda amezungumzia chanzo cha maji cha Bwawa la Milala. Bwawa la Milala linaweza likatoa maji kwa muda wa miezi minne tu.

Je, haoni kwamba, itakuwa ni kupoteza pesa kuwekeza katika chanzo ambacho kitatumika kwa muda wa miezi minne tu badala ya kwenda moja kwa moja kuchukua maji kwenye Ziwa Tanganyika? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa  
*Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru, lakini nimpongeze sana sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna anavyojibu maswali vizuri sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Waziri, lazima uitwe ndio uweze kuzungumza. Maana sikukuona umesimama.

Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru tena kwa mara nyingine, na kwa dhati ya moyo nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna anavyojibu maswali vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina rasilimali toshelevu zaidi ya bilioni 126 mita za ujazo. Sasa mkakati wa Wizara ni kutumia rasilimali toshelevu kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye ni Waziri wangu ambaye amenifunza mpaka leo nipo hapa, hili jambo tunalizingatia katika kuhakikisha kwamba wananchi hawa tunaenda kuwaondolea tatizo hili. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, sasa aulize swali lake.

Na. 375

**Kumaliza Changamoto ya Maji Kituo cha Utafiti na  
Chuo cha Kilimo UKirigulu**

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI** aliliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza changamoto ya Maji katika Kituo cha Utafiti na Chuo cha Kilimo UKirigulu?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Utafiti na Chuo cha Kilimo UKirigulu kilikuwa na Skimu ya Maji iliyojengwa mwaka 1965. Chanzo cha maji cha skimu hiyo ni Ziwa Victoria na ina matenki mawili ya maji. Moja lipo Kijiji cha Mwalogwabagole na lingine liko eneo la chuo hicho. Skimu hiyo ina vituo vya kuchotea maji 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa mradi kwa ajili ya ukarabati wa skimu hiyo umekamilika na katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi 630,733,364 ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji na kutahusisha ulazaji wa mabomba mapya kilometra 40.4 na ukarabati wa matenki mawili katika Kituo cha UKirigulu na Kijiji cha Mwalogwabagole yenye lita za ujazo 225,000. Chuo cha UKirigulu pamoja na Vijihi vya Mwalogwabagole, Buganda, Nyagholongo, Ngudama, Nyamule, Mwagala, Nyamikoma vitanufaika baada ya kukamilika kwa mradi na ukarabati wa skimu hiyo na jumla ya wananchi 19,658 watanufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, swali la nyongeza.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nasikitika sana kwamba majibu haya, ndiyo haya haya ambayo huwa yanatolewa kila mwaka. Unajua kinachouma ni kwamba, vyanzo vya maji vyote vikubwa unavyovijua vinavyopeleka maji Tabora, Nzega, Igunga, Kahama na Shinyanga vinatoka Misungwi, lakini wana-Misungwi hawapati fursa ya kupata miundombinu ya maji. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri: Ni lini Chuo cha UKiriguru na Kituo cha Utafiti kitapata maji? Kwa sababu, majibu haya, ni haya haya ya miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi, hiki nilichokijibu ndiyo mpango mkakati wa Wizara. Kama mnavyofahamu Wizara ya Maji tuko kwenye mpango mkubwa sana wa mageuzi. Hivyo,

tuache kuangalia mambo yaliyopita, tuangalie ya sasa hivi na utekelezaji wetu sisi ambao tuko, nafikiri mnauona. Kwa hiyo, napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, suala hili la maji katika hiki chuo mwaka ujao wa fedha kazi zinakuja kutekelezwa kadiri ya mipango ilivyo ndani ya Wizara.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 376

**Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Kata za Nkoanrua na Nkoaranga – Arumeru Mashariki**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Majengo ya Mahakama za Mwanzo katika Kata za Nkoanrua na Nkoaranga ambazo majengo yake yamebomoka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jengo la Mahakama ya Mwanzo Nkoanrua lilichomwa moto na wananchi na hivyo kushindwa kuendelea kutoa huduma katika eneo hilo. Aidha, jengo la Mahakama ya Mwanzo Nkoaranga katika Tarafa ya King'ori ni chakavu na hivyo kuhitaji kujengwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) yanaendelea ambapo

utajumuisha mahitaji yote ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi zote. Mpango huu utaweka kipaumbele zaidi kwenye ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo nchini. Lengo la Mahakama ya Tanzania ni kuhakikisha kuwa Tarafa zote 570 zilizopo nchini zinakuwa na Mahakama ya Mwanzo ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama za Mwanzo za Nkoanrua na Nkoaranga zitapewa kipaumbele katika ujenzi na ukarabati kwenye mpango huo.

Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Mahakama katika maeneo yetu, kwani kitendo cha kuchoma moto majengo ya Serikali hasa Mahakama, ni kitendo cha kulaaniwa na hakipaswi kurudiwa tena. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nitaomba kuuliza swali moja la nyongeza, ila naomba pia kwamba Serikali isiwe inatoa majibu tu kwa ajili ya kutuliza Wabunge, lakini kwa kweli ije na kutekeleza yale ambayo wanayasema kwenye majibu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; jiografia ya Jimbo langu la Arumeru Mashariki ni ngumu, kwa maana ya kwamba Mlima Meru ambaao ni mlima mrefu wa pili hapa nchini uko katikati ya jimbo na kuwafanya wananchi walioko Mashariki na Kaskazini mwa mlima huo, kupata shida kufuata huduma ambazo zinapatikana Kusini mwa mlima pamoja na kufika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

: Je, sasa hivi Serikali haioni kwamba ni muhimu sasa kujenga Mahakama ya Mwanzo Kata ya Ngarananyuki ili wananchi walioko Kaskazini mwa mlima huo waweze kupata huduma za Mahakama? Nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tuko kwenye mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2025/2026 nchi nzima itakuwa imefikiwa na Mahakama za Mwanzo kwenye ngazi za Makao Makuu ya Tarafa zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Ngarananyuki kupata Mahakama, tunalichukua ingawa katika kipindi hiki cha fedha ambacho tunakijadili sasa kilishapita, tutalipa umuhimu kwenye kipindi kijacho cha fedha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Naibu Waziri Tarafa ya Ikuo haina huduma kabisa ya Mahakama; na ni umbali wa kilometra karibu 170 kwenda kufuata huduma ya Mahakama kwenye Tarafa ya Matamba:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama kwenye Tarafa ya Ikuo kwa sababu kwa muda mrefu tumekuwa tukiomba huduma hiyo na hatujapewa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi na jibu la nyongeza la Mheshimiwa, tutakuweka kwenye kipaumbele kwenye bajeti baada ya hii tunayojadili leo. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Philipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wilaya ya Songwe ni Wilaya mpya toka mwaka 2016 na nimekuwa nikiahidiwa hapa kila mwaka kwamba tutajenga Mahakama ya Wilaya, lakini mpaka sasa Serikali haina mpango wowote. Viwanja viro, hati ipo, lakini mpaka leo hakuna jengo la Mahakama. Nirudie tena kwa mara ya tano:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Wilaya ya Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mulugo naomba tu asiwe na wasiwasi. Katika kipindi kijacho hiki cha fedha ambacho mmetupitishia bajeti yetu Songwe imo kwenye huu mpango. Kwa hiyo, muda mfupi ujao tutaanzisha hii miradi ya ujenzi katika eneo lake kwa kupitia fedha ambazo mmeziidhinisha wenyewe hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mahakama ya Mwanzo ya Liuli ilijengwa toka kipindi cha mkoloni na ikawa imeharibika sana na kilichotokea ni Mahakama kuhama kabisa eneo hilo na kwamba shughuli za Mahakama haziendelei:-

Je, ni lini Mahakama hiyo itarejeshwa katika nafasi yake kama ilivyokuwa mwanzo hapo Liuli?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunakiri kwamba Mahakama nyingi zimechakaa. Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ni kwamba, mkakati wa kukarabati na kujenga majengo mapya kwenye maeneo ambayo hayana Mahakama, ukomo wake ni 2025 ambapo namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo la Liuli tunalichukua na katika kipindi kijacho cha fedha tutahakikisha tunawasogezea hii huduma ya ukarabati wa Mahakama yao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Buhigwe, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hitaji la Nkoaranga ni sawa sawa na hitaji la Wilaya ya Buhigwe. Wananchi wa Buhigwe wanapata huduma za Mahakama ya Wilaya kwenye Wilaya nyingine ya Kasulu:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Buhigwe, bahati mbaya sana jina lake sikulisia vizuri, lakini nikupongeze sana kwa ku...

**NAIBU SPIKA:** Anaitwa Mheshimiwa Felix Kavejuru.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kave...!

**NAIBU SPIKA:** Kavejuru.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Hee, hili mpaka ushibe kwanza. Atanisamehe tu. Natambua jina lake,

nitalifuatilia ili kuliweka vizuri, maana nadhani wote hamwezi kulitamka vizuri sana lazima utakosea kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wa mwaka 2021/2022 ambao tayari bajeti yake imeshapitishwa Buhigwe ipo katika mpango wa kujengewa Mahakama ya Wilaya. Kwa hiyo, asubiri tu mageuzi kwenye eneo lake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilipaswa kuleta matangazo kwenu, lakini naona Makatibu bado hawajaleta hayo matangazo. Kwa hiyo, tunaendelea na ratiba yetu. Tangazo litakapokuja, wageni wetu mtatangazwa, msiwe na wasiwasi.

Katibu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja mahususi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni 55 (2) na (3) ambayo unaweza ukatoa hoja mahususi Bungeni; kwa sababu ya muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la mauaji ya wivu wa kimapenzi. Mwezi uliopita Songea kuna mwanafunzi ameuawa lakini juzi Iringa mwanafunzi amuawa kwa wivu wa mapenzi. Kwanza nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa niaba yao tulaani kitendo hicho cha uuaji wa wanafunzi kwa wivu wa mapenzi. Vile vile kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania, tunalaani mauaji ya wanawake na ukandamizaji wa wanawake kwa ukatili wa kuwaua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya jamii yetu kumejengeka tabia kwamba mwanaume kumpiga mwanamke ni jambo la kawaida kabisa; na jambo hili linapelekea wanaume wengine kufikia hatua sasa ya kuwaua

wanawake. Tumeona watoto wa kike na wanawake wanauawa mara kwa mara kwa kupigwa na wanaume zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wachawi; unaambiwa mwanamke mwenye macho mekundu ni mchawi, anauawa. Unajiuliza, hakuna mwanaume mchawi? Kwa hiyo, wanaume wenyewe macho mekundu wenyewe sio wachawi! Kwa hiyo, mfumo dume na ukandamizaji wa kijinsia bado upo kwa nguvu. Naomba Waheshimiwa Wabunge hasa wanawake tuendelee kulaani hii tabia, tuendelee kuikemea na kuipigia kelele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo mingi ya Asasi mbalimbali za Kimataifa hairuhusu kabisa vitendo hivi vinavyoendelea vya ukatili wa kuwaua wanawake. Naomba sasa kwa kuwa jambo hill linaendelea kwa kujirudia mara kwa mara kwa kuwaua wanawake na wanafunzi wanaouawa kwa wivu wa mapenzi, naomba Bunge lako lijadili ili kukomesha kabisa jambo hili ambalo limekuwa ni baya sana kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa anaunga mkono hoja. Hajatoa hoja na Wabunge mmesimama wawili tu hapo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah amesimama kwa mujibu wa kanuni ya 55 ndiyo aliyoitaja (1) na (2) akieleza hapo kuhusu jambo ambalo limetokea katika jamii yetu, lakini wakati akieleza hoja hiyo ameeleza mambo mengi pia ambayo yanafanana ama yanashabihiana na jambo hilo alilolieza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wa kanuni ni kanuni ya 54 ndiyo ambayo ingeweza kumsimamisha Mbunge kanuni ya 55 inaweka masharti ili jambo alilosimama nalo Mbunge kwa mujibu wa kanuni ya 54 liwe limetimiza masharti ya kanuni ya 55. Pamoja na changamoto hiyo ya

kutajwa kwa kanuni, nieleze kidogo tu kwamba kweli jambo hili linasikilisha na siyo kwa maana ya haya matukio mawili tu ambayo yametajwa ya wanafunzi kuuawa, matukio kama hayo yamekuwepo kwenye jamii yetu. Serikali inajitahidi kwa upande wake, lakini bado yanaendelea.

Nafikiri kama Mbunge alivyosema wakati akizungumza, ni muhimu sisi kama Wabunge kushiriki kwenye hili zoezi zima: moja, la kuwaelimisha wananchi ambao tunawawakilisha, mambo haya yazungumzwe kwa uwazi; yasipozungumzwa, watu wengine hufikiri pengine mpenzi wake huyo mmoja akipotea ama kwa namna yoyote ile wameachana, basi Maisha yanaishia hapo. (*Makof*)

Tujitahidi kutoa elimu kwa vijana wetu, lakini kwa sababu ameeleza hili jambo kwa mapana sana, wako wazee wanaouawa kwa imani za kishirikina; wengine wanauawa, utasoma hapa mtoto kamuua mzazi wake kwa sababu ameambiwa ukimuua kuna utajiri; na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, jambo hili siyo kwa hao wawili tu waliouawa, lakini ni vitendo tu vya kufanya ukatili wazee, wanawake na pia Watoto, kwenye jamii yetu sisi tuwe sehemu ya kuielimisha jamii juu ya mambo yanayotokea na namna ya kukabiliana nayo.

Kwa upande wa Serikali kwa namna hoja hii ilivyokuja ni nzito na ya muhimu, lakini siyo jambo la dharura kwa masharti ya kanuni zetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali yetu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yuko hapa, nawaomba sana m jitahidi kwanza kuelimisha kama ambavyo mmeelimisha jamii imeelewa, hata wao wenyewe wanashiriki kwenda kusema Polisi mambo yanayotokea kwenye jamii. Basi hata mnapowaelimisha kuhusu usalama ule wa jumla na haya nayo mwaelimishe wananchi.

Hata hivyo, wale wanaobainika na kuthibitishwa kwamba wamefanya vitendo hivyo, basi wachukuliwe hatua kali ili mtu ajue kwamba akifanya kitendo kama hicho ni mwisho wa maisha yake na yeye pia. Sasa inapotokea mtu anafanya kitendo cha ukatili halafu anakuwepo tu kwenye

jamii, hilo linaleta changamoto kubwa, ikiwa ni pamoja na watu ambao wanahalalisha kuwapiga wake zao, au kuwapiga watu ambao wana mahusiano nao kwenye mapenzi, haiko sawa sawa.

Kwa hiyo, hiyo ni kazi yenu Polisi, kwa maana ya Wizara, mtu akienda kushitaki kwamba amepigwa, basi mchukue hatua zinazostahili kisheria. Msipofanya hivyo, mtu ataona ni sawa tu. Mke kachelewa kurudi nyumbani, anampiga, yeye akichelewa kurudi hamna mtu anampiga. Sasa vitu kama hivyo lazima vibadilike.

Sasa hivi kwa sababu tuko katika harakati za kuona namna ambavyo mtoto wa kike anaweza kupewa fursa sawa na mtoto wa kiume, lazima mtoto wa kike ajengewe mazingira kwamba kupigwa siyo kawaida. Nafikiri tunavyo mtaja taja Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ule ni mfano wa mwanamke bora, nasi wengine tunafuatia hapo. Basi tuonyeshe mifano mizuri kwenye jamii hasa kwenye mambo haya ya ukatili, tusiyafumbie macho. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, yeye alikuwa ameomba nilisemee hilo. Kwa hiyo kwa mujibu wa kanuni zetu, hatutaweza kulifanya ni jambo la dharura kuanza kulijadili. Kwa hiyo, hayo ni maelezo ya jumla, Mheshimiwa Waziri ameshasikia hapa na hatua stahiki zitachukuliwa.

Nilete kwenu tangazo la wageni tulionao siku ya leo. Tutaanza na wageni walioko jukwaa la Mheshimiwa Spika. Kwanza ni wageni wangu watatu ambao ni mabalizi wa mazingira kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Haji Manara. (*Makof/Vigelegele*)

**MBUNGE FULANI:** Msemaji wa dunia huyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, sijamaliza! Jamani, Waheshimiwa Wabunge makofi hayo yanaashiria kwamba msemaji wa Kimataifa ameingia Bungeni leo. Sawa. (*Makof/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa leo Msemaji huyu wa Kimataifa wa timu ambayo inatuwakilisha Kimataifa ameambatana na mkewe, Ndugu Naheed Abdallah. Karibu sana. Pia wameongozana na Ndugu Cherrie Khamis ambaye wengi wanamfahamu kwa jina la Monalisa. Karibu sana sana. Sasa hawa ni mabalozi wa mazingira lakini pia Monalisa ni Balozi wa *Tulia Trust*, karibu sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wangu wengine 171 ambaao ni vijana wa hamasa na viongozi wa wilaya ya UVCCM kutokea Mbeya Mjini wakiongozwa na Ndugu Ramadhani Shekaoneka ambaye ni Mwenyekiti na Ndugu Steven Shija ambaye ni Katibu wa UVCCM na Ndugu Modo Emmanuel ambaye ni kiongozi wa hamasa. Sasa wote msimame kwa pamoja. Karibuni sana. Ni vijana hawa kutoka Mbeya Mjini.

Waheshimiwa Wabunge, ukisikia watu wanasema sema huko, wajue tuko vizuri Mbeya Mjini. Tuko vizuri sana. Sasa kwa sababu walismama wote pamoja, hebu wale viongozi wasimame; Ndugu Ramadhani Shekaoneka, Mwenyekiti wao na pia Ndugu Steven Shija, Katibu pamoja na Ndugu Modo Emmanuel, Kiongozi wa Hamasa. Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii ambaao ni viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Allan Kijazi. Sasa hawa kwa sababu watapata fursa ya kutajwa, atasimama mmoja mmoja kadri anavyotajwa. Dkt. Allan Kijazi, Katibu Mkuu, karibu sana sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro tena ambaao ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TANAPA*, Jeneral George Waitara, Mkuu wa Majeshi Mstaafu huyu; tunaye pia Meja Jenerali Mstaafu Semfuko, Mwenyekiti wa Bodi ya *TAWA*, karibu sana; tunaye pia Dkt. Siima Bakengesa ambaye ni Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya *TFS*, karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Mheshimiwa Jaji Mstaafu Thomas Mihayo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TTB*, karibu sana; tunaye pia Profesa Kokela ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi - *NCT*, karibu sana. Wapo pia wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ambao ni familia yake, wakiongozwa na mke wake, Ndugu Flora Mdima, karibu sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mmemwona jamani wifi yetu na shemeji yetu. Usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa yuko salama kabisa. Hamjamwona vizuri! Haya shemeji yetu na wifi yetu hebu simama kidogo, hawajakuona Waheshimiwa Wabunge. Karibu sana. (*Makofii*)

Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Makofii hayo yanaashiria uzito wa kazi yenye aliyonayo Mheshimiwa Waziri siku ya leo hapa mpaka kesho. (*Makofii*)

Vile vile yupo Mwakilishi wa Balozi wa Ujerumani nchini, Ndugu Richard Shaba, karibu sana. Pia wapo wageni 36 wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ambao ni wanafunzi kutoka *SUA* wanaosoma Shahada ya Usimamizi Utalii wakiongozwa na Ndugu Aslam Habibu. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pia wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Zarina Hassani ambaye ni Balozi wa Hiari wa Utalii. Sijui amekaa upande gani? Eeh, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, huyu ni Balozi wa Hiari wa Utalii, ameongozana na wageni wengine ambao nitawasoma baada ya muda kidogo. Katibu.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro. (*Kicheko/Makofii*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kujadili na kuitisha Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee na kwa masikitiko makubwa, naomba niungane na wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waheshimiwa Wabunge wote, Chama cha Mapinduzi na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile natoa pole kwa Watanzania wenzangu kwa kuondokewa na viongozi wengine wakuu wakiwemo Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema Peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole

kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, wananchi na familia za marehemu kwa kuondokewa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justice Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhamwe; Mheshimiwa Khatib Said Haji, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara. Vifo wa Wabunge hao vimeleta majonzi makubwa kwa Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla kutokana na kukosa michango yao muhimu katika utendaji wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na baadhi ya watumishi kupoteza maisha na wengine kujeruhija wakiwa wanatekeleza majukumu ya uhifadhi wa maliasili. Vile vile natoa pole kwa wananchi ambao wamepoteza maisha na waliopata madhara kutokana na wanyama wakali na waharibifu. Namwomba Mwenyezi Mungu awaponye majeruhi na azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapijwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania; na Mheshimiwa Balozi Hussein Athman Katanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kusimamia majukumu ya sekta mbalimbali. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Aloyce Andrew Kwezi, Mbunge na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge kwa ushirikiano, maoni na ushauri wanaoendelea kutoa kwa Wizara. Maoni na ushauri wao umeendelea kuwa chachu ya mafanikio katika kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Wizara itaendelea kushirikiana kikamilifu na Kamati hii na Bunge lako kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yake na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii ambayo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Aidha, nawashukuru viongozi wenzangu wa Wizara akiwemo Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge Naibu Waziri; Dkt. Allan Herbert Kijazi, Katibu Mkuu; na Ndugu Ludovick James Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu; kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru Watendaji Wakuu na Watumishi wa Wizara; na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa namna ya kipekee, naomba kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa, Bi Florah Ndumbaro; na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nydingi za maliasili na malikale zenye mchango mkubwa katika uendelezaji utalii, ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira. Mathalan, utalii huchangia wastani wa asilimia 17 ya Pato la Taifa; asilimia 25 ya fedha za kigeni na huzalisha ajira takriban milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande

mwagine, Sekta ya Misitu na Nyuki huchangia asilimia 3.5 ya pato la Taifa; asilimia 5.9 ya mapato yatokanayo na biashara ya nje na ajira takriban milioni nne kwa mwaka. Sekta hii huchangia zaidi ya asilimia 90 ya nishati ya kupikia nchini kutokana na miti, yaani mkaa na kuni. Kutokana na mchango huo, rasilimali hizo zitaendelezwa na kusimamiwa ipasavyo ili ziendelee kuchangia zaidi katika uchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 218.55 kutokana na vyanzo vinavyosimamiwa moja kwa moja na Wizara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021, Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 147.28 sawa na asilimia 67 ya lengo.

Aidha, taasisi za Wizara ambazo makusanyo yake yanapitia *TRA* ambazo ni *TANAPA*, *NGORONGORO* na *TAWA* ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 584.63. Hadi mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021, Taasisi hizo zilikusanya jumla ya shilingi bilioni 89.57 sawa na asilimia 15 ya lengo la makusanyo. Kutofikiwa kwa malengo kulisababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa *Covid-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 114.59 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Aprili, 2021, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 64.59 sawa na asilimia 56 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imepata mafanikio mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imefanikiwa kuboresha miundombinu ya huduma za utalii katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, Wizara imenunua kivuko cha *MVRubondo* chenye ukubwa wa tani

25 ambacho kina uwezo wa kubeba magari manne na watu 25 kwa wakati mmoja. Hatua hizi zitasaidia kuongeza idadi ya watalii na mapato zaidi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kupokea watalii licha ya uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa *COVID-19* ambapo watalii 620,867 kwa mwaka 2020 walitembelea nchini ikilinganishwa na matarajio ya watalii 437,000 yaliyokadiriwa awali kwa kuzingatia uwepo wa ugonjwa huo, sawa na asilimia 142 ya lengo. Aidha, jumla ya watalii wa ndani 571,353 walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Mafanikio hayo yalitokana na mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaliwa kwa Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii (*SOPs*) katika kipindi cha *COVID-19*. Kwa upande mwingine, Tanzania imefanikiwa kuwa mionganoni mwa nchi chache za Afrika zilizofanikiwa kupata Muhuri wa *Safe Travel* wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (*WTTC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia jitihada za Wizara za kuboresha shughuli za uhifadhi na kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali, Tanzania imepata tuzo za Kimataifa zifuatazo: Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi bora Barani Afrika, kuwa mshindi wa pili Afrika na wa 12 duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wafuatiliaji wa ukurasa wake katika mtandao wa kijamii wa *Instagram* kwa mwaka 2020. Hifadhi hii pia imetambuliwa na Gazeti Maarufu la Forbes la nchini Marekani kama kivutio cha pili duniani mionganoni mwa vivutio bora 21 vya kutembelewa mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Serengeti na Tarangire zimeshinda tuzo ya *Traveler's best of the best 2021*. Kwa upande mwingine, Kiwanja cha Ndege cha Msembe katika Hifadhi ya Taifa Ruaha kimefanikiwa kuwa kiwanja chenye mandhari nzuri zaidi Afrika kwa mwaka 2020. Sambamba na hilo, *TANAPA* imetangazwa kuwa mshindi wa kundi la dhahabu mionganoni mwa washindi 51 kutoka nchi 39 duniani wa tuzo ya huduma za viwango kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuvutia watalii, Wizara imefanikiwa kuendeleza mazao mbalimbali yakiwemo utalii wa ikolojia; utalii wa jiolojia; utalii wa faru; utalii wa kuona wanyamapori nyakati za usiku; utalii wa farasi; utalii wa kupiga makasia; na uvuvi wa kujiburudisha. Aidha, katika kuendeleza utalii wa malikale, Wizara imeanzisha makumbusho mpya katika eneo la Urithi wa Dunia la Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Wizara imefungua fursa za shughuli za utalii katika Ukanda wa Kaskazini Magharibi kwa kuanzisha utalii wa maji katika Ziwa Victoria na Ghuba ya Speke. Jitihada hizo, zitachangia ongezeko la idadi ya watalii, wastani wa muda wa mtalii kukaa nchini na mapato yatokanayo na shughuli za kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imeanzisha mashamba mapya mawili ya miti ya Makere Kusini liliopo katika Wilaya ya Kasulu lenye hekta 30,000 na Mwanhala liliopo Wilaya ya Nzega lenye hekta 3,000 na hivyo kuongeza idadi ya mashamba ya miti ya Serikali Kuu kutoka 23 hadi 25. Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo wananchi, imepanda jumla ya miche milioni 3.51 katika maeneo tofauti ya Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara na uvunaji haramu wa mazao ya misitu. Kutoka na juhudhi hizo ujangili umepungua kwa takribani asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utatuza wa Migogoro baina ya Wanyamapori na Binadamu (2020 - 2024). Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri mbalimbali imeendelea kufanya doria na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na

waharibifu. Kwa namna ya kipekee naomba nitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara ya kwanza Wizara ilizindua namba maalum za simu (*hotlines*) ambazo siyo za kulipiwa kwa ajili ya kupata taarifa za haraka kuhusu matukio hayo kutoka kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Wizara imekamilisha maandalizi ya Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu; na kuandaa Mtaala wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu utakaotumika kutoa mafunzo kwa watumishi. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za uwindaji wa wenyeji; mashamba, bustani na ranchi za wanyamapori; uuzaji wa nyamapori; uwindaji wa kitalii; na maeneo maalum ya uwekezaji kwenye hifadhi za wanyamapori inayojulikana kama *SWICA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa lina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji utalii kwenye hifadhi za Taifa 22. Katika kutekeleza jukumu hilo, shirika limetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuboresha mahusiano katika hifadhi na jamii ambapo elimu ya uhifadhi imetolewa kwa vijiji 402; kuvijengea uwezo vikundi 54 vinavyopakana na hifadhi za Taifa kwa lengo la kuviwezesha kushiriki katika kukabiliana na ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (*TAWA*) ina jukumu la kusimamia uhifadhi na kuendeleza utalii katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo matatu ya ardhioevu. pia ni mwangalizi na mshauri wa shughuli za uhifadhi katika maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (*WMA*), mashamba, bustani, ranchi na Kituo cha kulelea wanyamapori wenye matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Mamlaka imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya siku doria 99,341; kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kuepuka na kujikinga dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu; na kuanzisha vituo vya

Askari vya kudumu kwa ajili ya kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yenyé matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ina jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi, uendelezaji wa utalii na ustawi wa jamii zinazoishi ndani ya eneo la Hifadhi. Aidha, kupitia programu ijlikanayo kama *Ngorongoro Crater App*, jina la Hifadhi ya Ngorongoro limepata mwitikio mkubwa kwa kufuatiliwa na watu takriban bilioni 1.8 kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii. Kupitia utaratibu wa masoko mtandao, idadi ya watu duniani wanaofuatilia vivutio vya utalii vilivyopo eneo la Ngorongoro imeongezeka kutoka milioni 1.35 mwezi Juni, 2020 hadi watu milioni 6.96 kufikia mwezi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Huduma za Misitu una jukumu la kusimamia hifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki katika maeneo ya misitu 463 iliyohifadhiwa. Katika hatua nyingine, Wakala umeendelea kutekeleza na kuwezesha shughuli za upandaji miti katika mashamba ya Serikali, maeneo ya watu binafsi na taasisi mbalimbali. Katika hatua hiyo, tani 7.78 za mbegu bora za miti zimezalishwa, miche 32,331,910 na vipando 52,790 vya mikoko vimeoteshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeteketeza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati nchini ambayo ni utalii wa mikutano na matukio, fukwe, meli, michezo na utamaduni; kuainisha maeneo ya fukwe yanayofaa kwa ajili ya shughuli za utalii; na kuandaa Mwongozo wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Utalii wa Meli katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, Wizara pia imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza na kukuza utalii kupitia matukio ya michezo na utamaduni. Kwa ujumla, matukio hayo yamekuwa yakitoa

fursa ya kutangaza vivutio vya utalii katika maeneo ya malikale, wanyamapori, misitu na nyuki na hivyo kuwa chachu ya kuhamasisha makundi mbalimbali ya kijamii kushiriki katika utalii wa ndani. Juhudi hizo zitaongeza la idadi ya watalii na ukusanyaji mapato na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa malikale. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa mwaka 2020/2021, Wizara imebainisha fursa za uwekezaji katika maeneo 18 ya malikale na vituo vya Makumbusho katika mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma, Mara na Arusha. Shughuli za uwekezaji zitakazofanyika katika maeneo hayo ni pamoja na migahawa ya kisasa, studio, maduka ya zawadi, bustani, huduma za kifedha, maduka ya bidhaa za asili na utamaduni na maeneo ya kuweka kambi za utalii. Kutokana na fursa hizo, wadau mbalimbali wanakaribishwa kuwekeza katika maeneo yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Shirika la Makumbusho la Taifa limeandaa mpango wa jumla wa uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 90 ya malikale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika limeendelea na zoezi la kukusanya taarifa za kihistoria za Marais kwa ajili ya kutumika kama kumbukumbu kwenye Makumbusho ya Marais itakayojengwa Jijini Dodoma. Aidha, Shirika limeanza maandalizi ya programu ya kuenzi historia na falsafa ya Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere inayofahamika kama Mwl. Nyerere@100. Sambamba na hatua hiyo, Wizara kupitia Makumbusho ya Taifa imeanzisha klabu za historia na uzalendo mashulenii.

Katika kuhakikisha somo la historia na uzalendo linawafikia wanafunzi ipasavyo mashulenii, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imefanikiwa kufungua klabu 16 za historia na uzalendo katika Mikoa ya Ruvuma na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutekeleza miradi sita ya maendeleo. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa wa mpango wa bajeti wa mwaka 2020/2021 yamefanuliwa zaidi kuanzia ukurasa wa tisa hadi ukurasa wa 102 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa *COVID-19* duniani ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri sekta ya utalii na hivyo kupungua kwa mapato yanayotokana na sekta hiyo; kuwepo kwa mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi, hali hiyo imesababisha kuathirika kwa uoto wa asili na kupungua kwa malisho ya wanyamapori; uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa shughuli za kibinadamu; uwepo wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori; mlipuko wa magonjwa kati ya binadamu na wanyamapori; na uwepo wa matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na uwepo wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi na mali zao, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha udhibiti wa wanyamapori husika. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha vikosi vya kudhibiti wanyamapori hao, kutumia mbinu za kielektroniki za kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori kwa kuwafunga vifaa maalum hasa katika maeneo yenye matukio mengi pamoja na kutoa elimu ya namna ya kujikinga. Katika hatua nyingine, Wizara imezindua namba maalum za simu hotlines kwa ajili ya kupata taarifa kwa haraka kuhusu matukio hayo. Sambamba na hatua hizo, Wizara imeandaa mipango ya usimamizi na udhibiti wa moto na kuendelea kutoa elimu kwa jamii zinazopakana na maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, makadirio ya maduhuli yatakayokusanya na Sekta ya Maliasili na Utalii ni jumla ya Shilingi bilioni 689.34. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 478.01 zitakusanya kupitia

Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kutokana na vyanzo vya *TANAPA, NCAA* na *TAWA* na shilingi bilioni 211.33 zitakusanywa kuititia Wizara na Taasisi zake. Utaratibu wa ukusanyaji wa mapato umezingatia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 ambapo mapato yanayotokana na rasilimali za maliasili na utalii yanakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kuititia *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara na Taasisi zake inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 571.63. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 418.86 ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 152.77 za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara itatekeleza mipango mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Wanyamapor wa Mwaka 2021 mpaka 2032; kukamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara 2021/2032, kuendelea kudhibiti matukio ya wanyamapor wakali na waharibifu, kuratibu utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi kuboresha usimamizi wa shoroba ya wanyamapor na kufanya tathmini ya hali ya mapori tengefu ili kupunguza mgongano baina ya binadamu na wanyamapor.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shughuli hizo, Wizara itaendelea kuboresha huduma za utalii. Katika kutekeleza ibara ya 67 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayoekelekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kukuza na kuimarisha utalii wa uwindani na wanyamapor, Wizara imebuni mkakati unaovutia mitaji mikubwa na kwa muda mrefu katika maeneo maalum ya vitalu vya uwindaji ujulikanao kama *Special Wildlife Investment Concession Areas (SWICA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuhudumia mashamba 23 ya miti yenye ukubwa wa hekta 445,554.7. Katika kutelekeza bajeti ya mwaka 2021/2022

Wizara itatoa mafunzo ya usimamizi wa misitu kwa Kamati za Maliasili za Vijiji 97 kwa ajili ya kuiongezea uwezo wa kulinda na kusimamia rasilimali za misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia uendelezaji wa viwanda nchini, *TFS* inaendelea kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda na misitu ambapo inatarajia kuuza mita za ujazo milioni moja kutoka mashamba ya miti 13 na zaidi ya mita za ujazo 700,000 kutoka misitu ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na jitihada za kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, meli pamoja na kutekeleza mradi wa kuendeleza utalii wa mikutano na matukio. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuchukuwa hatua za kuirejesha sekta ya utalii katika hali yake ya awali baada ya athari za *Covid 19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wadau katika kuendeleza sekta ya utalii nchini kupitia jukwaa la majadiliano baina ya sekta ya Umma na sekta binafsi pamoja na matukio ya mkakati ya uwezeshaji wa masuala ya utalii. Aidha Wizara kupitia *TTB* itatumia mbinu mbalimbali kutangaza utalii wa ndani na wa nje nchini kwa kuratibu na kushiriki maonesho ya utalii katika masoko ya msingi ya kimkakati na yale yanayoibuka yakiwemo katika nchi za Marekani, Urusi, China, India, Australia Israel, nchi za Bara la Ulaya, Falme za Kiarabu na Kanda ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kutangaza utalii wa ndani kupitia maonesho na matamasha mbalimbali yakiwemo Karibu *Kill Fair*, Siku ya Utalii Duniani, Karibu Kusini, Siku ya Vimondo Duniani, *Rock City Marathon*, *Kill Marathon*, *Tulia Marathon*, *Majimaji Serebuka*, *Afrika Trade Fair*, pamoja na *Lamadi Utalii Festival*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipee, naomba kuliharifu Bunge lako Tukufu, Serikali kupitia Wizara itaaniszha utalii mahususi wa lugha ya Kiswahili (*Swahili Tourism*

Package). Katika aina hii ya utalii, mtalii ataunganishwa na vifurushi mbalimbali vyta utalii ambavyo vinaendana na lugha pamoja na utamaduni wa Kiswahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Shirika la Makumbusho la Taifa litaendelea na shughuli mbalimbali ikiwemo ujenzi wa makumbusho ya marais itakayojengwa Jijini Dodoma. Katika mwaka 2021 Wizara itatekeleza miradi nane ya maendeleo. Orodha ya miradi hiyo inapatikana katika bajeti ya Wizara ya mwaka 2021/2022 ambayo imefafanuliwa zaidi ukurasa wa 106 mpaka ukurasa wa 152 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii tena kuwashukuru: Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kullongoza Bunge letu Tukufu. Pia nawashukuru wadau wate kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee naishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali, pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee Wizara inaishukuru Klabu ya Soka ya Simba kwa kutangaza utalii kupitia mpango wao wa *Visit Tanzania*. Naomba pia vilabu vingine vifuate nyayo za Club ya Simba Sports Club. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi na maliasili, malikale na uendelezaji wa utalii. Natoa rai kwa wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Ni matumaini yangu kuwa kupitia ushirikiano huo, malengo ya uhifadhi yatafikiwa kwa haraka na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 571,632,424,000/= kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo, shilingi 418,859,544,000/= ni kwa

ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 152,772,880,000/= ni miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 153,537,684,000/= za mishahara; na shilingi 265,321,860,000/= ni za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 113,893,184,000/= fedha za ndani; na shilingi 38,879,699,000/= fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ([www.maliasili.go.tz](http://www.maliasili.go.tz))

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofî*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA  
DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB.), WAKATI  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 -  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **1.0 UTANGULIZI**

**1.** *Mheshimiwa Spika*, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mwenyezeki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**2.** *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Aidha, kwa namna ya pekee na kwa masikitiko makubwa naomba niungane na

wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waheshimiwa Wabunge wote; Chama Cha Mapinduzi; na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano (5).

**3. *Mheshimiwa Spika***, hakika uzalendo, uchapakazi na umahiri wake katika kuliongoza Taifa letu pamoja na mchango wake mkubwa katika kulinda, kutetea na kuimarisha shughuli za uhifadhi wa maliasili na uendelezaji utalii nchini, hautasahaulika kamwe na utaendelea kukumbukwa na kuenziwa daima. Miongozo na maelekezo yake yameiwezesha Wizara na Taifa kwa ujumla kupata mafanikio na kusonga mbele katika maeneo mbalimbali. Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wenzangu kwa kuondokewa na Viongozi wengine Wakuu wakiwemo: Mheshimiwa Maalim Self Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**4. *Mheshimiwa Spika***, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, wananchi na familia za marehemu kwa kuondokewa na Waheshimiwa Wabunge wafuataao: Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambarwe; na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara. Vifo

vya Wabunge hao vimeleta majonzi makubwa kwa Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla kutokana na kukosa michango yao muhimu katika utendaji wa Bunge letu. Aidha, natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na baadhi ya watumishi kupoteza maisha, na wengine kujeruhiwa wakiwa wanatekeleza majukumu ya uhifadhi wa maliasili. Vilevile, ninatoa pole kwa wananchi ambao wamepoteza maisha na walipata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye majeruhi na azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa kuendelea kuaminipa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Balozi Hussein Athman Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kusimamia majukumu ya Sekta mbalimbali. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeverti wa Bunge na wenyeverti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** kwa dhati kabisa, niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Aloyce Andrew Kwezi (Mb.) na Makamu Mwenyeverti Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya (Mb.) kwa ushirikiano, maoni na ushauri wanaoendelea kutoa kwa Wizara. Maoni na ushauri wao umeendelea kuwa chachu ya mafanikio katika kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Wizara itaendelea kushirikiana kikamilifu na Kamati hii na Bunge lako kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yake na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika sekta.

**7. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii ambayo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Aidha, ninawashukuru viongozi wenzangu wa Wizara akiwemo Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb.), Naibu Waziri; Dkt. Allan Herbert Kijazi, Katibu Mkuu; na Ndugu Ludovick James Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu; kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vilevile, ninawashukuru Watendaji Wakuu na watumishi wa Wizara; na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, kwa namna ya kipekee ninaomba kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa Bibi Florah Ndumbaro na Wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

**8. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii inajumuisha sehemu kuu tano (5) ambazo ni Utangulizi; Majukumu ya Wizara; Mchango wa Maliasili na Utalii katika Uendelezaji wa Uchumi Shindani na Viwanda; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

## **2.0 MAJUKUMU YA WIZARA**

**9. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kuandaa na kufanya mapitio ya miongozo ya sera, sheria, kanuni, mikakati mbalimbali; kusimamia ulinzi wa rasilimali za maliasili na malikale; kuendeleza na kutangaza utalii; kushirikisha wadau; kusimamia ukusanyaji wa maduhuli; na kujenga uwezo wa kusimamia Sekta ya Maliasili na Utalii.

### **3.0 MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA UCHUMI NA VIWANDA**

**10. *Mheshimiwa Spika*,** Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 imebainisha mikakati mbalimbali ya kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu kuititia sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili na uendelezaji utalii. Utekelezaji wa Dira hiyo kuititia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/2017 - 2020/2021) ni kielelezo kikuu cha mafanikio ya nchi yetu kuingia katika kundi la nchi zenyechumi wa kati mwaka 2020 kabla ya matarajio ya awali ya mwaka 2025.

**11. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za maliasili na malikale zenyechumi wa mchango mkubwa katika uendelezaji utalii, ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira kwa ujumla. Utalii huchangia wastani wa asilimia 17 ya Pato la Taifa; asilimia 25 ya fedha za kigeni na huzalisha ajira takriban milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Aidha, sekta hii huchochaea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi ikiwemo viwanda, biashara, kilimo, mifugo na usafirishaji.

**12. *Mheshimiwa Spika*,** rasilimali za misitu na nyuki huchangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa; asilimia 5.9 ya mapato yatokanayo na biashara ya nje na ajira takriban milioni nne kwa mwaka. Misitu huchangia katika uhifadhi wa baioanuai za mimea na wanyama, uhifadhi wa udongo na vyanzo vya maji na hurekebisha mfumo wa hali ya hewa na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, misitu inachangia ukuaji wa sekta nyingine za uzalishaji kama vile maji, kilimo, mifugo, viwanda na nishati. Sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 90 ya nishati ya kupikia nchini kutokana na miti (mkaa na kuni) huku takriban asilimia 90 ya umeme ukizalishwa kwa nguvu ya maji ambayo vyanzo vyake vingi viko katika maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa upande mwingine, mazao ya nyuki hutumika kama chakula na malighafi katika viwanda vya kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwemo vipodozi na madawa. Nyuki ni mchavushaji mkuu wa mimea

ambapo husaidia kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya chakula na uhifadhi wa mazingira.

**13. *Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maliasili ni moja ya sekta muhimu zinazochangia kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda nchini. Mathalan, Sekta ya Misitu huchangia takriban asilimia 90 ya vifaa vya ujenzi na samani zinazotumika majumbani. Kwa kuzingatia mchango wa Sekta ya Maliasili katika uchumi wa nchi yetu, na hasa katika kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, napenda kutoa rai kwa Watanzania wote na wadau kwa ujumla kushirikiana na Wizara katika kuhakikisha uhifadhi, ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali hizi unaendelezwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

#### **4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021**

**14. *Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umezingatia miongozo mbalimbali, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020; Hotuba ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la 11 mwaka 2015; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango Mkakati wa Wizara (2016/17 - 2020/2021); sera na sheria za sekta za usimamizi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii; na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

##### **4.1 Ukusanyaji Maduhuli**

**15. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 218,546,602,092** kutokana na vyanzo vinavyosimamiwa moja kwa moja na Wizara ikiwemo TFS. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2021, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 147,278,726,762** sawa na asilimia 67 ya lengo. Aidha, taasisi za Wizara ambazo makusanyo yake yanapitia TRA ambazo ni Shirika la Hifadhi

za Taifa Tanzania - TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 584,626,710,590**. Hadi mwishoni mwa mwezi Aprili 2021, Taasisi hizo zilikusanya jumla ya **Shilingi 89,571,667,291** sawa na asilimia 15 ya lengo la makusanyo. Kutofikiwa kwa malengo hayo kulisababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

#### **4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**16. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 114,593,952,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 69,573,850,000** zilikuwa za matumizi ya kawaida na **Shilingi 45,020,102,000** za miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2021, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya **Shilingi 64,587,552,684** sawa na asilimia 56 ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha **Shilingi 48,847,760,664** za matumizi ya kawaida na **Shilingi 15,739,792,020** za miradi ya maendeleo.

#### **4.3 Utekelezaji wa Maagizo ya Mheshimiwa Rais**

**17. *Mheshimiwa Spika***, katika Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitao tarehe 06 Aprili, 2021 wakati akiwaapisha Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na baadhi ya Wakuu wa Taasisi, Wizara ya Maliasili na Utalii ilipewa maagizo mawili (2) ambayo ni: kushughulikia changamoto za matumizi mseto na mimea vamizi katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; na suala la uchimbaji wa madini katika maeneo yaliyohifadhiwa.

**18. *Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Maliasili na Utalii imeanza kuyafanya kazi maagizo yaliyotolewa kwa hatua za awali. Mathalan, kwa upande wa changamoto ya matumizi mseto katika eneo la Ngorongoro, tarehe 08 Aprili, 2021 chini ya uenyekiti wangu, Wizara ilifanya kikao na uongozi wa Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwa ajili ya kuanza kutekeleza maelekezo hayo. Hatua inayoendelea

kwa sasa ni kufanya tathmini na kuandaa taarifa itakayowezesha Serikali kufanya maamuzi stahiki. Kutokana na umuhimu wa suala hilo, Wizara kwa kushirikisha wadau mbalimbali itaandaa mapendeleko na kuyawasilisha katika ngazi za maamuzi Serikalini ili kupata namna bora ya kutatua changamoto hiyo kwa manufaa mapana ya Taifa. Katika hatua nyingine, Wizara inaendelea kufanya tafiti kwa kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu kikiwemo Chuo Kikuu cha Nelson Mandela ili kupata suluhisho la kudumu kuhusu tatizo la mimea vamizi katika eneo hilo.

**19. *Mheshimiwa Spika*,** kuhusu uchimbaji wa madini katika hifadhi, mnamo tarehe 13 Aprili 2021, Wizara chini ya uenyekiti wangu ilikutana na taasisi za uhifadhi zilizo chini ya Wizara na kujadili kwa kina namna ya kutekeleza agizo hilo. Kwa ujumla, Wizara itafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Madini na kuchambua kwa kina faida na hasara ya kuchimba au kutochimba madini katika maeneo hayo. Pamoja na maagizo hayo, Wizara pia itazingatia maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoynatoa Bungeni tarehe 22 Aprili, 2021.

#### **4.4 Mafanikio**

**20. *Mheshimiwa Spika*,** katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:

##### **4.4.1 Kupungua kwa Ujangili na Uvunaji Haramu wa Maliasili**

**21. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Mathalan, matokeo ya sensa ya mwaka 2020 yameonesha kuongezeka kwa idadi ya tembo katika Mfumo Ikolojia Serengeti kutoka 6,087 mwaka 2014 hadi 7,061 mwaka 2020. Mafanikio ya kupungua kwa ujangili, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na kuongezeka kwa

wanyamapori yamechangiwa pamoja na mambo mengine, kuendeshwa kwa siku doria 746,413 zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 5,609; kuvunjwa kwa mitandao 95 ya ujangili; na kuzuiliwa kwa matukio 302 ya ujangili kabla hayajatendeka. Jitihada nyingine ni pamoja na ujenzi wa minara mitatu (3) ya mawasiliano ya redio katika maeneo ya Oldeani, Losirwa na Kreta ya Empakai. Kutokana na juhudhi hizo, ujangili umepungua kwa takriban asilimia 90.

#### **4.4.2 Kupungua kwa Mimea Vamizi katika Maeneo ya Hifadhi**

**22. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Mimea Vamizi (National Invasive Species Strategy and Action Plan, 2019 - 2029), Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kufanya tafiti juu ya mtawanyiko, madhara na kubaini mbinu za kukabiliana na mimea vamizi ndani ya hifadhi na maeneo yanayopakana na hifadhi. Katika hatua za awali imebainika uwepo wa aina 25 za mimea vamizi ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela umebaini njia ya asili ya kudhibiti mimea vamizi aina ya *Gutenbergia cordifolia*, *Tagetes minuta* na *Bidens schimperi* inayopatikana katika Kreta ya Ngorongoro na eneo la Ndutu. Pamoja na mbinu hizo, Wizara imeendelea kutumia mbinu nyingine za kupambana na mimea vamizi zikiwemo kung'oa na kufyeka mimea hiyo. Hatua hizi zimevezesha kutokomezwa kwa mmea vamizi aina ya gugu karoti kwa zaidi ya asilimia 90. Vilevile, Wizara imefanikiwa kudhibiti mimea mingine vamizi kwa asilimia 15.6 kwenye eneo la Kreta ya Ngorongoro lenye ukubwa wa hekta 5,301 ambalo limeathirika na mimea hiyo.

**23. *Mheshimiwa Spika*,** katika hatua nyingine, Wizara imefanikiwa kuondoa mimea vamizi kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 2,269 katika hifadhi za Taifa za Arusha, Kitulo, Serengeti, Katavi, Milima ya Mahale, Ziwa Manyara, Mikumi, Milima ya Udzungwa, Ibanda - Kyerwa, Rumanyika - Karagwe, Tarangire, Gombe, Kitulo, Kisiwa cha Saanane na Kilimanjaro kwa lengo la kuboresha maeneo ya malisho. Aidha, jumla ya miti ya asili 2,700 imeoteshwa katika hifadhi

za Taifa Kilimanjaro na Kitulo katika maeneo ambayo mimea vamizi imeng'olewa. Jitihada hizi zimeboresha ustawi wa maeneo ya malisho ya wanyamapori.

#### **4.4.3 Kupandishwa Hadhi Maeneo ya Hifadhi**

**24. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuhifadhi rasilimali za misitu, Wizara imepandisha hadhi Msitu wa Essmingori uliopo Wilaya ya Monduli wenyewe hekta 6,070 kuwa Hifadhi ya Msitu ya Mazingira Asilia na hivyo kuongeza hifadhi za misitu ya mazingira asilia kutoka 19 hadi 20. Aidha, Wizara imepandisha hadhi maeneo 30 mapya ya misitu yenye ukubwa wa jumla ya hekta 139,869 kuwa hifadhi katika wilaya za Chunya, Iringa, Same, Korogwe, Lushoto, Handeni, Muheza, Mwanga, Buhigwe, Mkuranga, Chemba, Newala, Ileje, Dodoma, Ilala, Bukoba, Mbeya Vijijiini, Butiama, Misenyi, Kongwa, Mpwapwa, Kondoa, Madaba na Monduli. Aldha, hifadhi za nyuki sita (6) zenyе ukubwa wa hekta 19,134 katika wilaya za Ileje, Handeni, na Chemba zimetangazwa na hivyo kuongeza idadi ya hifadhi za nyuki kutoka moja (1) hadi saba (7).

#### **4.4.4 Kuboresha Miundombinu ya Utalii**

**25. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imefanikiwa kuboresha miundombinu ya huduma za utalii kwa kujenga na kukarabati barabara, kambi za utalii na njia za utalii wa kutembea kwa miguu. Katika hatua hiyo, barabara zenyе jumla ya urefu wa kilometra 73.4 zimejengwa na kilometra 8,599.8 zimekarabatiwa ndani ya maeneo ya hifadhi za Taifa, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, hifadhi za misitu ya mazingira asilia, mashamba ya miti, mapori ya akiba pamoja na vituo vya malikale. Aidha, kambi za kitalii na loji zenyе jumla ya vitanda 670 zimejengwa katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa lengo la kuboresha huduma za malazi na kuhamasisha utalii wa ndani. Vilevile, njia za utalii wa kutembea kwa miguu zenyе urefu wa kilometra 927 zimejengwa katika maeneo yaliyohifadhiwa ya misitu na wanyamapori. Hatua hii itawezesha kuimarika kwa huduma za utalii katika maeneo hayo.

**26. *Mheshimiwa Spika*,** katika hatua nyingine, Wizara imefanikiwa kujenga malazi ya kitalii ya gharama nafuu yenye jumla ya vitanda 105 katika Hifadhi za Taifa Saadani (71), Tarangire (12), Mkomazi (12) na Kitulo (10) kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani. Aidha, Wizara imeanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa hoteli yenye hadhi ya daraja la nyota tatu katika eneo la Rubambagwe, Chato pamoja na ujenzi wa lango la Naabi katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Hoteli hii inajengwa kwa lengo la kuchochea utalii katika Ukanda wa Kaskazini Magharibi. Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa uzio wa umeme wenyewe urefu wa kilometra 13 katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi ili kuendeleza utalii wa faru ndani ya hifadhi hiyo. Katika hatua nyingine, Wizara imenunua kivuko cha *MV Rubondo Island* chenyehukubwa wa tani 25 ambacho kina uwezo wa kubeba magari manne (4) na watu 25 kwa wakati mmoja. Kivuko hicho kitasaldia na kuboresha utoaji wa huduma kwenye hifadhi na maeneo ya vivutio vilivyoko Ziwa Victoria na hivyo kuleta ufanisi zaidi katika maeneo husika.

#### **4.4.5 Kuendelea kwa Shughuli za Utalii katika Kipindi cha COVID-19**

**27. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania imeendelea kupokea watalii licha ya uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19. Kwa kuzingatia mwenendo wa ukuaji wa sekta ya utalii nchini, katika mwaka 2020, Wizara ilitarajia kupokea jumla ya watalii 1,867,000. Makisio hayo yalikuwa ni kabla ya kutokea kwa janga la COVID-19. Baada ya mlipuko wa COVID-19, Wizara ilifanya tathmini ya athari za ugonjwa huo katika sekta ya utalii na kuweka makisio mapya ya jumla ya watalii 437,000 yaliyozingatia hali halisi ya uwepo wa COVID-19. Katika kufanikisha lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliweka mikakati mbalimbali ya kupambana na madhara ya janga hilo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii - SOPs katika kipindi cha COVID-19 kwa kuzingatia maelekezo ya Shirika la Afya Duniani na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na kuandaa Mpango wa Kuirejesha Sekta ya Utalii Nchini katika Hali ya Awali kabla ya Kuathiriwa na

COVID-19. Kutokana na juhudhi hizo pamoja na uwepo wa COVID-19, Tanzania kwa mwaka 2020 ilifanikiwa kupata watalii 620,867 wa kimataifa na watalii 571,353 wa ndani walio tembelea vivutio mbalimbali nchini.

**28. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande mwingine, Tanzania imefanikiwa kuwa mionganoni mwa nchi chache za Afrika zilizofanikiwa kupata Muhuri wa *Safe Travel*/wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (WTTC). Vigezo vilivyotumika kutoa muhuri huo ni pamoja na WTTC kujiridhisha na hatua za kukabiliana na maambukizi ya COVID-19; nchi husika kutoa mwongozo wa kiafya wa kuzingatiwa na wasafiri wanaoingia na kutoka nchini (COVID-19 Travel Advisory); na kuonesha kwa vitendo utayari wa kupo kea wageni ili kuwajengea imani watalii katika masoko ya kimataifa kuwa Tanzania ni mahali salama kutembelea.

**29. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania pia imeendelea kufungua masoko mapya ya utalii ikiwemo nchi za Ursi, Poland na Ukraine; na kuorodheshwa na nchi ya Ursi kuwa mionganoni mwa nchi tatu (3) duniani ambazo ni salama kwa wananchi wake kutembelea. Mafanikio haya yamechangiwa na juhudhi mbalimbali za utangazaji vivutio vya utalii kidijitali kuitia mitandao ya kijamii ikiwemo Twitter, Facebook, Wechart, YouTube, Instagram hususan kampeni yaâ*Tanzania is Ready*, pamoja na *live streaming*. Vilevile, Wizara imeandaa video 25 zikiwemo zenye kutangaza vivutio vya Tanzania kwa utambulisho ujulikanao kama Tanzania Unforgettable! na video maalum kuonesha utekelezaji wa SOPs katika kukabiliana na maambukizi ya COVID-19.

#### **4.4.6 Kuongezeka kwa Umaarufu wa Hifadhi za Tanzania Duniani**

**30. *Mheshimiwa Spika*,** kufuatia jitihada za Wizara za kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali na kuboresha shughuli za uhifadhi, Tanzania imepata tuzo za kimataifa zifuatazo: Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi bora barani Afrika kwa mwaka 2020, tuzo iliyotolewa na taasisi ya *World*

*Travel Awards*, Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa mshindi wa pili Afrika na wa 12 duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wafuatiliaji wa ukurasa wake katika mtandao wa kijamii wa *Instagram* kwa mwaka 2020, tuzo iliyotolewa na Taasisi ya *Mainland Aggregates Limited* ya nchini Marekani; na Hifadhi za Taifa Serengeti, Kilimanjaro na Tarangire kushinda tuzo ya *Traveler best of the best 2021*, iliyotolewa na Taasisi ya *Trip Advisor Award*. Vilevile, Hifadhi ya Taifa Serengeti imetambuliwa na Gazeti Maarufu la Forbes la nchini Marekani kama kivutio cha pili (2) duniani mionganoni mwa vivutio bora 21 vya kutembelewa mwaka 2021. Aidha, Kiwanja cha Ndege cha Msembe katika Hifadhi ya Taifa Ruaha kimefanikiwa kuwa kiwanja chenye mandhari nzuri zaidi Afrika kwa mwaka 2020, tuzo iliyotolewa na taasisi ya *Private Fly Scenic Airport*. Sambamba na hilo, TANAPA imetangazwa kuwa mshindi wa kundi la dhahabu mionganoni mwa washindi 51 kutoka nchi 39 duniani wa tuzo ya huduma za viwango kwa mwaka 2020, tuzo iliyotolewa na Taasisi ya *European Society for Quality Research* (ESQR).

#### **4.4.7 Kuongezeka kwa Mashamba na Upandaji Miti**

**31. *Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imeanzisha mashamba mapya mawili (2) ya miti ya Makere Kusini yaliyopo katika Wilaya ya Kasulu lenye hekta 30,000 na Mwanhala lilitopo Wilaya ya Nzega lenye hekta 3,000 na hivyo kuongeza idadi ya mashamba ya miti ya Serikali Kuu kutoka 23 hadi 25. Aidha, Shamba la Miti Wino (hekta 38,258) lilitopo Mkoa wa Ruvuma na Shamba la Miti Silayo (hekta 69,700) lilitopo Mkoa wa Geita yalizinduliwa rasmi mwezi Januari, 2021. Kwa upande mwingine, Wizara imefanikiwa kuzalisha jumla ya vipando vya mikoko 52,790 na miche ya miti 32,331,910 iliyopandwa katika mashamba ya Serikali, taasisi za umma na binafsi. Jitihada hizi zimelenga kuongeza uhifadhi wa ardhi, balonuai za mimea na wanyama, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi na kuhakikisha upatikanaji wa mazao ya misitu kwa matumizi mbalimbali.

#### **4.4.8 Kuimarisha Huduma za Utalii kwa Njia ya Kielektroniki**

**32. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha ubora wa huduma za malazi, upatikanaji wa takwimu za watalii na ukusanyaji wa mapato, Wizara imeanzisha na kuzindua mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma za malazi nchini katika daraja za ubora ujulikanao kama AserT (Accomodation Services in Tanzania). Mfumo huo unawezesha wamiliki wa huduma za malazi na chakula nchini kujitathmini wenyewe katika ubora wa huduma zao za malazi na chakula kabla ya kupangwa katika daraja za ubora kwa kutumia vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tanzania imekuwa nchi ya kwanza katika Jumuiya hiyo kuwa na mfumo huo wa kielektroniki ambao ulizinduliwa rasmi mwezi Disemba, 2020. Aidha, Wizara imefanikiwa kuboresha mfumo wa *MNRT Portal* kwa ajili ya kusajili wageni wanaolala katika maeneo ya huduma za malazi, kutoa vibali, kukusanya takwimu na uendeshaji wa minada ya uuzaji vitalu.

#### **4.4.9 Kuendeleza Mazao Mapya ya Utalii**

**33. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuvutia watalii, Wizara imefanikiwa kuendeleza zao la utalii ikolojia katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia; utalii wa jiolojia kwa kubainisha maeneo mengine yenye sifa za utalii huo nje ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mathalan Kimondo cha Mbozi Mkoani Songwe; utalii wa faru na utalii wa kuona wanyamapori nyakati za usiku katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi; utalii wa farasi katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; utalii wa kupiga makasia kwenye eneo la Gurusi Swamp ndani ya Hifadhi ya Taifa Tarangire; na uvuvi wa kujiburudisha katika Hifadhi ya Taifa Ruaha. Aidha, katika kuendeleza utalii wa malikale, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imeanzisha makumbusho mpya katika eneo la Urithi wa Dunia la Kilwa Kisiwani iliyozinduliwa tarehe 09 Aprili, 2021. Sambamba na hilo, Wizara imefungua fursa za shughuli za utalii katika Ukanda wa Kaskazini Magharibi kwa kuanzisha utalii wa maji katika Ziwa Victoria na Ghuba ya Speke. Kuanzishwa kwa mazao hayo, kutachangia ongezeko la idadi ya watalii, wastani wa muda

wa mtalii kukaa nchini na mapato yatokanayo na shughuli za kitalii.

#### **4.4.10 Kuanzishwa kwa Mradi Maalum wa Uendelezaji Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE)**

**34. *Mheshimiwa Spika*,** katika hatua za kutekeleza lengo la kuongeza watalii hadi kufikia milioni 5 ifikapo mwaka 2025, kama ambavyo imebainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020 - 2025), Ibara ya 67(a)(ii), Wizara imekamilisha maandalizi ya kuanza Mradi Maalum wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio. Mradi huo pamoja na shughuli nyiningine, utawezesha ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Kimataifa chenye uwezo wa kuhudumia mikutano na shughuli za maonesho kwa wakati mmoja. Mradi huu utaanza kutekelezwa rasmi katika mwaka wa fedha 2021/2022, ambapo utaendeleza zao la utalii wa mikutano na matukio nchini lenye fursa ya kuleta matokeo ya haraka katika ukuaji wa sekta ya utalii.

#### **4.4.11 Kushiriki Kikamilifu katika Mradi wa Kimkakati wa Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere**

**35. *Mheshimiwa Spika*,** katika utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115, Wizara kuititia TFS ilipewa jukumu la kusafisha eneo la mradi lenye ukubwa wa ekari 234,164. Pamoja na changamoto na ugumu wa mazingira ya eneo, ikiwemo ukosefu wa miundombinu ya barabara, mvua, uwepo wa wanyamapori wakali na mawasiliano hafifu, TFS kwa kushirikiana na JWTZ imefanikiwa kusafisha jumla ya ekari 133,473 ambayo ni asilimia 57 ya eneo lote la mradi. Kwa upande mwingine, Wizara kuititia TANAPA imeendelea kutoa ulinzi ili kufanikisha shughuli za mradi kuendelea kama ziliwyopangwa. Baada ya kukamilika kwa mradi huu, pamoja na uzalishaji wa umeme, eneo hilo litatumika kwa shughuli za utalii. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili

na Utalii ilitembelea eneo la mradi tarehe 24 Aprili, 2021 kwa ajili ya kukagua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa jukumu la Wizara la kusafisha eneo husika. Kwa ujumla, Kamati iliridhishwa na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa jukumu hilo. Aidha, mradi huo ukikamilika utaongeza shughuli mbalimbali za utalii zikiwemo utalii wa kuvua Samaki kwa kujiburudisha (sport fishing) na utalii wa kutumia boti.

#### **4.4.12 Kuanzishwa kwa Klabu za Historia na Uzalendo**

**36. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha historia ya Tanzania inaenziwa, Wizara imefanikiwa kuzindua Klabu za Historia na Uzalendo katika shule 18 za Sekondari katika Mikoa ya Dar es Salaam na Ruvuma. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa klubu hizo katika shule mbalimbali nchini. Vilevile, programu 110 za elimu ya urithi wa utamaduni, malikale pamoja na utalii zimefanyika katika shule za msingi na sekondari nchini kwa lengo la kuhamasisha vijana kuwa na uzalendo na kuthamini nchi yao.

#### **4.4.13 Kuboreshwa na Kuimarika kwa Vituo vya Malikale**

**4.4 *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha maeneo ya malikale yanaimarika na kuvutia watalii, Wizara imeboresha vituo vya malikale kwa kujenga barabara yenyе urefu kwa kilomita tano (5), ukuta na njia ya watembea kwa miguu katika Kituo cha Kolo; kuweka umeme katika Kituo cha Mapango ya Amboni; kukarabati vyoo katika Kituo cha Mwl. Nyerere, Butiama na jengo la kihistoria la soko la watumwa katika Kituo cha Mikindani. Sambamba na hilo, Wizara imeanza kuhifadhi taarifa za maeneo ya malikale, mikusanyo na urithi wa utamaduni kidijitali, hatua ambayo itasaidia kuimarisha uhifadhi na kujitangaza kidijitali. Maeneo yaliyoainishwa na taarifa zake kuhifadhiwa ni pamoja na vituo vya Bagamoyo, Kilwa Kisiwani, Songo Mnara, Kilwa Kivinje, Kolo, Kaole, Isimila na Laetoli.

## **4.5 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka**

### **4.5.1 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Katika Maeneo ya Hifadhi**

**37.** *Mheshimiwa Spika*, katika kutatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua katika kutatua migogoro hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kuhakiki mipaka ya hifadhi yenyе urefu wa kilometa 97, kusafisha kilometa 1,554 na kuweka alama za mipaka (beacons) 788 na mabango 180 katika maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori. Aidha, jumla ya miti 6,250 imepandwa katika mipaka ya hifadhi 84 ya misitu ya asili. Kwa upande mwengine, Wizara imeweka jumla ya maboya 66 katika Hifadhi za Taifa Saadani na Rubondo kama alama za mipaka kwenye eneo la maji. Pia, Wizara imeanza zoezi la kuhakiki mipaka kwenye maeneo ya mallkale na Urithi wa Utamaduni ikiwemo vituo vya Kalenga, Amboni, Engaruka, Engaresero, Isimila, Tembe la Kwhihara, Ujiji Kigoma, Tongoni, Kunduchi na Kaole.

### **4.5.2 Ushirikishaji Wadau kwenye Shughuli za Uhifadhi na Utalii**

**38.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutambua mchango wa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi na sekta binafsi katika uhifadhi wa maliasili na uendelezaji utalii. Katika kutekeleza azma hii, Wizara imetoa elimu ya uhifadhi katika vijiji 418 vinavyopakana na hifadhi za Taifa, mapori ya akiba na wananchi wanaoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Katika hatua nyingine, mikutano ya kuelimisha kamati za maliasili imefanyika katika vijiji 451, na elimu ya usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki imetolewa kwa wadau 1,979 kutoka vijiji 540 vinavyopakana na hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, vikundi 127 vya ufugaji nyuki vimeanzishwa na mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki yametolewa kwa wafugaji 2,608 ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.

**39.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuhamasisha, kuboresha na kuimarisha huduma za utalii, Wizara imefanya mkutano na

wadau wa utalii nchini uliofanyika tarehe 03 - 06 Machi, 2021 Mjini Morogoro. Mkutano huu ulihusisha taasisi za umma na sekta binafsi wakiwemo wakala wa safari za anga, wawindaji wa kitalii, wasafirishaji watalii, waongoza watalii na watoa huduma za malazi. Mkutano huo ulishirikisha wadau takriban 440 ambaao walipata fursa ya kujadili mikakati mbalimbali ya kuongeza idadi ya watalii, kuendeleza mazao ya utalii, kuongeza wigo wa mapato, changamoto zinazoikabili sekta ya utalii pamoja na mapendekezo ya utatuzi. Aidha, Wizara ilifanikisha mkutano wa Kimataifa wa *UNESCO Global Geopark* uliofanyika mwezi Disemba, 2020 kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulihudhuriwa na wataalam wa masuala ya jijolejia takriban 600 kutoka nchi mbalimbali duniani kwa lengo la kuutangaza utalii wa miamba wa nchi za Afrika na Uarabuni. Pia, mikutano ya Kamati za Uwezeshaji Utalii - TFC pamoja na Jukwaa la Majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - PPD imefanyika Jijini Arusha mwezi Oktoba, 2020. Vilevile, Wizara imesaini upya Hati ya Makubaliano - MoU na Shirikisho la Vyama vya Utalii nchini - TCT mwezi Disemba, 2020 ili kuimarisha ushirikiano.

**40. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhamasisha uhifadhi na uendelezaji wa utalii nchini, Wizara imeandaa na kurusha vipindi 70 vya televisheni, 51 vya radio na makala 36 kuhusu uhifadhi na vivutio vya utalii. Vilevile, Wizara imefanya warsha katika wilaya saba (7) za Mkoa wa Mwanza. Kupitia warsha hizo, wadau wa malikale na urithi wa utamaduni walijengewa uwezo wa kubaini na kutambua maeneo yenye sifa ya kuwa malikale na urithi wa utamaduni ili yaweze kutumika kwa shughuli za utalii. Aidha, Wizara imefanya mkutano na wadau wa malikale mwezi Agosti 2020, Mjini Morogoro ili kujadili namna bora ya kuboresha Sheria ya Malikale.

#### **4.5.3 Uendelezaji wa Dodoma ya Kijani**

**41. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuendeleza Makao Makuu ya nchi Dodoma kwa kujenga na kuboresha miundombinu na huduma mbalimbali za kijamii. Katika kufanikisha juhudhi hizo,

Wizara inaendelea na mikakati ya upandaji miti ili kuboresha mandhari ya Jiji la Dodoma kupitia Kampeni yake ya "Dodoma ya Kijani". Hadi kufikia mwezi Aprili 2021, jumla ya miche 3,505,280 imepandwa katika maeneo tofauti ya Jiji la Dodoma kwa kushirikiana na wadau wakiwemo wananchi. Wizara itaendelea na kampeni hiyo ili kuwezesha Makao Makuu ya nchi na Serikali kuwa na hali ya hewa nzuri na kuvutia makazi na shughuli za uzalishaji.

#### **4.5.4 Utawala na Uendelezaji Rasilimaliwateru**

**42. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kufanya tathmini na mapitio ya miundo kwa lengo la kujumuisha Idara ya Uratibu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu katika muundo wa Wizara pamoja na kujumuisha majukumu ya Jeshi hilo katika miundo ya taasisi za uhifadhi. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kununua vitendea kazi na kuboresha miundombinu ya ofisi ikiwemo ununuzi wa magari 48, mitambo tisa (9), ujenzi wa ofisi mpya 20 na nyumba 82 za watumishi katika maeneo ya hifadhi. Vilevile, Wizara imeweza watumishi 637 kushiriki katika mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi ambapo watumishi 170 wameshiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi 467 mafunzo ya muda mfupi. Sambamba na hilo, Wizara imeajiri jumla ya watumishi 674 katika kada mbalimbali na kutoa elimu ya masuala ya maadili, rushwa na usalama mahali pa kazi kwa watumishi 170.

**43. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imeendelea kusimamia ustawi na afya za watumishi kwa kuwawezesha watumishi wanaoishi na VVU kupata lishe bora. Aidha, watumishi 267 wamepewa mafunzo kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) pamoja na kupewa ushauri nasaha na chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Ini. Ili kuimarisha mahusiano na afya za watumishi, Wizara imeendelea kuratibu programu za mazoezi kwa watumishi na kuandaa mabonanza ya michezo yaliyoshirikisha watumishi 210 wa Wizara na taasisi nyingine.

#### **4.5.5 Ushiriki katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa**

**44. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii, Wizara imeshiriki katika mikutano mbalimbali kwa lengo la kutekeleza makubaliano ya kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara ilishiriki katika mikutano wa dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Utalii na Usimamizi wa Wanyamapori wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa ngazi ya Makatibu Wakuu uliofanyika mwezi Februari, 2021 kwa njia ya mtandao. Lengo la mikutano huo ilikuwa ni kupitia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii, Mkakati wa kutangaza Utalii wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mkakati wa Kurejesha Sekta ya Utalii katika hali yake baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 na rasimu kuhusu mapitio ya vigezo vyatupanga huduma za malazi na chakula katika viwango vyatubora. Pamoja na mikutano huo, Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa kwa njia ya mtandao.

#### **4.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara**

##### **4.6.1 Sekta ya Wanyamapori**

**45. *Mheshimiwa Spika*,** Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya tafiti za wanyamapori ndani na nje ya maeneo ya hifadhi. Utekelezaji wa majukumu hayo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura 283, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282, Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284 na Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura 260. Aidha, majukumu haya yanatekelezwa kupitia Idara ya Wanyamapori, TANAPA, NCAA, TAWA, TAWIRI, TWPF, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori – Mweka (CAWM), Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi (PWTF) na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC).

#### **4.6.1.1 Masuala Mahsusini ya Sekta ya Wanyamaporini**

##### **(i) Utatuzi wa Migogoro Baini ya Wanyamaporini na Binadamu**

**47. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamaporini wakali na waharibifu, Wizara imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utatuzi wa Migogoro baina ya Wanyamaporini na Binadamu (2020 - 2024). Mkakati huo unalenga kuweka njia bora na endelevu za kukabiliana na wanyamaporini na kuimarishe mahusiano na wananchi kwa kuhakikisha jamii inayoiishi karibu na maeneo ya hifadhi inapata elimu ya namna ya kukabiliana na wanyamaporini wakali na waharibifu.

**48. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na wanyamaporini wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi. Aidha, Wizara imeendelea kutumia teknolojia ya kufuatilia nyendo za tembo, simba na fisi kwa kuwafunga vifaa maalum (radio collars) ili kurahisisha ufuatiliaji wa wanyamaporini hao. Katika kufanikisha zoezi hilo, jumla ya makundi 42 ya tembo katika Mfumo Ikolojia Serengeti, Ziwa Natron na Manyara - Tarangire; na makundi 17 ya simba katika Mifumo Ikolojia Serengeti na Ruaha - Rungwa wamevishwa mikanda ya mawasiliano ili kuwezesha ufuatiliaji wa mienendo yao. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu imeendelea kufanya doria na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na tatizo la fisi wanaokula mifugo ikiwa ni pamoja na kuharibu maficho ya wanyamaporini hao. Hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara ni pamoja na kuendelea kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamaporini wakali na waharibifu ambapo jumla ya Shilingi 1,251,825,000 zimelipwa. Wizara itaendelea kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali katika jitihada za kukabiliana na wanyamaporini hao.

**(ii) Uvamizi wa Shoroba na Maeneo Mtawanyiko wa Wanyamapori**

**49. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na uvamizi wa shoroba na maeneo mtawanyiko wa wanyamapori kutokana na shughuli za kibinadamu, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanya tathmini ya shoroba nchini kwa ajili ya kuandaa mikakati ya kuzihifadhi ili kuruhusu mtawanyiko wa wanyamapori. Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha uwepo wa shoroba 61, kati ya hizo, shoroba 20 zimeonekana kuhitaji kupewa kipaumbele ili kuzirejesha katika hali yake ya awali ili zisiendelee kuvamiwa. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi. Hatua hizi zitasaidia pamoja na mambo mengine kuruhusu mzunguko ya wanyamapori kutoka eneo moja la hifadhi kwenda maeneo mengine ya hifadhi pasipo kuzuilliwa na shughuli za binadamu na kurejesha mifumo ya asili ya wanyamapori hao.

**4.6.1.2 Idara ya Wanyamapori**

**50. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarishe ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Wizara imekamilisha maandalizi ya Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu; na kuandaa Mtaala wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu utakaotumika kutoa mafunzo kwa watumishi. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za uwindaji wa wenyeji; mashamba, bustani na ranchi za wanyamapori; uuzaaji wa nyamapori; uwindaji wa kitalii; na maeneo maalum ya uwekezaji kwenye hifadhi za wanyamapori - SWICA. Sambamba na hilo, Wizara imepunguza bei ya usajili wa eneo la kuuzia nyamapori kutoka Shilingi 250,000 hadi Shilingi 100,000 ili kuwawezesha wananchi wengi kufungua bucha na kunufaika na rasilimali za wanyamapori. Vilevile, Mkakati wa Kitifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara umefanyiwa mapitio na Mkakati mpya wa miaka 10 (2020/2021 - 2030/2031) unaandalishiwa. Pia, Wizara imekamilisha mwongozo wa uanzishaji wa bucha za nyamapori unaolenga kurahisisha

utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Uuzaji wa Nyamapori za mwaka 2020.

#### **4.6.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA**

**51. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika lina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji utalii kwenye hifadhi za Taifa 22. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limeendelea kuboresha mahusiano kati ya hifadhi na jamii ambapo elimu ya uhifadhi imetolewa kwa vijiji 402 vinavyopakana na hifadhi za Taifa. Sambamba na hilo, Shirika kwa kushirikiana na wadau limevijengea uwezo vikundi 54 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Arusha, Ruaha, Saadani, Kisiwa cha Rubondo, Kisiwa cha Saanane, Mikumi na Mkomazi kwa lengo la kuvizewesha kushiriki katika kukabiliana na ujangili. Vilevile, ili kudhibiti maambukizi ya magonjwa kati ya wanyamapori na mifugo, Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limetoa chanjo kwa mifugo 618 wakiwemo mbwa na paka katika vijiji 19 vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale.

**52. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuboresha huduma za utalii, Shirika liko katika hatua za mwisho za kuingia katika mfumo wa usimamizi wa ubora unaotambulika Kimataifa wa ISO 9001:2015 (Quality Management System). Faida za kuingia katika mfumo huo ni kujenga hali ya kuaminika katika soko la utalii kimataifa, kuongeza ubora wa huduma, kuongeza fursa za kuingia katika masoko mapya ya utalii pamoja na kuongeza ufanisi. Pamoja na hatua hiyo, jumla ya watumishi 460 wamepatiwa mafunzo ya ukarimu kwa wateja ili kuboresha huduma ya ukarimu kwa mteja.

**53. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Shirika limeendelea kupanua wigo wa uwekezaji kwa kutenga maeneo mapya 45 ya huduma za malazi yenye uwezo wa vitanda 3,250 kwa ajili ya uwekezaji katika hifadhi za Taifa Nyerere (35), Mto Ugalla (6) na Kigosi (4). Aidha, Shirika limetenga jumla ya maeneo 14 kwa ajili ya uwekezaji maalum wa kitalii katika hifadhi za Taifa Nyerere (4), Ruaha (4), Burigi - Chato (1), Katavi (1), Kigosi (2) na Mto Ugalla (2). Vilevile, Shirika limeanzisha mazao manne (4) ya utalii kwa lengo la

kukidhi mahitaji ya watalii na kuongeza siku za wageni kukaa hifadhini katika hifadhi za Taifa Ruaha, Mkomazi na Tarangire. Mazao hayo ni pamoja na utalii wa uvuvi wa kujiburudisha, utalii wa kuona wanyamapori usiku, utalii wa kula chakula porini na utalii wa kupiga makasia. Sambamba na hilo, Shirika limeendelea kukamilisha taratibu za awali za uanzishwaji wa zao jipya la utalii wa kiberenge katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro.

**54. *Mheshimiwa Spika*,** katika hatua ya kutangaza utalii kidijitali, Shirika limeandaa na kusambaza video fupi 83 na mabango ya kielektroniki 139 yenye jumbe mbalimbali kuhusu vivutio vya utalii vinavyopatikana katika hifadhi za Taifa. Sambamba na hilo, Shirika limeendesha kampeni tano (5) za kuhamasisha utalii wa ndani kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo kampeni ya *Bunge na Utalii*. Vilevile, Shirika limeshiriki katika maonesho nane (8) ya ndani na kuhamasisha utalii kupitia siku ya utalii duniani, sherehe za mwisho wa mwaka, siku ya wapendanao na siku ya wanawake duniani. Pia, Shirika limeendelea kutumia fursa mbalimbali za kuhamasisha utalii kwenye masoko ya nje ikiwa ni pamoja na kushiriki mikutano sita (6) ya kidijitali.

**55. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma, Shirika limeboresha miundombinu ya TEHAMA katika hifadhi za Taifa Burigi - Chato, Nyerere, Kigosi, Ibanda - Kyerwa, Rumanyika - Karagwe na Mto Ugalla. Aidha, mifumo ya teknolojia na mawasiliano ya huduma ya mtandao imeboreswa katika malango 50 ya hifadhi za Taifa Tarangire, Mikumi, Udzungwa, Kisiwa cha Rubondo, Kilimanjaro, Serengeti, Mkomazi, Katavi, Gombe, Arusha, Ziwa Manyara, Kitulo, Ruaha, Milima ya Mahale, Ibanda - Kyerwa, Burigi - Chato na Nyerere. Katika hatua nyine, Shirika limeendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga madaraja mawili (2) katika Hifadhi ya Taifa Tarangire na Kitulo, kukarabati kilometra 7,100 za barabara katika hifadhi za Taifa 18 na kutengeneza kiwanja cha ndege katika Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla.

**56. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Shirika limejenga ofisi pamoja na kufanya ukarabati wa Nyumba ya Kumbukizi ya Mwl. Nyerere iliyopo Magomeni, jijini Dar es Salaam. Aidha, Shirika limekarabati jengo la Kituo cha Living Stone Ujiji, Kigoma pamoja na kuweka umeme katika Kituo cha Makumbusho ya Kumbukizi ya Mtwa, Mkwawa Kalenga. Sambamba na hilo, Shirika limeboresha vionyeshwa katika vituo vya Caravan Serai - Bagamoyo pamoja na kuweka mabango elekezi katika vituo hivyo. Pamoja na hatua hiyo, Shirika limeimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kufunga mtambo pamoja na kuweka vifaa na mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa njia ya kielektroniki katika vituo vitano (5) vya malikale vya Nyumba ya Kumbukizi ya Mwl. Nyerere Magomeni, Caravan Serai - Bagamoyo, Dkt. Livingstone Ujiji - Kigoma, "Mtwa" Mkwawa Kalenga na Zana za Mawe Isimila.

**57. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika limeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba 39 katika hifadhi za Taifa kama ifuatavyo: Ruaha (20), Kisiwa cha Rubondo (4), Burigi - Chato (8), Gombe (3) na Mkomazi (4) pamoja na ofisi mbili (2) katika hifadhi za Taifa Kilimanjaro na Kisiwa cha Rubondo. Sambamba na hilo, Shirika limeanza ujenzi wa mfumo wa maji katika Hifadhi ya Taifa Ruaha. Vilevile, Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limenunua boti mbili (2) na injini mbili (2) za boti kwa ajili ya kuimarisha doria katika Hifadhi ya Taifa Nyerere. Kwa upande mwingine, Shirika limenunua magari 35 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi na uendelezaji utalii katika hifadhi za Taifa Nyerere (12), Mikumi (4), Ruaha (11) na Milima ya Udzungwa (5); na Makao Makuu (3). Pia, mitambo minne (4) ya barabara imenunuliwa kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa Ruaha.

**58. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha ulinzi Shirika limeendelea kutumia mbinu za kisasa kwa kufanya doria zinazoongozwa na taarifa za kiintelijensia pamoja na kutumia vifaa vya kielektroniki. Katika hatua hii, jumla ya siku doria 251,926 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 2,967 ambaao walichukuliwa hatua mbalimbali

za kisheria. Aidha, nyara za Serikali pamoja na silaha mbalimbali zikiwemo bunduki 69 aina ya *submachine gun*, *shortgunna rifle*- 458 na magobore zilikamatwa. Vilevile, doria maalum 44 zimefanyika katika hifadhi za Katavi (4), Ziwa Manyara (2), Serengeti (2), Burigi - Chato (4), Nyerere (6), Tarangire (8), Mto Ugalla (5), Mkomazi na Kilimanjaro (3), Mikumi (3) na Milima ya Udzungwa (3) pamoja na eneo la Loliondo (4). Jithada hizi zimewezesha kudhibiti ujangili wa tembo na faru ndani ya hifadhi za Taifa na kupunguza vikundi vya ujangili. Hatua nyingine iliyochukuliwa ni kufunga vifaa vitatu (3) vya mawasiliano ya mtandao mpana katika hifadhi za Taifa Serengeti na Mkomazi kwa ajili ya kuimarisha ufuatilaji wa faru.

#### **4.6.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania - TAWA**

**59. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka ina jukumu la kusimamia uhifadhi na kuendeleza utalii katika mapori ya akiba 22, mapori tengefu 29 na maeneo matatu (3) ya ardhioevu. Aidha, Mamlaka ni mwangalizi na mshauri wa shughuli za uhifadhi katika maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapor - WMAs, mashamba 34, bustani 30, ranchi sita (6) na Kituo kimoja (1) cha kulelea wanyamapor wenye matatizo mbalimbali.

**60. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha kuwa wananchi na mali zao wanakuwa salama dhidi ya wanyamapor wakali na waharibifu, Mamlaka imedhibiti jumla ya matukio 1,152 yaliyoripotiwa kutoka wilaya 61. Matukio hayo yalihuisha tembo, simba, mamba, chui, kiboko, fisi na nyati. Kupitia doria hizo, jumla ya wanyamapor 111 waliuawa kutokana na kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao. Mamlaka inaendelea na juhudhi za kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kuepuka na kujikinga dhidi ya wanyamapor wakali na waharibifu. Vilevile, Mamlaka imeanzisha vituo vya Askari vya kudumu kwa ajili ya kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapor wakali na waharibifu katika maeneo yenye matatizo hayo.

**61. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendeleza utalii na kuboresha mazingira ya kazi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa njia za watembea kwa miguu zenyе urefu wa mita 850 katika eneo la Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani (mita 700) na Pori la Akiba Mpanga Kipengere (mita 150). Aidha, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa barabara zenyе urefu wa kilometra 205, madaraja madogo 11 na makalavati sita (6) katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere, Swagaswaga, Mkungunero, Pande, Lukwika - Lumesule na Msanjesi. Sambamba na hilo, Mamlaka imejenga nyumba 11 za watumishi, ofisi tatu (3) na vituo vitano (5) vya askari katika mapori ya akiba ya Maswa, Mkungunero, Swagaswaga, Moyowosi, Rungwa, Pori Tengefu Ziwa Natron na Kikosi Dhidi Ujangili (KDU) katika Kanda ya Kati (Manyoni) na Serengeti (Bunda).

**62. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuboresha biashara ya uwindaji wa kitalii na kuongeza uwazi, Mamlaka imeendelea kutumia mfumo wa *MNRT Portal* kuendesha minada kwa njia ya kielektroniki ambapo vitalu vitatu (3) vya uwindaji wa kitalii vimeuzwa. Kupitia mnada huo, Mamlaka imekusanya jumla ya Dola za Kimarekani 99,000 sawa na ongezeko la asilimia 83 ya Dola za Kimarekani 54,000 ambazo zingepatikana endapo vitalu hivyo vingeuzwa kwa utaratibu wa awali wa ugawaji vitalu kupitia kamati maalum. Aidha, jumla ya leseni 36 za ufugaji wa wanyamapori zimetolewa kwa wawekezaji kwa ajili ya bustani 16, mashamba 14 na vituo sita (6). Vilevile, leseni 34 zimetolewa kwa ajili ya kuendesha biashara ya nyamapori.

**63. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori kwa kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa kufanya siku doria 99,341 na kutumia taarifa za kiintelijensia. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 1,518, meno ya tembo mazima 70 na vipande 62, nyamapori kilo 411 na bunduki 206 za aina mbalimbali zikiwemo *rifle* (5), *shot gun* (5), *submachine gun* (1), *Mark IV* (1) na gobore (194). Aidha, Mamlaka imeendelea kutumia kikosi cha mbwa wanusao katika viwanja vya ndege vya

kimataifa vya Kilimanjaro (KIA) na Julius Nyerere (JNIA) ili kudhibiti usafirishaji haramu wa nyara za Serikali. Vilevile, jumla ya watumishi 150 walipatiwa mafunzo ya Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu na kufanya jumla ya watumishi wa Mamlaka waliopatiwa mafunzo hayo kufikia 1,138 sawa na asilimia 60 ya watumishi wote wa Mamlaka.

**64. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imekamilisha mipango ya jumla ya usimamizi wa mapori ya akiba Mkungunero na Kijereshi na mipango ya kanda za usimamizi wa mapori ya akiba Swagaswaga na Mpanga Kipengere. Aidha, mipango ya usimamizi ya mapori ya akiba Selous na Pande ipo katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Mipango hii inalenga kuboresha usimamizi na matumizi ya rasillimali za maeneo hayo.

#### **4.6.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro - NCAA**

**65. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ina jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi, uendelezaji wa utalii na ustawi wa jamii zinazoishi ndani ya eneo la Hifadhi. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, Mamlaka imeimarisha miundombinu kwa kuendelea na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 4.4 ya kushuka kreta kwa kiwango cha tabaka gumu la mawe na barabara ya kutoka Golini hadi Ndutu yenye urefu wa kilometra 23 ya kiwango cha changarawe. Aidha, Mamlaka imekarabati barabara zenyе jumla ya kilometra 271 ndani ya hifadhi ikiwemo kilometra 90 zilizopo ndani ya Eneo la Kreta. Katika hatua nyingine, Mamlaka imeendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga vyoo vipyaa katika eneo la Ngoitoktok na Olduvai pamoja na kukarabati vyoo katika malango makuu ya Loduare na Endoro. Pia, mitambo mitano (5) na malori matano (5) yamenunuliwa kwa ajili ya kuongeza uwezo wa Mamlaka kuhudumia na kushughulikia miundombinu ndani ya Hifadhi. Jitihada hizi zimepunguza adha iliyokuwepo na kuboresha shughuli za utalii ndani ya eneo la Hifadhi. Vilevile, Mamlaka ipo katika hatua za awali za ujenzi wa makao makuu ya Mamlaka katika Wilaya ya Karatu.

**66. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka imeendelea kuimarisha nyanda za malisho ndani ya hifadhi kwa kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kutokomeza Mimea Vamizi (2019 - 2024) kwenye eneo la hifadhi. Katika utekelezaji wa mkakati huo, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imerejesha uoto wa asili kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 4,707 zilizoharibiwa na kupanda jumla ya miti 476,000 ndani na nje ya hifadhi. Hatua hizi zitasaidia kuongeza eneo la nyanda za malisho kwa wanyamapori ambalo limeathiriwa kwa kiasi kikubwa.

**67. *Mheshimiwa Spika*,** katika juhudi za utangazaji utalii, Mamlaka imetengeneza App maalum ijlukanayo kama *Ngorongoro Crater App* kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo ndani ya hifadhi. Sambamba na hili, Mamlaka imetengeneza video fupi 150 na *photobook* ya wanyamapori ambayo itauzwa kwa njia ya mtandao na kwenye maduka ya watalii. Aidha, kupitia programu hii jina la Hifadhi ya Ngorongoro limepata mwitikio mkubwa kwa kufuatiliwa na watu takriban bilioni 1.8 kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii ikiwemo *forums, blogs, web, news* na *videos clips*. Kupitia utaratibu wa masoko mtandao, idadi ya watu duniani wanaofuatilia vivutio vya utalii vilivyopo eneo la Ngorongoro imeongezeka kutoka 1,345,090 mwezi Juni, 2020 hadi watu 6,963,790 kufikia mwezi Aprili, 2021.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha huduma na maisha ya wananchi waishio ndani ya eneo la hifadhi na jamii inayozunguka eneo la hifadhi, Mamlaka imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya jamii. Miradi iliyotekeliza ni pamoja na ujenzi wa mtambo na uwekaji wa sola katika mradi wa maji Lemuta, ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya Kakesio, ufadhili kwa wanafunzi 1,811 kuanzia ngazi za shule ya msingi hadi chuo kikuu, utoaji wa chanjo ya kimeta kwa mifugo 270,000; chanjo ya CBPP kwa mifugo 100,000; chanjo ya PPR kwa mifugo 200,000; na chanjo ya ECF kwa ndama 8,000. Aidha, Mamlaka imenunua na kusambaza tani 900 za mahindi kwa wananchi wanaoishi katika eneo la hifadhi, kujenga choo katika Shule ya Msingi Endamagha iliyopo Wilaya ya Karatu na kuwezesha ujenzi

wa Hospitali ya Wilaya ya Karatu. Vilevile, Mamlaka imeweza ujenzi wa Kiteule cha Jeshi la Wananchi Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro na inaendelea na zoezi la uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardi kwa vijiji sita (6) vya Wilaya ya Karatu vinavyopakana na hifadhi. Pia, katika kuinua kipato cha wananchi, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine imehamasisha na kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa wafugaji 857 wanaoishi ndani na nje ya Hifadhi.

**69. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu imefanikiwa kurejesha magofu saba (7) na kuchimbua mifereji sita (6) ya umwagiliaji wa kale iliyokuwepo takriban miaka 700 iliyopita katika Magofu ya Engaruka. Aidha, Mamlaka imeboresha miundombinu katika Mapango ya Amboni, Tanga kwa kuweka taa maalum na kutengeneza njia za kutalii ndani ya mapango hayo. Vilevile, Mamlaka imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika Mkoa wa Songwe kuadhimisha Siku ya Kimondo Duniani ikiwa ni sehemu ya kukitangaza Kimondo cha Mbozi. Katika hatua nyingine, Mamlaka imefanya tathmini ya utambuzi wa sifa za kipekee katika maeneo ya Magofu ya Kale Engaruka, Nyayo za Engaresero, Makazi ya Mapango ya Mumba, Mapango ya Amboni, Kimondo cha Mbozi na maeneo jirani ili kuuza vivutio hivyo katika vifurushi vya pamoja vya zao la utalii wa malikale. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Taarifa kwa Watalii kwa ajili ya kutoa taarifa za awali za Bonde la Olduvai unaendelea katika eneo la njia panda ya kwenda Kituo cha Olduvai.

**70. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka imetenga maeneo mapya ya uwekezaji ambayo ni mahsus kwa ajili ya uwekezaji wa kimkakati. Hatua hiyo inaenda sambamba na mapitio ya Mwongozo na Utaratibu wa Uwekezaji kwa ajili ya kuboresha taratibu za uwekezaji katika eneo la Hifadhi. Aidha, Mamlaka imekamilisha Mpango wa Usimamizi wa Kanda wa Matumizi ya Ardi kwa ajili ya kutenga maeneo ya shughuli za uwekezaji ndani ya hifadhi. Lengo la jitihada hizo, ni kuongeza wigo wa uwekezaji kwenye huduma za malazi na

miundombinu mingine ya shughuli za utalii na hivyo kuongeza mapato na fursa za ajira kwa wananchi.

**71. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka imefanya jumla ya siku doria 26,490 zilizowezesha kukamatwa kwa wahalifu 61 wa makosa mbalimbali. Aidha, Mamlaka imeimarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ujangili, ufuatiliaji wa kila siku wa mtawanyiko wa tembo, faru na wanyama wengine walio hatarini kutoweke kwa kuwawekea vifaa maalum vya kufuatilia mienendo yao. Vilevile, Mamlaka imebaini na kupambana na mitandao ya ujangili katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Hifadhi.

**72. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma, Mamlaka imeanzisha Ofisi ndogo katika Jiji la Dodoma. Pamoja na kazi nyingine, ofisi hiyo itatoa huduma kwa wadau mbalimbali wa Mikoa ya Kanda ya Kati kuhusu shughuli za Mamlaka na Uhifadhi. Katika hatua nyingine, Mamlaka imeboresha vituo vya Kimondo na Mapango ya Amboni kwa kupeleka watumishi, magari na kuweka miundombinu ya TEHAMA. Aidha, Mamlaka imeboresha miundombinu ya TEHAMA katika vituo vya Loduare, Ndutu, Naabi, Olduvai Gorge na Nasera Rock na vituo vidogo vya Endamagha, Kakesio na Seneto. Lengo la hatua hii ni kurahisisha utoaji wa huduma hususan kwa watalii katika vituo mbalimbali vya malipo. Pamoja na hatua hizo, Mamlaka imeendesha mafunzo ya huduma na ukarimu kwa wageni kwa watumishi 340 ili kuboresha huduma.

#### **4.6.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor - TAWIRI**

**73. *Mheshimiwa Spika*,** Taasisi ina jukumu la kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapor nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, zoezi la kuidadi wanyamapor limefanyika katika Mfumo Ikolojia Serengeti; hifadhi za Taifa Burigi - Chato na Kigosi; na Pori la Akiba Moyowosi ili kupata takwimu na kufahamu mwenendo wa wanyamapor. Matokeo ya zoezi hilo yanaonesha kwa sasa kuna idadi ya tembo 7,061, nyati 69,075 na twiga 6,680 katika Mfumo Ikolojia wa Serengeti; na

pundamilia 182, pofu 209 na swala pala 251 katika Hifadhi ya Taifa ya Burigi - Chato. Kulingana na matokeo hayo, takwimu zinaonesha kuwa katika Hifadhi ya Taifa Burigi - Chato pundamilia wameongezeka kwa asilimia 22, swala pala kwa asilimia 23 na uwepo wa pofu ambaao hawakuonekana katika sensa iliyofanyika mwaka 2014. Katika Mfumo Ikolojia wa Moyowosi - Kigosi, jumla ya spishi 26 za wanyamapori zilihesabiwa ambapo wanyamapor aina ya nyati 1,712, twiga 749, palahala 647, pundamilia 564, kongoni 535, pofu 169 na tembo 115 walionekana. Matokeo haya yanaonesha ongezeko la idadi na mtawanyiko wa wanyamapor ukilinganisha na sensa iliyofanyika mwaka 2014. Spishi zilizoongezeka ni pamoja na nyati asilimia 35, twiga asilimia 92 na spishi tatu (3) ambazo ni palahala, pofu na kongoni zilizoongezeka kwa zaidi ya asilimia 100.

**74. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimairisha afya za wanyamapor, Taasisi imeendelea kufuatilia afya za wanyamapor kwa kutoa tiba kwa takriban wanyamapor 36 katika mifumo ikolojia wakiwemo faru 8 (Mkomazi, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Ikorongo), tembo 7 (West Kilimanjaro), watoto wawili (2) wa tembo (Maswa na Manyoni), pofu 17 (West Kilimanjaro) na watoto wawili (2) wa faru katika Mfumo Ikolojia wa Serengeti na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Idadi kubwa ya wanyamapor wallotibiwa ni kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoathiri ustawi na afya za wanyamapor. Wizara inaendelea kuhimiza Jamii kutoa ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za wanyamapor.

**75. *Mheshimiwa Spika*,** katika hatua nyingine, Taasisi imefanya utafiti wa ugonjwa unaoathiri twiga (Giraffe Skin Disease - GSD) katika hifadhi za Taifa za Tarangire, Serengeti na Ruaha. Matokeo ya awali ya uchunguzi wa kimaabara yanaonesha kuwa ugonjwa wa twiga umesababishwa na bakteria na fangasi ambaao husambazwa na ndege aina ya *Oxpeckers* wanaokula kupe. Vilevile, minyoo waitwao *Thelazia spp* wameweza kupatikana maeneo ya mwili yaliyoathirika. Hata hivyo, uchunguzi wa kimaabara unaendelea ili kupata tiba na kuendelea kudhibiti maambukizi zaidi ya ugonjwa huo.

**76. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imefanya uchunguzi wa sababu ya vifo nya viumbe hai mbalimbali wakiwemo faru na tembo (Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Mkomazi), viboko (Mto Koga) na ndege maji na samaki (Ziwa Natron). Matokeo ya awali yanaonesha kuwa wanyamapor i wakubwa walikufa kwa kula mazao ambayo yalikuwa yamenyenyiziwa viuatilifu ambavyo ni sumu kwa wanyamapor i. Aidha, vifo nya ndegemaji na samaki ni matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi. Matokeo hayo yanaonesha kuwa uwepo wa shughuli za kibinadamu katika ukanda unaotenga hifadhi na maeneo ya jamii (buffer zones) unatishia maisha ya wanyamapor i, hivyo ni muhimu kuzingatia sheria za uhifadhi.

**77. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imefunga mikanda ya mawasiliano kwa wanyamapor i makundi 114 ikiwemo tembo 22 (Mfumo Ikolojia Serengeti, Ziwa Natron na Tarangire - Manyara), mbwa mwitu 7 (Ikolojia ya Serengeti), simba 17 (Ikolojia za Serengeti na Ruaha-Rungwa), faru 17 (Mfumo Ikolojia wa Serengeti), twiga 14 (Ikolojia za Tarangire na Serengeti), nyumbu 10 (Ikolojia za Tarangire na Serengeti) na tumbusi 7 (Mfumo ikolojia wa Serengeti). Zoezi hili linalenga kuaishaa mienendo ya wanyamapor i katika vipindi mbalimbali na maeneo yenye migogoro (conflict hotspots) pamoja na kupendekeza njia sahihi za kutatua migogoro hiyo. Sambamba na hilo, Taasisi imekamata na kuhamisha wanyamapor i kwa ajili ya kuendeleza na kuanzisha mashamba ya wanyamapor i yanayomilikiwa na Serikali na watu binafsi. Katika zoezi hili, zaidi ya wanyamapor i na ndege 700 walihamishwa kutoka kwenye maeneo ya wazi kwenda kwenye bustani mbalimbali za wanyamapor i nchini.

#### **4.6.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapor i - CAWM Mweka**

**78. Mheshimiwa Spika,** Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo katika ngazi za Cheti cha Msingi, Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kinafanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uhifadhi wa wanyamapor i na uendeshaji utalii. Katika kutekeleza hili, mwaka 2020/2021 Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 929

katika ngazi za Cheti cha Msingi, Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya uhifadhi na uongozaji utalii kwa jumla ya washiriki 480. Vilevile, jumla ya wahitimu 388 katika ngazi ya Cheti, Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili wametunukiwa vyeti.

**79. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo kimekamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200. Aidha, Chuo kinaendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 294. Katika hatua nyingine, Chuo kimekarabati majengo ya utawala, zahanati, mgahawa, madarasa manne (4), hosteli mbili (2) na barabara za ndani. Vilevile, Chuo kimeboresha miundombinu katika eneo la mafunzo kwa vitendo liliopo Kwakuchinja wilayani Babati kwa kuweka umeme katika nyumba tatu (3) za watumishi na kambi ya mafunzo; na kuchimba kisima cha maji na kujenga vyoo vya kisasa. Pia, magari makubwa mawili (2) yamenunuliwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Sambamba na hilo, Chuo kimeweka alama za mipaka (beacons) kwenye eneo jipya la mafunzo kwa vitendo lilioko katika Kijiji cha Arashi, Loliondo lenye ukubwa wa ekari 394.

#### **4.6.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapor Pasiansi**

**80. *Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapor Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapor na himasheria katika ngazi ya Astashahada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imedahili wanafunzi 343 katika fani za uhifadhi wanyamapor na himasheria, uongozaji watalii na usalama kwa ngazi ya Astashahada. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya utayari wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapor na Misitu kwa watumishi 741 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania. Katika hatua nyingine, Taasisi ilioa mafunzo ya muda mfupi kwa jumla ya vijana 111 wanaoshughulika na uhifadhi wa maliasili hususan, misitu na wanyamapor kutoka wilaya sita (6) za Mpanda,

Tanganyika, Uvinza, Kigoma, Simanjiro na Karatu. Villevile, Taasisi imeandaa mitaala miwili (2) kuhusu uongozaji wa watalii na usalama katika ngazi ya Astashahada na kuboresha mitaala ya usimamizi wa wanyamapori na himasheria. Pia, Taasisi inaendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maktaba.

#### **4.6.1.9 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu- Sekamaganga**

**81. *Mheshimiwa Spika*,** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga kina jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa ili kushiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kituo kimepata usajili wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundis wenyewe Na. REG/SAT/046 ili kutoa mafunzo ya waongoza watalii. Hatua hii imefanikisha kuanzishwa kwa kozi mpya ya Astashahada ya Awali ya Waongoza Watalii ambapo wanafunzi 11 wamedahiliwa. Aidha, Kituo kimetoa mafunzo ya usimamizi wa rasilimasili za maliasili kwa askari wa wanyamapori 151 wa vijiji katika Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mbarang'andu, Kisungule na Kimbanda (Namtumbo); na Nalika na Chingoli (Tunduru) pamoja na maeneo ya misitu ya Serikali ya Vilima vya Mlele; na Misitu ya Jamii ya Ushoroba wa Rungwa (Sikonge) na Enguserosambu (Loliondo). Villevile, Kituo kimetengeneza tovuti yenye anuani [www.cbctlikuyu.ac.tz](http://www.cbctlikuyu.ac.tz) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za Kituo. Pia, Kituo kimejenga bwalo na jiko na kununua vifaa vya mafunzo kwa ajili ya kufundishia.

#### **4.6.1.10 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF**

**82. *Mheshimiwa Spika*,** Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umewezesha kufanyika kwa operesheni maalum za kuzuia ujangili kupitia Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kuzuia Ujangili; kuhakiki na kulipa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali

na waharibifu; na kuwezesha kazi za utafiti na kuidadi wanyamapori. Aidha, Mfuko umewezesha utatuzi wa migogoro kati ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa; upandishwaji hadhi wa maeneo yaliyohifadhiwa; na mapitio ya sheria na kanuni za usimamizi wa uhifadhi wa wanyamapori. Vilevile, Mfuko umewezesha kujenga uwezo wa watumishi; na uratibu na ufuutiliaji wa utekelezaji wa Sera ya wanyamapori.

#### **4.6.2 Sekta ya Misitu na Nyuki**

**83. *Mheshimiwa Spika*,** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, utekelezaji wa shughulimbalimbali katika sekta hiyo unasimamiwa na Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224 na Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sura 270. Vilevile, uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi (FITI), Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora (BTI) na Mfuko wa Misitu (TaFF).

##### **4.6.2.1 Masuala Mahsusni ya Sekta ya Misitu na Nyuki**

###### **(i) Uongezaji Thamani Mazao ya Misitu na Nyuki**

**84. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha kuwa mazao ya misitu na nyuki yanayozalishwa hapa nchini yanaongezwa thamani, Wizara imeendelea kutoa elimu, kuhamasisha na kuwezesha wadau mbalimbali kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu na nyuki. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeandaa mipango 37 ya uvunaji wa mazao ya misitu katika misitu ya vijiji na matajiwazi katika wilaya za Handeni, Kilindi, Liwale, Ruangwa, Nachingwea, Namtumbo, Songea, Mbinga, Nyasa, Kilwa,

Lindi, Masasi, Nanyumbu na Tunduru. Pia, Wizara imenunua mashine mbili (2) za kisasa za kuchakata magogo ili kuongeza thamani ya mazao ya misitu katika wilaya za Ruangwa, Liwale, Tunduru, Namtumbo na Songea. Uimarishaji wa Shughuli za Utalii Ikolojia katika Hifadhi za Misitu

**85. *Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha shughuli za utalii ikolojia, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu katika hifadhi za misitu na nyuki. Miundombinu iliyoboreshwa ni pamoja na ukarabati wa njia za asili za watalii zenyе urefu wa kilometra 73.3, barabara zenyе urefu wa kilometra 128.8 na ujenzi wa maeneo mawili (2) ya kuweka mahema ya muda ya kitalii katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia ya Mlima Rungwe, Amani, Magamba na Kilombero. Aidha, Wizara imejenga lango moja (1), vyoo vitano (5) na banchi 10 katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia za Magamba, Kilombero na Mlima Rungwe. Vilevile, Kanuni za Uwekezaji wa Utalii kwenye maeneo ya hifadhi ya misitu zimeandalila na kutangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 85 la mwaka 2020. Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuwekeza katika shughuli za utalii ikolojia. Juhudi hizo zitaongeza idadi ya watalii, ajira kwa wananchi na mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Taifa.

**(ii) Kupandisha Hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania Kuwa Mamlaka**

**86. *Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali, kuimarisha upatikanaji endelevu wa mazao na huduma katika sekta ya misitu na nyuki pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Wizara imeanza taratibu za kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu kuwa Mamlaka. Ili kufikia azma hiyo, Wizara imekamilisha maandalizi ya nyaraka muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lengo ni kujenga uelewa wa pamoja na wadau hao na hatimaye kuwasilisha mapendekezo kwa ajili ya kufanya maamuzi kuitia ngazi mbalimbali ikiwemo ya Baraza la Mawaziri.

(iii) Tozo za Huduma na Mazao ya Misitu

**87. Mheshimiwa Spika**, tozo za mazao na huduma za Misitu zinasimamiwa kwa mujibu wa Kanuni ya Misitu iliyotolewa katika Gazeti la Serikali Na. 627 la mwaka 2020. Tozo hizi husimamiwa kwa kuzingatia Sheria ya Misitu Sura 323. Katika utekelezaji wa kanuni hizo, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu malipo ya tozo kulingana na thamani ya mazao na huduma itolewayo. Kufuatia malalamiko hayo, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kufanya mapitio ya kanuni hizo ili wananchi waendelee kunufaika kibiasara na mazao na huduma za misitu na Serikali kupata mapato yake.

**4.6.2.2 Idara ya Misitu na Nyuki**

**88. Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya tathmini na mapitio ya miongozo ya sera za sekta za misitu na nyuki na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa sera hizo. Aidha, Wizara imeandaa kanuni za: Uendeshaji wa Tafiti za misitu kwa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania kwa Tangazo la Serikali Na. 684 la mwaka 2020; Tozo ya Mazao na Huduma za Misitu kwa Tangazo la Serikali Na. 627 la mwaka 2020; na Kanuni za Mfuko wa Misitu za Kusimamia Utoaji wa Ruzuku kwa Tangazo la Serikali Na. 266 la mwaka 2021. Vilevile, Wizara imeandaa miongozo minne (4) ya: Kusimamia Shughuli za Uendeshaji wa Mashamba ya Miti wa mwaka 2021; Mafunzo na Huduma za Ugani za Ufugaji Nyuki wa mwaka 2020; Uanzishaji na Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki na Manzuki wa mwaka 2021; Taratibu za Utoaji Mafunzo na Huduma za Ugani katika Ufugaji Nyuki za mwaka 2021; na Matumizi ya Miti ya Misaji na Miti Mingine wa mwaka 2021 (Mwongozo huu pamoja na mambo mengine unasisitiza matumizi ya miti ambayo haikuwa imepewa kipaumbele katika utengenezaji wa samani kama vile misaji na miti mingine). Miongozo hii itaimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya misitu na nyuki na kuongeza tija pamoja na mapato ya Serikali.

**89. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya misitu na nyuki, Wizara iliratibu mikutano miwili

(2) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu - NAFAC na mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki - NABAC. Pamoja na mambo mengine, kamati hizo zilitoa maoni na ushauri kuhusu namna bora ya kusimamia na kuendeleza sekta ya misitu na nyuki. Aidha, Wizara ilifanya mkutano na viongozi wa vyama vya ushirika wa wafugaji nyuki uliofanyika Jijini Dodoma, mwezi Juni, 2020 kwa lengo la kujadili changamoto zinazokabili vyama hivyo. Vilevile, Wizara imeanza kufanya mapitio ya mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Taifa.

#### **4.6.2.3 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS**

**90. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala una jukumu la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki. Wakala unasi mamia jumla ya misitu 463 iliyohifadhiwa kisheria. Misitu hili inajumuisha mashamba ya miti 23, misitu ya mazingira asilia 20, hifadhi za nyuki 12 na misitu ya hifadhi 408. Aidha, Wakala umeendelea kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali zikiwemo Serikali za Mitaa kwa ajili ya kusimamia misitu.

**91. *Mheshimiwa Spika*,** katika juhudii za kudhibiti uvunaji na biashara haramu ya mazao ya misitu, Wakala umeimarisha shughuli za ukaguzi wa mazao ya misitu na nyuki kwa kufanya siku doria 3,529 katika misitu yote ambayo ipo chini yake. Doria hizo zimevezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 904 na mazao mbalimbali ya misitu yakiwemo magunia ya mkaa 33,876; mbao zenye mita za ujazo 1,906; nguzo 4,699; magogo yenye mita za ujazo 909; pamoja na fremu za milango na madirisha 1,195. Aidha, katika kuhakikisha usimamizi endelevu wa misitu, Wakala umeandaa mipango mipyaa ya usimamizi wa misitu 11 yenye jumla ya hekta 243,508 katika wilaya za Rufiji, Biharamulo, Muleba, Kahama, Bukoba, Misenyi, Geita na Kilwa.

**92. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala umeendelea kutekeleza na kuwezesha shughuli za upandaji miti katika mashamba ya Serikali, maeneo ya watu binafsi na taasisi mbalimbali. Katika hatua hiyo, Wakala umefanikiwa kuzalisha tani 7.78 za mbegu bora za miti, kuotesha miche 32,331,910 na vipando 52,790

vya mikoko. Miche na vipando hivyo vimeoteshwa katika mashamba ya miti ya Serikali na misitu ya mikoko katika eneo lenye ukubwa wa hekta 7,203.31. Aidha, miche mingine imegawiwa na kupandwa katika maeneo ya taasisi, vikundi vya kijamii na watu binafsi. Wakala pia umeotesha miche 6,250 ya miti ya asili katika hifadhi 84 za misitu, kupalilia hekta 17,997 na kupogoa hekta 6,461 za mashamba ya miti. Vilevile, Wakala umeimarisha mipaka ya misitu kwa kuhakiki kilometa 97, kusafisha kilometa 1,219, kuweka vizingi 595 na kuweka mabango 180 katika misitu mbalimbali.

**93. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kukabiliana na moto kichaa, Wakala umesafisha njia za kudhibiti moto kwenye misitu ya asili na mashamba ya miti yenye urefu wa kilometa 2,433; kujenga minara miwili (2) na kukarabati minara 17 ya kufuatilia matukio ya moto. Aidha, Wakala umeandaa mipango milne (4) ya usimamizi wa moto katika Wilaya ya Ludewa na kujenga uwezo kwa vikosi 15 vya zima moto vyenye jumla ya watu 282.

**94. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhamasisha ushiriki wa jamii kwenye shughuli za uhifadhi, Wakala umejenga mabweni mawili (2) katika shule mbili (2) za sekondari katika Wilaya ya Mufindi; na kugawa madawati 176 katika shule tatu (3) za msingi katika wilaya za Kondo na Mvomero. Vilevile, vifaa vya ujenzi kama vile saruji, mbao, nguzo, milango na madawati vyenye thamani ya Shilingi 172,434,399 viligawiwa kwa jamii katika wilaya za Lindi, Ilaje, Nyasa, Songea, Kaliua, Nkasi, Chunya, Nanyumbu, Kilwa, Kondo, Kisarawe, Kibiti, Kilombero, Mkuranga, Kilosa, Mbinga na Masasi.

**95. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhakikisha upatikaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya uchakataji wa mazao ya nyuki na kujenga uwezo wa jamii zinazojihusisha na Ufugaji nyuki, Wakala umeendelea kuhudumia manzuki 181 ambazo zimeweza kuzalisha tani 12.9 za asali na kilo 601.86 za nta. Aidha, Wakala umeanzisha vikundi vipyta 54 vya ufugaji nyuki na kutoa elimu ya ufugaji bora wa nyuki kwa wafugaji 1,751 ili kuwawezesha kujiongezea kipato. Vilevile, katika jitihada za kuwashakikisha Watanzania upatikanaji wa soko la mazao

ya nyuki nje ya nchi, Wakala ulikusanya sampuli 80 za asali kutoka wilaya 30 na kuzipeleka kwenye maabara ya kimataifa nchini Ujerumanî kwa ajili ya kupimwa ubora ambapo majibu yalionesha kuwa asali kutoka Tanzania ilikidhi viwango vya ubora unaotakiwa katika nchi za Ulaya kwa asilimia 90. Pia, Wakala umetoa vifaa vya ufugaji nyuki ikiwemo mizinga 695 katika wilaya za Bukoba (200), Gairo (250), Chato (50), Lindi (10), Lushoto (10), Ludewa (30), Hanang (100) na Kilolo (45).

**96. *Mheshimiwa Spika***, Wakala umeendelea kuboresha ustawî wa watumishi kwa kuweka mazingira wezesi ya kufanya kazi katika maeneo ya misitu na malikale. Katika kutekeleza hilo, Wakala umekarabati nyumba 22 na mifumo saba (7) ya maji katika mashamba ya miti tisa (9) ya Buhindi, Kiwira, Longuza, Mtibwa, North Kilimanjaro, Ruvu Kaskazini, Rondo, Ukaguru na Sao Hill. Aidha, ujenzi wa nyumba 29 za watumishi na majengo 15 ya ofisi unaendelea katika Kanda sita (6) ambazo ni: Nyanda za Juu Kusini, Magharibi, Kaskazini, Mashariki, Kusini na Kanda ya Ziwa. Vilevile, ujenzi wa vituo vitatu (3) vya ulinzi umeanza katika hifadhi tatu (3) za misitu za wilaya za Kasulu, Sikonge na Mlele.

#### **4.6.2.4 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI**

**97. *Mheshimiwa Spika***, Taasisi ina jukumu la kufanya na kuratibu utafiti wa misitu na ufugaji nyuki na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki nchini. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imefanya utafiti ili kubaini ubora na thamani halisi ya spishi saba (7) za miti ya mbao. Utafiti huo ulihusisha spishi za miti ya mkuruti (*Baphia kirki*), mgonga chuma (*Ambiygonorcarpus andogensis*), mgama (*Manilkara mochisa*), mbebeti (*Diallium holtzii*), mnangu mweusi (*Guibourtia schliebenii*), mtunda (*Manilkara sensibarensis*) na mnake mweusi (*Xylopia parviflora*) katika misitu ya asili iliyopo Kibiti, mkoani Pwani. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mbao za miti hiyo zina viwango vya ubora kwa matumizi ya ujenzi wa madaraja, nyumba, boti na kutengeneza samani. Miti hii itapunguza utegemezi wa

matumizi ya mbao zilizozoleka za miti ya mninga na mkongo na kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Taifa.

**98. *Mheshimiwa Spika*,** Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine imeendelea kufanya utafiti juu ya uvunaji wa utomvu kwenye miti ya misindano ili kubaini umri sahihi wa kuvuna utomvu, madhara yake kwenye ukuaji wa miti na ubora wa mbao. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa mti mmoja (1) wa msindano wenyе umri wa kuanzia miaka mitano (5) unaweza kutoa utomvu wenyе uzito wa kilogramu kati ya 0.5 na 1.98 kwa mwezi. Aidha, imebainika kuwa uvunaji wa utomvu hauna madhara kwenye ubora wa mbao ya miti iliyofikia umri wa kuvunwa. Hivyo, uvunaji wa utomvu ambaو una soko kubwa nje ya nchi hususan, China ni fursa nyingine katika kuongeza wigo wa mazao ya misitu na hivyo kuongeza Pato la Taifa.

**99. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuwezesha uhifadhi na uendelezaji wa miti ya asili inayotumika kwa tiba asilia, Taasisi imefanya utafiti wa miti inayotumika kama dawa na ilio hatarini kutoweka kwa lengo la kuitambua na kuihifadhi. Kufuatia utafiti huo, miti ya aina ya nengonengo (*Securidaca longipenduculata*), mlungulungu (*Zanthoxylum chalybeum*) na mzima (*Terminalia sericea*) imebainika kutumiwa na wenyеji kama dawa asilia kwa magonjwa mbalimbali ya binadamu. Kufuatia utafiti huu, Taasisi imeanza mkakati wa kuhifadhi miti hiyo kwa utafiti zaidi na kuhakikisha uendelevu wake. Kwa upande mwengine, ili kupunguza kasi ya matumizi ya nishati ya mkaa na kuni, Taasisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu ya matumizi ya nishati mbadala ikiwemo majiko ya umeme (*electric pressure cooker*) yanayotumia nishati kidogo ya umeme kupikia katika Manispaa ya Morogoro. Taasisi itaendelea kuhamasisha jamii katika maeneo mengine kuhusu matumizi ya nishati mbadala hasa katika maeneo ya miji.

**100. *Mheshimiwa Spika*,** Taasisi imefanya Kongamano la Kimataifa la Kisayansi Kuhusu Kuboresha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu na Nyuki kwa maendeleo endelevu, uchumi wa viwanda na kukuza Pato la Taifa.

Kongamano hilo lilifanyika mwezi Februari, 2021 Jijini Dar es Salaam na lililenga kutoa matokeo ya tafiti na fursa kwa wadau kutoka sehemu mbalimbali duniani kwa kujadili usimamizi na uendelezaji wa sekta ya misitu na nyuki. Aidha, jumla ya wadau 197 walishiriki kongamano hilo kutoka ndani na nje ya nchi zikiwemo nchi za Kenya, Ethiopia, Afrika Kusini, Nigeria na Ufini na wengine walishiriki kwa njia ya mtandao. Vilevile, jumla ya maandiko 30 ya kisayansi na mada chokozi saba (7) ziliwasilishwa; na maonesho ya bidhaa mbalimbali za Misitu na nyuki yalifanyika. Vilevile, Mpango Kamambe wa Taifa wa Utafiti wa Misitu wa Tatu (2021 - 2031) na Mpango Kamambe wa Taifa wa Utafiti wa Nyuki wa Kwanza (2021 - 2030) ulizinduliwa rasmi.

#### **4.6.2.5 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**101. *Mheshimiwa Spika***, Vyuo vya taaluma ya misitu na ufugaji nyuki vinajumuisha Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - BTI. Vyuo hivyo vimepewa jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wanafunzi 867 na kuboresha miundombinu kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala. Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wanafunzi 224 na kimekarabati madarasa matatu (3), geti moja (1) na kujenga kingo za barabara za ndani ya Chuo. Vilevile, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 408 na kinaendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga jengo la kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki pamoja na ukarabati wa jengo la utawala.

#### **4.6.2.6 Mfuko wa Misitu Tanzania - TaFF**

**102. *Mheshimiwa Spika***, Mfuko una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mfuko umeghamaria ujenzi wa majengo ya viwanda vitatu (3) na ukarabati wa majengo ya viwanda viwili (2) vya kuchakata

na kufungasha mazao ya nyuki katika Halmashauri za wilaya za Sikonge, Bukombe, Mlele, Kibondo na Nzega. Aidha, Mfuko umetoa ruzuku kwa jumla ya miradi 71 kwa ajili ya kuboresha uhifadhi wa misitu kupitia upandaji miti na ufugaji nyuki ambapo miradi 58 inaendelea na miradi 13 ni mipya.

**103. *Mheshimiwa Spika*,** kazi nyingine zilizoteklezwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa ajili ya kuanzisha vitalu vya miti na upandaji miti katika shule 60 za mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Shinyanga, Dodoma, Singida na Simiyu. Aidha, Mfuko umegharamia mafunzo ya wanafunzi 20 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada ya fani za misitu, viwanda vya misitu na ufugaji nyuki. Kwa upande mwingine, Mfuko umewezesha kufanya mapitio ya mchango halisi wa sekta ya Misitu katika Pato la Taifa, kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kuchapisha matokeo ya utafiti wa misitu na nyuki na utoaji wa vibali vya kufanya utafiti wa misitu na kuboresha miundombinu ya kufundishia ya vyuo vya misitu na nyuki. Aidha, Mfuko pia umewezesha kamati za ushauri wa masuala ya misitu (NAFAC) na nyuki (NABAC) kutekeleza majukumu yake.

#### **4.6.3 Sekta ya Utalii**

**104. *Mheshimiwa Spika*,** Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii nchini. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999; na kusimamiwa na Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura 364. Vilevile, jukumu hilo hutekelezwa kupitia Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT).

##### **4.6.3.1 Masuala Mahsusni katika Sekta ya Utalii**

###### **(i) Uendelezaji wa Mazao ya Utalii ya Kimkakati**

**105. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea na jitihada za kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati nchini ambayo ni utalii wa mikutano na matukio, fukwe, meli, michezo na utamaduni. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeainisha maeneo ya

fukwe yanayofaa kwa ajili ya shughuli za utalii katika Manispaa ya Kigamboni na Kisiwa cha Mafia ili kuvutia uwekezaji wa utalii. Aidha, rasimu ya Hati ya Makubaliano - MoU baina ya Wizara na Wizara ya Viwanda na Biashara kuititia Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji - EPZA imeandaliwa ili kuwezesha maeneo yaliyoainishwa kutangazwa kimkakati kuwa Kanda Maalum za Kiuchumi za Uendelezaji Utalii.

**106. *Mheshimiwa Spika*,** sambamba na hilo, Wizara imepata eneo lenye ekari 22.4 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Dar es Salaam kwa ajili ya uwekezaji ambalo litaendelezwa kuititia Mradi wa Utalii wa Mikutano na Matukio - MICE. Pia, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Utalii wa Meli katika Bandari ya Dar es Salaam. Juhudi hizo zitaongeza mchango wa sekta ya utalii kuititia ongezeko la idadi ya watalii na ukusanyaji mapato. Pamoja na jitihada hizo, Wizara pia imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza na kukuza utalii kuititia matukio ya michezo na utamaduni. Kwa ujumla, matukio hayo yamekuwa yakitoa fursa ya kutangaza vivutio vya utalii katika maeneo ya malikale, wanyamapori, misitu na nyuki na hivyo kuwa chachu ya kuhamasisha makundi mbalimbali ya kijamii kushiriki katika utalii wa ndani.

#### **(ii) Kuhamasisha Utalii wa Ndani**

**107. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuhamasisha utalii wa ndani, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuanzisha na kuendesha programu na kampeni mbalimbali. Programu na kampeni hizo ni pamoja na *Bungeni na Utalii wa Ndani*, *Visit Tanzania*, *Twenzetu Katalii*, *Twenzetu Kinature*, *Twenzetu Makumbusho*, *Maliza Mwaka na Utalii wa Ndani*, *Mtaa kwa Mtaa na TANAPA*, *Valentine Mbugani - Tukutane Hifadhini Tu*, *Msimu wa Nyumbu Kuzaa*, *Siku ya Utalii Duniani*, *Wanawake na Utalii*, *CRDB Mbugani*, *NMB Mbugani*, *Museum Art Explosion*, *Dar es Salaam City Tour*, *Museum Univesity Hub*, *Ngorongoro Talent Challenge*, *Editors Forum* na *Sherehekeea Sikukuu ya Wafanyakazi Mbugani*. Kuititia kampeni hizo, wananchi wamehamasika kutembelea hifadhi, maeneo ya

malikale na makumbusho. Kwa upande mwagine, Wizara imeendelea kuendesha mashindano ya *Ngorongoro Talent Challenge Competition* yanayolenga kuibua vipaji na uhamasishaji utalii wa ndani, hususan kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini. Utekelezaji huo pia unahusisha uratibu wa mihadhara ya utalii na kuhamasisha utalii kwa wanafunzi wa shule za sekondari za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani (kupitia mashindano ya Uwezo Awards) na vyuo vikuu katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha ikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Shule ya Biashara). Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za malazi za bei nafuu katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuchochea utalii wa ndani.

#### **4.6.3.2 Idara ya Utalii**

**108. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini na mapitio ya miongozo ya sera ya utalii na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo. Aidha, Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 ambapo Muswada wa marekebisho ya Sheria hiyo umesomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Pili (2) wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uliofanyika mwezi Februari, 2021. Katika hatua nyingine, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imebaini vivutio 51 vya utalii vilivyopo katika mikoa ya Geita, Kagera na Mwanza. Vivutio hivyo ni pamoja na maeneo ya fukwe, wanyamapori na uoto asilia, urithi wa kiutamaduni, sanaa na kazi za mikono za aina mbalimbali ambazo ni fursa katika kukuza utalii.

**109. *Mheshimiwa Spika***, katika kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato, Wizara imeendelea kuhakiki na kuhuisha orodha ya huduma za malazi zinazopaswa kulipa Tozo ya Kitanda Siku. Kazi hii imefanyika katika mikoa 19 na kuwezesha ongezeko la huduma za malazi kutoka 1,238 mwaka 2015 hadi 1,815 mwaka 2020. Aidha, mafunzo ya kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa *MNRT Portal* yametolewa kwa watoa huduma za malazi ili kuwawezesha kusajili wageni kidijitali. Mafunzo hayo yamefanyika katika mikoa saba (7) ambapo jumla wadau 507 walishiriki. Katika hatua nyingine, Wizara

inaendelea na uhakiki wa huduma za malazi katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Iringa, Tanga, Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Mara na Pwani. Vilevile, Wizara imesajili wakala wa biashara za utalii wapya 55 na hivyo kufanya idadi yao kufikia wakala 2,210. Katika hatua nyingine, kaguzi za wakala wa biashara za utalii zimefanyika katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Manyara, Morogoro, Mara, Iringa, Njombe na Arusha ili kubaini wakala wanaofanya biashara kinyume na sheria.

#### **4.6.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania - TTB**

**110. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi ina jukumu la kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi imehuisha mikakati ya utangazaji utalii wa ndani na wa kimataifa na mwongozo wa kuteua na kusimamia mabalozi wa hiari wa utalii ili kuleta ufanisi katika utangazaji utalii. Aidha, Bodi iliratibu ziara za mafunzo ya wanahabari na wakala wakubwa wa utalii wa kimataifa walitembelea maeneo ya vivutio vya utalii nchini kwa lengo la kuvifahamu na kuvitangaza katika nchi wanazotoka. Waandishi na wakala hao walitoka kwenye masoko mbalimbali yakiwemo Urusi, Israel, Uhispania, Jamhuri ya Czech, Ufaransa, Uswidi, Marekani, Japan, ukanda wa Afrika na Falme za Kiarabu. Katika hatua nyingine, Bodi iliandaa video mbalimbali za kutangaza utalii na kuzisambaza kupitia mitandao ya kijamii ambapo jumla ya watu 8,791,000 walifuatilia.

**111. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi imeendelea kutumia watu maarufu na mabalozi wa hiari wa utalii na ofisi za balozi zetu katika nchi mbalimbali kutangaza na kuhamasisha watalii kutembelea Tanzania. Aidha, Bodi imefanya vikao katika kanda sita (6) za kimkakati na Balozi 36 za Tanzania katika nchi mbalimbali duniani kwa njia ya mtandao kwa lengo la kueleza utayari wa Tanzania katika kupokea wageni wakati wa mlipuko wa ugonjwa COVID -19. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na balozi hizo imefanya vikao na wakala wa utalii katika nchi 11. Pia, Bodi imeshiriki katika makongamano ya utangazaji utalii kwa njia ya mtandao kama vile *Travel Turkey Izmirla* nchi ya Uturuki, *Tanzania - Nigeria Tourism, Investment*

and Trade Forum la nchi ya Nigeria na *Travel with Sense of Africa through Eastern Africa* liliolandaliwa na Kampuni ya Sense of Africa. Kutokana na juhudhi hizo, nchi imeendelea kupokea makundi ya watalii kutoka nchi za Urosi, Marekani, Uingereza, Ujerumanu, Ufaransa, Italia, Uswisi, Poland, Israel, Japan, Uchina, Uhispania, Jamhuri ya Czech, India, Uholanzi, Uturuki, Ukraine, Ubelgiji, Uswidi, Oman, Australia na watalii kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

**112. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi imeendelea kuhamasisha matumizi ya utambulisho mpya wa utalii wa nchi yetu *Tanzania, Unforgettable!* na kutangaza utalii kuititia matukio mbalimbali kama vile Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Kilimo (Nanenane), Maonesho ya Afrika Mashariki, Msafara wa waendesha Baiskeli kumuenzi Baba wa Taifa - *Twende Butiama, Ushoroba festival, Tamasha la Sauti za Busara, Kili Marathon, Rock City Marathon, Serengeti Marathon* na maonesho ya sarakasi ya *Mama Africa*. Kwa upande mwingine, Bodi iliandaan kampeni mbalimbali za kuhamasisha utalii wa ndani. Pia, katika kuhamasisha wanafunzi kutembelea maeneo ya vivutio, Bodi ilifanya mihadhara katika shule na vyuo vya elimu ya katina ya juu katika mikoa ya Arusha, Iringa, Dar es Salaam na Mwanza. Sambamba na hilo, Bodiimeanzisha Kitengo Maalum cha Mikutano na Matukio chini ya Kurugenzi ya Masoko kwa ajili ya kuratibu na kuitangaza Tanzania kama kituo bora cha kufanyia mikutano ya kimataifa duniani.

#### **4.6.3.4 Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT**

**113. *Mheshimiwa Spika*,** Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani ya utalii, ukarimu na uratibu wa matukio katika ngazi ya Astashahada na Stashahada pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na tafiti katika fani hizo. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,087 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau katika mnyororo wa utalii wapatao 220. Vilevile, katika mwaka 2019/2020 jumla ya wanafunzi 455 wamehitimu mafunzo katika

ngazi ya Astashahada na Stashahada. Kwa upande mwininge, Chuo kimeanzisha Kampasi mpya ya Mwanza yenye uwezo wa kudahili wanafunzi 550.

***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha na kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko, Chuo kimefanya mapitio ya mitaala tisa (9) na kuandaa mitaala mipy minne (4) katika fani ya Ukarimu na Utalii. Pamoja na mitaala hiyo, Chuo kimeanzisha Idara ya Taaluma ya Utalii katika Kampasi ya Arusha. Aidha, Chuo kimeendelea na mikakati ya kuhamasisha makundi mbalimbali kushiriki katika mafunzo ya utalii. Katika kutekeleza hilo, Chuo kimefadhilis wasichana 35 kushiriki mafunzo ya utalii ngazi ya Astashahada katika Kampasi ya Mwanza. Chuo pia kiliandaa chapisho la kitaalam kufuatia Kongamano la Kimataifa liliojulikana kama *Linking Industry with Academia in Tourism and Hospitality Sector in Developing Countries (LIATH-DC)* liliofanyika mwaka 2020 Jijini Dar es Salaam kujadili namna ambayo vyuo vinaweza kushirikiana na wadau wa sekta kupunguza changamoto ya wahitimu kutokidhi mahitaji ya soko.

**114. *Mheshimiwa Spika***, Chuo kimeboresha miundombinu kwa kukarabati majengo katika Kampasi za Bustani, Arusha na Temeke. Aidha, vitendea kazi na vifaa mbalimbali vyatolea mafunzo vimenunuliwa katika Kampasi za Mwanza, Bustani, Arusha na Temeke. Vilevile, Chuo kimefanya tafiti na kutoa ushauri wa namna bora ya uendeshaji wa hoteli zinazomilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii.

#### **4.6.4 Sekta ya Mambo ya Kale**

***115. Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa malikale. Aidha, sekta ina jukumu la kutafiti, kubaini, kukusanya na kutoa elimu ya malikale na urithi wa utamaduni. Sekta hii inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera ya Malikale ya mwaka 2008; Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Sekta ya malikale inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT).

#### **4.6.4.1 Masuala Mahsus ya Sekta ya Mambo Kale**

##### **(i) Masalia ya Mjusi Mkubwa wa Dinosaria Yaliyohifadhiwa Nchini Ujerumani**

**117. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya mwaka 1906 hadi 1913 watafiti wa Kijerumani wakiwa katika harakati za kutafuta madini waligundua masalia ya mijusi wakubwa waliojulikana kama Danosaria (Dinosaurs) katika Kilima cha Tendaguru kilichopo mkoani Lindi. Masalia hayo ni baadhi ya vielelezo muhimu vyta chimbuko la maisha ya viumbi hai walioishi hapa nchini zaidi ya miaka milioni 150 iliyopita na sehemu nyingine za dunia. Aidha, wakati wa utafiti huo unafanyika Tanganyika ilikuwa koloni la Ujerumani na kwa nyakati hizo hapakuwa na miundombinu ya kiuhifadhi, uwezo wa kifedha na watalaam wa fani husika. Hali hii ilisababisha masalia hayo kusafirishwa kwenda nchini Ujerumani kwa uchambuzi zaidi na uhifadhi wa kitaalam.

**118. *Mheshimiwa Spika*,** sehemu ya masalia hayo kwa kipindi cha sasa ni mjusi mkubwa anayeoneshwa katika Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Naturkunde Berlin, Ujerumani. Taarifa za kitaalam zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya mijusi huyo ni masalia halisi kutoka Tendaguru Tanzania na asilimia 40 ni malighafi za kibunifu kwa ajili ya kupata umbo halisi la mijusi. Vilevile, mijusi yule ameunganishwa kwa vyuma na gundi ngumu kwa ajili ya kutengeneza onesho la kudumu. Uhifadhi wake unatumia ujuzi, miundombinu na teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi visukuku (fossils) duniani. Aidha, kwa kutambua umuhimu na faida zitokanazo na rasilimali za malikale yakiwemo masalia ya Dinosaria kwa uchumi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wamekuwa wakionyesha nia ya kutaka masalia hayo yarudishwe nchini. Katika kutekeleza matakwa ya Waheshimiwa Wabunge na Wananchi, Wizara kuititia Makumbusho ya Taifa inaendelea na majadiliano na Makumbusho ya Naturkunde, Berlin yenye lengo la kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha mjadala kati ya nchi ya Ujerumani na Tanzania ili kurejesha/kunufaika na masalia hayo.

**(ii) Uwekezaji katika Maeneo ya Malikale**

**119. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendeleza Sekta ya Malikale, kwa mwaka 2020/2021, Wizara imebainisha fursa za uwekezaji katika maeneo 18 ya malikale na vituo vya Makumbusho katika mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma, Mara na Arusha. Shughuli za uwekezaji zitakazofanyika katika maeneo hayo ni pamoja na migahawa ya kisasa, studio, maduka ya zawadi, bustani, huduma za kifedha, maduka ya bidhaa za asili na utamaduni na maeneo ya kuweka kambi za utalii za muda. Kutokana na fursa hizo, wadau mbalimbali wanakaribishwa kuwekeza katika maeneo yaliyobainishwa.

**(iii) Uimarishaji wa Mifumo ya Uhifadhi wa Malikale**

**120. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeanzisha mfumo wa kidijitali wa kuhifadhi mikusanyo ya malikale na urithi wa utamaduni katika Makumbusho ya Taifa. Mfumo huu utasaidia kuonesha na kuhifadhi uhalisia wa mikusanyo na maeneo ya malikale kwa muda mrefu. Aidha, mfumo utasaidia watafiti na wageni kutoka ndani na nje ya nchi baada ya kulipia kuona mikusanyo na malikale wakiwa mbali na hivyo kusaidia utangazaji, uhifadhi na usalama wa mikusanyo hiyo. Vilevile, itasaidia Wizara kujitangaza katika eneo la urithi wa kiutamaduni na malikale pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Lengo kuu la Serikali ni kuhakikisha kuwa taarifa za malikale na urithi wa utamaduni zilizopo zinahifadhiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

**4.6.4.2 Idara ya Mambo ya Kale**

**121. *Mheshimiwa Spika*,** katika kubaini hali ya uhifadhi kwenye maeneo ya malikale nchini, Wizara imeanza kufanya tathmini katika vituo vya malikale vya Kalenga, Isimila, Kunduchi, Bagamoyo na Kilwa Kisiwani. Kufuatia tathmini hiyo, uhakiki wa mipaka umefanyika katika eneo la magofu ya Enguruka wilayani Monduli na kituo cha Zana za Mawe cha Isimila - Iringa ili kuwezesha maeneo hayo kupata hati miliki. Aidha, upimaji wa mipaka umefanyika katika Kituo cha Kalenga,

Iringa na Hati ya umiliki kutolewa. Kwa upande mwingine, Wizara imeandaa mpango wa miaka mitano (2020/2021 - 2024/2025) wa uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya malikale yaliyopo katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Tanga na Dar es Salaam.

**122. *Mheshimiwa Spika*,** katika jithada za kuendelea kuhifadhi maeneo ya malikale na urithi wa kiutamaduni, Wizara imebainisha na kuandaa taarifa za maeneo 34 ya malikale katika mikoa ya Dar es Salaam (18), Ruvuma (12) na Lindi (4) ili kuhuisha rejest ya maeneo ya malikale. Maeneo hayo ni yale yenye historia ya Mwalimu Nyerere, vita vya majimaji na wapigania uhuru. Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu matamasha ya Kumbukizi la Vita vya Majimaji, Kuenzi Azimio la Arusha na Siku ya Kimondo Duniani ambapo elimu ya uhifadhi na uendelezaji wa malikale na urithi wa utamaduni ilitolewa.

#### **4.6.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania - NMT**

**123. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika lina jukumu la kufanya utafiti, kuhifadhi, kukusanya, kuonesha na kuelimisha umma kuhusu urithi wa utamaduni wa asili wa Taifa. Katika kutekeleza hilo, Shirika limeandaa mpango wa jumla wa uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 90 ya malikale. Katika kutekeleza mpango huo, ukarabati wa jengo la Soko la Watumwa katika Mji Mkongwe Mikindani umefanyika na kanzidata ya taarifa za mikusanyo ya mji huo imeandaliiwa. Pamoja na hatua hiyo, Shirika limeboresha miundombinu ya vituo kwa kukarabati vyoo katika Kituo cha Mwalimu Nyerere Butiama na kukarabati nyumba za asili za baadhi ya makabila kwa kufuata ramani ya Tanzania katika Kituo cha Kijiji cha Makumbusho.

**124. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendelea kuhamasisha wananchi kutembelea Makumbusho ya Taifa na Urithi wa utamaduni, Shirika limeandaa onesho la historia ya Tanzania kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanzania. Onesho hilo limetembelewa na wageni mbalimbali wa kitaifa na kimataifa wakiwemo Mama

Janet Magufuli, mke wa aliye kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Hayati John Joseph Pombe Magufuli na Mama Monica Chakwera, mke wa Rais wa Jamhuri ya Malawi. Aidha, kwa lengo la kutambua mchango wa wanawake katika harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Bara la Afrika, Shirika limeboresha onesho hilo kwa kujumuisha historia ya wanawake walioshiriki katika harakati za ukombozi. Kwa upande mwingine, Shirika limeandaa mpango wa kutangaza makumbusho na malikale kwa kutumia matamasha. Katika utekelezaji wa mpango huo, Shirika limeandaa kalenda ya matukio 42 kwa mwaka 2021 na tayari limefanya Tamasha la Kumbukizi la Vita vya Majimaji, Tamasha la kuenzi Azimio la Arusha, Tamasha la *Museum and Art Explosion* na kuanzisha gulio katika Kituo cha Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam litakalofanyika kwa mwezi mara moja na linalojulikana kama Kijjisoko.

**125. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika limeendelea na zoezi la kukusanya taarifa za kihistoria za Marais kwa ajili ya kutumika kama kumbukumbu kwenye Makumbusho ya Marais itakayojengwa Jijini Dodoma. Aidha, Shirika limeanza maandalizi ya programu ya kuenzi historia na falsafa ya Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere inayofahamika kama Mwl. Nyerere@100. Sambamba na hatua hiyo, Wizara kuititia Makumbusho ya Taifa imeanzisha klabu za historia na uzalendo mashulenii. Katika kuhakikisha somo la historia na uzalendo linawafikia wanafunzi ipasavyo mashulenii, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imefanikiwa kufungua klabu 16 za historia na uzalendo katika mikoa ya Ruvuma (6) na Dar es Salaam (10).

#### **4.6.4.4 Mfuko wa Mambo ya Kale**

**126. *Mheshimiwa Spika*,** Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 kwa lengo la kutekeleza majukumu ya kuhifadhi na utafiti wa malikale. Katika mwaka 2020/2021, Mfuko umewezesha kuandaa mkakati maalum wa kuenzi, kuweka kumbukumbu na kutangaza kazi alizozifanya Baba wa Taifa, Mwl. Nyerere. Katika hatua nyingine, Mfuko umeanza mapitio ya Mpango

Mkakati wake na kuandaa Mpango mpya wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026.

#### **4.6.5 Miradi ya Maendeleo**

**127. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 45,020,102,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi sita (6) ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 700,000,000** zilikuwa fedha za ndani na **Shilingi 44,320,102,000** ni fedha za nje. Hadi mwezi Aprili 2021, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 15,739,792,020** sawa na asilimia 35 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 51,600,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 15,688,192,020** ni fedha za nje. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

##### **4.6.5.1 Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini – REGROW**

**128. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, **Shilingi 30,495,601,578** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Hadi mwezi Aprili 2021, **Shilingi 5,776,178,445** zimetolewa na kutumika. Pamoja na matumizi hayo, kazi nyingine zikiwemo ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege na barabara ziko katika hatua mbalimbali za manunuzi. Baadhi ya kazi zilizotekelizwa ni pamoja na ununuzi wa magari 44, mitambo mitano (5) na vifaa vya doria kwa ajili ya usimamizi wa mradi; kutangaza vivutio vya utalii vilivypopo katika ukanda wa Kusini mwa Tanzania; na kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na Maji katika kijiji cha Itamba, Wilaya ya Mbarali. Aidha, tafiti mbili (2) za ikolojia ya magonjwa ya wanyamapori, hususan twiga na mabadiliko katika makazi ya wanyamapori; na uoto wa asili na ardhi katika hifadhi ya Taifa ya Ruaha zimefanyika.

##### **4.6.5.2 Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara**

**129. Mheshimiwa Spika**, mradi unatekelezwa na Wizara kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa - GEF na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa - UNDP. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, **Shilingi 583,775,000** ziliidhinishwa kwa

ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Hadi mwezi Aprili 2021, **Shilingi 429,485,000** zimetolewa na kutumika. Baadhi ya kazi zilizotekelawa ni ununuzi wa magari mawili (2) kwa ajili ya uratibu wa operesheni za kikosikazi; na ununuzi wa samani kwa ajili ya ofisi ya mradi.

#### **4.6.5.3 Mradi wa Panda Miti Kibashara – PFP**

**130. *Mheshimiwa Spika***, mradi unatekelezwa kwa ubia wa maendeleo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufini. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, **Shilingi 6,337,348,485** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Hadi mwezi Aprili 2021, **Shilingi 4,831,802,250** zimetolewa na kutumika. Baadhi ya kazi zilizotekelawa ni kuanzisha mashamba darasa 26 katika Wilaya za Makete (23) na Wanging'ombe (3) pamoja na mashamba 15 ya mbegu bora za miti katika Halmashauri za Mufindi, Kilolo, Mafinga, Njombe, Makambako, Ludewa, Wanging'ombe na Madaba. Aidha, utafiti kuhusu soko la mbao na mnyororo wa thamani katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya umefanyika. Vilevile, tanuru tano (5) kwa ajili ya kuwawezesha wazalishaji wa mkaa katika Wilaya ya Makete na trekta kwa ajili ya mafunzo ya vitendo vijijini yamenunuliwa.

#### **4.6.5.4 Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu - FORVAC**

**131. *Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Ufini. Mradi unalenga kuimarisha uwezo wa wananchi katika kusimamia rasilimali za misitu na kuongeza thamani ya mazao ya misitu. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, **Shilingi 7,103,376,937** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Hadi mwezi Aprili 2021, **Shilingi 4,650,726,325** zimetolewa na kutumika. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kuandaa mipango 15 ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji katika eneo la Hekta 70,000; mipango 26 ya usimamizi wa misitu ya vijiji; na mipango saba (7) ya usimamizi na uvunaji wa misitu katika konganiza Lindi na Ruvuma. Aidha, mashine mbili (2) za kisasa za kupasua mbao kwa ajili ya kongani za Lindi na Ruvuma zimenunuliwa; na utafiti wa miti ya mbao ambayo haipo kwenye soko kwa sasa umefanyika ambapo miti 14

imetambuliwa na kufanyiwa majaribio kwa ajili ya kuingizwa sokoni. Vilevile, miti aina ya misaji 450,000 imepandwa katika Wilaya ya Nyasa kwenye eneo la hekta 600 katika vijiji vinne (4) vya Liuli, Mkali 'A', Mkali 'B' na Lipingo.

#### **4.7 Changamoto na Utatuzi**

##### **4.7.1 Changamoto**

**132. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 duniani ambao umeathiri sekta ya utalii na hivyo kupungua kwa mapato yanayotokana na sekta hiyo. Aidha, kumekuwepo na mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi, hali iliyosababisha kuathirika kwa uoto wa asili na kupungua kwa malisho ya wanyamapori. Vilevile, uvamizi wa maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale kwa shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, mifugo na makazi umeendelea kuathiri shughuli za uhifadhi. Changamoto nyingine ni uwepo wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori ambao unasababisha uharibifu wa mali, vifo na mlipuko wa magonjwa kati ya binadamu na wanyamapori; kuendelea kuwepo kwa matukio machache ya ujangili; na uwepo wa matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi.

##### **4.7.2 Utatuzi wa Changamoto**

**133. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na changamoto zillizojitokeza katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara ilianda na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali. Kwa upande wa mlipuko wa COVID-19, Wizara ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii - SOPs; na kuandaa Mpango wa Kuirejesha Sekta ya Utalii Nchini katika Hali ya Awali kabla ya Kuathiriwa na COVID-19. Aidha, Wizara katika kukabiliana na hali ya mimea vamizi, imeendelea kushirikiana na taasisi za utafiti kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na mimea hiyo ndani ya maeneo ya hifadhi ikiwa ni pamoja

na kufanya tafiti na kutekeleza Mpango Mkakati wa Kutokomeza Mimea Vamizi. Vilevile, katika kukabiliana na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa, Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya maeneo hayo, kushirikisha jamii katika uhifadhi, kuwawezesha wananchi kuanzisha miradi ya kijamii na ya ujirani mwema na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa maeneo ya hifadhi za maliasili na malikale.

**134. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukabiliana na uwepo wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi na mali zao, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha udhibiti wa wanyamapori husika. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha vikosi vyta kudhibiti wanyamapori hao, kutumia mbinu za kielektroniki za kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori kwa kuwafunga vifaa maalum hasa katika maeneo yenye matukio mengi pamoja na kutoa elimu ya namna ya kujikinga na kutumia mbinu za asili za kuzuia wanyamapori hao kuingia kwenye maeneo ya wananchi. Wizara pia imeendelea kuimarisha mifumo ya kutambua na kuzuia matukio ya ujangili, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na biashara haramu ya nyara. Sambamba na hatua hizo, katika kukabiliana na matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi, Wizara imeandaa mipango ya usimamizi na udhibiti wa moto na kuendelea kutoa elimu kwa jamii zinazopakana na maeneo yaliyohifadhiwa.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**135. *Mheshimiwa Spika*,** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 - 2023/2024, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 - 2025, Sera mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), maagizo mbalimbali ya viongozi wa Serikali na mikataba ya kikanda na kimataifa. Aidha, Bajeti imezingatia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020.

**136. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na wadau katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali vyta sekta ambavyo ni pamoja na: kuendelea kuimarisha mikakati ya ukusanyaji maduhuli ya Serikali; kuendelea kuboresha sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia sekta; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ukiwemo Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE tourism); kukarabati na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi; kuboresha ulinzi na usalama wa rasilimali za maliasili na malikale; kuendeleza Sekta ya Misitu na Nyuki ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya upandaji miti na kuendeleza mazao ya nyuki; kuendelea kuimarisha uhifadhi, uwekezaji na utangazaji utalii; kuendelea kutatua migogoro ya ardhi inayojitokeza katika usimamizi wa Sekta ya Maliasili na Utalii; kuhakiki, kuendeleza na kutangaza maeneo ya malikale; kuendelea kuimarisha tafiti pamoja na mifumo ya takwimu na ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Maliasili na Utalii; na kuboresha mazingira ya kufanya kazi na kuendeleza rasilimaliwaitu.

## **5.1 Ukusanyaji Maduhuli**

**137. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, makadirio ya maduhuli yatakayokusanywa na Sekta ya Maliasili na Utalii ni jumla ya **Shilingi 689,345,854,249**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 478,014,580,522** zitakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana na vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA na **Shilingi 211,331,273,727** zitakusanywa kuititia Wizara na Taasisi zake ikiwemo TFS. Utaratibu wa ukusanyaji wa mapato umezingatia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 ambapo mapato yanayotokana na rasilimali za maliasili na utalii yanakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kuititia TRA. Vilevile, bajeti za taasisi ambazo mapato yake yanakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania zimejumuishwa katika Bajeti Kuu ya Serikali kuititia Wizara ya Maliasili na Utalii.

## 5.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**138.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 571,632,424,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 418,859,544,000** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 152,772,880,000** za Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 153,537,684,000** za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 265,321,860,000** za Matumizi Mengineyo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 113,893,184,000** fedha za ndani na **Shilingi 38,879,696,000** fedha za nje.

**139.** *Mheshimiwa Spika*, fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 23,081,864,000** kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 395,777,680,000** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Fedha za matumizi ya kawaida za Wizara zinajumuisha Shilingi **7,425,223,000** za Mishahara na **Shilingi 15,656,641,000** za Matumizi Mengineyo (O.C). Aidha, fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 146,112,461,000** za mishahara na **Shilingi 249,665,219,000** fedha za Matumizi Mengineyo (O.C).

**140.** *Mheshimiwa Spika*, bajeti ya Wizara mwaka 2021/2022 imeongezeka kwa **Shilingi 457,038,472,000** sawa na ongezeko la **asilimia 399** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021 ambayo ni **Shilingi 114,593,952,000**. Ongezeko hili limetokana na kujumuishwa kwa bajeti za TANAPA, NCAA na TAWA katika Bajeti Kuu ya Serikali; na maamuzi ya Serikali ya kutenga bajeti kwa taasisi na mifuko iliyokuwa inapokea fedha zilizotokana na asilimia 3 ya mapato ghafi ya TANAPA, NCAA na TAWA; na Tozo ya Maendeleo ya Utalii - TDL.

## 5.3 Kazi Zitakazotekelzwa na Wizara na Taasisi zake

### 5.3.1 Sekta ya Wanyamapor

#### 5.3.1.1 Idara ya Wanyamapor

**141.** *Mheshimiwa Spika*, kufuatia kuanzishwa kwa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapor na Misitu, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria za Uhifadhi wa Wanyamapor Sura

283 ili kuongeza wigo wa utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, Wizara itaandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kuhifadhi Wanyamapori (2021/2022- 2031/2032) na kukamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (2021/2022 - 2031/2032).

**142. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itaendelea kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu na kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi watakaoathiriwa na wanyamapori hao. Sambamba na hilo, Wizara itaendelea kuratibu utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa maamuzi ya Serikali kuhusu vijiji 920 vilivyopo ndani ya maeneo ya hifadhi. Vilevile, Wizara itafanya tathmini ya dhana ya ushirikishwaji wa jamii kwenye uhifadhi wa wanyamapori ili kuimarisha uhifadhi wa rasillimali hizo. Katika hatua nyingine, Wizara itaboresha usimamizi wa shoroba za wanyamapori na kufanya tathmini ya hali ya mapori tengefu ili kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

### **5.3.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA**

**143. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali litaendelea kutekeleza majukumu yake. Pamoja na masuala mengine, litaendelea kuimarisha ustawi wa wanyamapori, Shirika litachimba visima nane (8) katika hifadhi za Taifa za Ruaha na Katavi na kufanya ukarabati wa mabwawa matano (5) yenye jumla ya mita za ujazo 98,065 katika hifadhi za Taifa Serengeti, Mkomazi na Saadani kwa ajili ya upatikanaji wa maji kwa wanyamapori wakati wa kiangazi. Pia, Shirika litaboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 22,247 katika hifadhi za Taifa za Kitulo, Serengeti, Katavi, Milima ya Mahale, Ziwa Manyara, Mikumi, Kisiwa cha Rubondo, Milima ya Udzungwa, Ibanda - Kyerwa, Rumanyika - Karagwe, Tarangire, Gombe, Kitulo na Kilimanjaro na kuotesha miti ya asili 80,000 katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro.

**144. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kudhibiti maambukizi ya magonjwa kati ya mifugo na wanyamapori kwa kuwezesha chanjo za mifugo kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi na kuanzisha vikundi 28 vya uhifadhi kupitia mpango wa ujirani mwema. Vilevile, elimu ya uhifadhi itaendelea kutolewa katika vijiji 543 vinavyozunguka hifadhi zote za Taifa na kuwezesha vijiji 27 kunufaika na miradi ya ujirani mwema. Katika hatua nyingine, Shirika litaendelea kudhibiti majanga ya moto kwenye hifadhi kwa kutengeneza mipango sita (6) ya usimamizi wa mioto kichaa katika hifadhi za Taifa Nyerere, Kigosi, Mto Ugalla, Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe. Aidha, Shirika litaimarisha ufuatiliaji wa matukio ya mioto kichaa katika maeneo ya hifadhi kwa kuboresha matumizi ya *satellite*. Sambamba na hilo, Shirika litatekeleza Mipango ya Usimamizi wa Moto katika hifadhi na kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi kwa ajili ya kukabiliana na mioto kichaa.

**145. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kupanua wigo wa uwekezaji kwenye hifadhi za Taifa kwa kutenga maeneo 103 ya ujenzi wa loji na kambi za kudumu kwa ajili ya malazi ya wageni yenye uwezo wa vitanda 4,604 katika hifadhi za Taifa Kitulo, Mkomazi, Nyerere, Saadani, Ruaha, Kigosi, Ibanda - Kyerwa, Mto Ugalla, Rumanyika - Karagwe na Burigi - Chato. Pia, Shirika litaendelea na ujenzi wa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tatu katika Hifadhi ya Taifa Katavi na kujenga malazi ya gharama nafuu yenye jumla ya vitanda 116 kwa ajili ya watalii wa ndani katika hifadhi za Taifa Mikumi, Nyerere na Burigi - Chato.

**146. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kupanua wigo wa mapato kwa kuanzisha mazao mapya ya utalii ikiwemo kuendeleza ujenzi wa uwanja wa mchezo wa gofu eneo la Fort Ikoma nje kidogo ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Vilevile, Shirika litanunua boti ya kitalii kwa ajili ya kuanzisha zao jipya la utalii wa maji katika Ziwa Victoria utakaouniganisha hifadhi za Taifa za Kisiwa cha Rubondo, Kisiwa cha Saanane, Burigi - Chato na Serengeti (kupitia Ghuba ya Speke/Serengeti). Kuendelea na ujenzi wa mradi wa uzio wa faru kwa shughuli

za kitalii katika Hifadhi ya Taifa Burigi - Chato; kuanzisha utalii wa uvuvi wa samaki katika hifadhi ya Taifa Tarangire, Mikumi, Burigi - Chato, Mto Ugalla, Kisiwa cha Rubondo na Kisiwa cha Saanane; utalii wa michezo katika Hifadhi ya Taifa Mikumi; na utalii wa kutembea kwenye daraja la kamba katika Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa.

**147. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kuboresha huduma za utalii kwa kujenga barabara mpya zenyet urefu wa kilometa 2,256 katika hifadhi za Taifa za Burigi - Chato, Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa, Nyerere, Katavi, Kigosi, Kitulo, Milima ya Mahale, Mkomazi na Mto Ugalla. Kwa upande mwingine, Shirika litajenga daraja 18 na kalavati 157 katika Hifadhi ya Taifa Tarangire. Aidha, njia za watalii kutembea kwa miguu zenyet urefu wa kilometa 841 zitakarabatiwa katika hifadhi za Taifa Arusha, Mkomazi, Kilimanjaro na Milima ya Udzungwa. Pia, viwanja vipyta vya ndege 14 vitajengwa katika hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi na Nyerere na vituo vya utalii vitano (5) katika hifadhi za Taifa Serengeti, Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na Nyerere. Kazi nyingine zitakazotekelizwa ni pamoja na ununuzi wa magari 34, mtambo wa barabara mmoja (1), boti 11 kwa ajili ya doria, injini za boti mbili (2) na pikipiki 21.

**148. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi kwa kufanya siku doria 326,500 na kuwezesha operesheni maalum za kuzuia matukio ya ujangili. Vilevile, Shirika litaongeza idadi ya vifaa vya doria kwa kununua silaha na mahema. Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha ukaguzi wa maeneo kwa kutumia ndege ndogo za doria pamoja na kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ruaha, Mkomazi, Tarangire, Mikumi na Kisiwa cha Rubondo.

**149. *Mheshimiwa Spika*,** mipango mingine itakayotekelizwa katika kipindi cha 2021/2022 ni pamoja na ujenzi wa hoteli ya kitalii katika eneo la biashara la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere - *Terminal 3*, Jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini, ambayo ndio mmiliki wa eneo hilo; hoteli ya kitalii eneo la

Magamba liliopo umbali wa kilometra 7 kutoka Uwanja wa Ndege wa Mpanda; na kuendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika litaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kujenga nyumba 39 katika hifadhi za Taifa za Kisiwa cha Rubondo, Burigi - Chato, milima ya Mahale, Ruaha, Gombe, Serengeti, Mikumi, Milima ya Udzungwa, Nyerere na Mkomazi.

### **5.3.1.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania - TAWA**

***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha miundombini ya utalii, Mamlaka itafungua kilometra 386 za barabara za utalii katika mapori ya akiba ya Maswa, Pande, Rungwa, Mpanga Kipengere, Kijereshi, Lwafi, Wami - Mbiki na Lukwika Lumesule. Aidha, Wizara itajenga madaraja Matano (5) katika Pori la Akiba Msanjesi na Pori Tengefu la Ziwa Natron na kujenga njia za utalii wa kutembea kwa miguu zenyenye urefu wa mita 75 katika eneo la kihistoria la Magofu ya Kilwa Kisiwani. Pamoja na hayo, Mamlaka itajenga mabanda ya kulala wageni katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere; na jengo la mapokezi katika eneo la Bustani ya Wanyamapor, Tabora na Pori la Akiba Pande. Aidha, vituo 12 vya kukusanya mapato vitajengwa katika mapori yaakiba Kijereshi, Mkungunero, Lukwika Lumesule na Swagaswaga; mapori tengefu ya Kilombero na Ziwa Natron; na eneo la Ndarakwayi. Vilevile, Mamlaka itajenga lango katika Pori la Akiba Maswa na kambi nne (4) za watalii katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere, Maswa na Pande.

**150. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa vitalu vya uwindaji dhidi ya ujangili na uvamizi wa maeneo hayo kutokana na shughuli za kibinadamu ambazo ni kilimo, makazi na ufugaji; kutangaza shughuli za uwindaji katika maonesho mbalimbali ya kimataifa, hususan katika masoko makubwa ya Marekani, Ufaransa, Uingereza, Ubelgiji, Ujapan na Afrika Kusini; kupanua wigo kwenye masoko yanayochipukia ya Mashariki ya kati, China na Urusi; na kubuni mbinu mbalimbali

za kuhakikisha vitalu vinapata wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha vifurushi kwa bei maalum.

**151. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki katika uwekezaji wa ufugaji wa wanyamapori, Wizara itafanya marekebisho ya sheria, kupanua wigo wa uwekezaji katika biashara ya ufugaji wa wanyamapori, kupunguza bei za wanyamapori mbegu na kuanzisha Kitengo maalum kwa ajili ya ukamataji wa wanyamapor (Wildlife Capture Facility) ili kuwezesha ukamataji kufanyika kitalaam na kwa bei nafuu. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa kuboresha usimamizi wa biashara ya mabucha ikiwa ni pamoja na kuainisha fursa za upatikanaji wa nyamapor na kuhamasisha uanzishaji wa shughuli za ufugaji wanyamapor ili kuendeleza upatikanaji wa nyamapor kwa wananchi. Hatua hizo pamoja na manufaa mengine, zitachangia katika kuboresha biashara ya mabucha ambayo imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ya ukosefu wa nyamapor.

**152. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi kwa kufanya siku doria 284,460 katika mapori ya akiba, mapori tengefu, maeneo ya ardhioevu (Ramsar sites) na WMAs. Aidha, jumla ya watumishi 325 watapatiwa mafunzo ya ukakamavu na utayari ya Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapor na Misitu. Kwa upande mwingine, Mamlaka itanunua helikopta moja (1), boti tatu (3), trekta mbili (2) na magari nane (8) kwa ajili ya shughuli za doria. Vilevile, ili kuimarisha ulinzi wa wanyamapor, maisha na mali za wananchi, Mamlaka itajenga karakana mbili (2) kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo ya taasisi na kujenga vituo viwili (2) vya askari katika mapori ya akiba Maswa na Lwafi.

**153. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza Ibara ya 67(a)(i) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 inayowielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kukuza na kuimarisha utalii wa uwindaji wa wanyamapor, Wizara imebuni mkakati unaovutia mitaji mikubwa na kwa muda mrefu katika maeneo maalum ya vitalu vya uwindaji

ujulikanao kama ***Special Wildlife Investment Concession Area (SWICA)***. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imetunga kanuni za kuongoza uwekezaji huo (*The Wildlife Conservation - Special Wildlife Investment Concession Areas) Regulations, 2021*). Pamoja na masuala mengine, kanuni hizo zinatoa utaratibu wa uwekezaji unaolenga kuimarisha Uhifadhi wanyamapor, kuendeleza biashara ya utalii na kuboresha huduma za utalii nchini kwa kushirikisha kijamii. Kwa kutekeleza mpango huo, mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii yataongezeka takriban mara tatu ya uwezo wa sasa wa uzalishaji wa vitali hivyo na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania. Matokeo haya ni kutokana na upembuzi yakinifu wa modeli ya kifedha (financial model) iliyofanyika.

**154. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka itaendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa watumishi wake, miundombinu kwa ajili ya jamii zinazopakana na maeneo ya hifadhi na kutangaza utalii wa uwindaji. Katika kutekeleza azma hiyo, nyumba saba (7) za watumishi na ofisi tano (5) zitajengwa pamoja na kununua vitendea kazi. Aidha, madarasa mawili (2) yatajengwa katika kijiji cha Usinge - Moyowosi na soko la samaki Kilombero. Kwa upande mwingine, Mamlaka itashiriki katika maonesho ya kimataifa ya kutangaza utalii hususan uwindaji wa kitalii katika nchi za Japan, Urusi, Afrika ya Kusini, Uarabuni na Ulaya.

#### **5.3.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro - NCAA**

**155. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka itaendelea kutekeleza jukumu lake la uhifadhi kwa kuboresha miundombinu katika eneo la Hifadhi kwa kujenga kilometra 40 za barabara kutoka eneo la Ndutu hadi Kakesio na kilometra 78 za barabara kutoka *Viewpoint* hadi Naiyobi kwa kiwango cha changarawe; kukamilisha taratibu za ujenzi wa kilometra 83 za barababara kuu kutoka geti la Loduare hadi Golini kwa kiwango cha tabaka gumu; na kufungua mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometra 75 katika eneo la Ndutu. Aidha, Mamlaka itakarabati kilometra 606 za mtandao wa barabara na viwanja vya ndege vya Ndutu na Ngorongoro. Vilevile, Mamlaka itaendelea kukiongezea nguvu kitengo cha

usimamizi wa miundombinu kwa kununua mitambo mitano (5) na malori matano (5). Katika hatua nyingine, Mamlaka itaweka miundombinu wezeshi kwenye maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa kimkakati wa huduma za malazi. Hatua hii itaongeza urahisi wa watalii kuvifiki vivutio na kufanyika kwa doria katika maeneo ya hifadhi.

**156. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka itaendelea kuboresha nyanda za malisho kwa kudhibiti mimea vamizi kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 5,000 katika maeneo ya Ndutu na Kreta ya Ngorongoro kwa kung'oa, kufyeka, kuandaa moto mpango na kudhibiti moto holela katika maeneo ya hifadhi na maeneo yanayozunguka hifadhi. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaotesha na kugawa miche 550,000 kwa jamii za wenyeji waishio ndani na nje ya hifadhi.

**157. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukuza utalii wa malikale, Mamlaka itaendelea kuviongezea thamani vituo vya Amboni Tanga na Kimondo Mbeya kwa kuimarisha miundombinu na ulinzi. Aidha, Mamlaka itajenga vituo vya habari kwenye vituo hivyo, kubuni na kuanzisha bidhaa mpya za utalii wa malikale pamoja na kufanya matamasha ya urithi wa utamaduni na mambo kale ili kuvutia watalii zaidi na kuongeza mapato. Vilevile, Wizara itanza kukusanya taarifa za kihistoria katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi. Katika mpango huo, Jiwe la Mbui na Nyayo za Kale Litembo zitafanyiwa tathimini kwa lengo la kuendeleza kama moja ya maeneo muhimu yenye urithi wa Taifa.

**158. *Mheshimwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itapandisha hadhi msitu wa hifadhi wa Matogoro kuwa hifadhi ya mazingira asilia. Hatua hii inatokana na umuhimu wa ikolojia na bioanuai zilizopo ndani ya hifadhi ya msitu huo na uwepo wa milima ya Matogoro yenye miamba iliyofanyiwa tafiti kwa ajili ya utalii jiolojia (*Geopark*). Lengo la hatua hii ni kuimarisha uhifadhi na kuendeleza shughuli za utalii ikololojia katika msitu huo. Vilevile, Wizara itahamasisha ufgaji nyuki kibiashara katika hifadhi hiyo kwa ajili ya utalii wa nyuki (*Apitourism*) na kama njia mbadala ya kuongeza kipato kwa jamii. Utalii jiolojia na utalii wa nyuki ni mazao

mapya ya utalii ambayo yatachangia kukua kwa utalii katika ukanda wa Kusini mwa Tanzania.

**159. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuongeza mapato yatokanayo na utalii, Mamlaka itaanisha mazao mapya ya utalii yakiwemo *night game drive, canopy walk* na *zipline* kwenye eneo la Makoromba na Ziwa Eyasi na utalii wa makasia kwenye Kreta ya Empakaai. Aidha, Mamlaka itaendelea kutumia mbinu ya masoko mtandao (digital marketing) kutangaza vivutio nya Ngorongoro na maeneo ya malikale ya Mapango ya Amboni, Kimondo cha Mbozi, Engaresero, Engaruka na Mumba. Katika hatua nyingine, Mamlaka itajenga kituo cha taarifa kwa watalii katika kituo cha Mumba. Aidha, Mamlaka itaanza taratibu za kuzifukua nyayo za kale za Laetoli kwa lengo la kuvutia watalii zaidi na kusanifu michoro kwa ajili ya ujenzi wa Makumbusho ya Viumbe Bahari (Marine Museum) unaotarajiwa kujengwa katika eneo la Mapango ya Amboni Tanga.

**160. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka katika kuboresha huduma na maisha ya wananchi waishio ndani ya eneo la hifadhi na jamii inayopakana na eneo la hifadhi, itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya afya, elimu, maji, chanjo ya mifugo na chakula cha ruzuku. Katika kutekeleza jukumu hili, Mamlaka itafadhili wanafunzi 1,924 kuanzia ngazi za shule ya msingi hadi chuo kikuu; na kutoa chanjo za kimeta CCBP, PPR, na ECF kwa mifugo. Vilevile, NCAA itatekeleza miradi ya maji kwa kujenga bwawa la maji; mtandao wa mabomba ya maji; majosho; na vituo nya maji katika eneo la Misigyo, Oldonyogol na Masamburai. Kwa upande mwingine, NCAA katika kuongeza kipato cha wananchi waishio ndani maeneo yanayozunguka hifadhi itakamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki katika Wilaya ya Karatu.

**161. *Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka itaendelea kuimarisha Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu kwa kufanya siku doria 36,000 katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Pori tengefu la Loliondo; Aidha, Mamlaka itajenga jumla ya vituo nya askari vipyta kumi (10) katika maeneo ya Kakesio, Selela,

Lositete, Kambi ya Simba, Empakaay, Loresho na Pori Tengefu la Loliondo. Vilevile, Mamlaka itakarabati vituo kumi (10) vya askari katika maeneo ya Esirwa, Kakesio, Seneto, Lemala, Naiyobi, Endulen, Nainokanoka, Eyasi, Karatu, na Mbolumbulu. Katika hatua nyingine, Mamlaka itejenga malango matatu ya kuingia wageni katika eneo la Pori tengefu la Loliondo ili kuimarisha ukaguzi na makusanyo ya maduhuli.

### **5.3.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor Tanzania - TAWIRI**

**162. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Taasisi itafanya sensa za wanyamapor katika Pori la Akiba Liparamba, mifumo ikolojia Ruaha – Rungwa, Katavi – Rukwa, Saadani – Wami mbiki na Ziwa Natroni – West Kilimanjaro. Aidha, katika kutekeleza Mkakati wa kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapor, Taasisi itaendelea kuidadi na kufanya tafiti katika maeneo ya mtawanyiko na shoroba zinazoshabihiana na mifumo ikolojia tajwa. Vilevile, TAWIRI kwa kushirikiana na wadau wanaotekeleza Mradi wa REGROW itaboresha shughuli za utafiti wa wanyamapor katika mikoa ya Kusini kwa kuanza ujenzi wa kituo cha utafiti katika eneo la Kihesa - Kilolo, Iringa mjini.

### **5.3.1.6 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapor Mweka**

**164. *Mheshimiwa Spika*,** Chuo kitaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti cha Msingi, Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili katika fani ya Uhifadhi Wanyamapor na Utalii pamoja na mafunzo ya muda mfupi kutegemeana na mahitaji ya wateja ikiwemo waongoza watalii na usimamizi wa mashamba ya wanyamapor. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kupitia mitaala 10 iliyopo na kutengeneza minne (4) mipya; kuboresha Kitengo cha TEHAMA; na kuboresha miundombinu ikiwemo ujenzi wa madarasa na vyoo katika maeneo ya mafunzo kwa vitendo yaliyopo Kwakuchinja, wilayani Babati na Loliondo wilayani Ngorongoro. Vilevile, Chuo kitachimba kisima cha maji na kujenga vyoo vya kisasa na darasa. Aidha, Chuo kitaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya uzio wenye urefu wa mita 350

katika kampasi kuu na ujenzi wa jengo la mafunzo awamu ya kwanza. Katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo porini, Chuo kitanunua magari mawili (2).

#### **5.3.1.7 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu- Sekamaganga**

**165. *Mheshimiwa spika*,** Kituo kitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 150, kati ya hao, Askari Wanyamapor wa Vijiji ni 80, Viongozi na Wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji 20, Waongoza Watalii 30 na kozi maalumu 20. Aidha, Chuo kitajenga maabara moja (1) na bweni moja (1). Vilevile, Chuo kitakarabati nyumba mbili (2) za watumishi, ukumbi wa mikutano na bweni. Sambamba na hilo, Kituo kitaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa WMA's za Mchimalu (Nanyumbu), Ndonda (Nachingwea), Mungata (Rufiji) na MBOMIPA (Iringa). Pia, Chuo kitafuatilia na kupata ithibati (accreditation) kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufund - NACTE.

#### **5.3.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapor Pasiansi**

**166. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Taasisi itadahili wanafunzi 400 katika fani za uhifadhi wa wanyamapor, himasheria na uongozaji wa watalii na usalama. Aidha, Taasisi itakamilisha ujenzi wa maktaba na tanki la maji safi lenye uwezo wa lita za ujazo 100,000 katika eneo la mafunzo kwa vitendo Fort-Ikoma, Serengeti. Vilevile, Taasisi itakamilisha ujenzi wa uzio wa chuo, kuboresha miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za Kampasi Kuu, kufanya tafsiri ya sheria na kanuni kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na kuanzisha shamba la wanyamapor ili kuongeza mapato kwa Taasisi.

#### **5.3.1.9 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapor Tanzania - TWPF**

**167. *Mheshimiwa Spika*,** Mfuko utaendelea kuwezesha uhakiki wa matukio ya wanyamapor wakali na waharibifu na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wanaoathirika. Aidha, Mfuko utaendelea kuwezesha Kikosi Kazi cha Taifa cha

Kuzuia Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori kutekeleza majukumu yake. Vilevile, Mfuko utawezesha taratibu za kupandisha hadhi maeneo yaliyohifadhiwa na kufanya marekebisho ya sheria na kanuni za Sekta ya wanyamapori.

### **5.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki**

#### **5.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki**

**168. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Misitu na Ufugaji Nyuki za Mwaka 2002 na itatafsiri Sheria, Kanuni na Miongozo ya Idara kwa lugha ya Kiswahili. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kuanda mikakati ya Kitaifa ya uendelezaji biashara ya mkaa na mkaa mbadala, uendelezaji wa miti ya mianzi (bamboo), uhandisi bidhaa za mbaao (Engineered Wood Product - EWP), killimo mseto, uongoaji wa ardhi, uwekezaji kwenye biashara ya mazao ya nyuki pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii.

**169. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itaandaa mwongozo wa usimamizi wa mashamba ya miti, rejesta ya wafugaji nyuki na kubaini mchango halisi wa Sekta ya Misitu na Nyuki kwenye pato Ghafi la Taifa. Aidha, Wizara itaratibu utangazwaji (*gazzetment*) wa hifadhi za misitu na nyuki na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa viwanda vya misitu na ufugaji nyuki. Vilevile, Wizara itawezesha watumishi watano (5) kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu pamoja na watumishi watano (5) wa TAFORI kupata mafunzo yatakayowawezesha kufanya utafiti wa ufugaji nyuki.

**170. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itawezesha vikao vinne (4) vya Kamati ya Ushauri wa Misitu - NAFAC na vikao vitatu (3) vya Kamati ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki - NABAC. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuratibu siku ya upandaji miti Kitaifa, siku ya misitu duniani na siku ya nyuki duniani; na kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa vyama vya ushirika na wadau wengine wa ufugaji nyuki.

### 5.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

**171. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala utaendelea kuhudumia mashamba 23 ya miti yenye ukubwa wa hekta 445,354.7 kwa kuzalisha tani 22 za mbegu bora za miti, kuotesha miche 33,185,000, kupanda miti kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 7,833, kupalililia hekta 44,430, kupogoa miti hekta 13,773 na kupunguza miti katika hekta 6,044. Aidha, Wakala utaananza mashamba mawili mapya ya miti yenye ukubwa wa hekta 84,500 katika wilaya za Tunduru na Kasulu pamoja na kukamilisha taratibu za kuhifadhi kisheria maeneo mapya yenye ukubwa wa hekta 121,100. Vilevile, Wakala utaendelea na utaratibu wa kupandisha hadhi misitu ya Kwamngumi, Bamba Ridge, Segoma, Mpandaline, Uvinza, Nou, Hasama na Matogoro yenye ukubwa wa hekta 348,078 kuwa hifadhi ya misitu ya mazingira asilia.

**172. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi - NLUPC itaandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 40 vinavyopakana na Hifadhi za Misitu. Vilevile, Wakala utaimarisha mipaka ya misitu 183 kwa kupima upya na kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilometra 314.84, kusafisha mipaka yenye kilomita 2,592.28, kuweka vizingi 1,452 na mabango 1,958. Aidha, katika kuimarisha ulinzi na kudhibiti uharibifu wa misitu, Wakala utaandaa mipango ya usimamizi wa misitu 58 yenye ukubwa wa hekta 1, 267,518.15; kufanya jumla ya doria 3,277 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki; na kufanya operesheni maalum katika hifadhi za misitu. Pia, Wakala utaendelea kuimarisha mfumo wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu kwa kutoa mafunzo kwa watumishi 300, kuanzisha kambi mbili (2) za kijeshi na kununua vifaa mbalimbali yakiwemo magari na silaha.

**173. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Wakala utaendelea kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii kwa kutoa vifaa vya ujenzi katika Serikali za vijiji vitano (5), shule 578 na taasisi 206. Aidha, Wakala utaendelea kuimarisha maeneo yenye vivutio vya utalii ikolojia kwa kuboresha miundombinu ya malazi, njia za kupita wageni,

vituo vya ulinzi na huduma pamoja na usimamizi kwenye hifadhi saba (7) za mazingira asilia. Wakala pia utakarabati kilomita 157.3 za barabara za ndani ya hifadhi za misitu asilia, kilomita 335 za njia za kutembea watalii na kambi 29 za kupumzikia. Vilevile, Wakala utajenga kilomita 18 za barabara mpya ndani ya hifadhi za misitu, majengo manne (4) ya ofisi, kituo kimoja cha taarifa kwa watalii, vibanda vinne (4) vya watalii, madaraja nane (8) ya kitalii (boardwalks), kambi nane (8) za kupumzikia watalii na minara 10 ya kuona mandhari. Aidha, Wakala utaandaa maandiko 6,655, Makala moja, vipindi 25 vya redio na 14 vya television kwa ajili kutangaza masula ya utalii ikolojia.

**174. Mheshimiwa Spika**, Wakala utaendeleza kuboresha vituo sita (6) vya malikale vya Michoro ya Kolo (Kondo), Magofu ya Kaole na Mji wa Zamani wa Bagamoyo (Pwani), Tembe la Livingstone (Tabora), Jengo la Zamani la Afya (Tabora) na Magofu ya Tongoni (Tanga). Katika kutekeleza azma hiyo, Wakala utajenga kambi moja (1) yenye mahema ya kudumu na kibanda cha kitalii katika Kituo cha Hifadhi ya Kolo; kibanda cha kupumzikia wageni na kituo cha michezo ya watoto katika Hifadhi ya Tongoni; kukarabati jengo la mnara wa Mgonera na makaburi ya Mwamakula na Wajerumanii katika hifadhi ya Mji Mkongwe- Bagamoyo.

**175. Mheshimiwa Spika**, Wakala utaboresha mifumo yake ya kusimamia misitu, kudhibiti uvunaji na ufuatiliaji wa biashara ya mazao ya misitu na nyuki pamoja na kudhibiti upotevu kwa kutumia mfumo wake fungamanishi unaofahamika kama *Forest Resource Management Information System* (FREMIS). Wakala pia utanunua mashine 50 za kukusanya maduhuli na utaendelea kutoa mafunzo maalum kwa timu ya maafisa 15 watakaotumika kutoa msaada wa kiufundi wa masuala ya mifumo ya kukusanya maduhuli.

**176. Mheshimiwa Spika**, Wakala utatoa mafunzo ya usimamizi wa misitu kwa Kamati za Maliasili za Vijiji 97 kwa ajili ya kuziongezea uwezo wa kulinda na kusimamia rasilimali za misitu. Aidha, wananchi na wadau wengine wa mazingira watashirikishwa kupanda miti 7,070,000 katika maeneo

mbalimbali ikiwemo mashambani, maeneo yaliyoharibika pamoja na kandokando ya vyanzo vya maji. Kati ya miche hiyo, miche 1,000,000 itapandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma katika kuendeleza kampeni ya *Dodoma ya Kijani*. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaanzisha na kusimamia vitalu sita (6) vya miche ya miti katika maeneo mbalimbali nchini vyenye uwezo wa kuzalisha miche milioni 6.1 kwa wakati mmoja. Hatua hii inalenga kuongeza upatikanaji wa miche bora na ya kutosha kwa shughuli za kuongoa ardhi na kuboresha mazingira.

**177. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala utaendelea kuelimisha umma kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki kupitia maadhisho ya Siku ya Mazingira Duniani; Siku ya Nyuki Duniani na Utundikaji Mizinga Kitaifa; Siku ya Kupanda Miti Kitaifa; maonesho ya Saba Saba; maonesho ya Nane Nane; na Siku ya Utumishi wa Umma. Aidha, Wakala utaandaa na kurusha vipindi 22 vya televisheni, vipindi 60 vya redio na kusambaza nakala 12,000 zenye jumbe mbalimbali zinazohamasisha upandaji miti na utunzaji wa rasilimali za misitu na nyuki. Wakala pia utafanya mikutano ya kampeni ya kuzuia mioto katika vijiji 241 vinavyopakana na misitu ya hifadhi.

**178. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala utaendelea kuimarisha rasilimali za nyuki kwa kusimamia manzuki 181 za nyuki na kuzalisha tani 96 za asali na tani saba (7) za nta. Ili kuongeza uzalishaji, Wakala utaanzisha mashamba matatu (3) maalum ya nyuki katika wilaya za Kondo, Songea na Manyoni. Vilevile, Wakala utapandisha hadhi maeneo yenye ukubwa wa hekta 630.8 kuwa hifadhi za nyuki. Kwa upande mwingine, Wakala utatoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa taasisi 20, vikundi 138 vyenye wafugaji 1,490 na kutoa mizinga 1,000 na seti 100 za mavazi. Vilevile, Wakala utawezesha upimaji wa sampuli za asali ili kuthibitisha ubora na kufungua fursa ya biashara ya zao hilo la nyuki katika nchi za Jumuiya ya Ulaya pamoja na mataifa mengine.

**179. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala utaendelea kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vya misitu ambapo

unatarajiwa kuuza mita za ujazo 1,082,903 kutoka mashamba ya miti 13 na zaidi ya mita za ujazo 700,000 kutoka misitu ya asili. Wakala pia utasaini mikataba na wafanyabiashara wa magogo wapatao 755 ili kuwahakikishia upatikanaji wa malighafi. Aidha, Wakala utatoa elimu ya biashara ya mazao ya misitu na nyuki kwa wadau 820.

**180. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala utajenga ofisi 15, nyumba nane (8) za watumishi na vituo 23 vya ulinzi ndani ya hifadhi ya misitu na kukarabati majengo 59. Aidha, Wakala utanunua magari 29 likiwemo lori moja, matrektta mawili (2), pikipiki 40 na mtambo mmoja (1) kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki. Vilevile, Wakala utajenga barabara mpya za misituni zenye urefu wa kilomita 92, makaravati 32, madaraja 27 na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 1,468. Vilevile, Wakala utatoa mafunzo mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wake ikiwemo mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 70 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 785.

### **5.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI**

**181. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Taasisi itafanya tafiti tano (5) mpya kuhusu uzalishaji na matumizi ya mazao yatokanayo na miti ya mlonge na ubuyu; suluhisho la mioto ya misituni; utambuzi wa misitu na tathmini ya aina ya mazao ya misitu; miti ya dawa na matunda ya asili; na uzalishaji na uendelezaji wa mianzi katika maeneo mbalimbali. Pia, Taasisi itaendelea kufanya utafiti kuhusu ubora wa mbaao kutoka kwenye misitu mbalimbali nchini na kuendelea kufanya utafiti unaohusu uvunaji wa utomvu kwenye miti ya misindano ili kubaini umri sahihi wa kuvuna utomvu na madhara kwenye ukuaji wa miti hiyo. Aidha, Taasisi itaandaa mkakati wa uendelezaji Kilimo Misitu.

**182. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki na kuimarisha sekta ya ufugaji nyuki nchini, Taasisi itafanya tafiti za kuainisha uwezo wa uzalishaji wa mazao ya nyuki kulingana na maeneo ya kiikolojia, namna ya kukuza na kuendeleza usimamizi wa makundi ya nyuki na namna

bora ya kuendesha viwanda vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki. Aidha, Taasisi itafanya utafiti wa athari ya mimea vamizi katika uzalishaji wa asali eneo la Manyoni.

#### **5.3.2.4 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**183. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI kitadahili wanafunzi 300 wa mafunzo ya muda mrefu na wanafunzi 50 wa mafunzo ya ufundi stadi wa viwanda vya misitu. Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI kitadahili wanafunzi 1,000 na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - BTI kitadahili wanafunzi 420. Aidha, Chuo cha FITI kitaanzisha kampasi mpya katika mji wa Mafinga mkoani Iringa na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya viwanda vya misitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Kwa upande mwagine, Chuo cha FTI kitakarabati mabweni ya wanafunzi matatu (3), madarasa matatu (3), nyumba tano (5) za watumishi, ukumbi mmoja wa mihadhara na kuweka geti jipya katika lango kuu la kuingia chuoni. Chuo pia kitafanya marejeo ya mitaala ya kozi tano (5). Vilevile, Chuo cha BTI kitaanza hatua za awali za kuanzisha Utalii wa Nyuki kwa kujenga miundombinu katika Msitu wa Hifadhi ya Nsimbo. Chuo pia kitajenga jengo la maabara na maktaba pamoja na kutoa elimu ya ufugaji nyuki wenye tija kwa wafugaji nyuki 200 wa Wilaya za Kasulu, Kibondo, Uvinza, Sikonge, Urambo na Uyui. Lengo la Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa wataalam wenye weledi stahiki kwa ajili ya kusimamia sekta ya misitu na nyuki ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa.

#### **5.3.2.5 Mfuko wa Misitu Tanzania**

**184. *Mheshimiwa Spika***, Mfuko utaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya uanzishwaji wa viwanda vinne (4) vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki vinavyojengwa katika Wilaya za Sikonge, Bukombe, Mlele, na Kibondo. Aidha, Mfuko utaendelea kugharamia ujenzi wa kiwanda cha mazao ya nyuki kinachojengwa Wilayani Nzega pamoja na kuwezesha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya

kukusanya mazao ya Nyuki katika mikoa ya Songwe, Mbeya na Katavi.

**185. *Mheshimiwa Spika*,** Mfuko utagharamia miradi mipya 54 na miradi 60 inayoendelea ya uanzishwaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shulenii katika wilaya 30 za mikoa nane (8) yenye maeneo ya nyanda kame. Aidha, Mfuko utatoa ruzuku kwa miradi 15 ya vikundi vya vijana na wanawake vya ufugaji nyuki katika mikoa yenye fursa kubwa za ufugaji nyuki. Katika hatua nyingine, Mfuko pia utagharamia miradi 15 ya ruzuku maalum kwa lengo la kuongeza malighafi za viwanda vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki na miradi ya kuanzisha mashamba mapya ya miti ya kupandwa. Aidha, Mfuko utaendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi 27 inayoendelea ya uhifadhi na uendelezaji wa misitu na miradi 115 inayoendelea ya ufugaji nyuki. Vilevile, Mfuko utawezesha Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI kufanya na kuratibu tafiti tatu (3) za kimkakati zenyenye lengo la kuendeleza sekta ya Misitu na Nyuki.

### **5.3.3 Sekta ya Utalii**

#### **5.3.3.3 Idara ya Utalii**

**186. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 na Kanuni zake pamoja na kukamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, pamoja na Programu ya Maendeleo ya Utalii nchini. Kwa upande mwingine, Wizara itaendelea na jitihada za kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, utalii wa meli pamoja na kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Utalii wa Mikutano na Matukio ikiwemo kufanikisha ujenzi wa kituo cha kisasa cha kimataifa cha mikutano na matukio katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Uendelezaji wa mazao ya utalii nchini unaenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya kuongeza idadi ya watalii, wastani wa siku za mtalii kukaa nchini na mapato. Aidha, katika jitihada za kupanua wigo na kuongeza mapato ya Serikali, Wizara itaendelea kusajili

wakala wapya wa biashara za utalii nchini na kufanya uhakiki pamoja na ukaguzi kwa wakala wa biashara za utalii katika kanda nne (4) ikihusisha kanda za Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi.

**187. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara itaendelea kuchukua hatua za kuirejesha sekta ya utalii katika hali yake ya awali baada ya athari za COVID-19. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza Mpango wa Kurejesha Sekta ya Utalii katika Hali ya Awali (2020/2021 - 2024/2025) baada ya kutokea kwa janga la COVID-19. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka husika za Serikali pamoja na wadau katika utekelezaji wa Mwongozo wa kudhibiti maambukizi ya COVID-19 na kuimarisha vituo vya huduma za kiafya katika maeneo ya vivutio vya utalii vya kimkakati.

**188. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma za malazi nchini katika daraja za ubora - AserT kwa kuhamasisha watoa huduma za malazi na chakula nchini kutumia mfumo huo kutathmini ubora wa huduma zao. Aidha, Wizara itaendelea kuhakiki na kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora nchini kwa kuzingatia vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC. Sambamba na hilo, Wizara itawajengea uwezo wataalam wa ndani kuhusu namna ya kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa kazi hiyo nchini. Vilevile, katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu za watalii na taarifa za wageni wanaotumia huduma za malazi nchini, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za malazi katika mikoa 12 kuhusu namna ya kusajili wageni kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa *MNRT - Portal*.

**189. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wadau katika kuendeleza sekta ya utalii nchini kupitia jukwaa la majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na mikutano ya Kamati ya Uwezeshaji wa Masuala ya Utalii. Kwa upande mwengine, Wizara itaendelea kubaini maeneo ya fukwe, vivutio vya utalii na maeneo yenye

fursa za uwekezaji wa shughuli za utalii katika mikoa ya Mbeya, Simiyu, Njombe, Morogoro, Lindi, Tanga, Pwani, Mtwara, Rukwa na Ruvuma. Aidha, Wizara itaendelea kushiriki shughuli za mikutano na maonesho yanayolenga kuendeleza utalii.

#### **5.3.3.4 Bodi ya Utalii Tanzania - TTB**

**190. *Mheshimiwa Spika*,** mwaka wa fedha 2021/2022, Bodi itatumia mbinu mbalimbali kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi itaratibu na kushiriki maonesho ya utalii katika masoko ya msingi, kimkakati na yale yanayoibukia yakiwemo Marekani, Urusi, China, India, Australia, Israel, nchi za Bara la Ulaya ikiwemo Ujerumanu na Ufaransa, Falme za Kiarabu na Kanda ya Afrika.

**191. *Mheshimiwa Spika*,** utangazaji katika masoko ya kimataifa utaendelea kufanyika kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo: kuweka matangazo ya vivutio katika masoko ya kimkakati; kuandaa video maalum na machapisho kwa ajili ya vyombo vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii kulenga makundi mbalimbali ya masoko ndani na nje ya nchi; na kuandaa ziara za mafunzo (familiarization trips) kwa wakala wa utalii na waandishi wa habari wa kimataifa. Halikadhalika, mkazo utawekwa katika kuibua vivutio vipyta na kutangaza mazao ya utalii ikijumuisha utalii wa mikutano na matukio, meli, fukwe, malikale, ikolojia, jiolojia, michezo, madini na utamaduni kuititia *Cultural Tourism Programme* ambayo Wizara inaitekeleza kuititia Bodi ya Utalii. Aidha, Wizara itaanisha utalii mahsus wa lugha ya kiswahili (Swahili Tourism Package). Katika aina hii ya utalii, mtalii ataunganishiwa vifurushi mbalimbali vya utalii ambavyo vinaendana na lugha husika. Mathalan, mtalii atawenza kulipa mara moja na kuwezesheha kupata muda wa kujifunza lugha ya kiswahili kwa hatua ya awali; kununua bidhaa za Kitanzania (mfano vitenge, khanga na vinyago); na kuandaliwa matukio mbalimbali ya kiutamaduni yakiwemo ngoma na vyakula vya asili.

**192. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi kwa kushirikiana na Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi, itaendelea kutangaza utalii kwa kuandaa ziara za mafunzo kwa wanahabari na wakala wa utalii wa kimataifa; kutumia watu mashuhuri na mabalozi wa hiari wa utalii; na kuweka matangazo ya vivutio vyta utalii wa Tanzania kwenye masoko ya kimkakati katika nchi za nje. Vilevile, Wizara itaanzisha utaratibu wa kushindanisha Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi na kutoa motisha kwa Balozi zitakazofanya vizuri. Katika hatua nyingine, utangazaji utalii itaendelea kufanyika kwa kutumia makundi ya watu maarufu kama wanamichezo, wasanii wa muziki na filamu wa ndani na wa kimataifa. Aidha, Bodi itaendelea kuhamasisha wadau kutumia utambulisho wa utalii wa Tanzania wa *Tanzania, Unforgettable!*

**193. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi itaimarisha utangazaji utalii kwa njia ya kidijitali kwa kutumia studio maalum ya kufuatilia mienendo, mapendezi (likes) na maoni ya watalii, na kurusha taarifa na matangazo yenye ushawishi chanya kwa watalii katika masoko mbalimbali. Aidha, Bodi itaendelea kuimarisha matumizi ya tovuti ya kutangaza utalii ([www.tanzaniatourism.go.tz](http://www.tanzaniatourism.go.tz)) na matumizi ya mitandao ya kijamii ikiwemo *Twitter, Face Book, YouTube* na *Instagram*.

**194. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi itaendelea kutangaza utalii kupitia maonesho na matamasha mbalimbali yakiwemo: onesho la Kimataifa la Biashara - Dar es Salaam (Sabasaba); Maonesho ya Kilimo (Nanenane), Karibu - Kili Fair, Siku ya Utalii Duniani na Karibu Kusini; matamasha ya Majimaji na Siku ya Vimondo Duniani; *Rock city Marathon, Kili Marathon* na *Mbeya Tulia Marathon*. Maonesho mengine yatakayofanyika ni Tamasha la Mvinyo Dodoma, *Majimaji Selebuka Festival, East Africa Trade Fair* na *Lamadi Utalii Festival*. Katika hatua nyingine, Bodi itaandaa onesho la SITE. Aidha, Bodi itatoa elimu kwa umma kuhusu utalii wa ndani kupitia vyombo vyta habari ikiwa ni pamoja na chaneli maalum ya kutangaza utalii *Tanzania Safari Channel* na mitandao ya kijamii. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuweka mabango ya kutangaza utalii katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza na Mbeya.

### **5.3.3.5 Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT**

**195. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo na kudahili wanafunzi katika fani za ukarimu na utalii kwa ngazi za Astashahada na Stashahada kwa wanafunzi 1,537. Sambamba na hatua hiyo, Chuo kitatoa mafunzo kwa wadau 629 katika mnyororo wa utalii. Vilevile, Chuo kitanunua vitendea kazi na vifaa vyta mafunzo kwa vitendo katika kampasi zake zote nne (4) na kukarabati miundombinu katika Kampasi za Bustani, Temeke, Arusha na Mwanza. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuendelea kutafiti na kutoa ushauri katika fani ya utalii, ukarimu na uratibu wa matukio; na kuandaa mkutano wa pili wa kimataifa unaolenga kuboresha utoaji huduma katika sekta ya utalii na kuongeza miundombinu katika Kampasi ya Arusha.

### **5.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale**

#### **5.3.4.3 Idara ya Mambo ya Kale**

**196. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281; miongozo ya uhifadhi wa malikale, utafiti na uwekezaji; na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya malikale. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa malikale na urithi wa utamaduni kwa kanda tatu (3). Pamoja na hilo, Wizara itahakiki na kupima mipaka ya maeneo 15 ya malikale ikiwa ni mojawapo ya mkakati wa kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migogoro katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara itaratibu mikutano miwili (2) ya wadau kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya malikale. Pia, Wizara itaendelea kubaini maeneo ya malikale na kuyatangaza katika gazeti la Serikali ili kuyapa ulinzi kisheria.

#### **5.3.4.4 Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT**

**197. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika litaanza ujenzi wa Makumbusho ya Marais

itakayojengwa Jijini Dodoma; na litaweka onesho la Kudumu la Tembo katika Makumbusho ya Elimu Viumbe Arusha. Aidha, Shirika litaendelea kuhifadhi na kuendeleza urithi wa malikale na mikusanyo kwa kujenga stoo moja (1) na kukarabati stoo nne (4) za mikusanyo. Villevile, Shirika litaendelea kushirikisha wadau katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya malikale. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea kutangaza vivutio vya malikale na makumbusho ili kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutumia matukio, maonesho na matamasha mbalimbali. Sambamba na hilo, Shirika litafanya tafiti, kukusanya na kuhifadhi mikusanyo ya asili na kiutamaduni, kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji wa makumbusho mpya kwa watu na taasisi binafsi. Pia, Shirika litaendeleza programu mbalimbali za kutoa elimu ya historia na uzalendo nchini kwa kufungua klabu 220 katika mikoa ya Morogoro (40), Dar es Salaam (100), Dodoma (40) na Singida (40).

#### **5.3.4.5 Mfuko wa Mambo ya Kale - NAF**

**198. *Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mfuko utawezesha ukarabati wa jengo la Mwl. Nyerere Mikindani; na uandaaji wa miongozo ya utafiti na uwekezaji katika maeneo ya malikale. Aidha, utawezesha kazi ya kubaini maeneo ya malikale na urithi wa utamaduni na kuweka jira nukta katika maeneo 20 yaliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#### **5.4 Miradi ya Maendeleo**

**199. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 152,772,880,000** kutekeleza miradi nane (8) ya Idara na miradi itakayotekelozwa na taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 38,879,696,000** zitatoka kwa Washirika wa Maendeleo (Fedha za Nje) na **Shilingi 113,893,184,000** zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Fedha za Ndani), sawa na asilimia 74 ya fedha zote za maendeleo. Fedha za maendeleo **Shilingi 152,772,880,000** zinajumuisha **Shilingi 40,079,696,000** kwa ajili ya miradi itakayotekelozwa na Idara mbalimbali ndani ya

Wizara na **Shilingi 112,693,184,000** za Miradi itakayotekelawa na Taasisi (TANAPA, NCAA na TAWA).

**200. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itatekeleza miradi nane **(8)** ya maendeleo kama ifuatavyo: -

- Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Nyanda za Juu Kusini - REGROW;
- Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili;
- Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara;
- Mradi wa Panda Miti Kibiashara;
- Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki;
- Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki - BEVAC;
- Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu - FORVAC; na
- Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio - MICE.

## **6.0 SHUKRANI**

**201. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutumia nafasi hii tena kuwashukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Pia, ninawashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee, nizishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, taasisi za kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi.

Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi za Kimataifa ni pamoja na: AfDB, AWF, AWHF, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. Aidha, ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Ninatoa rai kwa wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Ni matumaini yangu kuwa kupitia ushirikiano huu malengo ya uhifadhi yatafikiwa kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

## **7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022**

**202. Mheshimiwa Spika**, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 571,632,424,000** kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 418,859,544,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 152,772,880,000** ni za miradi ya maendeleo.

**203. Mheshimiwa Spika**, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 153,537,684,000** za mishahara na **Shilingi 265,321,860,000** za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 113,893,184,000** fedha za ndani na **Shilingi 38,879,696,000** fedha za nje.

## **8.0 HITIMISHO**

**204. Mheshimiwa Spika**, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: [www.maliasili.go.tz](http://www.maliasili.go.tz)

**205. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa kabla sijamwita Mwenyekiti kuja kusoma maoni ya Kamati, nilete kwenu tangazo ambalo tulikuwa hatujamaliza... (*Makof!*)

Jamani hizo ni ishara kwamba mambo ni mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nawataja wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kutoka Jijini Dar es Salaam na nilisema wameongozwa na Ndugu Zarina Hassan ambaye ni Balozi wa Hiyari wa Utalii. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, wengi mniamfahamu kwa jina la *Zari the Boss Lady*. Sasa usimame Zari, Wabunge wakuone Balozi wa Hiyari. Huyu ndiye mzazi mwenzie na *Diamond Platinumz*. Kwa hiyo, naamini watashirikiana vizuri kuhakikisha vivutio vyetu vya utalii vinajulikana na pia wanatuletea watalii wengi, kwa sababu hawa watu huwa wanaambatana na watu wengi. Kwa hiyo, hata ye ye kuwepo tu hapa Dodoma, jamani Dodoma mmetembelewa. (*Makof!*)

Hayam ye ye ameongozana na Aneth Charity Ruthsas, sijui ndiyo yupi? Haya karibu sana. Yupo pia Onesmo Amos, karibu sana; yupo pia Ashrafu Lukamba, karibu sana. Huyu Lukamba ndio yule mpiga maarufu sana? Aah, haya, sawa jamani na mpiga picha wake amekuja hapa. (*Makof!*)

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani ambaye ni Waziri wa Nishati ambao ni Wawakilishi wa Balozi wa Norway; na hawa ni Ndugu Romsloe Borge na Ndugu Neema Shayo. Sijui wamekaa upande gani hawa? Haya. (*Makof!*)

Wapo pia wageni 20 wa Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni Viongozi wa

Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa, Ndugu Ellen Bogohe. Karibuni sana viongozi wetu wa Umoja wa Wanawake kutoka Mwanza. (*Makofii/Vigelegele*)

Tunao pia wageni 64 wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambaa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimboni Mbozi, Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Ndugu Allan Mwawalo. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 24 wa Mheshimiwa Issa Mtemvu ambaa ni Wenyeviti, Makatibu wa Hamasa wa UVCCM kutoka Jimbo la Kibamba, Ubungo, Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mke wa Mheshimiwa ambaye ni Ndugu Halima Mkinywa. Karibuni sana. Mke wa Mheshimiwa Issa Mtemvu ndio yupi? Eeh, karibu sana wifi yetu na shemeji yetu. Mheshimiwa Issa Mtemvu yuko salama kabisa humu ndani, usiwe na wasiwasi. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ambaa ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Ambwene Yessaya (AY) na Ndugu Nifasha Alloys. Sijui wamekaa sehemu gani hawa? Aah, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sijui na hawa Mheshimiwa Waziri ana mpango wa kuwapa ubalozi ama vipi, lakini simfahamu sana Ndugu Nifasha Alloys, lakini Ambwene Yessaya anatuwakilisha vizuri kwenye muziki. Tunakushukuru sana kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Stella Ikupa, ambaye ni Mtumishi wa Mungu kutoka Jijini Dar es Salaam na huyu ni Ndugu Frank Muvinga. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambaa ni Wafamasia wa sekta binafsi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mfamasia Gervace Mwalla. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Asia Halamga ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jijini Dodoma ambao ni Ndugu Josepha Madulu, Ndugu Eliya Janikila na Ndugu Ibzan Ruheta. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Minza Mjika ambao ni familia yake kutoka Jijini Arusha wakiongozwa na mtoto wake Ndugu Maulu Emmanuel. Karibu sana (*Makofi*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni viongozi wapya wa *Pharmaceuticals Society of Tanzania*. Hawa ni Wafamasia kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na; hee, sasa hapa ndani Waziri sijui alisemaje kuhusu matumizi ya neno Rais; lakini wakiongozwa na Rais wao Mfamasia Fadhili Hezekiel. Karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimepewa taarifa hapa kwamba kuanzia siku ya tarehe 10 mpaka tarehe 16 Juni, 2021 Wafamasia watakuwa na kongamano kuelezea wananchi matumizi sahihi ya dawa za binadamu. Kwa hiyo, hawa ndio viongozi na nafikiri Waheshimiwa Wabunge kongamano hilo litakuwa ni muhimu sana kushiriki ili sisi wenyewe tufahamu matumizi sahihi ya dawa, lakini pia tuweze kuwaelimisha wananchi wetu wasinywe dawa kabla hawajaandikiwa na daktari. (*Makofi*)

Tunao pia Wageni 11 wa Mheshimiwa Joseph Kamoga ambao ni Wana-Ludewa wanaoishi Dodoma wakiongozwa na Ndugu Lumuli Mtake. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Judith Kapanga ambaye ni mchambuzi binafsi wa Kimataifa wa masuala ya kiuchumi kupitia *BBC, OW, VOA, TBC1, ITVna Azam TV*, Ndugu Walter Nguma. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 32 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni Wajumbe wa Baraza la UVCCM Mkoa wa Mwanza, wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa, Ndugu Jonas Lufungulo. Karibuni sana vijana kutoka Mwanza. Huyu

Mheshimiwa Ng'wasi Kamani anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. Kwa hiyo, vijana wa Mwanza mlileta chuma kabisa hapa. (*Makof*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanaotoka Tarime Mkoa wa Mara wakiongozwa na Ndugu Elphaz Sylvester. Sijui wamekaa upande gani? Karibuni sana vijana kutoka *UDOM*. (*Makof*)

Pia tunao wageni walio tembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni wawili kutoka *Dar es Salaam Institute of Technology* walio tembelea Bunge kwa ajili ya kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi na linavyoendesha shughuli zake; na hawa ni Meneja Mradi wa Gesi Asilia, Dkt. Esebi Nyari na Meneja Masoko Ndugu Benjamin Kamtawa. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, bila shaka hawa ndio walioleta gari lile ambalo linatumia gesi asilia. Kwa hiyo, twende tukalitazame wote hapo ili tuone namna ya kubadilisha magari yetu tuanze kutumia huo utaratibu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa kutosha humu ndani leo. Tunao wageni wengine ambao ni wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja; na hawa ni Ndugu Aron Muhoja ambaye ni mume wa Mheshimiwa Mbunge. Simama kwanza shemeji wa Wabunge, wanataka wakuone vizuri. Nashukuru sana. Kama ulivyoona hapa, naona mkeo anafanya kazi nzuri Wizarani, alikuwa anafanya yanayompasa humu ndani. Pia wameongozana na Ndugu Grace Masanja, Ndugu Celina Mango na Ndugu Tabu Masanja. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine linalotoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* na huyu ni Mheshimiwa Abbas Tarimba, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho siku ya Jumamosi tarehe 5 Juni, 2021 saa 10.00 jioni kwenye Uwanja wa Jamhuri hapa

Dodoma kutakuwa na mechii ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*), mpira wa miguu. Sasa hii *Bunge Sports Club* wote mnafahamu inaitwa *Ndugai Boys*. Kwa hiyo, huwa hawatoki bila magoli; na hapa Mheshimiwa Spika alisema *TBC* wajiaandae kwa magoli matatu. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kwenye mchezo huo ambaa Mheshimiwa Gwajima, japo sijamwona kwenye mazoezi, lakini naamini atakuwa sehemu ya hii Ndugai Boys kwa sababu alikuwa anacheza huko zamani. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, pia kutakuwa na mechii ya *Bunge Queens* na Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo. Huu ni mpira wa pete. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. Huu sitaki kuusemea sana kwa sababu mimi ndio nyota mwenyewe wa *Bunge Queens*. Kwa hiyo, mje mtazame. Hapa naambiwa *goalkeeper* lakini kwa kweli naona kuna mtu anataka kunisaidia kutoa matangazo huko, lakini tuko vizuri, tutawatoa kimasomaso Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi, mje mwangalie tunafanya mazoezi vizuri. (*Kicheko/Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratibu yetu.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Kwezi aje awasilishe maoni ya Kamati.

Naona Maliasili mmeanza kutoa funzo jipya humo ndani; vizuri sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Au ni jambo mljadili kwenye kamati hili? (*Kicheko/Makofii*)

Karibu utusomee maoni ya Kamati.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuwasilisha

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uhai alionijalia mimi pamoja na Wabunge wote wanaofuatilia wasilisho hili katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili. Kabla ya kuondelea kutoa maoni, nitangulie kuomba kuwa taarifa yote iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ina sehemu tatu ambapo Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili ni Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Sehemu ya Tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati na Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020; Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii na kushughulikia Bajeti za Wizara hiyo. Uchambuzi wa Bajeti ilitanguliwa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha

2020/2021. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 114. Kati ya fedha hizo, shilingi billioni 69.6 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi billioni 45 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 700 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 44 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara hii yanapatikana ukurasa wa pili wa taarifa ya Kamati kwenye Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hususan za miradi ya maendeleo unakwamisha juhudzi za Wizara kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa muda unaopangwa. Aidha, kutokupatikana kwa fedha za nje za miradi ya maendeleo ambayo ndiyo bajeti kubwa dhidi ya fedha za ndani, kumekwamisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uhifadhi. Jedwali limeambatanishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Idara mbalimbali za Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na taasisi na mifuko iliyochini ya Wizara hiyo ziliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 65. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara hii ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 23.4, sawa na asilimia 36 ya malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba kiwango hicho ni pungufu kwa takribani shilingi bilioni 26.9 ukilinganisha na makusanyo ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 50.4. Upungufu huo ilitokana na changamoto ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu (*COVID-19*) yaliyoikumba Tanzania na dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, mashirika ya uhifadhi chini ya Wizara ambayo ni *TANAPA*, *TAWA*, Ngorongoro na *TFS* yaliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 738 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya hifadhi zetu. Hadi kufikia Machi, 2021 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni

165, sawa na asilimia 22.4 ya malengo waliyojiwekea. Kamati inahoji uhalisia wa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kama ulifanyika kulingana na hali halisi kwa kuwa tofauti ya ukusanyaji na makadirio ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Kamati iliweza kushuhudia utekelezaji wa mikakati mbalimbali iliyowekwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto ya Ugonjwa wa *Corona* ilipotembelea maeneo mbalimbali ya utalii wakati wa ukaguzi wa miradi. Hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuwa na mikakati endelevu ya kukabiliana na Ugonjwa wa *Corona*. Majedwali Na. 2 na Na. 3 yana taarifa kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepata tafsiri kwamba, ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA* ni wa kusuasua na kwamba Taasisi hizi zimeathirika sana na tatizo la Ugonjwa wa *COVID-19* uliyoikumba dunia na Taifa kwa ujumla. Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa Taasisi za *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA* zitasimamia vyema mikakati ilizojiwekea katika mwaka 2021/2022 ili kuweza kufikia lengo la makusanyo waliojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza *TFS*kwa kufanya vizuri katika ukusanyaji wa maduhuli. Ni maoni ya Kamati kuwa Taasisi nyingine za Wizara hii zitasimamia mikakati waliyojiwekea ili kufikia malengo ya ukusanyaji maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Mikoa ya Iringa na Mbeya kuanzia tarehe 12 hadi tarehe 15 Machi, 2021. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kulikuwa na Mradi wa *REGROW* ambao unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Mradi huu ni wa miaka sita na ulianza Desemba, 2017 na unatarajiwaa kukamilika Desemba, 2023. Lengo kuu la mradi huu ni kufungua fursa za vivutio vilivyopo katika ukanda wa kusini mwa Tanzania kwa

kutekeleza mradi wa kuendeleza baadhi ya maeneo muhimu yenye vivutio ili kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii kwenye uchumi na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unatekelezwa katika Hifadhi za Taifa za Mikumi, Ruaha, Udzungwa na Nyerere. Kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 shilingi bilioni 30.4 ziliidhinishwa ili kutekeleza mradi huo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 200 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 30.2 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi wakati Kamati inakagua mradi huu, shilingi bilioni 4.5 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwenye mambo kadhaa ikiwemo usimamizi na uboreshwaji miundombinu katika maeneo ya kipaumbele ya kuendeleza utalii, ununuzi wa mitambo, ununuzi wa malori na vifaa vingine kwa ajili ya matengenezo ya barabara na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na miradi inayotekelzwa kupitia mradi wa *REGROW*, Kamati ilibaini kwamba changamoto kubwa inayoikabili Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni Barabara itokayo Iringa Mjini kuelekea ndani ya Hifadhi ya Ruaha pamoja na Ruaha yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilibaini kwamba Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ina vivutio vingi vya kitalii wakiwemo wanyamapori na ndege ambao hawapatikani katika hifadhi nyininge Tanzania na Afrika kwa ujumla. Changamoto iliyopo ni kutojulikana kwa hifadhi kwa Watanzania walio wengi na dunia nzima. Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kutenga bajeti inayotosheleze katika kutangaza utalii wa ndani na nje ya nchi, hususan kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa pili uliotembelewa ni Mradi wa Panda Miti Kibiashara. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi katika Mkoa wa Iringa. Mradi huu ni ubia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ufini (*Finland*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu ni *Euro* milioni 9.8, sawa na shilingi bilioni 26.6. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 25 zitatolewa na Serikali ya Ufini na shilingi bilioni 1.2 zitatolewa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu una lengo la kuchocha maendeleo endelevu na jumuishi katika sekta ya misitu na mnyororo mzima wa thamani ili kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya mradi, makundi mawili yanahusisha wakulima wadogo wa miti walioanzisha na kutunza mashamba yao na wajasiriamali wadogo na wa kati wanaoanzisha na kuboresha biashara zao zinazotokana na mazao ya misitu ambayo yamejumuishwa katika mradi katika hatua zote za awali za mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 mradi uliidihi nishiwa kutumia shilingi bilioni 6.3. Hadi kufikia Machi, 2021, kiasi cha shilingi bilioni 3.2 kimetumika katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi ikiwemo utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi huu Wizara imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda mbalimbali, kuboresha hali ya mazingira na mandhari, kuhifadhi ardhni na vyanzo vya maji, kujenga misingi ya ajira zinazotokana na kazi mbalimbali na kuwa chanzo cha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni kuchelewa kupata misamaha ya kodi kwa vifaa vilivyotolewa kama msaada na kuiingizwa nchini kutopteka na taratibu za upatikaji wa msamaha huo; pili, mlipuko wa Ugonjwa *COVID-19*; changamoto hii ilichelewesha kuanza kwa mradi na

manunuzi ya vipuri na vifaa vya mafunzo; na tatu upatikanaji wa eneo kwa ajili ujenzi wa kituo cha mafunzo. Kwa sasa mradi upo katika eneo la mtu binafsi na inaugharimu mradi takribani *Euro* 3,000 kwa mwezi kwa ajili ya kulipia pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati ilishauri Serikali kutoa msamaha wa kodi mapema na *TFS* kutenga eneo litakalotumika kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Upasuaji Miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu bajeti husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa namna ambavyo ilizingatia kikamilifu ushauri wake katika baadhi ya maeneo. Ni maoni ya Kamati kwamba maeneo ambayo Serikali inaendelea kuyazingatia yafanyiwe kazi kwa haraka ili kuweka mazingira mazuri ya utalii na uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022; Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii imepanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 65 kutoka katika idara mbalimbali, taasisi na mifuko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba makadirio haya ni pungufu kwa shilingi bilioni sita, sawa na asilimia 8.8 ukilinganisha na

Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa shilingi billioni 71.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mashirika na taasisi za uhifadhi ambayo ni *TANAPA*, Ngorongoro, *TAWA* na *TFS*, Wizara inakusudia kukusanya shilingi bilioni 478. Makadirio haya ni pungufu ya asilimia 22 ya makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa ni shilingi bilioni 738.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya hali ya Ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu (*COVID-19*) kuathiri sekta ya utalii duniani kote, ni dhahiri kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 yanaweza yasifikasiwe. Hivyo basi, Wizara inashauriwa kusimamia mikakati na mipango endelevu iliyojewekea katika kukabiliana na Ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu ili makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ya taasisi na mashirika ya uhifadhi yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 418 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha inayoombwa, shilingi bilioni 153.5 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 265 inaombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake, imebaini kwamba bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa shilingi bilioni 265.3, sawa na asilimia - 381, ukilinganisha na bajeti ya shilingi bilioni 69.6, sawa na asilimia 26 kwa matumizi kama hayo katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko hilo kubwa sana na limetokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni Taasisi za *TAWA*, *TANAPA* na Ngorongoro kujumuishwa katika Bajeti ya Serikali kuititia Wizara ya Maliasili na Utalii; pili, kujumuisha katika Bajeti ya Serikali taasisi zilizokuwa zinapata bajeti zake kutoka 3% za mapato ghafi ya *TANAPA* na Ngorongoro; na tatu,

kuanzishwa kwa Idara ya uratibu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu (Jeshi Usu) ambalo limeanza kutengewa bajeti kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, kwa kuwa Serikali ilifanya uamuvi wa kuzileta pamoja Taasisi za TANAPA, TAWA na Ngorongoro katika bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ni imani ya Kamati kuwa Serikali imejipanga kuzisimamia ipasavyo taasisi zilizo chini yake na kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 152.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwaa, shilingi bilioni 38 ni fedha za nje, na shilingi bilioni 113 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Mpango wa Maendeleo inaongezeka kwa shilingi bilioni 107.8, sawa na asilimia 86, ukilinganisha na bajeti ya shilingi bilioni 45 ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, katika bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani ni ongezeko la shilingi bilioni 113.1 ukilinganisha na bajeti ya maendeleo ya shilingi milioni 700 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kutenga fedha nydingi kutoka vyanzo vya ndani dhidi ya nje, kwa kuwa taarifa zimeonesha fedha za nje za miradi ya maendeleo zimekuwa hazipokelewi na Wizara kwa kiwango kinachotakiwa, hivyo kuathiri maendeleo ya miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2021/2022, Kamati imepata tafsiri kuwa kama fedha zilizotengwa zitatolewa kwa wakati na Wizara kusimamia vema utekelezaji wa miradi iliyopo na inayoendelea, ni maoni ya Kamati kuwa Wizara itaonesha matokeo chanya katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ni maoni ya Kamati. Kwanza ni mwenendo wa bajeti na upatikanaji wa fedha. Kwa kuwa, kumekuwepo na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo, katika bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, jambo ambalo limesababisha Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kusimamia sekta nzima ya Maliasili na Utalii, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge inatolewa kwa wakati na kwa kiasi kinachotosheleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kufanya hivi, Wizara itakuwa na uwezo wa kupanga kulingana na vipaumbele vyaa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni makusanyo ya maduhuli katika sekta ya utalii. Kwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kumekuwa na changamoto kubwa katika ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara na taasisi zake, kutokana na changamoto hiyo kumesababisha kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na namna ya taasisi hizo kuijendesha zenyewe; Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(1) Wizara kuititia taasisi na idara zake ziwawekee malengo, (*target*) Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizochini yake kwa maana ya kila robo, na malengo hayo yawe ndiyo kipimo cha utendaji kazi wao;

(2) Wizara ibuni mikakati endelevu ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo kushirikiana na Wizara ya Elimu, TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu, katika kuratibu namna bora kupata watalii wengi wa ndani hususan Wabunge, taasisi na idara mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali, mikoa na Halmashauri za Wilaya zote, vyuo, wanafunzi wa Sekondari na Shule za Msingi.

Aidha, Wizara kuainisha changamoto zilizopo katika utaratibu uliopo wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara na kuziwasilisha katika Kamati kwa ajili ya kutolea mapendekezo;

(3) Kwa kuwa mlipuko wa *COVID-19* umeathiri kwa kiasi kikubwa utalii wa kutoka nje, Kamati inaishauri Serikali kuimarishe utalii wa ndani kwa kutangaza vivutio vya utalii wa ndani, kuanzisha kitengo cha utalii katika kila wilaya ili kiweze kuratibu masuala ya utalii wa ndani na kuelimisha Umma wa Tanzania kuwa utalii siyo kwa wageni tu. Hatua hii itasaidia kuongeza makusanyo ya maduhuli na kufikia lengo; na

(4) Serikali kuchukua hatua za ziada ili kuvutia watalii kutoka nje ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na Ugonjwa wa *COVID-19*, kama uvaaji wa barakao na upimaji wa Virusi vya Corona kwa hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ni shilingi bilioni 152.7 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ukiilinganisha na mwaka 2020/2021 bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii ilikuwa shilingi bilioni 45 bila uwepo wa taasisi; na kwa kuwa ongezeko hilo ni kutokana na Taasisi za TANAPA, Ngorongoro na TAWA kujumiushwa katika bajeti ya Serikali, ni maoni ya Kamati kuwa Wizara haijajipanga vema kuratibu shughuli za usimamizi wa miradi ya maendeleo hususan katika maliasili, malikale na uhifadhi, ili kuendana na llani ya Chama cha Mapinduzi Sura ya Pili (uk. 110-115).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya miradi ya maendeleo ya Wizara ili kusaidia Wizara hii kuratibu vema mikakati ya usimamizi wa maliasili na kuondoa migogoro inayoendelea katika hifadhi zetu kati ya wanyamapori wakali na binadamu pamoja na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya utalii, ni maoni ya Kamati kuwa kwa kipindi kirefu Wizara imejikita katika kutangaza utalii wa wanyama zaidi kuliko vivutio vingine vya utalii kama utalii wa fukwe (*marine tourism*), utalii wa malikale (*traditional tourism*), utalii wa misitu (*forest tourism*) na utalii wa nyuki (*api tourism*). Hali hii imesababisha Serikali kupoteza mapato mengi kutoka

kwenye vyanzo ambavyo vikiwekeza na kusimamiwa vizuri vitaongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kamati imebaini uwepo wa changamoto katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za utalii hapa nchini kama vile hoteli kuwa na bei kubwa, mikataba kwa wafanyakazi, waongoza utalii na wapagazi isiyordhisha. Ili kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa shughuli za utalii hapa nchini, Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo:-

(1) Serikali kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Utalii hapa Nchini. Mfano, kuhuisha Bodi ya Utalii kuwa Mamlaka ya Kusimamia Utalii Tanzania (*Tanzania Tourism Regulatory Authority*). Kuanzishwa kwa mamlaka hii kutaleta uwiano mzuri katika uendeshaji wa shughuli za utalii ikiwemo udhibiti wa bei na tozo mbalimbali za huduma ya utalii;

(2) Serikali ianzishe kitengo maalumu cha biashara (*Special Business Wing*) ndani ya Wizara, ambacho kitajikita katika kuandaa modeli za kibiashara (*business models*), pamoja na kuunganisha (*harmonization*), mikakati ya kiutalii kutoka kwa TAWA, NGORONGORO, TANAPA na TFS. Kwa kufanya hivyo, kutapelekea kuwepo kwa mikakati ya pamoja (*Single Tourism Strategy*) kwa kutangaza utalii wa ndani na nje kwa taasisi zote;

(3) Juhudi za kutangaza vivutio vya Utalii iongezwe kupitia michezo kwa kutumia wachezaji maarufu, vyombo vya habari vya Kimataifa kwa mfano, CNN, DSTV, Aljazeera na BBC. Aidha, Wizara kuweka mikakati endelevu ya kutangaza utalii wa ndani (*Domestic Tourism*) hususan vivutio vya malikale ili viweze kujulikana;

(4) Wizara Kupitia Idara ya Malikale ifanye tathmini ya vivutio vya kitalii katika mikoa yote nchini ikiwemo visiwa ambavyo kwa sasa havitumiki kama utalii na vingeweza kutumika katika utalii sanjari na kuweka mikakati ya kuviendeze ili vitumike kutangaza utalii wa ndani;

(5) Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuendelea ihai kishe inajikita katika kuimarisha miundombinu ya barabara, mawasiliano ya simu, *canteen* na *hostels* zilizomo ndani ya hifadhi zetu. Kwa kufanya hivyo kutasaidia hifadhi zetu ziweze kufikika na kuhudumia watalii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi wa *REGROW* unatekelezwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, mradi huo ulianzishwa rasmi Desemba, 2017 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2023 na kwa kuwa mradi huu utakuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza hifadhi zetu, kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Wizara kuweka mkakati wa namna ya kuendeleza Mradi wa *REGROW* baada ya wafadhili wa nje kukamilisha ufadhili wao;

(ii) Wizara kutenga bajeti itakayowezesha ukarabati wa barabara zilizomo ndani ya Hifadhi ya Ruaha ili kuwezesha watalii kufika eneo hilo ikiwa ni pamoja na wizara kufanya mazungumzo na Wizara ya Miundombinu ili kupata kipaumbele cha ujenzi wa barabara inayotoka Iringa Mjini kwenda Hifadhi ya Ruaha. Ni maoni ya Kamati kuwa kukamilika kwa ujenzi wa barabara hii kutasaidia ongezeko la watalii katika Hifadhi ya Ruaha na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA*. Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza idadi kubwa ya hifadhi kutoka 16 hadi 22. Kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya sita, ni hifadhi tano5 tu kati ya 16 zilizokuwa zina uwezo wa kuijiendesha zenyewe na kuzalisha ziada inayosaidia kuendesha Hifadhi za Taifa nyingine 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali ya kifedha ya shirika kwa sasa na taratibu zilizopo za ukusanyaji wa maduhuli sanjari na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, ni maoni ya Kamati kuwa shirika hili litashindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Jambo

litakalosababisha kudhoofisha shughuli za utalii. Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Kuweka utaratibu wa Taasisi ya *TANAPA* kupata fedha za kujiendesha kwa wakati na kwa ukamili. Mfumo uliopo sasa unafanya *TANAPA* kuwa na mazingira magumu ya kibiashara kwakuwa matumizi madogo madogo ya taasisi hiyo yatalazimika kusubiri pesa kutoka Hazina ili kutekeleza, ambapo mlolongo wake ni mrefu ambao unaweza kuathiri ufanisi wa biashara ya Utalii; na

(ii) Ni kuimarisha Chuo cha Utalii nchini kwa kuanzisha kampasi kikanda, hatua hii itasaidia kasi ya kuongeza idadi ya vijana wengi kusomea fani ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, miradi inayotekelze na Wakala wa Misitu (*TFS*) imetoea matokeo chanya na mafanikio makubwa kiuchumi na kwa upande wa uhifadhi wa mazingira mfano shamba la miti *Sao Hill*. Kamati ilielezwa kuwa, shamba hili linachangia wastani wa 35% ya pato la *TFS* kwa mwaka. Aidha, *Sao Hill* kwa miaka mitano, kuanzia 2015 mpaka 2020 imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 216.3 sawa na wastani wa bilioni 43 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kumekuwepo na changamoto kubwa ya uharibifu wa misitu hasa inayomilikiwa na vijiji na Halmashauri za Wilaya, hali iliyopelekea Kamati hii kuishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa na Wizara, ilionyesha kwamba mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu (*TFS*) kuwa Mamlaka umeanza kwa kukusanya taarifa na kuandaa andiko litakalopelekwa ngazi za juu kwa maamuzi; na lengo la uamuza huu ni kuanzisha mamlaka moja itakayokuwa na nguvu za kisheria za kudhibiti matumizi ya rasilimali zote za misitu nchini, bila kujali umiliki wake. Kamati inashauri Serikali kuharakisha zoezi hili na kulitaarifu Bunge kwa hatua zitakazochukuliwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti lijalo;

(ii) Kwa kuwa rasilimali za misitu zinazosimamiwa na wadau mbalimbali na usimamizi umegawanyika katika makundi mbalimbali hali iliyochangia kuwepo kwa migongano na mwingilio kwa majukumu ya usimamizi kati ya *TFS* na *TAMISEMI* kwa maana ya vijiji na wilaya, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione uharaka wa kuanzishwa mamlaka moja ya kusimamia Sekta ya Misitu ili kuleta ufanisi;

(iii) *TFS* ina utaratibu wa kutoa fedha kwa vikundi kwa ajili ya kusaidia kuhamasisha mradi wa kupanda miti kibiashara, kwa kuwa fedha hizo zinaonyesha matokeo chanya na kuendeleza kwa mradi huo, kamati inashauri fedha hizo zitolewe kwa mfumo wa *Revolving Fund* ili kusaidia ongezeko la upandaji miti katika Taifa hususan katika maeneo yenye mradi huo.

(iv) Kupitia *TFS* ifanye tathmini ya aina ya miti inayofaa katika mikoa yote nchini na kiasi cha miti inayohitajika. Tathamini hiyo ifanyike kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Mikoa;

(v) Aidha, *TFS* waongeze kasi ya kupanda miti kibiashara katika maeneo mbalimbali nchini hasa maeneo ya pande ya Dodoma, Singida, Manyara na Shinyanga ili kuhifadhi mazingira na kuongeza pato la Taifa;

(vi) Kwa kuwa kanda ya kusini ndiyo inayoongoza kwa kuwa na miradi mingi ya miti ya mbao hapa nchini; na kwa kuwa hadi sasa hakuna chuo mahususi kwa masuala ya misitu na mbao ukanda wa kusini; ni maoni ya kamati kuwa Serikali ianzishe Kampasi ya *Forest Industries Training Institute* katika mikoa inayolima miti kwa wingi mfano, Mbeya, Iringa na Njombe. Kwa kufanya hivyo, itasaidia wakulima wa misitu na wawekezaji wa misitu kunufaika na huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa maoni yafuatayo kwenye Sekta ya Nyuki;

(i) Kutoa kipaumbele kwa kuwekeza katika Sekta hii kwa kutoa elimu kwa wafugaji, upatikanaji wa mizinga ya

kisasa pamoja na uanzishwaji wa viwanda vyta kuchakata mazao ya nyuki. Kwa kufanya hivyo itasaidia kuongeza ajira na pato la Taifa.

(ii) Kuanzisha mamlaka moja ya kusimamia Misitu na Nyuki nchini. Kuanzishwa kwa mamlaka hiyo ni hitaji la kisera la kupambana na changamoto za Sekta ya Nyuki na Misitu, lakini pia ni hitaji la Ibara ya 69 ya llani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020.

(iii) *TAWA* tangu ianze kutekeleza majukumu yake mwaka 2016, imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kuimarisha uhifadhi kunakotokana na kupunguza ujangili, kudhibiti vitendo vyta uingizaji na ulishaji wa mifugo katika mapori mbalimbali na mapori tengefu. Aidha, kupitia *TAWA* tunalo Jeshi USU.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati imeshauri Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Wizara ifanye tathmini na kuona iwapo kuna uwezekano na ulazima wa kuanzishwa kwa Sheria mahsusii kuiwezesha *TAWA* kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, tathmini hiyo ibainishe maeneo ya kisera, kisheria na kibajeti ambayo yanaweza kuathiri kutokana na mapendekezo ya tathmini;

(ii) Wizara ibuni mkakati endelevu wa kuthibiti mapema uvamizi wa maeneo ya hifadhi. Mfano, kuwa na mpango kabambe na jumuishi kwa jamii zinazozunguka hifadhi (*participatory Wildlife-Human Conflict Management Program*), pamoja na wadau wa maendeleo na asasi za kiraia kuliko kusubiri maafa na shughuli mbalimbali za kilimo na ufugaji kushamiri ndipo hatua zichukuliwe. Kwa kufanya hivi kutapunguza kuchukua hatua za matukio na migogoro iliyopo sasa kati ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi na Wanyama Waharibifu; (*Makof*)

(iii) Wizara kutumia technolojia katika kutambua dalili za uvamizi wa wanyama hasa katika maeneo yaliyo na

mitandao na kutoa taarifa haraka pale panapotokea uvamizi sanjari na kuainisha maeneo yote yenyeshoroba na kuwaelimisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo juu ya kutoyaharibu na kuyavamia.

(iv) Wizara iweke mkakati endelevu wa kuvuna mamba kwenye mikoa ambayo imekumbwa kwa kiasi kikubwa na mamba ambayo inaleta madhara kwa wananchi kuliwa. Kwa kufanya hivyo kutasaidia kulinda usalama wa wananchi, lakini pia kuwapa wananchi uhuru wa kufanya shughuli zao za kiuchumi.

(v) Kuhusu uvamizi wa mifugo katika hifadhi na adhabu zinazotolewa linahitaji mjadala mpana ikiwa ni pamoja na wafugaji kuelimishwa kuacha kuchunga mifugo yao kiholela na kuanza kufuga kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika Uwindaji wa Kitalii; kuanzia mwaka 2017 Sekta ya Utalii imepata mtikisiko mkubwa baada ya Serikali kufuta leseni za umiliki wa vitalu vya uwindishaji wa wanyamapori. Hali hii imesababisha wamiliki wengi kurudisha vitalu na sababu za vitalu vingi kuwa wazi. Aidha, mfumo wa ugawaji wa vitalu kwa njia ya *administrative leasing* ilichangia kwa kiasi kikubwa uwepo wa mazingira ya rushwa katika ugawaji wa vitalu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na mfumo wa ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada. Hata hivyo, kamati inaishauri Serikali kuboresha mfumo huo wa vitalu ili vitalu vyote viweze kunadiwa na kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kupata Fidia za Mjusi aliyepo Ujerumani. Kamati inatambua juhudimbalimbali zinazofanywa na Bunge lako Tukufu na zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali kuhusu mjusi Dinosaria aliyeko Berlini Ujerumani. Hata hivyo, juhudihizo hazijaunganishwa pamoja ili kupata msimamo wa Serikali unaoratibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mambo ya Kale. Kamati inaona pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Wajumbe waliotumwa kufuatilia masalia hayo mwaka 2010, Kamati inaishauri mambo yafuatayo:-

(i) Juhudi zilizozofanywa na wadau mbalimbali ziunganishwe pamoja na kupata msimamo wa Serikali kuhusu masalia ya Dinosaria aliyepo ujerumani.

(ii) Kuwepo na Mpango kazi mahususi (*Plan of Action*) wa lini wazo hili litatekelezwa, kwani limechukua muda mrefu tangu lianze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mapitio ya Sheria; ni maoni ya Kamati kuwa Sera ya Utalii 1999, Sera ya Misitu 1998 na Sera ya Ufugaji Nyuki 1998 zimepitwa na wakati kwa kuwa ni za muda mrefu sana. Vilevile Sheria ya Malikale Na. 2 ya Mwaka 1964 iliyofanyiwa marekebisho 1979 imepitwa na wakati. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuitia upya sera na sheria hizi ili ziletwe, ziweze kukidhi azma ya kuleta maendeleo yanayoendana na mabadiliko ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri nane chini ya Mwenyekiti wao, Mheshimiwa William Lukvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Mapendekezo ya vijiji 925 vilivyopatikana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Kamati:-

(i) Serikali kukamilisha zoezi la kufanya tathmini na kupitia mipaka ambayo bado ina migogoro kati ya hifadhi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo, kwa kukamilisha tathmini hiyo, kutaondoa migogoro iliyopo kwa sasa na kuwafanya wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo.

(ii) Serikali kuitia wizara kuacha kuharibu mali za wananchi wa maeneo hayo yakiwemo mazao, wanyama na nyumba mpaka tathmini itakapotolewa na kutangazwa kwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kuku...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili imegonga. Kwa hiyo, maliza kwa sababu ulishasema taarifa yako iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee taarifa hiyo, lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na Mto Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, na ninaomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,  
MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA  
2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO  
KWA MWAKAWA FEDHA 2021/2022 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

#### **1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ina sehemu kuu tatu (3) ambapo sehemu ya kwanza ni Utangulizi, sehemu ya pili ni Uchambuzi wa kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na, uchambuzi wa makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Sehemu ya tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati na Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020; Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya **Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii** na kushughulikia Bajeti za Wizara hiyo. Uchambuzi wa Bajeti ultanguliwa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA FEDHA 2020/2021

#### 2.1 Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Fungu 69** liliidhinishiwa bajeti ya **shilingi bilioni 114,593,952,734**. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 69,573,850,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi bilioni 45,020,102,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **shilingi milioni 700,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 44,320,102,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2021 Wizara ilipokea jumla ya **shilingi bilioni 42,876,557,300** ikiwa ni sawa na **asilimia 37.4** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kati ya fedha zilizopokelewa, **shilingi bilioni 12,301,691,237** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 45** ya bajeti iliyotengwa kwa matumizi ya kawaida, na **shilingi milioni 51,600,000** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikiwa ni sawa na **asilimia 7.4** ya fedha za ndani

Iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha za nje zilizopokelewa ni **shilingi bilioni 11,701,013,058** sawa na **asilimia 26** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa, mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hususani za miradi ya maendeleo unakwamisha juhudzi za Wizara kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa muda unaopangwa. Aidha, kutopatikana kwa fedha za nje za miradi ya maendeleo ambazo ndio bajeti kubwa dhidi ya fedha za ndani, kumekwamisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uhifadhi. Jedwali lifuatato linaonesha mwenendo wa upatikaji wa fedha fungu 69 kwa mwaka 2020/2021.

**Jedwali Na. 1:** Mwenendo wa Upatikaji wa Fedha Funau 69

Na.	Idara/Taasisi/ Wakala	Bajeti iliyoidhinishwa 2020/2021	Kiasi kilichotakiwa kupokelewa hadi Februari, 2021	Fedha zilizopokel ewa hadi Februari, 2021	% ya bajeti iliyoidhi nishwa
<b>1. Matumizi ya Kawaida</b>					
i)	Matumizi Mengineyo	18,721,305,000	12,480,870,000	10,886,352,488	58
ii)	Mishaha	50,852,545,000	33,901,696,666	20,237,591,754	40
	JUMLA 1	<b>69,574,150,000</b>	<b>46,382,566,667</b>	<b>31,123,944,242</b>	<b>45</b>
<b>2. Miradi ya Maendeleo</b>					
iii)	Miradi ya Maendeleo Nje	44,320,102,000	29,546,734,666	11,752,613,058	26.5
	Miradi ya Maendeleo Ndani	<b>700,000,000</b>	<b>466,666,667</b>	<b>51,600,000</b>	<b>7.4</b>
	Jumla	45,020,102,000	30,013,401,333	11,752,613,058	26
	JUMLA KUU (1 & 2)	<b>114,593,952,000</b>	<b>76,395,968,000</b>	<b>42,876,557,300</b>	<b>37.4</b>

## 2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Idara mbalimbali za Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na taasisi na mifuko ilio chini ya Wizara hiyo ziliidhinishwa kukusanya **Shilingi bilioni 65,256,218,761**. Hadi kufikia Marchi, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya **shilingi bilioni 23,428,330,747**, sawa na **asilimia 36** ya malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba kiwango hicho ni pungufu kwa takribani **shilingi bilioni 26,940,607,072** ukilinganisha na makusanyo ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa **shilingi bilioni 50,368,937,819** Mapungufu hayo yalitokana na changamoto ya ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID -19) yaliyoikumba Tanzania na Dunia nzima.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, mashirika ya uhifadhi chini ya Wizara ambayo ni TANAPA, TAWA, NCAAA na TFS yaliidhinishiwa kukusanya **shilingi bilioni 738,230,093,590** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya hifadhi zetu. Hadi kufikia machi, 2021 makusanyo yalikuwa **shilingi bilioni 165,192,291,419** sawa na **asilimia 22.4** ya malengo waliyojiwekea. Kamati inahoji uhalisia wa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kama ulifanyika kulingana na hali halisi kwakuwa tofauti ya ukusanyaji na makadirio ni kubwa sana.

**Mheshimiwa spika**, Kwa upande mwingine kamati iliweza kushuhudia utekelezaji wa mikakati mbalimbali iliowekwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto ya ugonjwa wa corona ilipotembelea maeneo mbalimbali ya utalii wakati wa ukaguzi wa miradi. Hivyo, kamati inaipongeza Wizara kwa kuwa na mikakati endelevu ya kukabiliana na ugonjwa wa korona. Jedwali lifuatalo linaonyesha mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli Fungu 69 kwa mwaka 2019/2020 na 2020/2021

**Jedwali Na. 2:** Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli Fungu 69 kwa mwaka 2019/2020 na 2020/2021

UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA MACHI FUNGU 69, 2019/2020 NA 2020/2021					
Idara	Makusanyo 2019/2020	Makadirio 2020/2021	Kilichotakiwa Kukusanywa Feb, 2021	Kilichokusany wa	%
Utawala na Rasilimali Watu, Utalii na Mfuko wa Taifa wa Mambo kale	16,418,466,865	22,657,242,000	15,109,729,333	8,487,845,818	37.5
Taasisi	16,834,009,092	18,846,563,910	12,564,375,940	9,394,005,804	50
Mifuko ya Uhifadhi TAFF na TWPF	17,116,461,862	23,752 412,851	15,834,941,901	5,543,479,125	23
<b>Jumla</b>	<b>50,368,937,819</b>	<b>65,256,218,761</b>	<b>43,509,047,174</b>	<b>23,428,330,747</b>	<b>36</b>

Chanzo: Randama za Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/21

**Jedwali Na. 3:** Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli Fungu 69 (Taasisi za Wizara) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na linganisho kwa mwaka 2019/2020.

Taasisi	Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020	Makadilio na Makusanyo hadi Februari, 2021 (Mwaka wa Fedha 2020/2021)			
		Makadilio kwa Mwaka 2020/2021	Kiasi kilichotakiwa kukusanya hadi Februari, 2021	Makusanyo hadi Februari, 2021	%
		(i)	(ii)	(iii)	(iv)
TANAPA	251,805,883,647	363,899,596,000	294,292,720,135	38,494,906,907	11
NCAA	123,858,764,000	162,663,179,000	108,442,119,333	22,460,300,565	14
TAWA	42,677,529,107	58,063,935,590	38,709,290,393	14,699,241,062	25
TFS	127,195,486,643	153,603,383,000	97,220,377,679	89,537,842,885	58
<b>JUMA</b>	<b>545,537,663,397</b>	<b>738,230,093,590</b>	<b>538,664,507,540</b>	<b>165,192,291,419</b>	<b>22.4</b>

*Chanzo: Randama za Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/21*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepata tafsiri kwamba, ukusanyaji wa mapato katika taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA ni wa kusuasua na kwamba Taasisi hizi zimeathirika sana na tatizo la ugonjwa wa UVIKO 19 ulioyikumba Dunia na Taifa kwa ujumla. Hivyo, ni maoni ya kamati kuwa Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA zitasimamia vyema mikakati iliyojivekeza katika mwaka 2021/2022 ili kuweza kufikia lengo la makusanyo walijivekeza. Aidha, kamati inaipongeza TFS kwa kufanya vizuri katika ukusanyaji wa maduhuli, ni maoni ya kamati kuwa Taasisi zingize za Wizara hii zitasimamia mikakati walijivekeza ili kufikia malengo ya ukusanyaji maduhuli kwa mwaka 2021/2022.

### 2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo mitatu (3) kati ya miradi 6 iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Lengo la ukaguzi huo lilikuwa ni kujiona hali halisi ya utekelezaji wake kulingana na bajeti iliyotengwa katika kila mradi uliokaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo katika mikoa ya Iringa na Mbeya kati ya tarehe 12 hadi tarehe 15 Machi, 2021. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa utekelezaji wake ni :

### 2.3.1 Mradi Na. 5203 – Usimamizi wa maliasili na Uendelezaji wa Utalii kanda ya kusini (Resilient Natural Resources for Tourism and Growth-REGROW)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Mradi huu ni wa miaka 6 na ulianza Rasmi Disemba 21, 2017 na unatarajiwa kukamilika Disemba, 2023. Lengo kuu la mradi ni kufungua fursa za vivutio vilivypo katika ukanda wa kusini mwa Tanzania kwa kutekeleza mradi wa kuendeleza baadhi ya maeneo muhimu yenye vivutio ili kuongeza mchango wa sekta ya utalii kweni uchumi na maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa katika hifadhi za Taifa za Mikumi, Ruaha, Udzungwa na Nyerere. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 **shilingi bilioni 30,495,601,686** ziliidhinishwa ili kutekeleza mradi huo. Kati ya fedha hizo **shilingi milioni 200,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 30,295,601,686** ni fedha za nje. Hadi wakati Kamati inakagua mradi, **Shilingi bilioni 4,579,169,894.54** zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwenye mambo kadhaa ikiwemo usimamizi na uboreshwaji miundombinu katika maeneo ya kipaumbele ya kuendeleza utalii, ununuzi wa Mitambo mikubwa, ununuzi wa Malori na vifaa vingine kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Viwanja vya ndege.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na miradi inayotekelawa kupitia mradi wa (REGROW) Kamati ilibaini kwamba changamoto kubwa inayoikabili Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni Barabara itokayo Iringa mjini kuelekea ndani ya hifadhi pamoja na barabara zilizomo ndani ya hifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati ilibaini kuwa, hifadhi ya Taifa ya Ruaha ina vivutio vingi vya kitalii vikiwemo wanyama pori na ndege ambao hawapatikani katika hifadhi zingine Tanzania na Africa kwa ujumla, changamoto iliyopo ni kutojulikana kwa hifadhi kwa Watanzania walio wengi na Dunia nzima. Hivyo, ni maoni ya kamati kuwa Wizara itaendelea kutenga bajeti inayojitosheleza katika kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi hususani kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

### **2.3.2 Mradi Na. 4647- Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mkoa wa Iringa. Mradi huu unatekelezwa kwa ubia baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya ufini (finland). Katika mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti iliyotengwa kwajili ya mradi ni Euro 9,870,000 sawa na shilingi 26,649,000,000 kati ya fedha hizo shilingi 25,380,000,000 zitatolewa na Serikali ya ufini na Shilingi 1,269,000,000 zitatolewa na Serikali ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalengo la kuchochaea maendeleo endelevu na jumuishi katika Sekta ya misitu na mnyororo mzima wa thamani ili kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa Taifa. Ili kufikia malengo ya mradi makundi makuu mawilli yanahusisha wakulima wadogo wa miti wanaoanzisha na kutunza mashamba yao na Wajasiriamali wadogo na wa kati wanaoanzisha na kuboresha biashara zao zitokanazo na mazao ya misitu ambayo yamehusishwa katika mradi katika hatua zote za awali za mradi.

**Mheshimiwa Spika**. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 mradi uliidihiishiwa kutumia kiasi cha shilingi 6,337,348,485 hadi kufikia Machi 2021 kiasi cha shilingi 3,208,826,676 zimetumika katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi ikiwemo Utafiti. Katika utekelezaji wa mradi huu Wizara imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo Kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda mbalimbali, Kuboresha hali ya mazingira na mandhari, Kuhifadhi Ardhi na vyanzo vya maji, Kujenga misingi ya ajira zinazotokana na kazi mbalimbali na Kuwa chanzo cha mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati baada ya kutembelea maeneo ya Mradi ilibaini changamoto zifuatazo:-

- a. Kuchelewa kupata misamaha ya kodi kwa vifaa vilivytotolewa kama msaada na kuiingizwa nchini kutoptaka na taratibu za upatikaji wa msamaha huo;

- b. Mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) changamoto hii ilichelewesha kuanza kwa mradi na manunuzi ya vifaa vya mafunzo; na
- c. Upatikanaji wa eneo kwa ajili ujenzi wa Kituo cha Mafunzo. ( Chuo cha mafunzo ya Upasuaji miti). Kwa sasa mradi upo katika eneo la mtu binafsi na inaugharimu mradi takriban Euro elfu tatu kwa mwezi kwa ajili ya kulipia pango.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na Changamoto hizo Kamati ilishauri Wizara kuendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kupata msamaha wa kodi mapema na TFS kutenga eneo litakalotumika katika ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya upasuaji miti.

#### **2.4 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati.**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kiliarifu Bunge lako tukufu kwamba, katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine hayajazingatiwa kikamilifu kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti. Kwa muhtasari, naomba niweke msisitizo katika machache yaliyozingatiwa kikamilifu na baadhi yanayoendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni;-

- a. Kamati ilishauri Serikali ichukue hatua za haraka za kukabiliana na athari za UVKO-19 katika sekta ya Utalii na pia kupunguza tozo katika hifadhi (park fees) na kutoa masharti nafuu ya maombi ya viza (visa Exemption) ili kuvutia Watatalii wengi zaidi kutoka nje;
- b. Kamati ilishauri kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na mashirika ya uhifadhi

yakiwemo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) wawe na Mkakati/ Mpango wa Dharura(Contingency Plan) endapo litatokea jambo lolote ambalo litaathiri sekta ya utalii, mashirika hayo ya uhifadhi yawefe kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi;

c. Kamati ilishauri Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza tozo zinazolipwa na taasisi za uhifadhi (TANAPA, NCAA, TAWA na TFS kutokana na athari za COVID-19; na

d. Kamati ilishauri kwamba, Miradi mingi ya Sekta ya maliasili inategemea sana fedha za kigeni, lakini fedha zinazotolewa ni kidogo hivyo, Bajeti ya matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ya Wizara iongezwe fedha ili iendane na mahitaji halisi ya Wizara.

**Ushauri unaoendelea Kutekelezwa ni:-**

a. Kamati ilipendekeza kwamba, Wizara iharakishe mchakato wa kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ili kuwa mamlaka itakayokuwa na nguvu za kisheria katika kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu nchini.

b. Kamati ilishauri kwamba Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi zipitiwe kwa kuwa viwango vya malipo vlivyopo haviridhishi. Kamati ilifuatilia utekelezaji wa ushauri huu, ili kujua hatua iliyofikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na jitihada ambazo zimefanywa za kuanzisha mkakati wa kitaifa wa kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu kama Tembo, Simba, Mamba na Nyoka ili kupunguza athari kwa mifugo na binadamu, Kamati ina maoni kwamba ushauri huu haujafanyiwa kazi ipasavyo na hivyo basi, Wizara inapaswa kutekeleza ushauri huu kwa wakati.

c. Kamati ilishauri Wizara iandae Mkakati madhubuti wa makusanyo ambao utaakisi hali iliyopo hivi sasa ya mlipuko

wa ugonjwa wa Corona. Mkakati huo uende sambamba na kutoa ahueni kwa wafanyabiashara mbalimbali waliowekeza katika sekta ya utalii ambao wamekuwa msaada katika kulisiaidia taifa kukusanya mapato yake katika sekta hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa namna ambavyo ilizingatia kikamilifu ushauri wake katika baadhi ya maeneo tajwa hapo juu. Ni maoni ya Kamati kwamba maeneo ambayo Serikali inaendelea kuyazingatia yafanyiwe kazi kwa haraka ili kuweka mazingira mazuri ya utalii na uhifadhi hapa nchini.

## **2.5 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022**

### **2.5.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/2022 **Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii** imepanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi bilioni 65,256,218,761** kutoka katika idara mbalimbali, taasisi na mifuko chini ya Wizara. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba makadirio haya ni pungufu kwa **shilingi bilioni 6,282,212,183** sawa na **asilimia 8.8** ukilinganisha na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa **shilingi bilioni 71,538,430,944**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mashirika na taasisi za uhifadhi ambayo ni TANAPA, TAWA, NCAA na TFS, Wizara inakusudia kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 478,014,580,522**. Makadirio haya ni pungufu ya **asilimia 22** ya makadirio ya makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa ni **shilingi 738,230,093,590**.

Ulingenisho wa Makadirio ya Ukusanyaji Maduhuli ya Taasisi ya TANAPA, NCAA na TAWA kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Mwaka wa Fedha 2021/2022

## Jedwali Na. 4

Na.	Taasisi	Makadirio kwa mwaka wa fedha 2020/2021	Makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022	Ongezeko /Pungufu
1	TANAPA	363,899,596,000	253,704,221,522	43
2	NCAA	162,663,179,000	162,663,179,000	0
3	TAWA	58,063,935,590	61,647,180,000	6
<b>JUMLA KUU</b>		<b>584,626,710,590</b>	<b>478,014,580,522</b>	<b>22</b>

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto ya hali ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya (COVID-19) kuathiri sekta ya utalii duniani kote, ni dhahiri kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 yanaweza yasifikasiwe. Hivyo basi, Wizara inashauriwa kusimamia mikakati na mipango endelevu iliyojivekea katika kukabiliana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu ili makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2021/2022 ya taasisi na mashirika ya uhifadhi yaweeze kufikiwa.

### 2.5.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 **Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii** inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 418,859,544,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha inayoombwa **shilingi bilioni 153,537,684,000** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 265,321,860,000** inaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake, imebaini kwamba bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **shilingi bilioni 265,321,860,000** sawa na **asilimia - 381** ukilinganisha na Bajeti ya **shilingi bilioni 69,573,850,000** sawa na **asilimia 26** kwa Matumizi kama hayo katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko hilo kubwa limetokana na sababu zifuatazo:-

- a. Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA kujumuishwa katika bajeti ya Serikali kuititia Wizara ya Maliasili na Utalii;

- b. Kujumuisha katika bajeti ya Serikali taasisi zilizokuwa zinapata bajeti zake kutoka asilimia 3% za mapato ghafi ya TANAPA na NCAA; na
- c. Kuanzishwa kwa Idara ya uratibu wa Jeshi la uhifadhi wa wanyama pori na misitu (Jeshi Usu) ambayo limeanza kutengewa bajeti kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya kamati kuwa, kwa kuwa Serikali ilifanya uamuza wa kuzileta pamoja Taasisi za TANAPA, TAWA na NCAA katika bajeti ya Wizara ya maliasili na Utalii, ni imani ya Kamati kuwa Serikali imejipanga kuzisimamia ipasavyo Taasisi zilizo chini yake na kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

## 2.6 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, **Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii** inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 152,772,880,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa, **shilingi bilioni 38,879,696,000** ni fedha za nje, na **shilingi bilioni 113,893,184,000** ni fedha za ndani.

Bajeti ya Mpango wa Maendeleo inaongezeka kwa **shilingi bilioni 107,751,928,000** sawa na **asilimia 86** ukilinganisha na bajeti ya **shilingi bilioni 45,020,102,000** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Aidha, katika bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani, kuna ongezeko la **shilingi bilioni 113,193,184,000** ukilinganisha na bajeti ya maendeleo ya **shilingi milioni 700,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za Kutenga fedha nyingi kutoka vyanzo vya ndani dhidi ya nje, kwakuwa taarifa zimeonyesha fedha za nje za miradi ya maendeleo zimekuwa hazipokelewi na Wizara kwa kiwango kinachotakiwa hivyo kuathiri maendeleo ya miradi husika.

**Jedwali Na.5:** Mwenendo wa Bajeti ya Fungu 69 kwa mwaka 2020/21 na 2021/22

MATUMIZI	2020/2021	2021/2022	ONGEZeko/ PUNGUFU
Mishahara	50,852,545,000.00	153,537,684,000.00	102,685,139,000
OC	18,721,305,000.00	265,321,860,000.00	246,600,555,000
Maendeleo Ndani	700,000,000.00	113,893,184,000.00	113,193,184,000
Maendeleo Nje	44,320,102,000.00	38,879,696,000.00	5,440,406,000
Jumla Maendeleo	45,020,952,000.00	152,772,880,000.00	107,751,928,000
<b>Jumla ya ulinganifu</b>	<b>114,593,952,000</b>	<b>571,632,424,000.00</b>	<b>457,039,472,000</b>

*Chanzo: Randama za Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2020/21*

**Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2021/2022, Kamati imepata tafsiri kuwa kama fedha zilizotengwa zitatolewa kwa wakati na Wizara kusimamia vema utekelezaji wa miradi iliyopo na inayoendelea, Wizara itapata matokeo chanya katika utekelezaji wa majukumu yake.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa na kamati naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika maeneo yafuatayo:-

- 1) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha
- 2) Makusanyo ya Maduhuli
- 3) Bajeti ya Maendeleo
- 4) Uendeshaji wa Shughuli za utalii
- 5) Mradi wa REGROW
- 6) Ufanisi wa Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA).
- 7) Ufanisi wa Wakala la Misitu (TFS).
- 8) Umuhimu wa Sekta ya Nyuki

- 9) Ufanisi wa Usimamizi wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA).
- 10) Ufanisi wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii (WMA).
- 11) Umuhimu wa Uwindaji wa Kitalii.
- 12) Utaratibu wa kupata Fidia kwa Mjusi (Donasaria) aliyeo Ujerumani.
- 13) Mapitio ya Sera na Sheria.
- 14) Kuhusu Taarifa ya Mawaziri kukamilisha Tathmini ya Vijiji 975.

### **3.1 Mwenendo wa Bajeti na Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa, kumekuwepo kwa mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo na matumizi menginayo katika bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, jambo ambalo limepelekea Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kusimamia sekta nzima ya Maliasili na Utalii.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa katika Bajeti ziwe zinatolewa kwa kiasi kinachotosheleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kufanya hivi, Wizara itakuwa na uwezo wa kupanga kulingana na vipaumbele vyaya utekelezaji wa majukumu yake.

### **3.2 Makusanyo ya maduhuli Katika Sekta ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kumekuwa na changamoto kubwa katika ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara na Taasisi zake, kutohuna na changamoto hiyo kumepelekea kususua kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na namna ya taasisi hizo kujidesha zenyewe, Kamati inaishauri mambo yafuatayo:-

a. Wizara Kupitia Taasisi na Idara zake ziwawekee malengo, (Target) Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizochini yake na malengo ya makusanyo kwa kila robo mwaka (quarter) na malengo hayo yawe ndio kipimo cha utendaji kazi wao;

- b. Wizara ibuni mikakati endelevu ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo kushirikiana na Wizara ya Elimu, Tamisemi na Ofisi ya Waziri Mkuu, katika kuratibu namna bora kupata Watalii wengi wa ndani hususani Wabunge, Taasisi na idara mbalimbali za serikali na zisizo za kiserikali, Mikoa na Halmashauri za wilaya zote, Vyuo, Wanafunzi wa Sekondari na Shule za msingi. Aidha Wizara kuainisha changamoto zilizopo katika utaratibu uliopo wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara na kuziwasilisha katika kamati kwaajili ya kutolea mapendekezo;
- c. Kwakuwa mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19 umeathiri kwa kiasi kikubwa utalii wa kutoka nje, kamati inaishauri Serikali kuimarisha utalii wa ndani kwa kutangaza vivutio vya utalii wa ndani, kuanzisha kitengo cha Utalii katika kila Wilaya ili kiweze kuratibu masuala ya utalii wa ndani na kuelimisha umma wa Tanzania kuwa utalii sio kwa wageni tu. Hatua hili itasaidia kuongeza makusanyo ya maduhuli na kufidia pengo la kukosekana kwa fedha za kigeni zilizotokana na utalii wa nje;
- d. Serikali kuchukua hatua za ziada ili kuvutia watalii kutoka nje ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na ugonjwa wa COVID 19, kama uvaaji wa barakao na upimaji wa virusi vya corona kwa hiari.

### **3.3 Mpango wa Bajeti ya maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kimsingi bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii bila kujumuishwa kwa Taasisi zilizoko chini yake bado hajaongezeka, Kwa ujumla wake bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ni **shilingi bilioni 152,772,880,000** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. ukilinganisha na mwaka 2020/2021 bajeti ya maendeleo ya wizara ilikuwa **shilingi bilioni 45,020,952,000** bila uwepo wa Taasisi, na kwa kuwa ongezeko hilo ni kutokana na taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA kujumiushwa katika bajeti ya serikali, ni maoni ya kamati kuwa Wizara hajajipanga vema kuratibu shughuli za usimamizi wa Miradi ya maendeleo hususani katika maliasili, malikale na uhifadhi, ii kuendana na llani ya Chama Cha Mapinduzi Sura

ya Pili (uk. 110-115). Kamati inaishauri Serikali, kuongeza bajeti ya miradi ya maendeleo ya Wizara ili kusaidia Wizara hii kuratibu vema mikakati ya usimamizi wa maliasili na kuondoa migogoro inayoendelea katika hifadhi zetu kati ya wanyamapori wakali na binadamu pamoja na kuhifadhi mazingira.

### **3.4 Uendeshaji wa Shughuli za Utalii**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Utalii ni maoni ya kamati kuwa kwa kipindi kirefu Wizara imejikita katika kutangaza utalii wa Wanyama zaidi kuliko vivutio vingine yya utalii kama Utalii wa Fukwe (Marine Tourism), Utalii wa malikale (Traditional Tourism), Utalii wa Misitu (Forest Tourism) na Utalii wa Nyuki (Api Tourism). Hali hii imepekelea Serikali kupoteza mapato mengi kutoka kwenye vyanzo ambavyo vikiwekezwa na kusimiwa vizuri vitaongeza mapato ya Serikali. Aidha kamati imebaini uwepo wa changamoto katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Utalii hapa nchini kama vile hoteli kuwa na bei kubwa, mikataba ya wafanyakazi, waongoza utalii na wapagazi isiyoridhisha. Ili kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa shughuli za utalii hapa nchini kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo;

a. Serikali kuanzisha Mamlaka ya udhibiti wa shughuli za utalii hapa nchini. Mfano; kuhuisha Bodi ya Utalii kuwa Mamlaka ya kusimamia utalii Tanzania (*Tanzania Tourism Regulatory Authority TTRA*). Kuanzishwa kwa Mamlaka hii kutaleta uwiano mzuri katika uendeshaji wa shughuli za utalii ikiwemo udhibiti wa bei na tozo mbalimbali za huduma za utalii;

b. Serikali ianzishe kitengo maalumu cha biashara (*Special Business Wing*) ndani ya Wizara, ambacho kitajikita katika kuandaa modeli za kibiashara (*business models*) pamoja na kuunganisha (*harmonization*) mikakati ya kiatalii kutoka TAWA, NCAA, TANAPA na TFS. Kwa kufanya hivyo kutapelekea kuwepo kwa mkakati wa pamoja (*Single Tourism Strategy*) wa kutangaza utalii wa ndani na nje kwa Taasisi zote;

c. Juhudi za kutangaza vivutio vya Utalii ziongezwe kupitia michezo kwa kutumia wachezaji maarufu, vyombo vya habari vya Kimataifa mfano. CNN, DSTV, Aljazeera na BBC Aidha, Wizara kuweka mikakati endelevu ya kutangaza utalii wa ndani (Domestic Tourism) hususani vivutio vya malikale ili viweze kujulikana;

d. Wizara Kupitia Idara ya malikale ifanye tathmini ya vivutio vya kitalii katika mikoa yote nchini ikiwemo visiwa ambavyo kwa sasa havitumiki kama utalii na vingeweza kutumika kama utalii sanjali na kuweka mikakati ya kuviendeleza ili vitumike kutangaza utalii wa ndani;

e. Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 na kuendelea ihakikishe inajikita katika kuimarisha miundombinu ya barabara, mawasilano ya simu, canteen na hostels zilizomo ndani ya hifadhi zetu, kwa kufanya hivyo kutasaidla hifadhi zetu ziweze kufikika na kuhudumia watalii kwa ufanisi zaidi.

### **3.5 Mradi wa REGROW**

**Mhesimiwa Spika**, kwakuwa mradi wa REGROW unaotekelozwa katika hifadhi ya Taifa ya Ruaha Mradi huo ulioanza Rasmi Disemba 21, 2017 na unatarajiwa kukamilika Disemba, 2023 na kwa kuwa mradi huu utakuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza hifadhi za Taifa letu. Kamati inaishauri mambo yafuatayo:-

a. Wizara kuweka mkakati wa namna ya kuendeleza Mradi wa REGROW baada ya Wafadhili wa nje kukamilisha ufadhili wao.

b. Wizara kutenga bajeti itakayowezesha ukarabati wa barabara zilizomo ndani ya Hifadhi ya Ruaha ili kuwezesha Watalii kufika eneo hilo ikiwa ni pamoja na Wizara kufanya mazungumzo na Wizara ya Miundombinu ili kupata kipaumbele cha ujenzi wa barabara itokayo Iringa Mjini kwenda hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Ni maoni ya kamati kuwa Kukamilika kwa ujenzi wa barabara hii kutasaidia ongezeko la Watalii katika hifadhi ya Ruaha na kuongeza pato la Taifa.

### **3.6 Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya Hifadhi za Taifa kutoka hifadhi 16 hadi 22. Kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya 6, ni hifadhi 5 kati ya 16 zilizokuwa zina uwezo wa kuijendesha zenyewe na kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesha Hifadhi za Taifa nyingine 11.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hali ya kifedha ya shirika kwa sasa na taratibu zilizopo za ukusanyaji wa maduhuli sanjari na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, Ni maoni ya Kamati kuwa shirika hili litashindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Jambo litakalopelekea kudhoofisha shughuli za utalii. Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo;:-

a. Kuweka utaratibu wa Taasisi ya TANAPA kupata fedha za kuijendesha kwa wakati na kwa ukamilifu. Mfumo uliopo sasa unaifanya TANAPA kuwa na mazingira magumu ya biashara ya utalii kwakuwa matumizi madogo ya taasisi hiyo yatalazimika kusubiri pesa kutoka hazina ili kuyatekeleza ambapo mlolongo wake ni mrefu ambao unaweza kuathiri ufanisi wa biashara ya Utalii.

b. Kuimarisha Chuo cha utalii nchini kwa kuanzisha kampasi kikanda. Hatua hii itasaidia kasi ya kuongeza idadi ya vijana wengi kusomea fani ya utalii.

### **3.7 Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, miradi inayotekelawa na TFS imetoa matokeo chanya na mafanikio makubwa kiuchumi na kwa upande wa uhifadhi wa mazingira mfano shamba la miti la Sao hili. kamati ilielezwa kuwa, Shamba hili linachangia wastani wa **asilimia 35%** ya mapato ya TFS yote kwa mwaka, aidha, Sao hill kwa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2015 mpaka 2020 limekusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 216.3** sawa na wastani wa **shilingi bilioni 43** kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, kumekuwepo na changamoto kubwa ya uharibifu wa misitu hasa inayomilikiwa na vijiji na Halmashauri za Wilaya, hali iliyopelekea Kamati hii kuishauri Serikali mambo yafuatayo;

- a. Kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa na Wizara, ilionyesha kwamba mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuwa Mamlaka umeanza kwa kukusanya taarifa na kuandaa andiko litakalopelekwa ngazi za juu kwa maamuzi, na Lengo la uamuzi huu ni kuanzisha mamlaka moja itakayokuwa na nguvu za kisheria za kudhibiti matumizi ya rasilimali zote za misitu nchini, bila kujali umiliki. Kamati inashauri Serikali kuharakisha zoezi hili na kulitaarifu Bunge juu ya hatua zilizochukuliwa katika Mkutano ujao wa Bunge la Bajeti.
- b. Kwa kuwa rasilimali za misitu zinasimamiwa na wadau mbalimbali na mfumo wa usimamizi umegawanyika katika makundi mbalimbali hali inayochangia kuwepo kwa migongano na mwigiliano katika jukumu la usimamizi kati ya TFS na TAMISEMI (Halmashauri ya Wilaya na Viji). Ni maoni ya kamati kuwa Serikali ione uharaka wa kuanzishwa kwa **mamlaka moja ya kusimamia Sekta ya Misitu** ili kuleta ufanisi.
- c. TFS ina utaratibu wa kutoa fedha kwa vikundi kwa ajili ya kusaidia na kuhamasisha Mradi wa panda miti kibiashara, na kwakuwa fedha hizo zimeonyesha matokeo chanya katika kuendeleza mradi huo kamati inashauri fedha hizo zitolewe kama *Revolving Fund* ili kusaidia ongezeko la upandaji miti kwa taifa letu hususani maeneo yanayonufaika na mradi huo.
- d. Wizara ifanye utafiti na Tathmini ya aina ya miti inayofaa katika mikoa yote nchini na kiasi cha miti inayohitajika. Tathamini hiyo ifanyike kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Mikoa.
- e. Wizara iongeze kasi ya kupanda miti kibiashara maeneo mengine nchini hasa maeneo kame kama Dodoma, Singida, Manyara na shinyanga ili kuhifadhi mazingira na kuongeza pato la Taifa.

f. Kwakuwa kanda ya kusini ndiyo inayoongoza kwa kuwa na miradi mingi ya Miti ya mbao hapa nchini na kwakuwa hadi sasa hakuna chuo mahususi kwa masuala ya misitu na mbao ukanda wa kusini, ni maoni ya kamati kuwa Serikali ianzishe Kampasi ya *Forest Industries Training Institute* (FITU) katika mikoa inayolima miti kwa wingi mfano; - Mbeya, Iringa na Njombe kwa kufanya hivyo kutasaidia wakulima wa misitu na wawekezaji wa miti ya mbao kunufaika na huduma hii.

### **3.8 Sekta ya Nyuki**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Nyuki inayo fursa kubwa ya kuchangia katika pato la Serikali lakini kamati imebaini sekta hii haijapewa uzito unao stahili. Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo; -

a. Kutoa kipaumbele cha kuwekeza katika Sekta hii kwa kutoa elimu kwa wafugaji, upatikanaji wa mizinga ya kisasa pamoja na uanzishwaji wa viwanda vyta kuchakata mazao ya nyuki, kwa kufanya hivyo itachangia kuongeza ajira kwa upande mmoja na kuchangia pato la Taifa hasa fedha za kigeni;

b. Kuanzisha mamlaka moja ya kusimamia Misitu na Nyuki nchini, kuanzishwa kwa mamlaka hiyo ni hitaji la kisera la kupambana na changamoto za Sekta ya nyuki na Misitu lakini pia ni hitaji la Ibara ya 69 (e) ya Ilani ya Uchaguzi toleo la mwaka 2020.

### **3.9 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania(TAWA)**

**Mheshimiwa Spika,** TAWA tangu ianze kutekeleza majukumu yake Mwaka 2016, imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kuimarika uhifadhi kunakotokana na kupungua kwa ujangili, kudhibitiwa kwa vitendo vyta uingizaji na ulishaji wa mifugo katika Mapori ya Akiba na kuanzisha na kufanya mabadiliko ya kimfumo wa usimamizi wa uhifadhi kutoka wa kiraia kwenda Jeshi Usu. Aidha, TAWA imesaidia kuimarisha utalii kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vinavyosimamiwa na Mamlaka hiyo.

Hata hivyo, taasisi hiyo inakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo ongezeko la mwingiliano wa Binadamu na hifadhi za Wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo, Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo:-

a. Wizara ifanye tathmini na kuona iwapo kuna uwezekano na ulazima wa kuanzishwa kwa Sheria mahsus i kuiwezesha TAWA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, tathmini hiyo ibainishe masuala ya kisera, kisheria na kibajeti ambayo yanaweza kuathiriwa kutokana na mapendekezo ya tathmini hiyo.

b. Wizara ibuni mikakati endelevu ya kuthibiti mapema uvamizi wa maeneo ya uhifadhi mfano kuwa na mpango kabambe jumuishi na jamii zinazozunguka hifadhi (*participatory Wildlife-Human Conflict Management Program*) pamoja na wadau wa maendeleo na asasi za kiraia kuliko kusubiri maafa na shughuli mbalimbali zikiwemo za kilimo na ufugaji kushamiri ndipo badae hatua zichukuliwe. Kwa kufanya hivi kutapunguza kuchukua hatua kwa matukio na migogoro iliyopo kwa sasa kati ya wananchi wanoishi pembezoni mwa hifadhi na Wanyama wakali na Waharibifu.

c. Wizara itumia Technolojia katika kutambua dalili za uvamizi wa wanyama hasa kwenye maeneo yaliyo na mtandao na kutoa taarifa za haraka pale panapotokea uvamizi sanjari na kuanisha maeneo yote yenye shoroba na kuwaelimisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo juu ya kutoyaharibu na kuyavamia.

d. Wizara iweke mkakati endelevu wa **kuvuna Mamba** kwenye mikoa ambayo imekumbwa kwa kiasi kikubwa na madhara ya watu kuliwa na kuvamiwa na mamba. Kwa kufanya hivyo kutasaidia kulinda usalama wa wananchi lakini pia kuwapa wananchi uhuru wa kujikita kwenye shughuli za uzalishaji mali.

### **3.10 Ufanisi wa Hifadhi ya Wanyamaporii ya Jamii (WMA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa utekelezaji wa majukumu ya Hifadhi ya Wanyamaporii ya Jamii (*Wildlife Management Areas*) WMA umekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ugumu wa kupata wawekezaji na ufinyu wa Bajeti kufuatia kubadilishwa kwa taratibu za kukusanya mapato yatokanayo na utalii na kwa kuwa, kumekuwepo na changamoto ya WMA kutopata gawio la fedha kwa wakati, jambo ambalo linapelekea Watumishi wa WMA wakati mwingine kukosa Mishahara yao na fedha za kujidoresha kama taasisi. Ni maoni ya kamati kuwa mwenendo huo wa ucheleshwaji wa fedha za WMA unaweza kupelekea watumishi kukosa hamasa ya kazi na kupelekea ongezeko la majangili katika hifadhi zetu, kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

- a. Serikali kutoa fedha kwa wakati kwa mujibu wa Kanuni za WMA ili kuwezesha Taasisi hii kujidoresha kikamilifu sanjari na kulipa madeni yote wanayodaiwa na WMA kwa mwaka wa fedha 2020/2021.
- b. Serikali kutafuta namna bora itakayowezesha WMA kupata fedha zao kwa wakati katika miaka ijayo ya fedha ili kuepusha ucheleweshwaji wa fedha na changamoto zinazotokea katika WMA nchini.
- c. Kuhusu uvamizi wa mifugo katika hifadhi na adhabu zinazotolewa linahitaji mjadala mpana ikiwa ni pamoja na wafugaji kuelimishwa kuhusu kuacha kuchunga mifugo yao kiholela na kuanza kufuga kisasa.

### **3.11 Uwindaji wa Kitalii**

**Mheshimiwa Spika**, kuanzia Novemba, 2017 Sekta ya uwindaji wa kitalii imepata mtikisiko mkubwa baada ya Serikali kufuta leseni za umiliki wa vitalu vya uwindaji wa wanyama pori, hali hii imepelekea wamiliki wengi kurudisha vitalu na kusababisha vitalu vingi kuwa wazi. Aidha, mfumo wa ugawaji vitalu kwa njia ya (*Administrative leasing*) ilichangia kwa kiasi kikubwa uwepo wa mazingira ya rushwa katika ugawaji wa

vitalu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na mfumo wa ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada. Hata hivyo, kamati inaishauri Serikali kuboresha mfumo huo ili vitalu vyote viweze kunadiwa na kuchukuliwa.

### **3.12 Utaratibu wa kupata Fidia kwa Mjusi (Donasaria) aliyeo Ujerumani.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi mbalimbali zilizofanywa na Bunge lako Tukufu na zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali katika masuala yanayohusu Dinosaria (Mjusi aliyeo Berlini Ujerumani). Hata hivyo, hujudi hizo hazijaunganishwa pamoja ili kupata msimamo wa Serikali utakaoratibiwa na Wizara ya maliasili na Utalii na Wizara ya Mambo ya Nje. Kamati inaona pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Wajumbe waliotumwa kufatilia masalia hayo mwaka 2010, Kamati inaishauri Serikali kuwa;-

a. Juhudi zinazofanywa na wadau mbalimbali ziunganishwe pamoja ili kupata msimamo wa Serikali kuhusu masalia ya Dinosaria aliyeo ujerumani.

b. Kuwepo na Mpango kazi mahususi (*Plan of Action*) wa lini wazo hili litatekelezeka kwani limechukua muda mrefu tangu lienze kujadiliwa na wadau mbalimbali.

### **3.13 Mapitio ya Sera na Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya kamati kuwa Sera ya Taifa ya Utalii (1999), Sera ya Taifa ya Misitu(1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998) zimepitwa na wakati kwa kuwa ni za muda mrefu. Vilevile sheria ya Mambo ya kale Na. 2 ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979 imepitwa na wakati. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya Sera na Sheria hizi ili ziweze kukidhi azma ya kuleta maendeleo yanayoendana na mabadiliko ya sasa.

### **3.14 Kuhusu Taarifa ya Mawaziri kukamilisha Tathmini ya Vijiji 925**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri nane chini ya Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Mapendekezo ya vijiji 925 vilivyopakana na hifadhi za Taifa. Kamati inataarifa kuwa mapendekezo ya Kamati hii bado hayajakamilika hasa suala la tathmini ya vijiji 55 vinavyopakana na hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kutokana na hali hiyo wananchi wanaoshi pembezoni mwa hifadhi hizo wamekuwa wakihitaji kujua hatma ya maeneo yao kwa muda mrefu. kamati inashauri yafuatayo:-

- a. Serikali kukamilisha zoezi la kufanya tathmini na kuitia mipaka ambayo bado inamigogoro kati ya hifadhi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo. kwa kukamilisha tathmini hiyo kutaondo migogoro iliyopo kwa sasa na kuwafanya wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo.
- b. Serikali kuitia Wizara kuacha kuharibu mali za wananchi wa maeneo hayo yakiwemo mazao, wanyama na nyumba mpaka tathmini itakapotolewa na kutangazwa kwa wananchi.

### **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*):-

1. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Pius Chaya, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb
4. Mhe. Soud Mohammed Jumah, Mb

5. Mhe. Phillipo Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Ally Juma Makoa, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb
10. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
11. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
12. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb
13. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
14. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb
15. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb
16. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
17. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
18. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
19. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
20. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
21. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
22. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb
23. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb
24. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb
25. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Naibu Waziri Mhe. Mary Masanja (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Allan J.H.Kijazi pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai ambaye kwasasa ni Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro. Kwa nafasi ya Kipekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi kwa kuwa Katibu wa Kwanza Mwanamke katika Historia ya Bunge hili Tukufu, kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumanji Hussein Brambati, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Gerald Magili na Ndg. Michael Chikokoto, Katibu wa Kamati hii Ndg. Monica Mwamunyange na Msaidizi

wa Kamati Ndg. Mwimbe John, kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lipokee Taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivowasilishwa na mto Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Aloyce Andrew Kwezi, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,  
MALIASILI NA UTALII**

Juni, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuwasilisha maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na uchangiaji. Tunaanza na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wake wote katika Wizara hii. Pia nawapongeza sana Kamati kwa taarifa yao nzuri na uchambuzi wao mzuri sana ambao wameufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa miongozo yake ambayo ameitoa na hasa katika eneo la kumaliza migogoro ambayo imewagharimu sana wananchi, wafugaji na wakulima katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kwenda kwenye Randama ya Waziri ukurasa sita na wa saba. Kwenye ukurasa wa sita kwenye *item* namba nne kwenye malengo mahsusini ya Wizara, Mheshimiwa Waziri amezungumza namna ambavyo maelekezo ya Serikali ya kumaliza migogoro ya ardhi ambayo inahusisha wananchi wanaokaa karibu na hifadhi na pia migogoro inayohusisha wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa saba wa randama ya Mheshimiwa Waziri na nikikariri hotuba ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. Magufuli, ambayo imeeleza vizuri namna ambavyo lengo la Serikali ni kufikia watalii bilioni tano na kuongeza mapato kutoka bilioni 2.6 za sasa za mwaka 2016 kwenda mpaka shilingi bilioni tano ndiyo malengo ya Wizara katika miaka mitano ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuangalia katika maeneo hayo mawili, naomba nianze kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba Mheshimiwa Rais, mwaka 2019, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutambua uwepo wa migogoro mingi sana nchini, mwezi wa Tatu, tarehe 15 aliagiza kuundwa kwa kikosi kazi cha Wizara saba kikiongozwa na Wizara ya Ardhi kushughulikia na kushauri namna gani Serikali inaweza kumaliza migogoro katika maeneo mengi ambayo yamekuwa yakiwakabili wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu, kazi kubwa katika eneo hili ilifanyika. Tulikuwa tunazungumzia maeneo yenye migogoro, vijiji 366, ikaja ikagundulika ni zaidi ya 1,000, lakini katika uchambuzi uliofanywa katika hiyo *joint committee* ilioneckana karibu vijiji 975 vitaendelea kuwepo kutokana na mazingira na baadhi vilioneckana vitashughulikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa ni ya msingi kwamba nataka kufahamu maamuzi haya ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyatolea tangazo la Serikali na kuahidi utekelezaji; utekelezaji wake unafanyika lini? Kuchelewa kufanyika kwa utekelezaji huu kunawagharimu sana wananchi. Nataka nitoe mfano; katika Jimbo langu la

Geita Mjini, msitu wa Hifadhi wa Usindwake na msitu wa Geita Kata ya Mgusu asilimia 80 wapo ndani ya eneo ambalo zamani na mpaka sasa linahesabika kwamba ni hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha asilimia 80 kuwa katika hifadhi maana yake ni kwamba makazi yamo ndani ya hifadhi, wakulima wamo ndani ya hifadhi na mifugo waliyo nayo inachungwa ndani ya hifadhi. Sasa wananchi hawa wanakamatwa kila siku na wanapokamatwa hawakamatwi kwa sababu ni makosa yao ni kwa sababu tayari kuna shule, tayari kuna zahanati, tayari kuna barabara, tayari kuna shughuli za kiuchumi zinaendelea maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Serikali kumaliza tatizo hilli. Tayari lillishatolewa maelekezo, sasa sielewi anatekeleza nani? Wizara yako Mheshimiwa Waziri Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi au Wizara gani? Ninachojua ni jukumu la Serikali kumaliza mgogoro huu ambaou unawagharimu wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, faini katika maeneo haya ni kubwa sana. Anapokamatwa mfugaji ameingiza mifugo kwenye hifadhi, faini zake ni kubwa. Tuliona kwenye hotuba ya Wizara ya Kilimo na Mifugo, karibu ng'ombe milioni sita zimekamatwa, zimetaifishwa; na ni kwa mujibu wa sheria. Sasa lazima tumalize migogoro hii kwa maelekezo ya Serikali.

Nataka kujua kwa nini utekelezaji wa maagizo haya unaendelea kuchukua muda mrefu? (*Makofi*)

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Olelekaita.

## TAARIFA

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe tu mzungumzaji taarifa, kwamba Waziri wa Maliasili na Utalii tarehe 1 Januari, 2021 alitoa tangazo lifuatalo: "Ninyi ni Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu, fanyeni kazi zenu za kulinda maeneo mliyokabidhiwa kama kawaida. Mkikuta kuna ng'ombe wanamilikiwa na Dkt. Damas Ndumbo, ninyi kamateni, msije mkasema ng'ombe hawa ni wa Waziri, tuwaache, ninyi mkamate na mwapige mnada kama kawaida. Ng'ombe watakaokutwa ndani ya Hifadhi ni shilingi 100,000." Nataka tu nimpe taarifa kwamba hili tangazo siyo kwa mujibu kwa sheria. Hakuna sheria inayosema ng'ombe atozwe kwa kichwa shilingi 100,000. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Constantine Kanyasu, unaipokea taarifa hii?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo na ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, pengine na Mheshimiwa Waziri wa Sheria watoe ufanuzi kwenye hiyo sheria. Kwa sababu, hiyo sheria ukiiitazama haimpi *absolute right* anayekukamata kupiga hiyo *fine*. Ina vipengele vyake ambavyo vinakuwa *attested* kufika kwenye fine hiyo. Kutokana na *ignorance* ya wananchi wetu huku, *it is direct*, ukikamatwa mara shilingi 100,000/=, sasa utatengeneza masikini wangapi katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja yangu ya pili ambayo lengo letu ni kufikisha watalii milioni tano. Kwanza niendelee kuwapa pole wahifadhi wetu Tanzania kwa sababu, kuja kwa *COVID* kumewarudisha nyuma. Walikuwa wanakwenda vizuri sana, nilikuwa ninaamini baada ya muda mfupi tungelikuwa ni nchi ambayo inaongoza kwa utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili katika Afrika, nchi ambazo zinafanya vizuri sana katika utalii, Morocco wanapata watalii milioni 12.3 ambao maeneo mengi sana

wanachokwenda kuangalia kule ni *cultural*, pamoja na utalii ambao unahusisha sana mambo ya vyakula na maeneo mengine ambayo yamekuwa ni ya asili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Egypt* milioni 11.3; huko nako ni *cultural* na maeneo makubwa hapa ni *pyramids* pamoja na kuangalia *Pharaoh Tombs* na kadhalika. Eneo la tatu, ni *South Africa*, hawa wanapata watalii milioni 10; *most popular* ni kwa sababu ya safari na kitu kinaitwa *MICE*, mikutano ambayo inafanyika *South Africa*. Katika Afrika kwa mujibu wa *International Convention and Conference Association, South Africa* wanaongoza kwa Afrika nzima kwa *ku-host* mikutano mingi sana ambayo inapeleka watu wengi kule nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya nne ni Tunisia ambayo inapata watalii milioni 8.3 na nchi ya tano ni Zimbabwe. Nini kinawapeleka watu Zimbabwe? Ni kwenda kuangalia Victoria Falls. Sasa hapa nataka kuzungumza nini? Katika orodha yote hii ya nchi tano, kimsingi nchi ambayo kidogo watalii wanakwenda kwa ajili ya kuangalia wanyama ni *South Africa*. *South Africa* ni kwa sababu ya *improvement* yake katika miundombinu na namna ambavyo wametengeneza mazingira ya kufanya watalii waweze kwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi nydingi ambazo zinaongoza katika utalii, kinachowapeleka kule ni *cultural* pamoja na *heritage centers* ambazo ziko katika maeneo yale. Sasa ukiitazama vizuri Tanzania, ukaacha zile *traditional products* zetu zinazoleta watalii kwa maana ya safari, *beach*, labda kwa maana ya *hunting* na vitu vingine. Bado *tuna-lack product* ambayo inaweza kutuletea watalii wengi kwa mara moja na kufikisha watalii milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka *ni-emphasize* jambo moja, katika Afrika Mashariki, Rwanda sasa hivi wamekuwa *waki-host* mikutano mikubwa sana kidunia. Kwa nini? Kwa sababu ya ile Kigali *Convention Center*. Wametengeneza Kigali *Convention Center* ambapo

inafanyika mikutano mikubwa sana ya dunia. Nataka tu nitoe mfano; wamekuwa na Mkutano wa *Force Agenda Summit*, ambao ulikusanya maelfu ya watu; Mikutano ya Mo-Ibrahim, wamefanya mikutano ya *GMSA* ya *Mobile 360*, wamekuwa na mikutano mingi ambayo imeleta watu kutoka maeneo mbalimbali. *Why Rwanda?*

Moja, kwa sababu kwanza ni *free VISA*. ukiingia Rwanda unatoka dunia nzima, ukifika Kigali unakutana na *VISA* baada ya kufika, *VISA on arrival*. Hii imeondoa sana usumbufu, kwa hiyo, unaweza kwenda maelfu na maelfu ya mikutano pale na ukafika ukafanya mkutano wako lakini utapata *VISA on arrival*. Pia ni rahisi kupata *VISA* kwa masharti mepesi bila usumbufu wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, *connectivity*. Rwanda hana Shirika kubwa sana la Ndege, lakini anachokifanya ana ndege ndogo ambazo zinaweza kukupeleka kwenye *activity* nyingine. Kwenye eneo hili la mikutano anayeongoza ni *South Africa*, wa pili ni Rwanda; tatu hapa tuna Ethiopia, tuna Kenya, tuna Uganda. *Why Kenya na Uganda na wenyewe hivyo ni connectivity.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa, tunayo haja kubwa; watu wanaokuja kuangalia Wanyama, anaweza akaja mara moja na asirudi tena, lakini anayekuja kuangalia *cultural*, anaweza kuja mara ya kwanza, akarudi mara ya pili. Kwa hiyo. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimalizie eneo moja kwamba kutoa ushauri wangu. Tunaomba kuishauri Serikali kutafuta uwekezaji mahususi kwa ajili ya kuhamasisha...

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** ...utalii wa mikutano katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kabla ya yote naomba kutoa pole kwa Jimbo langu la Nkasi Kaskazini na kwa wazazi wa binti huyu kwa kuwa ni mpiga kura wangu, Petronela Mwanisawa aliyenyongwa na mpenzi wake. Kwa mazingira ya kawaida mionganoni mwa mikoa ambayo bado tulikuwa nyuma sana kielimu ni pamoja na Mkoa wa Rukwa. Inapotokea hasa tena kwa mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 22, kwa mazingira ya wazazi kama wale wa Mkoa wa Rukwa, inatia uchungu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua umekuwa mtetezi sana wa wanawake na umetoea mwongozo wako vizuri, lakini ni vizuri Serikali ikaliangalia jambo hili. Leo tunapoona adui wa kwanza sasa wa kumaliza maisha ya wanawake ni pamoja na mahusiano ya kimapenzi, iwe kwenye ndoa au mahusiano ya kawaida. Ni vizuri jambo hili likaangaliwa vizuri. (*Makof*)

Mheshimwia Naibu Spika, nami napenda kuchangia Wizara hii na kabla sijachangia niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na *cabinetyake*. Nawapongeza zaidi kwa sababu Waziri na Naibu wake

wamekuwa wasikivu na kuchukua hatua pale ambapo matatizo yanajitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Nkasi ni mionganini mwa wilaya ambazo zina migogoro ya kutosha juu ya wananchi na Hifadhi au Mapori Tengefu. Nitaanza na suala la mipaka katika Hifadhi kwa Mapori Tengefu. Nilizungumza ndani ya Bunge na Waziri Mkuu akatoa maelekezo kupitia Waziri wa Maliasili na Utalii kulingana na uzito wenyewe, lakini hapa nazungumza kulingana na mgogoro huo, imefikia mahali sasa wananchi walifikia hatua mpaka kumuua *Game*, jambo ambalo siyo zuri. Leo limefanyika Nkasi, litaendelea maeneo mengine. Lazima mfanye uchunguzi wa kutosha, nini kinapelekea migogoro hii kuendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, kwenye Wilaya yangu ya Nkasi nitataja kata chache tu ambazo zina migogoro. Kata ya Kabwe, Kata ya Kilando, Kata ya Kipili, Kata ya Kipundu na Kata ya Nkomoro. Nilifanya utafiti wa kutosha baada ya hii migogoro kuona inaendelea sana. Ukienda Kata ya Kirando, Kata ya Kipili, Kata ya Kabwe, mpaka wa kwanza kabisa uliwekwa mwaka 1948. Ukiangalia huo mwaka, idadi ya wakazi ilikuwa ni ya watu wachache sana. Huo mpaka ukabadilishwa mwaka 1992, ukabadilishwa tena mwaka 2002. Sasa ulivyobadilishwa mwaka 2002 ukarudishwa tena, kule kwenye ule mpaka uliwekwa mara ya kwanza mwaka 1948. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona hapo idadi ya watu imeongezeka kiasi gani kutoka mwaka 1948 mpaka leo mwaka 2021. Pamoja na kwamba mawazo ya Wabunge wengi tumekuwa tunaomba tuongezewe ardhi kutoka kwenye Mapori Tengefu au kwenye Hifadhi, jambo hilo halitakuwa suluhisho la kudumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri Wizara, kwa sababu, idadi ya watu inaongezeka, kuna haja kubwa sasa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Wizara inayohusika na mazingira, *TAMISEMI*, Uvuvu, pamoja na hizo

Wizara ambazo Mheshimiwa Rais aliona kuna umuhimu wa wao kukaa pamoja, kuna haja ya kwenda kupitia mipaka hii upya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama leo maumivu walijonayo wananchi wetu, wanaona ni kama Serikali ya Tanzania inaheshimu zaidi wanyama kuliko binadamu. Lazima tuwaondoe kwenye hiyo dhana. Tunaiongoaje? Matamko na makatazo bila mbadala, haina maana yoyote, inaleta unyanyasaji kwa wananchi wetu. Leo mkiwaambia wananchi hawa wako kwenye Hifadhi, Serikali ni moja, mnajua kwamba idadi ya watu inaongezeka. Hiyo mipaka ya mwaka 1948 kwa hali ya kawaida, kulingana na idadi ya watu inavyoongezeka, lazima migogoro itakuwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima Serikali ije na mbadala. Uki sema hili ni Hifadhi, lazima tuungane kwa pamoja tutenge eneo lingine. Kwa sababu, wengi wanaoathirika na hii mipaka ni wakulima, ni wafugaji na wavuvi. Lazima tutafute eneo mbadala na hapo tutakuwa tumekwenda kuondoa tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo jambo ni vizuri nikaliweka sawa. Adhabu zinazotolewa na watu wa TAWA, TANAPA na wengine wote, ni adhabu ambazo ni za ajabu sana. Wananchi wananyanyaswa. Mambo yaliyokuwa yanafanyika na Wakoloni, yanafanyika kwa watu wa TAWA. Jambo hili halikubaliki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekwenda walipokuwa wanaadhibiwa watu wa mpaka ule wa Korongwe, nilimwambia Mheshimiwa Waziri, mzee anapigwa, amekutwa nyumbani. Pia kuna mama amejifungua, ana siku mbili, nyumba yake inachomwa. Anaenda wapi na huyo mtoto? Yaani imefikia mahali haki za binadamu hazipo tena. Haya mambo hayakubaliki, hayakubaliki kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jambo hilo, inapotokea mwananchi ameliwa na mamba, ameliwa na kiboko, mnachelewa sana *ku-react* ninyi Wizara ya Maliasili,

lakini ikitokea mwananchi amekamatwa na aidha, nyama nyamapori kidogo, adhabu anayopewa ni wakati huo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea pia mfugaji amekamatwa kwenye Hifadhi, adhabu wanazopewa zinaanza siku hiyo hiyo. Hapa nina risiti kadhaa za wafugaji ambaao wamepewa adhabu. Ukifuatilia ule mgogoro pia kuna watu wenu ambaao ni watendaji ambaao sio waaminifu, wanachukua ng'ombe zilizokuwa nje huko wanazipeleka ndani kwenye Hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo, unajiuliza, kama wakazi wanaweza wakajenga nyumba, wakajenga shule, wana mashine pale za kusaga, hawa watu wa hifadhi walikuwepo. Wanakwenda kuchoma watu wamekaa zaidi ya miaka 10, miaka 20 Serikali ilikuwepo. Kwa nini mnashindwa kufanya hayo mambo mapema? Inatuonyesha kwamba kuna mambo yanayofanyika juu ya hao watendaji wachache, ambaao wanawaingiza wafugaji pale kwa mkataba na siku hiyo wasipowapa fedha, wanakwenda kufanya maamuzi kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna sehemu rushwa zipo, ni pamoja na eneo hili, ni lazima liangaliwe vizuri. Nakumbuka kauli ya Mheshimiwa Rais akiwa ndani ya Bunge kwenye hotuba yake ya mwisho, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, juu ya maliasili zinazopatikana ndani ya Hifadhi. Lile jambo alilolitamka ni vizuri sana, lakini kuna haja ya kufanya utafiti wa kutosha kwenye maamuzi haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama hata wale wananchi ambaao wanaibua labda madini, namna wanavyochukuliwa na wale watu wa *TAWA*, *TFS*, adhabu wanazopewa; kitendo cha kusema hapa nimegundua kuna madini; pamoja na kwamba ni nia njema ya Serikali leo kuruhusu madini na vitu vilivyoko kwenye Hifadhi kuvunwa, ni lazima tuwe na utaratibu mzuri utakaotumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kugundua, pia watu ambao ni wa eneo lile waweze kuwa wanufaika wa kwanza ili tuweze kuleta uthamani. Kwa sababu mimi naamini wahifadhi namba moja ni wale watu ambao wako karibu na Hifadhi. Jambo hilo likitumika kwa busara hiyo naamini kila mtu anapenda uhifadhi. Sasa tunahifadhi kwa ajili ya nani? Tunahifadhi kwa ajili ya wananchi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa, ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa tena nafasi hii. Naitwa Riziki Said Lulida, Mama Tembo, Mama Mjusi, Mama Selous na ni Balozi wa Utalii. Nataka niwapongeze kwa dhati katika Wizara ya Maliasili ikiongozwa na Waziri na Naibu Waziri. Pia kuna watu wamefanya kazi kubwa ya kusimamia utalii na maendeleo ya wanyamapor. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawataja kwa majina; kwanza inaongozwa na Mheshimiwa Ndugu Allan Kijazi. Kwa kweli amefanya kazi kubwa. Mheshimiwa Fred Manongi wa Ngorongoro, mpaka wanazeekea ndani ya utalii na kuweka heshima kubwa ya nchi hii. Wamefanya kazi kubwa. Bwana Silayo Dosantos katika *TFS*, mmeona hata mapato ya misitu yamekuwa makubwa na bila kusahau na wahifadhi wengine ambao wana upendo, ikiwemo sisi Wabunge ambao ni *Macchampion* wa kupenda maendeleo ya utalii ndani ya nchi hii. Tanzania ili tuendelee tunahitaji mapato ambayo yataisaidia nchi hii.

Katika upande wa maliasili ya Tanzania watalii wanakuja kwa ajili ya masuala ya wanyama watano tu, *big five* ambao ni Simba, Tembo, Nyati, Chui na Faru. Bila hivyo, kuwashifadhi hawa wanyama, basi hatutaweza kufanikiwa, tutarudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie wenzetu Kenya, Masai Mara ni eneo dogo sana, lakini wamefanya kazi kubwa sana ya kutangaza utalii kwa kupitia Masai Mara. Sasa nataka nami niwasaidie vile vile tuweze kufanya kazi ili tuweze kupata pato kubwa, kumsaidia Mheshimiwa Mama Samia Suluhu katika eneo hili la utalii, kama alivyokuwa *champion* kuhakikisha kuwa Tanzania yenye mapato ya ndani kupitia Hifadhi zetu pamoja na maliasili yetu inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo hayo ni kama ifuatayo: kama alivyozungumza ndugu yangu Kanyasu, kwa kupitia *International Conferences* na *Global Summit* kule ndio watu wanakwenda. Niulize *TANAPA* imewahi kwenda katika mikutano kama hiyo? Hawana *Fund*. Ujiulize Ngorongoro wanatangaza maeneo kama hayo? Hakuna. Hivyo lazima tatarudi nyuma na wenzetu wanatupita kwa ajili ya kutangaza na kuhakikisha matangazo *yao/promotion* zao na *marketing* zinakuwa kubwa na ndio maana unaona tunapitwa mpaka na Masai Mara ndogo kama ni wilaya tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kupitia *airlines*; leo ingia katika *KLM* unaiona Kenya inatangaza, *come to Kenya and visit Serengeti, Ngorongoro and Zanzibar*. Sasa unajuliza, tunakwenda wapi? Kwa nini wamefikia pale? Ni kwa sababu wanatangaza matangazo makubwa sana ya kidunia na ndio maana mapato yanapatikana. Kwa kupitia *ma-tour operators*, wengi wanakwenda, mimi nimewahi kutembea nao, lakini ni wachache. Wengi hawafanyi kazi ya kutosha. Kama wangefanya kazi ya kutosha, Tanzania hii ambayo tuna mbuga nyingi, tumeambiwa sasa hivi *TANAPA* wana 22. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa tumezipita nchi za Afrika zote kwa mapato, lakini kwa vile bado hatujaitangaza inabidi tufanye kazi kubwa ya utalii wa ndani. Tufanye kazi kubwa; na Watanzania hata Wabunge humu ndani; kuna Mbunge mwingine ukimwita unakujua Serengeti? Atakwambia mimi sikujui. Tulete mafunzo ya kutosha, tutembee nao Wabunge hawa wakaone haya

yanayozungumzwa. Mimi ni Mwenyekiti wa kupambana na ujangili ndani ya Bunge; nimetembelea mbuga, ndiyo maana nimeikoa Mbuga ya Burigi, imerudi katika Hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyamapori inabidi walindwe, lakini na wafugaji wanaingia ndani ya mapori wakiwa na *ma-rifles* na mabunduki makubwa sana. Wengi wao wanakwenda kibiashara na katika uindaji haramu. Kupitia mimi, nimekwenda pale kwa kuwa nimenyanyaswa kwa vile ni mfugaji, haikubaliki. Mimi naikataa hiyo. Naomba mafunzo yaje kila mara ili Wabunge waelimishwe. Wakielimishwa Wabunge kazi hii itakuwa rahisi. Tulikuwa na Mheshimiwa Keissy, alikuwa *champion* wa kupambana kuona wafugaji wanaonewa. Nikamwambia utaingia Kamati ya *Selous*. Aliyoyaona, mwenyewe amekuwa mpenzi mkubwa wa wanyamapori na tukamaliza migogoro hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la mjesi. Najua muda wangu ni mdogo sana. Nimelizungumzia suala la mjesi toka mwaka 2005. Hii maana yake, nami nahisi hata uchaguzi wangu nimekuja ili kuhakikisha suala la mjesi tunalimaliza. Nawe Mbunge, kama Naibu Spika ni *champion* naomba uwe mmojawapo katika *ma-champion* wa kupambana na kuhakikisha pato la mjesi linarudi katika nchi hii. Kwa maslahi mapana ya nchi yangu, nasema karibu sana. Tuko Wajumbe 20, lakini naona na wewe hatalikataa hili, unakaribishwa sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mjesi, *fossils* ambazo zimetoka Lindi, sasa hivi ziko sita Ujeruman. Vile vile tumeambiwa duniani kuna ndege wakubwa sita wametoka Tanzania, wako Ujeruman. Wengine wakaniambia, mama bado, ongeza harakati. Kuna vyura wa Kihansi, wako Marekani. Tunataka tujue sisi tunafaidika nini na vyura wa Kihansi ambao wako Marekani? Tumeambiwa tena kuna *chameleon* wako Australia. Tunataka kujua kule Australia tunapata faida gani na wale *chameleon* wetu wale, hawa nanii... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** *Chameleon kwa maana ya kinyongaa*  
au?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, eeh, ni vinyonga. Nisamehe sana, nimesahau Kiswahili kidogo, lakini nitazidi kujitahidi. *Chameleon* wako Australia kule, lakini tunataka kujuu tu wamefikia vipi? Bado ni maliasili, inabidi tuisimamie na tupambane nayo. Kuna vichwa vyaa watemi viko Ujerumani, vilichukuliwa miaka mingi sana. Tunaomba tuisimamie nayo. Hivi tunachozungumza, suala la hakimilikki, hata kama walichukua wakati wa Ukoloni, lakini Tanzania *it is the sovereign state* na tunajua kabisa Balozi wa Ujerumani amemleta mwakilishi wake. Tunataka tukitoka hapa mwezi wa Saba tunakwenda kufanya *event* kubwa Tendeguru na tunataka tutengeneze *MoU*, Tanzania ipate tozo kutokana na mapato ya mijusi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya mtu hailiki, ni lazima tupambane nayo na tukipata pato lile, nina imani kwamba nitakapoondoka hapa Bunge nitakuwa nimeacha *legacy* kubwa sana na kuhakikisha Wabunge wenzangu wanapotoka hapa, watakuwa *champion* wa kusimamia maliasili yetu ya Tanzania ambayo inatoweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la *NIASA Selous Corridor*, ni kama la Serengeti, Masai Mara. Wanyama wanatoka Tanzania Serengeti wakielekea Kenya na imetangazwa sana, lakini hii ya Tanzania ya *Selous NIASA* haijatangazwa. Hii ni Mbuga rasmi ya tembo. Nataka nikuambieni tu angalizi, hii mbuga imevurugwa sana na kutoa vitalu pembeni kabisa anapopita tembo. Hivyo, ina maana tembo akipita pale *anavurugwa*.

Nilihudhuria katika Mkutano wa *WTO* wakasema Tanzania *it is a lost Eden*. Mmeiacha Eden nzuri ya tembo inavurugwa na matokeo yake kwa vile Wabunge hawajui wanachokizungumza, wanaona wanaonewa, kumbe wao wanawaonea wanyamaporii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *corridor* zote za wanyamaporii zimekuwa *intervened*. Sasa unajiuiliza, tembo inabidi apite katika Miombo Forest, atapita wapi na ninyi mmeshaiharibu? Misitu mmeshakata, mmefanya fujo kubwa ya kukata misitu. Je, hawa wanyama watakwenda wapi? Simba wamemalizika mpaka hadi mwisho Serengeti unauliza, sharubu yuko wapi? Hii yote ni fujo ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mikoa ambayo hata umwambieje, yeye kila siku anataka kula kimolo. Wanajijua wenyewe! Sasa ukiona watu wale wanapenda nyamaporii maana yake wao ni majangili, ni watu ambaa wanafanya uharibifu mkubwa kwa wanyama. Tulikuwa na tembo kuanzia 2,000,000, wakaisha wakafika mpaka 300,000, wakafika mpaka 100,000, wakaisha mpaka 10,000. Tushukuru katika Serikali ya Awamu ya Tano tumewarudisha mpaka 47,000. Bado hatujafikia kundi la tembo tunalohitaji. Sasa kinachofanyika ni majangili wanafuata tembo. Wakiwafuata tembo, ni lazima na tembo naye atakuwa hakubali, atawaua. Sasa hapa lazima tukae chini. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana. Napenda wanyamaporii, napenda uhifadhi na utalii. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi mchana huu nami nichangie Wizara hii mahususi kwa uchumi wa Taifa letu. Awali ya yote kama ilivyo ada nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu

Waziri na Watendaji wote. Pamoja na ugumu uliopo kwenye Wizara hii, wanajitahidi kadri ya uwezo wao, kadri Mwenyezi Mungu alivyo wajaalia. Vile vile napenda kusema kwamba mchango wangu leo nitauanza moja kwa moja kwenye uhifadhi wa wanyamapor. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Taifa letu kama mchangiaji aliyepita alivyosema, Serikali ya Awamu ya Tano imedhibiti ujangili, uhifadhi umeongezeka, lakini matokeo ya udhibiti huu ndiyo haya malalamiko ambayo sasa hivi kila kona ya nchi yetu tunayapata, hasa wanyama hawa wanaoitwa tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kwenye Halmashauri ya Wilaya yangu ya Liwale ambako sehemu kubwa ndiyo tunaozungukwa na hifadhi ya Selous, wako wananchi wamehama kutoka mashambani wamerudi vijiji baada ya mazao yao kuharibiwa au kulima na wanyama hao wanaoitwa tembo. Kuna Kijiji kama Ngumbu, Milui, Kikulyungu, Mkutano, Mtawatawa, Barikiwa, Ndapata, Mpigamiti, Lilombe na Kimambi; baadhi ya wananchi wa vijiji hivi tayari wapo vijiji, wamerudi kutoka mashambani baada ya wanyamapor hasa hao jamii ya tembo kumaliza mazao yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, pamoja na kwamba tumeongeza uhifadhi, lakini bado sasa turejee kwa wananchi tuangalie ni namna gani wananchi wetu tunawakinga na ongezeko hili la tembo? Ongezeko la tembo ni zuri, tunapata mapato mengi, lakini lazima turejee, tuwe na mipango mikakati safi ya kuwanusuru wananchi wetu ili wasiendelee kuteseka na hatimaye kupata majanga ya njaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naomba nizungumzie suala la kifuta machozi. Sheria ya Kifuta Machozi ni ya muda mrefu sana. Hivi kama mwaka 1974 mtu alikuwa anapewa shilingi 500/= labda kutokana na umbali wa mazao yake yalivyoliwa au shilingi 1,000/=, hivi kweli kiwango kile tunaendelea kukitumia mpaka leo! Nawaomba sana kwa

kipande hicho tuongeze kiwango hicho angalau tuangalie namna tunavyoweza kuwasidia wananchi wetu. (*Makofi*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nampa Mheshimiwa Kuchauka taarifa katika mchango wake; hili tatizo la fidia ni kero maeneo mengi; na siyo tu ni kidogo, haitoki kwa wakati. Mfano, ni wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini, Kata ya Nyatwali; Natwali, Tamau, Serengeti, mbali ya kwamba tembo wanaharibu mazao yao, wanaomba fidia na fidia yenye hiyo ndogo haitoki kwa wakati. Kwa hiyo, nilikuwa taarifa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena. Muda wa kutoa taarifa siyo muda wa kuchangia. Mheshimiwa Kuchauka endelea na mchango wako.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naipokea taarifa yake kwa sababu hata mimi kwangu kuna malalamiko, wananchi wameliwa mazao yao, sasa hivi wana mwaka wa tatu hawajapata fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hapo hapo kwenye uhifadhi wa *Selous*. Sasa hivi Serikali imeimarisha utalii wa picha zaidi kuliko utalii wa uwindaji. Naiomba Serikali, ukanda huu wa *Selous* upande wa kusini kuanzia Kilwa, Liwale mpaka Tunduru, hatuna lango la utalii wa picha, matokeo yake baada ya kupunguza utalii wa uwindaji, umebakia utalii wa picha, lakini sisi kwetu tumebakia hatuna watalii na hatupati mapato yoyote yale.

Kwa hiyo, uwepo wetu wa hifadhi ya *Selous* tunakuwa kama vile hatuoni yale manufaa ya moja kwa moja. Kwa hiyo, naiomba Serikali kufikiria kuanzisha lango la utalii wa picha kwenye maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie kwenye WMAs. Waziri kwenye ukurasa wa 47 aya ya 59 ndiyo amezungumzia kidogo kuhusu WMAs. Lengo la Serikali kuanzisha WMAs hizi ni kushirikisha wananchi kwenye uhifadhi. Sasa tunawashirikishaje kama kwenye hotuba nzima umetaja kwenye aya moja, tena kamstari kamoja tu? Yaani hawa watu tunawashirikisha vipi? Kwa kweli kama Serikali ilikuja na lengo zuri kuimairisha WMAs ili kushirikisha wananchi kwenye uhifadhi ili wananchi wanaozunguka hifadhi hizo waone faida ya kuwa hifadhi zile, basi naiomba Serikali kuimarisha WMAs na kuona ni namna gani wanazisaidia hata kuwatafutia wawekezaji kwenye vitalu hivi ambavyo wamewekeza hao WMAs. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile fedha zao zinachelewa, hata pale wanapopata mtalii au mwekezaji mwenye Kitalu X, lakini bado mapato yao kutoka Serikalini yanachelewa sana. Hapo naiomba Serikali kuangalia upande wa WMAs. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nije kwenye uhifadhi wa TFS. Bunge liliopita niliuliza swali hapa kuhusu mpango wa uvunaji wa kitalu cha Nyelakipelele. Nashukuru Serikali wameshaleta mpango wa uvunaji wa msitu ule wa Nyelakipelele, lakini uvunaji wa pale ni wa holela. Ukipita hii njia kutoka Nachingwea kwenda Liwale, unapishana na malori usiku, yanabeba magogo. Mengine yana vibali, mengine hayana vibali, mengine yamegongwa na mengine hayagongwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naiomba Serikali, pamoja na nia njema ya kufungua uvunaji kwenye hifadhi hii ya msitu wa Nyelakipelele, bado tunaomba itupie macho uvunaji wa msitu huu, kwani ni wa ovyo mno na wala hauzingatii mazingira. Sidhani kama uvunaji ule ni endelevu, kwa sababu uvunaji endelevu ni kwamba watu wanavuna kwa mpango na miti ile lazima ipandwe mingine, lakini kwenye uvunaji wa msitu huo hakuna uvunaji endelevu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee kwenye ikama ya wafanyakazi kwenye Halmashauri zetu. Kwenye Halmashauri zetu utakuta mhifadhi au Afisa wa Wanyamapori yuko mmoja tu. Jambo hili ndiyo linaloleta mgogoro mpaka tunapata matatizo ya wanyamapori, tunashindwa kupata msaada kwa sababu Afisa wa Wanyamapori kwenye wilaya au kwenye Halmashauri, anakuwepo mmoja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, Serikali ni moja... (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami pia niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya, hasa Mheshimiwa Naibu Waziri ulishanitembelea Biharumlulo, nashukuru sana kwa sababu ulifanya ziara pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mtendaji Mkuu wa *TANAPA* ambaye pia ndio Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa *response* kubwa ambayo amekuwa anaifanya pale ambapo nimekuwa nikijaribu kuwasiliana naye juu ya mambo ambayo yanaendelea kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka kwa sababu ya muda pia; na kwa sababu ndiyo nachangia Wizara hii kwa mara ya kwanza tangu nimeingia humu kama Mbunge wa Biharamulo; na tukiwa na Hifadhi ya Burigi Chato; nachukua nafasi hii pia kutambua juhudu kubwa za Hayati Rais wa Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alihakikisha anatutoa katika pori hili la Burigi, pori ambalo limetumika katika utekaji na kuwanyanyasa watu wa Biharamulo kwa muda mrefu sana na hatimaye leo ni sehemu tunayojivunia tuki-*anticipate* tunaanza kupokea wageni muda siyo mrefu, hasa baada ya haya ambayo tunayatarajia kwenye bajeti hii yatakapokuwa yamefanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo kama matatu ya haraka haraka ya kwenda nayo kwa sababu ya muda. Jambo la kwanza, hifadhi hii imekuwa na kelele kidogo hasa kwa wakazi wa Biharamulo. Nadhani suala hili nimeshalifikisha kwa Waziri, lakini kikubwa ambacho kimekuwepo ni jina la hifadhi. Maana kwetu sisi wakati hii hifadhi inaundwa, imechukua sehemu ya Chato na sehemu ya Biharamulo ukiunganisha wilaya mbili kama hifadhi moja. Kwa upande wa Biharamulo kwa sababu pori lilikuwa linaitwa Burigi, wakazi wa Biharamulo walipoona sasa pori linaundwa hifadhi, linabaki jina Burigi na huku linabaki jina Chato, wakahisi kama vile sasa ni kwamba pori limesomeka chini ya Chato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imeleta kelele na Mheshimiwa Waziri nilimwambia, wakati wa kampeni ilikuwa ni saga kubwa sana. Hata leo nilikuwa na kipindi *Star TV* asubuhi. Siongelei hili suala kabisa, ni suala lingine, lakini mionganoni mwa mada zilizokuja ilikuwa ni mada ya jina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwa sababu mbuga hii inaunganisha wilaya mbili; tuna Wilaya ya Biharamulo na Wilaya ya Chato, nilikuwa naomba pale penye neno "*Burigi*" mridhie kubadilisha neno "*Burigi*" likae jina "*Biharamulo*." Mbuga isomeke "*Biharamulo Chato National Park*" ili wakazi wa Biharamulo ambao wanabebea sehemu kubwa ya hili pori waone kwamba juhudu kubwa ya kuwatoa

katika mateso na unyang'anyi wa watekaji wale, inaleta faida kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nilikuwa naliomba Mheshimiwa Waziri alichukue kwa niaba ya wakazi wa Biharamulo, wakubali ku-*amend* jina, kwa sababu kinachoonekana *Tourist Board* wakati wanaanzisha hiki kitu ni kwamba hawakutoa elimu ya kutosha kwa ajili ya wakati wa Biharamulo. Nasema hawakutoa elimu kwa sababu hata geti tu la kuingilia mbugani, uwanja mkubwa ambao tuna-*anticipate* kuutumia utakuwa ni uwanja wa Chato; kutoka Chato mpaka Biharamulo kama watalii wametua pale ni takribani kilometra 50. Unapofika Biharamulo huingii mjini, kwa sababu Mji wa Biharamulo barabara kubwa inatoka inaeleke Nyakahura na hatimaye inaelekea Rwanda na Burundi. Sasa mjini hutaingia kama unakwenda mbugani kule; na geti linalofuata liko kilometra 82 kutoka Biharamulo Mjini upande wa Nyakahura kule karibu unaelekea Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unafikiria, mgeni yupi ambaye utamtoa Chato *Airport*, kilometra 50 umtembeze, afike aone Mji wa Biharamulo kulia, unamkatisha mbuga kilometra 82 yule mgeni ndio anakwenda kuingia kwenye hifadhi kupitia Geti la Nyungwe, halafu tena aanze kutembea kurudi nyuma ya Biharamulo. Kwasababu *Basically*, hata Naibu Waziri alipokuja Biaharamulo tulimweleza, *Central/Burigi* lilipo, lile Ziwa Burigi ambalo linaunganisha Karagwe na Mulega, lipo nyuma ya Biharamulo pale; ni takriban kilometra 10 tu, ukipitia kati ya Ruziba, Kijiji cha Kitochembogo na Kitongoji cha Muungano, unatokea kwenye hifadhi, katikati kabisa kwenye ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulikuwa tunaomba, najua mtaongeza mageti, nilishaambiya kuwa kuna haja ya kuongeza geti na niliomba geti liongezwe. Sasa ninachoomba, geti litakaloongezwa *this time* litokee pale pale Biharamulo ili wageni hawa sasa wasizunguke umbali mrefu. Maana mgeni anapokwenda sehemu anataka aone Wanyama. Sasa ukianza kumtembeza kule na bado miundombinu haipo, itakuwa haisaidii. Kwetu sisi kwa wakazi

wa Biharamulo tunataka mbuga hii tuituimie kutangaza utalii na vile vile ku-*brand* wilaya yetu, maana imekuwa ni nyuma sana. Hii wilaya imekuwepo tangu mkoloni, lakini haijulikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba fursa hii na *geographical location* ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia pale iweze kutunufaisha. Mheshimiwa Waziri nikienda haraka haraka, nimeona hapa mnao mpango wa kujenga hoteli pia. Sasa nilikuwa naiomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii watusaidie kwenye *plan* ya kujenga hoteli hata sisi tupate angalau hoteli moja pale. Tukipata hoteli moja itatusaidia. Pia nimeona kwenye bajeti mna mpango wa kujenga barabara kilometra 2,256 pia sehemu ambayo mna madaraja takribani 18 na *culvert* 157.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba kwa sababu mbuga hii haina miundombinu kabisa kabisa. Tunaomba mtusaidie, wakazi wa Biharamulo watakapojua kwamba kilometra ngapi zimetengwa kwa ajili ya hii ya kwetu Burigi, Chato itatusaidia sasa hata sisi kujipanga ku-*grab* hizo *opportunities*. Maana najua kama ni ujenzi wa barabara hamtafanya nyie, nami nahitaji watu wangu kwa sababu mbuga ipo kwao, watumike na washiriki kwenye kujenga barabara na kuchukua *opportunities* za kufanya kazi hizo ili waweze kujinufaisha kimapato. Kwa sababu *basically* tunachokiangalia ni kwamba hii mbuga iwanufaishe wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba haya yazingaiwe kwa haraka kwa sababu ya muda. Ili haya yote yaweze kufanyika, lipo jambo moja. Tumekuwa tunaona kwamba mapato yote yanayokusanywa na *TANAPA* siku hizi yanakwenda *TRA*. Sasa hawa watu mvua inaponyesha na kwenye hifadhi hizi, maana tunazo taarifa kwamba mbuga zetu za Tanzania barabara zimeharibika kweli kweli, hata huduma zipo chini sana. Kwa sababu wanapoomba fedha ya miradi ya maendeleo kutoka Hazina mpaka irudi inachukua muda mrefu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi mbuga *basically* lazima zijiendeshe kibiashara, kwa sababu zinajiendesha kibiashara na tuna-*competition* na jirani zetu wa Kenya au watu wengine wanaotuzunguka, tunaomba kosa moja la mtendaji mmoja au watendaji wawili la kuharibu au kutapanya zile fedha isiwe adhabu ya kuharibu biashara ya utalii. Tunaomba Serikali ifikirie ku-*amend'hii* sheria, fedha irudi *TANAPA*, waikusanye, muweke usimamizi maalum, ili sasa watakapohitaji fedha ya kutengeneza barabara kule, tusianze wote kuomba kwenye kapu moja, kwa sababu hii ni sehemu ya biashara. Tunaporudi kuomba kwenye kapu moja, inakuja kutuchelewesha na inashindwa kufanya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Hassan Zidadi Kungu ajiandae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nami nitumie dakika chake nichangie kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mwalimu wangu wa Sheria kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na Naibu wake na pia watendaji kwenye Wizara hii, Katibu Mkuu na Taasisi wakiwemo Ngorongoro, *TFS* na wengine, hongereni kwa kazi nzuri. Wizara hii ilikuwa na kelele sana, lakini mmejitätahidi kuituliza na nadhani mtasonga mbele vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii Mheshimiwa Waziri kukushukuru kwa kukubali Naibu Waziri aje kufanya ziara Jimboni kwangu na kutembelea maeneo yale ambayo yameathiriwa na wanyamapori hasa Kata ya Mnara na Chiponda. Naibu Waziri karibu sana Mtama, tunakupenda na tutakupokea kwa mikono miwili, utembelee maeneo haya na kuona jinsi tulivyoathiriwa na wanyamapori. Nami sina

mashaka kwamba tutachukua hatua za kurekebisha maeneo haya na kupunguza athari zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza na kuishukuru Kamati kwenye hotuba yao wamegusia jambo ambalo ndilo nilitaka nilizungumze hapa; Jambo la sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii. Kamati wamekiri kwamba sekta hii kidogo imetikisika, imeyumba. Takwimu huwa hazidanganyi. Ukiangalia namba zinaonesha wazi kwamba liko tatizo. Bahati nzuri jambo hili tulanza kulizungumza ndani ya Bunge hapa miaka kama minne au mitatu iliyopita tukaanza kutoa mashaka yetu kwamba jamani mnapokwenda mtapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukizingalia takwimu, zinakubaliana na ripoti ya kamati kwamba sekta hii tusipochukua hatua itakwenda kufa na hapa ni pitie takwimu chache. Mwaka 2013 sekta hii ilikuwa na wawindaji wa kitalii 1,550, leo ukichukua takwimu za 2018/2019 wameshuka mpaka wamefika 473. Kutoka 1,550 mpaka 473, hili ni anguko kubwa sana, tusipochukua hatua tunakwenda pabaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapato ya Serikali, mwaka 2013 Serikali ilikuwa inapata mpaka dola milioni 27. Leo tumeshuka mpaka dola milioni nane. Hili ni anguko kubwa; 27 kwa 8. Mapato ya jumla ukikusanya tozo na vitu vingine tulikuwa tunakwenda mpaka dola milioni 100. Leo, milioni 25, maana yake tunaanguka. Mwaka 2013 tulikuwa na makampuni 60 yapo yanafanya kazi, leo yako chini ya 40. Maana yake tumeshuka kwa zaidi ya asilimia 50. Ukienda kwenye takwimu sasa za vitalu vyenyewe, vitalu ambavyo viko wazi sasa vinakaribia asilimia 50. Maana yake ni kwamba kuna anguko kubwa kwenye hii sekta na kama hatutachukua hatua za makusudi, Sekta hii itaanguka. Sekta hii kwenye Wizara ni eneo muhimu katika kufanya mchango wa Wizara kwenye uchumi wetu uendelee kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuiomba Serikali, ondokeni kwenye kuona kwamba mkishaamua jambo, hata

kama linafanya vibaya mnatakiwa kuendelea nalo, nadhani siyo sawa sawa. Kila mara mnakuja, tunawaonesha takwimu, tunaonesha mwelekeo ulivyo, lakini kwa sababu Serikali mmeshaamua, mnaamua kuendelea hivyo hivyo, hata kama tunakwenda kuanguka. Mheshimiwa Waziri mkiendelea hivi, maana yake mnahujumu sekta hii; na mkihujumu sekta hii, mnahujumu uchumi wa nchi. Kama mapato yameanguka kwa kiasi hiki na bado hatuchukui hatua, liko tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumefikaje hapa? Kweli kuna mchango wa tatizo la *Covid*, lakini tulianza kuanguka kabla ya *Covid* na tukaanza kusema kwamba tunaanguka. *Covid* ilipokuja ikapiga msumari kwenye anguko. Sasa katika mazingira haya, mategemeo yangu ilikuwa ni kwamba tuchukue hatua, kwa sababu tukichukua hatua tutakwamua anguko hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitalu hivi vinavyobaki wazi kila siku ya Mungu vinapoteza thamani yake. Wewe unajua katika vitalu vilivyobaki wazi leo karibu vitalu 14 havifai, maana yake tumepoteza rasilimali ya nchi. Kazi kubwa ya Wizara hii ni pamoja na kuhifadhi ndiyo kazi kubwa. Sasa kama uhifadhi unaharibika, tunachukua hatua tunakwenda kuharibu zaidi, mimi nadhani iko haja ya kuchukua hatua. Kwa hiyo, tumefikishwa hapa na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maamuzi Serikali tuliyafanya ya kubadilisha mfumo wa ugawaji wa vitalu. Ni kwa nia njema na hata Kamati wamekiri; nia ile njema lengo ilikuwa ni kuongeza *transparency*, kupunguza rushwa, kuondoa maneno; nia njema, lakini Mheshimiwa Waziri ule mfumo mliouweka una upungufu ndiyo maana vitalu mnavipeleka mnadani vinakosa soko, vinabaki wazi, vinapoteza thamani. Kadri siku zinavyokwenda rasilimali hii inaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu; moja, nendeni mkapitie upya huo mfumo mliouanzisha. Kaupitieni upya mpunguze matatizo yaliyomo *including* kuongeza *transparency*. Hivyo mlivyoweka haitoshi, bado una

upungufu mwangi ndiyo maana minada inafeli. Minada yote iliyofanyika, mnaapeleka vitalu vingi, mnauza vichache, mnarudisha vingi. Hapa ni kuonesha kwamba kuna upungufu kwenye mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili, wale ambao wana vitalu tayari msiwapeleke kwenye mnada. Kwanza wamepitia wakati mgumu wa *Covid*, wamewekeza kwenye hivi vitalu, wamewekeza miundombinu na wanavilinda kwa sababu vile ambavyo havina watu mmeviacha, ulinzi hakuna, miundombinu hakuna, vinapotea, vinaharibika, tunapoteza mapato. Kwa hiyo, wale ambao wako kwenye vitalu, ombi langu ni kwamba waongezeeni muda wa kuendelea kupanga kwenye hivi vitalu. Rekebisheni mfumo mlolioeta, vile vitalu tupu vipelekeni mnadani, endeleeni na utaratibu baada ya maboresho. Mkifanya hivi, naamini tutakuwa tume-save sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu. Mmesema vizuri kwenye bajeti yenu kwamba mnakwenda kupidia sera, sheria, taratibu na kanuni mbalimbali malizojiwekea. Serikali ya Awamu ya Sita moja ya lengo kubwa ni kuvutia wawekezaji. Hebu nendeni mkazipitie upya tuendane na wakati na wakati huo tuangalie na mazingira mengine. Mheshimiwa Waziri, hili kundi kubwa ambalo tumelipoteza maana yake moja, limekwenda kwenye maeneo mengine. Kwenda kule, linawenza lisirudi. Sasa tusiporekebisha tutaendelea kuanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ni matumaini yangu Serikali itachukua hatua tuiokoe Sekta ya Uwindaji hapa nchini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Zidadi Kungu na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Kipekee kabisa namshukuru

Mungu kutujaalia uzima na ninawashukuru sana wanawake wa Kilimanjaro walionipa hii nafasi ya kuja kuwasemea Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa moyo wa dhati kabisa niipongeze hii Wizara ya Maliasili na Utalii. Kipekee nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro; nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Masanja; Katibu Mkuu, Dkt. Allan Kijazi na pia niwapongeze watendaji wote na vile vile niwashukuru wale wa Kamati iliyowasilisha hoja mezani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa sababu nilitaka tu kusema hii Sekta ya Utalii iko mahututi hospitali. Iko mahututi kwa sababu kwa kweli walipigwa na mambo mengi, lakini zaidi sana na UVIKO 19. Wote waliokuwa na blashara za utalii wanalia, maduka au ofisi zao zimefungwa na hata wale wanyama waliokuwa wanachangamka wakiona magari yanazunguka kule, wamenyong'onyea sana. Naomba Wabunge wote kwa pamoja na wananchi wote tuungane tuhakikishe tunairudisha hii sekta katika hali ambayo italeta faida tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii inatuingizia nchi hii mapato (*GDP*) ya asilimia 21, lakini sasa unakuta yameshuka ghafla bila hata ile *graph* kwenda iki-*dwindle*, yaani imeshuka chup! Kwa sababu hali siyo nzuri. Hata hivyo ilianza kushuka, kama msemaji aliyenitangulia alivyosema baada pia ya mapato haya kwenda kwenye kapu kuu. Sasa jambo kubwa ambalo linatakiwa tukubali ni kwamba kuna mambo yanayofanyika hata kwenye hesabu, unafanya *trial and error* halafu kama haitekelezeki, yaani *if it doesn't work mnaamua sasa kusimamia njia moja*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu uharibifu mkubwa wa barabara za kwenye hifadhi hauwezi kuja kuwapeleka watalii katika hali salama. Mtalii anapotoka kwao anataka hata akija kutembea au hata kama ni mtalii wa ndani, amalize *route* yake kwa siku. Barabara zile zimeharibika, kwa sababu hakuna namna ambavyo

wanapata hela kwa haraka kwenda kuzitengeneza. Hii inakuwa siyo rafiki na haina afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Serengeti zimeharibika, Manyara zimeharibika na hata zile barabara za kupanda mlima Kilimanjaro zimeharibika. Sasa hivi *route ile*, ule muda uliokuwa unatumika kupanda mlima umeongezeka. Bahati tu ni kwamba mvua imenesha sana, hawapandi mlima sasa hivi kwa wingi, kwa sababu kila saa ni mvua na ukungu. Kwa hiyo, naomba tu, mvua zikisita, hela ipatikane kutoka Serikali Kuu, barabara zikatengezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata kile kibanda cha Mandare ambacho ni maarufu wanapotulia wale watalii wakifika kule juu, kiliungua na mpaka leo hakijakarabatiwa kwa sababu hela haijapatikana kwa urahisi. Hili siyo jambo zuri kabisa. Ukienda Afrika Kusini, ukiwa unataka kwenda *Table Mountain*, kile kifaa cha kukupeleka *Table Mountain* kinashughulikiwa kama vile ni jicho, kwa sababu ni utalii unaotangazika. Sasa sisi hata hii ya kupanda tu mlima inashhindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi mlima Kilimanjaro kunakuwa kuna ile *rescue route*; kuna wakati ambapo baada ya mvua kunakauka, mtu akiwasha kiberiti au sijui ni watu wale wabaya tu waharibifu wanawasha tu bila kujijua, basi inabidi waende waka-rescue. Barabara zile hazionekani tena na hakuna njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata vyoo vile vya kwenye *route* haviko katika hali nzuri. Hivi Watanzania tuko *serious* kweli! Hii tumeipa Wizara na bado hawana hela na tunasema kwamba hii Wizara inatuingizia mapato. Mimi naleta hiki kilio hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono kila atakayesimama asemee hali ya kurudisha hii Wizara katika hali nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wao walikuwa wanatuingizia mapato ya nje asilimia 25 na hiyo iko katika utalii, lakini pia unakuta kwenye huduma za jamii

wanatuingizia asilimia 60. Zimekwenda wapi? Ajira milioni 5.6 ni pamoja na wale *porters*, nachanganya wote; wale wanaobeba, wale waongozaji, wako huko huko. Sasa hivi nimesema nawasemea wale akina mama kwa sababu vijana wao wako nyumbani na wao, wanangoja mahindi yakomae wachome na mama zao. Vijana walikuwa hawakai ndani, wote wako njiani wanawasindikiza watalii. Naomba sana, hili jambo lifanyiwe kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu, ni bahati mbaya sana kwamba sio Wabunge wote wamepata fursa ya kwenda kutembelea Mbuga za Wanyama au Hifadhi. Naomba ikikupendeza, wakati ambapo mnafikiria huko kwenye Kamati ya Uongozi, mtenge fungu kidogo tu, nasi Wabunge tutaongeza wenyewe, tuwe kama *group* la Wabunge, watalii wa ndani. Wenzetu huko nje wanafanya, kwa nini hapa nje ishindikane? Haina haja tuko hapa tunazungumza jambo ambalo hatulielewi wala hatuzungumzi pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walitutembelea Kilimanjaro, Wabunge walemvu. Walikuja, walihamasisha, waliwaleta ma-*pilot*, walikuwa wanaongozwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, tulipanda nao mlima. Wale ni walemvu na tukaweza kupanda mlima na leo wanatutangaza huko nje. Leo asubuhi umetuambia Mabalozi wa Utalii wametutembelea wengi, sasa wataenda kutangaza halafu wakifika tutatembeaje? Naomba jambo hilo liangaliwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu misitu yetu. Nimeona kwamba waliomba kifunguliwe chuo kingine cha misitu, lakini nakumbuka kulikuwa kuna Chuo cha Olmotonyi. Sasa naomba wanapokuja kujibu waseme kile Chuo cha Olmotonyi kiliendaje? Au hakiendi vizuri ndiyo maana kinatakiwa kufunguliwa chuo kingine? Maana iliombwa katika ile *report* ya Kamati ya Kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji wa kwanza aliletta ugomvi wa mifugo na Mbuga za Wanyama. Nataka niseme hivi, Mungu alipoumba, aliumba kila kitu viwili viwili.

Wanadamu waliumbwaa wawili, simba wakaumbwa wawili; yaani wanyama, ndege na kila kitu na akasema enendeni mkazaane mwongezeka. Pia akampa mwanadamu utashi akatawale wanyama wote hao. Sasa leo tunawajua ng'ombe wetu walivyo na Tanzania wengi wanafuga ng'ombe wa kuswaga. Yuko Rais wetu mstaafu alisema mnaposwaga ng'ombe, mswagaji anakonda na ng'ombe wanakonda. Hivi kwa nini tusifuge hawa ng'ombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, niiliwa naomba kama nchi yetu na Serikali za Mitaa zitoe maeneo ambayo yanatosheleza kufuga ng'ombe wakanenepeshwa tukawa ni wafugaji wazuri, tukawa na maziwa mazuri kuliko kuhesabu tu kwa idadi, kuliko kwenda kuingilia wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Naomba tuwapatie hizo hela wakarejeshe. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Ziddu Kungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Cosato David Chumi ajandae.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa nianze na kuipongeza Wizara iliyoko chini ya Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Ndumbaro pamoja na Naibu Waziri kwa namna wanavyoweza kufanya kazi vizuri; na kwa ushahidi tu wa pekee kwa sababu pia hatu tarehe 22 aliweza kutembelea kwenye Jimbo langu hasa kwenye Kata tatu. Kata ya Kalulu, Jakika na Matemanga. Amejionea mwenyewe namna tulivyokuwa na kero kubwa ya tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nianze tu moja kwa moja na kueleza kwenye jimbo langu halafu baadaye nifuate Taifa. Jimbo la Tunduru Kaskazini kwa maana ya Wilaya ya Tunduru, tuna hifadhi za Taifa tatu na pia tuna hifadhi ya misitu ya asilia moja kwa maana ya Mwambesi na vile vile tuna hifadhi za wanyamapori za jamii

mbili, yaani Nalika na Chinguli. Vile vile tuna hifadhi za misitu asilia ya vijiji, saba. Kwa hiyo, utaona ni namna gani wilaya hii ilivyozungukwa na hifadhi za wanyamapori. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, yako maeneo mahususi kwa ajili ya ufügaji, lakini pia yako maeneo mahsusii kwa ajili ya ukulima na sisi wilaya yetu ni mahsusii kwa ajili ya kilimo. Tunalima korosho, mpunga, ufuta mbaazi na kadhalika, lakini kero kubwa ambayo tunaipata kutokana na kilimo ni kutokana na wanyama wakali na waharibifu, yaani tembo. Nikizungumzia athari kubwa ambazo tunazipata kutokana na wanyama hawa waharibifu na wakali, kwa miaka mitano tumepoteza maisha ya watu 24 kutokana na tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015/2016 waliuawa watu wawili na tembo; mwaka 2016/2017 waliuawa watu wawilli; 2017/2018 waliuawa watu saba na tembo; 2018/2019 waliuawa watu wanne; na 2019/2020 waliuawa watu tisa. Kwa hiyo, utaona takwimu ni namna gani watu hawa wanavyozidi kuongezeka kuuawa. Kwa hiyo, kero hii isipotatuliwa kwa umakini maana yake tunakwenda kupoteza nguvu kazi kubwa kweli kweli. Vile vile wanyama hao hao waharibifu kwa maana ya tembo, wameacha vilema vya kudumu kwa watu 20 kwa miaka mitano tu. Vile vile, ekari zilizoharibiwa na tembo zinazidi 4,679. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nakueleza uone ni kwa sababu gani tuna kero hii kubwa ya tembo katika wilaya yetu ya Tunduru. Sababu kubwa moja ni wafugaji kwenda kufuga katika maeneo ya hifadhi za wanyamapori. Pili, wakulima kuvamia maeneo ya misitu na pia kwenda kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya mapito ya wanyama (shoroba).

Vilevile tuna changamoto kubwa sana ambayo inasababisha kutokupunguza tatizo hili kubwa ambalo linatupata sisi kutokana na kwamba tunao Askari wa Wanyamapori ambao wako chini ya Halmashauri. Sasa tunaweza kuona kabisa Halmashauri zetu hazina bajeti kubwa ambayo inaweza kutatua changamoto kubwa ama

ika-facilitate kwa asilimia 100 Askari hawa wa Wanyamapori kwenda kutatua hizi changamoto kubwa za watu kuvamiwa na mashamba yao. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Askari wasiozidi tisa katika wilaya yenye kata 39 na vijiji 57, lakini askari hawa tisa wanaokwenda *field* ni saba tu. Kwa hiyo, utagundua tuna vijiji 157 lakini tuna askari saba; na kwa siku kuna kero ambayo wanatoa taarifa vijiji 15 mpaka 20 ambayo vinahitaji msaada wa kwenda kusaidiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Askari wa Wanyamapori naona kuna tatizo la kimfumo kwamba Askari wa Wanyamaporи wako chini ya Halmashauri; na tunajua kabisa Halmashauri zetu hazina uwezo wa kutosha.

Kwa hiyo, nashauri Askari wa Wanyamaporи hawa wawe chini ya Wizara kwa sababu tunakumbuka na tunafahamu mwanzo walipokuwa wako chini ya Wizara, maana yake ni kwamba walikuwa wanapata magari ya kutosha, walikuwa wana silaha za kutosha, lakini pia tulikuwa na askari wa kutosha. Kwa sasa, kwa sababu wako chini ya Halmashauri, maana yake bajeti yao ni ndogo. Hakuna Halmashauri inaweza kutenga fedha kwa ajili ya Askari hao wa Wanyamaporи. Tuna tatizo kubwa mno. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwa mfano kwenye Wilaya yetu ya Tunduru, kitengo hiki cha Askari wa Wanyamaporи wana silaha tisa, lakini silaha hizi ni za kizamani kweli kweli, maana yake zina zaidi ya miaka 40. Kwa hiyo, utakuta mara nyingine wakienda nazo porini zinakataa hata kufanya kazi.

Kwa hiyo, ndiyo maana nashauri hawa Askari wa Wanyamaporи wawe chini ya Wizara kwa sababu, Wizara ina Askari ambao wana silaha za kisasa kama vile *TAWA* na Ngorongoro pamoja na *TANAPA*. Pia utaona, pamoja na silaha hizi ambazo ni kuukuu, zina zaidi ya miaka 40 bado pia hata risasi zake pia zina bei ghali. Kwa maana ya risasi moja inanunuliwa kwa shilingi 23,000 mpaka shilingi 25,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wale wa TAWA wao wana silaha za kisasa, lakini pia risasi moja inauzwa kwa bei rahisi sana, shilingi 3,000. Kwa hiyo, Askari wa Wanyamapori wakiunganishwa na TAWA tunakwenda kuondoa hili tatizo kubwa ambalo linatukabili kwenye wilaya yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kushauri, kama wilaya yetu ni mahususi kwa kilimo, naomba sana, hawa wafugaji ambao wanaingia, basi wfuate utaratibu ambao unawekwa na Serikali. Kwa mfano, Halmashauri yetu imetenga vitalu vinavyozidi 200, lakini cha ajabu hawa wafugaji wakiingia na ng'ombe hawaendi kufuga kwenye vile vitalu na badala yake wanakwenda kufuga kwenye hifadhi za wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndiyo tatizo ambalo linasababisha kupata shida kubwa ya tembo kuwasumbua wananchi pamoja na kuwaua kwa sababu, wanapokwenda kufuga kwenye hifadhi zetu wale ng'ombe wanakuwa na harufu za dawa ambazo zinawakinga wao wasishambuliwe na wadudu. Kwa hiyo, ile harufu inawafanya wanyama hawa wakali kutoka nje ya hifadhi na badala yake kwenda kwenye maeneo ya binadamu. Sasa hili ni tatizo kubwa mno. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri, jambo la kwanza, kuwe na sheria ambayo inaweza ikawa kali kwa sababu tunaamini kabisa Watanzania imeshafika *stage* kwamba tukiwa na sheria laini, sheria nyepesi, hatutekelezi hiyo sheria. Kwa hiyo, mimi ningeomba kuwe na sheria ngumu... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Mrisho, Mashaka Gambo, ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa maoni yangu. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ili niweze kutoa maoni yangu katika Kamati ya Maliasili. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekuwa wakitoa ushirikiano wa kutosha kwetu sisi Wabunge mara tunapofikwa na matatizo. Niendelee kuwaomba waendelee hivyo hivyo kutusaidia sisi Wabunge wenzao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuishukuru Serikali kwa kuipatia Wilaya ya Meatu shillingi millioni 51 kwa ajili ya kulipa fidia na kifuta machozi. Fedha hii imelipwa kwa wananchi 272 kati ya wananchi 520, lakini malipo haya yamefanyika kwa walioathirika kwa kipindi cha nyuma kwa mwaka 2017/2018 na 2018/2019, hivyo kuendelea kuwepo kwa madeni kwa wananchi walioathirika kwa 2019/2021. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango hivi vimeduwa ni vya muda mrefu. Naomba kanuni ile ya mwaka 2011 ifanyiwe marekebisho ili viwango hivi viendane na hali halisi kwa kuwa haviridhishi wala haviakisi thamani ya uharibifu unaofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, mimi nilipenda Serikali ijikite zaidi katika kuzuia uharibifu ambao unasababisha vifo na pia kuingizia Serikali gharama kubwa. Tunavyoolekea, Serikali inaweza ikashindwa kumudu kulipa fidia na kifuta machozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa mikakati ambayo imekuwa ikiiweka. Imekuwa ikiandaa vijana kwa kuwapa mafunzo ya namna ya kukabiliana na wanyamapor wakali na waharibifu ambao pia

wanasababisha vifo kwa wananchi, lakini mafunzo haya yamekuwa yakinidu kwa muda kidogo na baadaye yanashindwa kwa sababu wale tembo wamekuwa wakizoea zile mbinu na kuleta uthubutu kufanya uharibifu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niungane na Kamati ya Maliasili kwa maoni yake kwamba ni vyema kuimarisha utendaji wa *TAWA* ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo masuala ya kibajeti. Naamini *TAWA* inao watumishi wa kutosha. Katika Pori la Akiba la Maswa hadi Januari 21, kulikuwa na watumishi 87. Watumishi hawa wanatosha; wakiwezeshwa kikamilifu wataweza kufanya doria zao kikamilifu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe maoni yangu, *TAWA* wajikite zaidi katika ile miezi ambapo sasa wananchi wameanza kuivisha mazao yao kwa kuweka doria zaidi ili tuweze kuokoa yale mazao yasifanyiwe uharibifu, lakini hata kuzuia vifo. Katika Wilaya ya Meatu miaka miwili iliypita wananchi 16 waliuawa na wananchi tisa waliuawa na tembo, lakini kama tukiweza kukabiliana vifo vitapungua na Serikali itapunguza gharama inayotokana na kulipa gharama za uharibifu huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mwananchi anayependa kufanyiwa uharibifu ili alipwe fidia. Hakuna ndugu anayependa ndugu yake auawe ili eti alipwe shilingi milioni moja kwa ajili ya kufuta machozi. Tuwekeze zaidi katika kuzuia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbinu nyingine nilitaka Serikali katika kukabiliana na wanyamapori wakali iwezekeze zaidi katika kutumia teknolojia kwa baadhi ya tembo, kuwawekea vifaa maalum vya kielektroniki kwa lengo la kufuatilia mienendo yao. Kazi hii imefanyika katika Pori la Akiba la Maswa katika *Ranch* ya Wanyamapori ya Makao; tembo 18 waliwekewa *radio call.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limeshindwa kuleta ufanisi kwa sababu, kwanza *access* ilitolewa kwa maafisa

wanne akiwemo *DGO* wa Meatu na walifanikiwa kuwaona wale tembo wakitoka kwenye maeneo kuingia katika maeneo ya wananchi, lakini changamoto kubwa hata wakiwaona, hawana magari, hawana silaha. Ni kwa namna gani wataweza kwenda kukabiliana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, maeneo manne yaliweza kubainika ambapo tembo wanaweza kutoka. Eneo la N'hangalililopo Jimbo la Kisesa, Mwanyaina sehemu ya Landani, Sabha na Witamia.

Ombi langu kwa Serikali, kijengwe kituo Mwamongo katika Jimbo la Meatu kwa Askari wa Wanyamapori, kijengwe Kituo cha Askari katika eneo la Landani Mwanyaina katika Jimbo la Meatu. Tukifanya hivyo tutarahishia kuweza kuwarudisha wanapoonekana katika zile *call/walizowekewa*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru mwekezaji Mwiba, kupitia *Frederick Conservation*, walifadhili ule uwekezaji wa kuweka *radio call*. Nami naamini wako tayari kuendelea kuleta ufadhili huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha *TAWA* naishauri Serikali ikubaliane na ile kanuni waliyoomba ibadilishwe katika kikao chao walichokifanya cha ujirani mwema *TAWA* na Maafisa Wanyamapori Meatu kwamba, asilimia 40 ya fedha inayotoka kwenye asilimia 25 ya uwindaji ipelekwe *TAWA* ili kuongeza nguvu zaidi. Kwa maana hiyo, wakiwa huko watanunua vifaa, watakuwa na magari kuliko urasimu unaofanywa na ofisi ya Mkurugenzi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo. Tutamalizia na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami kwa kuanza, naunga kabisa mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wakala wa Misitu Tanzania kwa niaba ya watu wa Mafinga kwa ushirikiano wao chini ya usimamizi wa Chama cha Mapinduzi tumeweza kujengewa mabweni mawili. Hivi ninavyozungumza tutapewa fedha kiasi cha shilingi milioni 130 kwa ajili ya kutengeneza lami nyepesi pale kwenye eneo letu la soko kubwa katika Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kutoa shukrani zangu za dhati, lakini yale mabweni tuliyojenga ni ya *girls*. Sasa *boys* wanatuuliza, pale *Luganga Secondary* na *Changarawe Secondary* wanasema mbona sisi mmetusahau? Kwa hiyo, natumia fursa hii pia kuwasilisha kama ombi kwa Serikali kwamba kama tumeanza na *girls, which is good*, kwa sababu, wako kwenye *higher risk*, basi tuwaangalie pia na *boys*. Nitumie nafasi hii pia kutoa wito kwa wawekezaji wengine walige Wakala wa Misitu Tanzania kwa sababu, tunashirikiana nao vizuri sana katika suala zima la *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumekuwa tukishirikiana nao, wakati mwingine tunaazima ma-*grader* kutoka *Sao Hill* sisi Halmashauri tunajaza mafuta tunatengeneza barabara zetu. Japokuwa mwaka huu walikuwa wametingwa sana, sasa naomba wakipunguza kutingwa kidogo, watusaidie ma-*grader* sisi tutajaza mafuta, tutapunguza kidogo kero ya barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, napenda nifahamishe Bunge lako na Watanzania kwa ujumla kwamba, msitu wa *Sao Hill*, kutokana na mapato yake, Serikali katika misitu inapata asilimia 35 kutoka katika Msitu wa *Sao Hill* tu

ambapo Makao Makuu yake yako pale Mafinga. Nitumie nafasi hii kuwashukuru sana kamati, walifanya pale ziara na hata katika taarifa yao wameandika na wameendelea kusisitiza umuhimu wa kuwa na *campus* ya Chuo cha Misitu pale Mafinga, kwa sababu, itasaidia hata wanafunzi kwenda kupata mafunzo kwa vitendo katika ule msitu ambao ni mkubwa katika Afrika Mashariki na Kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na ukubwa wa msitu huu ambao kwa mujibu wa takwimu kwa mwaka tunapata karibu takribani shilingi bilioni 42. Kati ya mwaka 2015 hadi 2020 tumeppata kama shilingi bilioni 216 kwa maana Serikali imepata hizo fedha. Hata hivyo, kasi ya wavunaji kwenda msituni imeendelea kupungua kutokana na wingi wa tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza hapa, kuna tozo 13 katika sekta ya misitu. Tozo mojawapo ni *LMDA*. Tozo hii ilianzishwa ili kuisaidia Serikali kupanda miti kwa sababu kwa muda mwingu lile shamba halikupanda miti. Sasa hivi miti imepandwa kwa wingi, naishauri Serikali ingetoa tozo hii ili kusudi kupunguza gharama za watu kwenda msituni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni tozo katika *VAT*. Najua tutakwenda kwenye Muswada wa Fedha. *VAT*ni Kodi ya Ongezeko la Thamani, lakini wananchi wa Mafinga na Mufindi anapoenda kukata tu ule mti nao anatozwa *VAT*. Ni ongezeko gani la thamani limeongezeka katika ule mti? Sasa matokeo yake wavunaji hawaendi kuvuna msituni, Serikali haipati mapato. *Of course* wanaenda kuvuna kwa wananchi ambao miti haitoshelezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kuna vitu amesema hapa Mheshimiwa Nape, hata katika wanyamapori, ziko tozo ambazo nadhani tuziangalie kwa macho mawili, kwa sababu, inavyokuwa sasa, yaani msitu unao, fedha hauna. Sasa unakosa shilingi kumi ambayo bora uikose shilingi kumi ambayo ingekuzalishia wewe shilingi 100 katika mtiririko mzima wa Ongezeko la Thamani. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, suala la *VAT*litazamwe sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ipo katika masuala ya wanyamapori, vitalu vingi sasa vimekaa *idle*. Vikikaa *idle* madhara yake wale watu wanaokuwa wanakodishwa vitalu, mojawapo ya masharti ni pamoja na kufanya uhifadhi katika vile vitalu. Sasa vikikaa *idle* maana yake kwamba uhifadhi unakuwa haifanyiki, vinashuka thamani. Kwa hiyo, Serikali ifike wakati tuangalie, kuna wakati bora ukose shilingi kumi ukapata shilingi 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni migogoro ya wakulima na wafugaji. Nasema hapa, bila kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, tutaendelea kila mwaka kuongeza maeneo. Nina takwimu hapa kidogo tu; katika Tanzania sisi, nchi yetu, *population wise*, yaani *population density*, sisi ni watu 67 per kilometer square. Nchi kama Rwanda ni watu 525 per kilometer square. Burundi 463 per kilometer square. Malawi 205 per kilometer square. Kwa hiyo, ukiangalia *population density* sisi siyo kwamba tuko over populated, ila tunachotakiwa kufanya ni kitu kimoja; tunaanza kwenye kilimo. Lazima tulime kilimo chenye tija. Hiki kilimo cha kudhani kwamba ukilima ekari nyingi ndiyo utapata mahindi mengi, hakitatusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ufugaji lazima tufuge ufugaji wenye tija. Siyo kwamba ukiwa na ng'ombe 10,000 ndiyo utapata maziwa mengi. Sasa kutokana na kwamba hatujawekeza tija katika kilimo kwamba, ekari moja inakupa gunia tatu, sasa kumbe eka moja ingekupa gunia 20 usingelima eka kumi. Sasa matokeo yake ili upate magunia 30 unalima ekari kumi; ili upate nyama nyingi, unafuga ng'ombe wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa wito kwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi wawasaidie wakulima na wafugaji wa nchi hii wafuge na kulima kwa tija. Vinginevyo ardhi ya nchi hii haitakaa itoshe. Watakuja watu wa Maliasili na Utalii hapa mtawasulubu. Hao ng'ombe hawataacha kwenda kwenye hifadhi na migogoro ya wakulima na wafugaji haitakaa iishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho, ni lazima tulime kwa tija, eneo dogo lizalische sana; tufuge kwa tija, eneo dogo upate mifugo inayokupa tija. Kinyume chake, nchi hii tutakuwa kila siku tuna-*declare* kuongeza maeneo ya wakulima na wafugaji wakati *we are not overpopulated* kama nchi nyingine ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge. Bila kufanya hivyo, migogoro haitakwisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, tutamalizia na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nishukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii na hasa ukizingatia kwamba, utalii upo Kaskazini. Karibu asilimia 80 ya mapato yote ya utalii yanatoka Kanda ya Kaskazini; na huwezi kuzungumza Kaskazini bila kuizungumza Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitajielekeza kwenye masuala machache. La kwanza, tunafahamu sote kwamba *Corona* imetuathiri sana kama Tanzania. Nilikuwa nasikia taarifa ya Waziri kwenye ukurasa wake wa saba na wa nane bado anazungumzia kwamba utalii unachangia pato la Taifa kwa asilimia 17 na unachangia fedha za kigeni kwa asilimia 25. Nadhani hizi taarifa ni za zamani sana kwa sababu kwa namna *Corona* ilivyotuathiri, mapato yetu yameyumba sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia taarifa zilizopo, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, *TANAPA* mpaka kufikia mwezi Februari, walikusanya asilimia 13, Ngorongoro asilimia 21 na *TAWA* asilimia 38. Ukiangalia pia taarifa ya Mheshimiwa Waziri ya leo kwenye ukurasa wake wa 10 na wa 11 anatuambia hadi kufikia mwezi wa Nne *target* yetu ilikuwa ni shilingi bilioni 584 na sisi tumekusanya shilingi bilioni 89 ambayo ni sawa sawa na asilimia 15, lakini ukienda kuangalia

pia kwenye *World Tourism Organization*, tunaambiwa kwamba mchango wa utalii kwenye *GDP* umeshuka kutoka asilimia 17.5 mpaka asilimia 11.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza, bado Wizara ya Utalii wanakwenda kuongeza tozo kwenye maeneo mbalimbali. Tukiangalia nchi zote za Afrika Mashariki; Uganda wamepunguza *park fees* kwa asilimia 50, Kenya wamepunguza *park fees* kwa asilimia 47, lakini Tanzania tunaongeza. Vilevile cha kushangaza, ukiangalia dunia nzima sasa hivi inahangaika kwenye kutoa ahueni kwenye sekta ya utalii, lakini Tanzania tunaongeza tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo tangazo hapa la *TANAPA* ambalo limetokana na *GN* ya Serikali ya tarehe 29 Juni, 2020 ambalo wanaongeza kipindi cha *High Season* tozo kutoka dola 60 mpaka dola 70 ambazo bado hazijaanza, wanategemea zianze tarehe mosi mwezi wa Saba, yaani mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia *TANAPA* hao hao kuna tozo nydingine ambayo pia wanakuja kuiongeza; ni tozo mpya hii, wanaita *Land Base, Land Fee*; yaani mtu amewekeza kwenye hifadhi zetu mfano Serengeti au maeneo mengine, analipa *Concession Fee*, kila mgeni aliylala pale analipa dola 50. Leo *TANAPA* wanakuja wanaongeza pia, inabidi mtu anayeweka kule kama ni *Seasonal Camp* inabidi alipe dola 2,000, kama anaweka *Permanent Tented Camp* alipe dola 20,000, kama ana *lodge* yake, alipe dola 50,000. Kwa hiyo, unashindwa kuelewa tatizo letu ni niní? Kila tukikaa tunafikiria kuongeza tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tatizo hili lipo *TANAPA* kwa sababu tunazo hifadhi 22 ambazo ziko chini ya *TANAPA*. Hifadhi ambazo zina uwezo wa kuijendesha hazizidi tano, hifadhi nydingine zote zinategemea hifadhi tano ziweze kuijendesha. Matokeo yake sasa kila wakilala wakiamka wanaongeza tozo Serengeti, wanaongeza tozo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba ni vizuri Serikali ikaiona changamoto hii ya *Corona* kwa uzito wake na kuangalia uwezekano wa kukaa vizuri na wenzetu wa *TANAPA* ili wasiweze kuongeza sana tozo kama ambavyo wanafanya. Mambo unayoyaona haya hayapo maeneo kama *NCAA*, wao mambo haya ya *Land Base* hayapo, lakini ukienda *TANAPA* kule unaweza ukayakuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona bado tuna kazi ya kufanya, Wizara ya Utalii ipitie hifadhi zote ambazo tunazo. Hifadhi ambazo hazizalishi, mfano mzuri ni Burigi Chato, hebu mtuletee taarifa hapa, ile hifadhi toka imeanzishwa imepokea wageni wangapi? Imeingiza kiasi gani? Mwisho wa siku pia inatumia gharama kiasi gani? Siyo tunaanzisha hifadhi nydingi, tunajiri watu wengi, tunapeleka gharama nydingi, halafu mwisho wa siku tunakwenda kuumiza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima mfahamu kwamba hizi gharama mnazoongeza, anayepewa hizi gharama ni mtalii. Ukimpa *tour operator*, anachokifanya yeye, anaingiza kwenye gharama zake, mtalii anayekuja anaongezewa gharama na kufanya *destination* inakuwa *very expensive*, kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri tukaliangalia vizuri suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine pia ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusiana na gharama za kupima *Corona*. Ukienda Kenya kupima *Corona* ni dola 30 hospitali za Serikali, *private* dola 50 ukija Tanzania dola 100. Sasa nashindwa kuelewa, hivi hata *Corona* pia ni fursa kwenye nchi yetu au ni changamoto!

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani na lenyewe pia tuliangalie vizuri, kwa sababu Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kafanya kazi kubwa na nzuri sana kuhakikisha kwamba tunakubaliana na dunia kwamba *Corona* ipo, tutachukua chanjo. Sasa hivi dunia imeanza kuelewa na tunaamini muda siyo mrefu tutaanza kupata wageni wengi zaidi. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najuliza pia, kwa nini Tanzania tuna kituo kimoja tu cha kupimia Corona, pale Dar es Salaam? Ukienda kwenye *airport*, sawa, wanachukua zile *rapid test*; ukienda Kenya wana vituo 47. Nadhani ni vizuri mambo haya tukayaangalia vizuri zaidi. Naona muda ni mdogo sana na hizi mada ni *very serious...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Imeshagonga kengele ya pili.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aboubakari Damian Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kufunga dimba, nami nichangie katika Wizara yetu ya Maliasili na Utalii.

Kama kawaida, kwa dhati ya moyo kwa kweli napenda kushukuru na kumpongeza shemeji yetu Wana-Kilombero, Waziri wetu Dkt. Ndumbaro kwa maana mama yetu anatoka kule na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary kwa sababu hawa walikuja Jimboni kwetu mapema sana na wakatusaidia kufanya jambo kubwa kabisa kuliko mambo mengine makubwa ya utalii na kulinda rasilimali ambayo haijawahi kufanyika maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza watu waliona askari wakifukuzwa hadharani baada ya kupatikana ushahidi wa kutosha kwamba askari wale walikuwa wanatuhujumu na kunyanyasa wananchi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwenye jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nashukuru kwa suala la soko. Alijibu hapa juzi Mheshimiwa Waziri kwamba yale maelekezo yake ya kutujengea Soko la Samaki zuri pale kwenye Daraja la Magufuli, yapo kwenye bajeti hii. Nami nawaomba Waheshimiwa Wabunge jamani tuchangie tuboreshe mwisho wa siku tupitishe bajeti hii ili Wana-Kilombero wapate Soko hili la Samaki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nataka nikuambie, kuna kijana mmoja hapa wa Kilombero, anasoma Chuo Kikuu hapa, ni *engineer amechora* soko zuri sana kama ishara ya *Panton lililowahi* kuzama zamani na wananchi na likaua watu. Ametengeneza soko *simple* la aina ile ambalo litakuwa na eneo la kupigia picha ili kuvutia watu wanaotaka kupiga picha kuonekana kwa daraja lille, lakini kuonekana kwa viboko na kuonekana kwa mamba ambao wanaenda kuota juu katika Mto Kilombero. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na hata Katibu Mkuu wetu, nimeambiwa analifanya kazi suala lile la ombi letu la kupata eneo la mita 50 katika Tarafa ya Mang'ula *Corner*. Nimemwomba sana Mheshimiwa Waziri na namwomba tena Katibu Mkuu wa Wizara mfikirie, kwa sababu Mkandarasi yuko *site*, ameanza kutandika lami. Sasa katikati pale kuna eneo linaitwa Mang'ula *Corner*, barabara imejikunja sana. Kunyoosha ile barabara Mkandarasi ameshindwa kwa sababu eneo ni la kwenu, anaambiwa zile mita 50 zilizoingia ni za Udzungwa kwa hiyo hawezikunyoosha barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, nitafurahi sana akirudi hapa aktiuambia kwamba tumepatiwa eneo lile na Mkandarasi; na Waziri wa Ujenzi ametuambia wazi kwamba akipata jibu lako anaweza kumwambia Mkandarasi akachonga ile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sisi tulipata nafasi, mimi na baadhi ya Wabunge kabla hatujawa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa na kaka yangu Mwana-FA

tulipanda Mlima Kilimanjaro mwaka 2019; na tulipofika pale juu tulifikisha picha ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kama ishara ya kumuenzi kwa mazuri ambayo alifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kushuka katika Mlima Kilimanjaro tuliandika mawazo na maoni yetu. Maana wageni wengi wanaotoka na tunaokutana nao kule juu; ni safari moja nzuri lakini ni hatari sana na safari ngumu. Wanafika pale juu, wanapopiga picha kwenye ule ubao pale kileleni, tulishauri kuwe na picha ya Baba wa Taifa upande wa kushoto na upande wa kulia wa kile kibao kuwe na picha ya Rais ambaye yuko madarakani. Naomba Wizara wajaribu kulifanya kazi suala hili. Kufika pale juu, kileleni siyo mchezo. Sasa mtu akifika pale, anakutana tu na maandishi kwamba "Hongera umefika juu ya kilele cha juu zaidi Afrika." Sasa kungekuwa na zile picha; ya Baba wa Taifa na Rais ambaye yuko madarakani, ingekuwa jambo zuri sana kwa utambulisho wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepanga pia na baadhi ya Wabunge na tutamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kwamba mwaka huu Mungu akipenda tutapanda tena Mlima Kilimanjaro, tutapandisha picha ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuionyesha Afrika na kuiambia dunia kwamba Tanzania ina thamini akina mama, inapenda wanawake na kwamba wanawake wanaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale Wabunge ambao wameagana na nyonga zao, wako tayari kupanda Mlima Kilimanjaro, wanione, tuliongeze lile *group* ili tupande pale juu tufikishe picha ya Mheshimiwa Mama Samia pale juu kileleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, mimi mwenyewe nilishapanda huo mlima, wala huna haja ya kuagana na nyonga Waheshimiwa Wabunge. Mjiandae tu, hata ambaye nyonga yake hawajaagana, anao uwezo wa kupanda mlima.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa sawa. Yeyote ambaye yuko tayari, tupande wote Mlima Kilimanjaro na tufikishe picha hiyo ya Mheshimiwa Mama Samia kumuunga mkono kwa mambo mazuri anayofanya katika nchi yetu na hususan mambo yale ambayo yanaongeza sekta ya utalii kwa ujumla na kuondoa zile dhana potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimdokeze Mheshimiwa Waziri jambo moja. Nimekuwa nikipata meseji nyingi sana kutoka kwa Kiongozi wa Wavuvi wa Ifakara anaitwa Shaibu Majiji; baadhi ya askari tena wameanza kunyanyasa wavuvi kinyume na maelekezo yako. Ulielekeza wavuvi wale wakienda kuvua, wavue kwa utaratibu kule kwenye maeneo ya hifadhi; wavue kwa nyavu zinazotakiwa, wavue samaki waondoke nao, wasijenge. Walikubali kufanya hivyo na walifurahi ahadi yako ya kujenga soko. Sasa kuna maneno maneno yameanza, kwa hiyo, naomba ulifatilie hilo, uone namna gani hawa askari wetu wazuri wa *TAWA* ambao wengine uliwapandisha vyeo, wanaoweza kusimamia maelekezo yako vizuri.

Mheshimiwa Waziri, lingine tunaloliomba, sisi ukivuka daraja la Magufuli kuna eneo linaitwa Limaomao, liko karibu zaidi na Mbuga ya Nyerere na zamani *Selous*, tulikuwa tunaomba Wizara yako ifikirie namna ambavyo mnaweza mkaweka geti pale, kwa sababu ni njia rahisi sana ya *game drive* ya kuingia Nyerere na kwenda *Selous* na itakuwa imeongeza mapato yetu. Ni kwamba ukivuka daraja la Magufuli pale kushoto, kuna njia zamani ilikuwa inatumika kwenda Mbuga ya *Selous* ambayo sasa hivi ni Nyerere. Kama tukipata geti pale, itatusaidia kuchangamsha mji wetu wa Ifakara na Jimbo letu la Kilombero. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, lingine ni tembo. Ukvuka Daraja la Ruaha, unaanza Jimbo la Kilombero kilometra takribani 35 unapakana na Mbuga ya Udzungwa. Mbuga hii ya Udzungwa ina tembo wengi sana na ni hifadhi yetu, nami naelewa *concern* yenu ya kulinda hifadhi yetu kwa sababu siyo mali yenu ni mali yetu sisi sote wananchi. Kuanzia hizo

kilometra 35, tembo wanavuka kutoka Udzungwa wanaiongia chini upande ambao wananchi wanaishi. Changamoto ni kubwa kweli kweli. Naomba mwapatie askari wale zana ili waweze kufika kwa wakati maeneo ya wananchi kuwafukuza tembo wanavyoingia mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna *issue* ya ushoroba na kwamba mmejenga daraja pale kama Serikali la kuhakikisha mnapitisha tembo kwamba wale tembo wanaenda kusalimiana, yaani kuna mashemeji wako Udzungwa, kuna wake sijui wako kule Nyerere, kwa hiyo, wanapita kila mara kwenda kusalimiana huko kama alivyosema Naibu Waziri, mmetengeneza njia maalumu chini ya daraja, mmejenga kwa daraja zuri kwamba wanavuka vizuri; mnawatengenezea *fence*. Tunaliunga mkono jambo hilo lakini kwa kweli kwa dharura sasa hivi, Askari wetu wale wanatakiwa kupewa magari, kupewa mafuta wafukuze tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimeenda kwenye msiba, tembo ameua mtu pale; na *issuesana* siyo fidia ndogo au fidia kubwa; ni mbinu gani tunafanya kuhakikisha tembo hawaui watu? Tembo wanapita kwenye njia yao, wakikua banda la mtu la udongo anaishi humo ndani, wanagonga, wanaenda mbele huko kula mpunga. Tembo wanapenda mpunga kweli Mheshimiwa Waziri. Sasa wasije wakatutia njaa kule tunakoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nisiseme mengi, nataka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge hapa watusaidie tuitishe hii mambo ili tupate lile soko na ile *issue* ya Mang'ula *Corner*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa uchangiaji. Tutakaoanza nao jioni leo ni Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Twaha Mpembwenwe, Mheshimiwa Anna

Richard Lupembe, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na wengine wataendelea kultwa kadri muda wetu utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao hawakupata fursa ya kuingia asubuhi wameingia baada ya tangazo la wageni. Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Rashid ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mipango Dodoma, wanaotoka Jimbo la Kiwani Pemba wakiongozwa na Spika wa Bunge wa Chuo hicho Ndugu, Muslim Chumu. Karibu sana karibuni sana wageni wetu.

Tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni Watendaji wa Kata kutoka Jimbo la Msalala Mkoani Shinyanga wakiongozwa na Ndugu Abel Kaholwe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Makete Mkoani Njombe, wakiongozwa na Ndugu Tegemea Mbogela. Karibuni sana. (*Makofi*)

Vile vile wapo wageni watano wa Mheshimiwa Aloyce Andrew ambao ni wadogo zake wanne na shemeji yake kutoka Mkoani Tabora wakiongozwa na mdogo wake ndugu Isaya Kifuka. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, nao ni wageni 29 ambao ni walezi wa watoto na wamiliki wa Vituo vya Kulelea Watoto Yatima kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa na Dodoma, wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake, wakiongozwa na Sister Prisila Zakaria. Karibuni sana na tunatambua mchango wenu wa kutusaidia kulea hawa watoto yatima. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.15 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kit*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi. (*Makofi*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya  
Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendea)*

**MWENYEKITI:** Ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru ninyi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Bunge la Kumi na Mbili, kunidhibitisha kuwa Mwenyekiti wa Bunge hilli (*Makofi*)

Pia nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati ya Uongozi chini ya uongozi dhabiti wa Spika wetu, Mheshimiwa Job Ndugai, pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Vilevile nakishukuru Chama changu kwa imani kubwa ambayo imenipa kwa kusimama hapa leo. (*Makofi*)

Ahsante Waheshimiwa Wabunge. Tunaanza na Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembewwe ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nikupongeze, umeenea vizuri. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza mchana huu kwenye sekta ya maliasili. Naomba nianze kwa kuungana na waliozungumza asubuhi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa sekta ya utalii kwa kazi nzuri wanazofanya kuinua na kuendeleza Sekta ya Utalii pamoja na changamoto mbalimbali zikiwepo *Covid 19* zilizoikabilii Taifa letu mwaka jana 2020 na sehemu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze zaidi na ninaona hili analifanya sana Naibu Waziri la kuhamasisha utalii wa ndani. Tukiweza kwa kweli kuwafanya Watanzania wengi kufanya utalii kwenye hifadhi zetu, tutakuwa tumechangia kwa kiwango kikubwa sana uchumi wa nchi na vile vile tutakuwa tumewafanya wananchi wafaidi rasilimali zao. Haipaswi watu tulio na rasilimali nyingi namna hii tuendelee kuzitazama kupitia runinga, kwenye picha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nami niwashajiishe Wabunge wenzangu, kinachofanywa na *TANAPA* pale nje tukitekeleze. Wanatuomba tukashiriki Ngorongoro. Mimi nipo tayari, nadhani na Wabunge wengi watakuwa tayari kwenda Ngorongoro, kama njia ya kuimarisha utalii wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza kwa kuanzisha *TFS* kama taasisi ya kusimamia eneo la misitu. Yako maeneo ya kuzungumza kwa ajili ya kuboresha, lakini kwa ujumla taasisi hii inatimiza wajibu wake vizuri maeneo yaliyo mengi ukiacha changamoto za hapa na pale, hasa nguvu inapotumika kupita kiasi. Ushauri wangu kwenye maeneo haya hasa *TFS* na maeneo mengine, kuendelea kutoa elimu. Tusichoke kutoa elimu kwa wananchi wetu na Umma kwa ujumla ili kuimarisha uvunaji wa miti au misitu endelevu na kuendelea kupanda miti mingine ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inabaki kuwa salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitegemea sera za mabavu hazitatufikisha mbali sana, utaendelea kutengeneza uhasama kati ya wananchi na Serikali yao. Jambo ambalo kwenye eneo hili linanipa shida kidogo ni pale ambapo mtu ameotesha miti yake mwenyewe, wala *TFS* hawakuja kumsaidia, akitaka kuvuna mti mmoja au miwili, anawekewa *conditions* nyingi bila sababu za msingi. Nilidhani hapa tungewatambua watu ambao wamejitokeza kuotesha misitu na wanapotaka kuvuna kwa kweli wasiandamane na masharti. Haya iwakute wale ambao wanakwenda kuvuna bila kuchangia kuotesha miti hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumza ni juu ya utalii kwa ujumla kitaifa na ninataka niangalie kanda zetu. Naipongeza nchi yetu kuwa na rasilimali za utalii karibu kila kona ya Tanzania; Kusini mpaka Kaskazini, Magharibi hadi Mashariki, kote kuna vivutio vya ama hifadhi au mapori tengefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani utakubaliana nami kwamba *set up* ya utalii wa nchi yetu, pamoja na kwamba maliasili zimetawanyika nchi nzima, ziko *circuit* zaidi *towards the North*, wakati vivutio vingine viko *towards the west, towards the South*, na *East* na kadhalika. Nataka niwaombe wakati ambako Kaskazini wamefanya vizuri sana, nataka niwapongeze kwa kweli, wapo wajasiriamali, wasafirishaji, watu wa kupokea watalii, hoteli nzuri, barabara nzuri na kadhalika; na hata *customer care* ipo vizuri, ni jambo jema sana. Ila najiuliza, hivi ilitokea kwa dharura tu hawa wakawa wazuri hivyo, kanda nytingine wakawa washamba? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake najiuliza, iweze kwa mfano umbali wa kufika Serengeti kutokea Mwanza haizidi kilometra 140, lakini kwa nini tumlazimishe mtu anayetaka kutembelea Serengeti ashuke *KIA* aanze kutembea kilometra zote hizo, kwenye *riskszote* za barabarani, mpaka aje kuifikia Serengeti, apite Ngorongoro, apite Manyara, *is too much!* Wakati bahati nzuri wenzetu wa Uchukuzi wamefanya kazi kubwa kuimarisha uwanja wa ndege wa Mwanza, sasa unaitwa Uwanja wa Kimataifa, sasa tunatamani kuona watalii wa Kimataifa wanaolenga kwenda Serengeti washuke Mwanza. Wakifika kule, watapata fursa ya kutembelea hiyo *west circuit* yote; wataona Rubondo, Saanane, Ibanda Kyerwa, Ibanda Rumanyika, Burigi Chato, Gombe, Fukwe za Ziwa Victoria *and so forth and so forth.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nawaomba Wizara, mje na mpango na mkakati madhubuti wa kufanya ukanda wa Magharibi nao pia uwe *busy* kwenye maeneo ya Kitalii kama ilivyo ukanda wa Kaskazini. Kinachoshangaza, unapita pale Serengeti *Ndabaka Gate* wala huoni pilikapilkila

za watalii wakiingia, lakini ukienda upande mwagine kwa kweli shughuli zipo nyingi za kutosha. Kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba hilo tuliangalie kama kweli tunataka kuimarisha maeneo yote ya nchi yetu yanufaika na hizi rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuzungumzia ushirikiano wa Wizara zinazogusa utalii kwa njia moja au nyingine. Nilikuwa naziangalia hapa karibu Wizara nyingi tu, karibu zote, labda nusu; Wizara ya Maliasili yenyewe, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Nishati, Wizara ya Mawasiliano, *mention* Wizara zote; Wizara inayoratibu watu wa dini, kuna makongamano ya Kitaifa na ya Kimataifa ya Dini, tukiweza hawa wote kuwahamasisha wakaja kwenye dini zao, lakini wakaenda kwenye utalii, tutakuwa tumechangia kupata rasilimali nyingi za fedha za kigeni. Tuna taasisi nyingine hata za ndani, *Scouts* wanaweza wakahamishiwa wakaenda huko kufanya mikutano yao, lakini wakaenda kwenye utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza ya Kitaifa naomba niguse Butiama. Hapa nina jambo moja, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Pale Butiama kuna hifadhi inaitwa Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Kyanyari, lakini kwa kweli ukiangalia vile vilima vya Kyanyari hakuna msitu, ni mlima tu umenyanuka wenyewe hivi labda na majani mafupi, hakuna mti hata mmoja, lakini mmeita hifadhi na ika-cost watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamekuwa pale tangu mwaka 1974, mmeenda kuweka *beacons* mwaka 2013 na mkaondoa kaya 220 kwenye hekta zao walizokuwa wanazimiliki na kufanya shughuli za kiuchumi 1,500. Sisi tunasema, lingefanyika sawa, lakini liwe shirikishi. Wananchi hawakushirikishwa, vijana wanakuja *TFS* kutoka Musoma, wakabandika ile, wakaondoka. Linalowakera wananchi wa pale, wakati mnasema hii ni hifadhi, ameibuka huko mwekezaji wa madini, amepewa vibali vya kuwa na vitalu kumi kwenye eneo lile lile. Sasa tunajuliza hapa, kama

unawaondoa hawa kwa ajili ya hifidhi, iweje leo ukaribishe mwagine aendelee na shughuli za uchimbaji na utafutaji wa madini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba niseme moja hili la utalii Butiama. Butiama ni kwa Baba wa Taifa. Watu wanakwenda pale mara nyingi, lakini naona wanaishia kufanya ibada kwenye kaburi la Baba wa Taifa na kuondoka au kupita kwenye ile makumbusho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Butiama ni eneo ambalo lina vitu ambavyo wangeweza kujifunza vyta kitamaduni. Mfano, tuna makabila yasyopungua 10; kuna Wairegi, Wakenye, Wakirobha, Wakabwa, Wazanaki, Waluo, Wajita, Waruri, Wakwaya, Wasimbiti, Wasukuma na Kadhalika. Haya makabila, ni faida, kuna tamaduni pale. Vyakula vyao ni tofauti; kwa hiyo, nilidhani mje mtusaidie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sagini. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa jioni hii. Awali ya yote, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu ya Wataalamu wote kwa jitihada kubwa ambazo wanazifanya za kuboresha utalii na kutunza Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye eneo la Mbuga ya Katavi. Mkoo wa Katavi una Mbuga ya Katavi na jirani Mkoo wa Kigoma tuna Mbuga ya Gombe na Yamahale ambazo ziko Jirani. Eneo hili halijawekewa mazingira mazuri

ya kutangaza utalii kwenye ukanda huu. Naomba sana Serikali iangalie ukanda wa Magharibi kwamba kuna vivutio vingi na vizuri ambavyo vinaweza vikashawishi watalii wakaja kwenye maeneo ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo Ziwa Tanganyika; ni utalii ambao unaweza kabisa ukawavutia wawekezaji na watalii wakaja kuangalia madhali nzuri ya kule. Sasa karibu asilimia kubwa, utalii unaotangazwa ni wa upande mmoja tu wa mikoa ya Kaskazini. Naiomba sana Wizara ilekeze nguvu kama walivyokuwa wameagiza kwamba sasa watawekeza kwenye ukanda wa kusini na nyanda za juu, halikadhalika kwetu kule magharibi wapeleke nguvu kuutangaza utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie eneo la *game reserve* ya Lwafi. *Game reserve* ya Lwafi inapakanana msitu wa *Nkamba Forest* ambao unamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Kwa bahati mbaya sana, Pori la Akiba la Lwafi linatoa leseni ya uwindaji; na karibu sehemu kubwa wanapoenda kuwinda wanaenda kwenye pori la msitu wa *Nkamba*. Sasa msitu huo tunaishia tu kuuifadhi lakini hatuna manufaa ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, pale ambapo wawindaji wanapotokea kwenye Pori la Lwafi, wanakuja msitu wa *Nkamba Reserve*, fedha zinazoitajika pale tuzipate kuitia Halmashauri ya Tanganyika. Ni eneo muhimu ambalo hatunufaiki nalo. Naamini wahusika watalifuatilia ili wajue ukweli ukoje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo hifadhi ya misitu inayomilikiwa na *TFS* ya Pori la Msaginya, *Mpanda North East* na Msitu wa Kabungu. Maeneo haya yalishapoteza sifa ya kuwa na uhifadhi kwenye hii misitu. Mheshimiwa Rais alipokuja akiambatana na timu ya Mawaziri, walitokea ufanunzi kwenye maeneo haya ambayo hayana uendelezwaji. Msitu wa Msaginya umejaa wafugaji humo ndani, kuna miji ya watu, kwa hiyo, sifa ile haipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu wa *Mpanda North East* kwanza kuna makazi ya Katumba ambayo yana watu wengi. Katika msitu huu, sifa iliyokuwa imewekwa katika kipindi hicho, haipo. Nilikuwa naomba mshungulikie ile migogoro ambapo tunacho Kijiji cha Ngomalusambo, Kijiji cha Vikunge, Kijiji cha Majalila na vijiji vinginevyo ambavyo viko kwenye Jimbo la Mheshimiwa Anna Lupembe muweze kuvishughulikia tutoe ile migogoro ambayo haipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya haya tutakuwa kwanza tumemuenzi Mheshimiwa Rais ambaye alitoa maelekezo na ninaamini Katibu Mkuu wa sasa ana kumbukumbu, pale tulipofanya ziara tukapitia kwenye Mbuga ya Hifadhi ya Katavi, tukaandaliwa chakula; karibu wanyama wa aina zote walipatikana pale. Kwa hiyo, naomba eneo hili mlishungulikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Msitu wa Tongwe Mashariki na Msitu wa Tongwe Magharibi ambapo tunapakana na eneo la Mbuga ya Mahale na pia tuna Msitu wa Nkamba. Misitu yote hii mitatu inamiliikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika na tumefaulu kuilinda vizuri, kwa sababu tunadhamini kile ambacho kinafanywa; na wananchi sasa hivi walishaanza kuelimika, wametunza ile misitu wakiamini inawasaidia. Tayari tumeanza kunufaika, tunavuna hewa ya ukaa na vijiji sasa hivi vinapata fedha kupitia utunzaji wa misitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri, najua yupo Meneja wa Kanda ya Magharibi wa *TFS*. Huyu amekuwa akijihuisha kuhujumu misitu kwenye maeneo ya kwetu. Huyu Meneja anashirikiana na wavunaji haramu wa misitu na kuwanyanyasa wafugaji wa nyuki wapatao 12,000 ambao wamo kwenye ile misitu. Sasa naomba huyu mumshungulikie ipasavyo. Kinyume na hapo, mtaleta matatizo na watu watakaa bila kuwa na imani. Pia ameenda mbali sana, badala ya kulinda huo msitu, anafikiria kugawa vitalu vyaa wafugaji. Nashangaa sana kwamba bado mko naye mpaka sasa hivi. Naomba hili mkalishughulikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi, naomba Serikali ishungulikie migogoro ya vijiji nilivyovitaja hapo. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba pia niwatambulische kwenu Kiongozi anayekaimu Shughuli za Serikali Bungeni, ambaye ni Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makof*)

Ahsante. Mheshimiwa Twaha Mpembewne, tuendelee.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia katika Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika mustakabali mzima wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, nilikuwa naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuifanya kwa muda mrefu sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nichukue fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe binafsi, hicho kimekupendeza kweli kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu umegawanyika katika sehemu kubwa mbili; nitachangia Kitaifa halifu nitarudi pale Jimboni kwangu Kibiti ambapo tuna matatizo makubwa sana ya msingi katika sekta hii au katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimepitia vizuri zaidi hotuba ya Mheshimiwa Waziri, haikuweza kutueleza kwa kina zaidi katika baadhi ya maeneo fulani fulani, lakini naomba niguse maeneo mawili tu. Eneo la kwanza nitagusa katika suala zima la utalii wa ndani, halifu eneo la pili, nitagusa katika suala zima la *country tourism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la utalii wa ndani, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hakutuambia hasa mikakati ya Serikali au mikakati ya Wizara; nini tunachokwenda kukifanya ili kuweza kuhakikisha utalii wa ndani vile vile nao unakwenda kuchangia katika pato la Taifa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna mambo mengi sana yamefanyika, mengi yameelezwa, mojawapo ikiwa ni suala la Simba kuweza kuitangaza Tanzania, "Visit Tanzania." Swali ambalo tunapaswa tujiulize, tufanye *evalution kwamba Visit Tanzania imetusaidia nini katika suala zima la utalii?* Kwa sababu tunaweza tukafanya *advertisement nyingi sana*, lakini *at the end of the day*, lazima tujue hizi *advertisement ambazo tunazifanya tunazi-evaluate* vipi? Tunazi-*quantify* vipi *in terms of* hawa watalii na fedha ambazo zinakuja kutumiwa na watalii? Hili ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nitegemee tu kwamba wewe pamoja na wataalam wako mkiwa mnakaa katika mikakati ambayo inakuwa inaendelea katika kuweza kuboresha masuala mazima ya *internal tourism*, hizi *activities* tunazozifanya lazima tufanya *self-evaluation*, zimesaidia vipi? Hili ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala zima la *hunting tourism*. Naomba niguse pale ambapo Mheshimiwa Nape alipokuwa amegusa asubuhi kwamba kuanzia mwaka 2013 na kuendelea mapato yale yaliyokuwa yanapatikana katika suala zima la *hunting tourism* yamekuwa yakipungua kidogo kidogo. Tumeambiwa mwaka 2013 tulikuwa tunapata mpaka dola milioni 27, lakini *todate* tunazungumzia kwenye Dola milioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, mfumo wa kugawa vitalu hauna shida, uko vizuri kwangu mimi, kwa sababu Serikali walikuwa wamechukua maamuzi hayo kwa kwa kuzingatia kwamba tunakwenda kutokomeza mambo yale ya ubadhilifu yaliyokuwa yanafanya kwenye vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi zaidi cha kufanya nafikiri kuna kitu kimoja hapa lazima tukiangalie. Kwenye *economics* kuna kitu kinaitwa *law of demand* na *law of supply*. Kwenye *law of demand* tunaamini kwamba *the higher the demand, the higher the price*; na kwenye suala zima la *law of supply* tunaamini kwamba *the highest supply*, basi *the low the price if other factors zinakuwa zina-remain constant*. Tuelewe tu, hapo hapo kwenye *economics*, kuna kitu kinaitwa *product substitutes*, yaani kama kuna *product* fulani ambayo inaendana na *product* nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wetu kitu ambacho wamejisahau, tulitoka kwenye Dola 7,000 katika kuuza vitalu hivi, tukaenda kwenye Dola 30,000, sasa hivi tuko kwenye Dola 80,000. Tumeambiwa kwamba tuna vitalu karibia 40 vyote hivyo viko katika mazingira kwamba havina watu na vingine 14 viko katika hali mbaya sana. Tafsiri yake ni kwamba, twende kwenye *basics* za *economics* kwamba pale ambapo pana *demand* ya hali ya juu sana. Ni mategemeo yetu kwamba sisi tunaweza kukaviuza vitalu hivi kwa bei ya juu, hakuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke tu kwamba, sisi tuna *competitors* wetu vile vile. Ni vyema zaidi katika sekta hii ya *hunting tourism* lazima tuweze kufanya kazi ya ziada ili sasa kuweza kufahamu *competitors* wetu wana-add value vitu gani vinavyoweza kuwavutia wale watu wanaokwenda kuwindha kule? Maana yake ni nini? Ni kwamba vitalu tunavyo, nasi Tanzania *we are biological reach*, lakini very unfortunately tunashindwa kuutumia huu utajiri tuliokuwanao vile ipasavyo. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri akae na wataalam wetu, ili sasa tuweze kujua ni kitu gani ambacho wenzenetu wanakifanya ili nasi vile vile tuweze kufanya tuweze kuwavutia watu waje kuwekeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nilikuwa naomba vilevile niguse katika sehemu nzima ya mambo ya mapato. Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba kuna fedha tunakusudia kuzikusanya katika mwaka wa fedha huu karibia shilingi bilioni 478.01 katika sekta yetu

kule TAWA, Ngorongoro, hizi fedha zote zinakwenda moja kwa moja kule *TRA*. Ni vyema sasa wangeweza kutuambia mikakati gani ambayo tunakwenda kuifanya ili kuweza kufikia lengo hili? Vinginevyo tunaweza tukawa tunazzungumza hizi namba lakini tafsiri pana ni kwamba, tunaweza tukawa tunashindwa kufikia malengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nilikuwa naomba sasa niende jimboni kwangu. Mheshimiwa Waziri naomba tusikilizane vizuri sana hapa. Wewe ni rafiki yangu, mtani wangu, maana unatokea kule kusini kusini; na mkae mkijua kwamba sisi ndio tuna barabara pale. Mkiwa mnaleta taabu Mheshimiwa Waziri unaweza ukashindwa kuja Dodoma huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo moja la msingi sana kule. Serikali mwaka 2017/2018 illifanya zuio kwa makusudi mazima, tena mazuri zaidi ya kuweza kulinda mazingira jinsi ya uvunaji wa mikoko. Mwaka 2019 Serikali ilituma wataalam ili sasa kwenda kuifanya tathmini, mikoko ile itaenda kuvunwa vipi na kuweza kulinda mazingira? Mwaka 2020 wataalam wale walikuja katika maeneo husika, maeneo mengi sana ambayo yanazungukwa na maziwa pamoja na mito ili kuja kuwaeleza kwamba tathmini imeshakamilika na kwa namna moja ama nytingine Serikali itatoa tamko ni jinsi gani sasa mikoko ile itawezwa kuvunwa ili tusiweze kuharibu mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri, kule kwangu mimi kuna maeneo ya *delta*, nina kata kama tano; kuna Kata ya Kiongoroni, Kata ya Maparoni, Kata ya Mbochi, Nsala, Salale; vile ni visiwa. Hii mikoko ni mali tuliyopewa na Mungu, tunajua lazima tulinde mazingira. Sasa ni jambo la msingi tuweze kujua ni jinsi gani wananchi wale wanakwenda kuokoka katika kuivuna mikoko hii. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu Mheshimiwa Waziri, utakapokuja kuifanya *wind-up* hapa, uje kutupa tamko la Serikali, nini tunachoenda kukufanya ili wananchi wale waruhusiwe kuivua mikoko ile? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na la msingi ni suala zima la wajasiriamali wangu pale Kibiti. Kuna wajasiriamali hawa ambao wanafanya shughuli za randa hizi. Inasikitisha sana, wananchi wale tunawaita wajasiriamali, wanatengeneza vitanda na vitu vingine, lakini cha kusikitisha tu ni kwamba tozo ambazo wanatozwa ni nyingi sana. Kuna urasimu wa hali ya juu kiasi kwamba watu hawa wanashindwa hata kuweza kufanya shughuli hizo.

Kwa hiyo, naomba wa Kihesa wanaenda kulipa *TFS*, ambayo inawachaji shilingi 55,000/=. Kuna tozo wanaenda kulipa *TRA*, kuna tozo wanaenda kulipa Halmashauri, kuna tozo wanakwenda kulipa katika vijiji husika. Sasa hawa wajasiriamali tunawasaidia vipi? (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwomba Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, wakati huo anajiandaa, Mheshimiwa Joseph George Kakunda pamoja na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso wajiandae. (*Makofii*)

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nikupongeze kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, kiti kimekufaa, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uhai na uzima na ametupa kibali sasa hivi tuko ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tukiendelea kufanya shughuli mbalimbali za Kiserikali. Naomba nimshukuru na kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kazi kubwa

ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu ya Tanzania. Tunaona jitihada zake, na kazi zake, nasi tunaendelea kumuunga mkono kwa asilimia mia moja ili aweze kufanikiwa kuijenga nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri. Waziri ni mtani wangu pamoja na mdogo wangu, hongereni kwa kazi kubwa, tunaona jitihada zenu mnazozifanya. Naomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Kijazi kwa kazi kubwa. Tunajua anahangaika, ametokea mbali pamoja na kupitia Wizara hii katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimpongeze Mkurugenzi wa *TFS*, ni msikivu *chief* ni msikivu, lakini sasa vijana wake ndio tatizo. Naomba nianze kwa *TFS* ambayo ni tatizo kupitia wananchi wetu. Tunajua Serikali ni moja, lakini ukienda katika maeneo yetu ya vijiji *TFS* wamejtenga wao kama wao. Wanafanya kazi wao kama wao, hawathamini kabisa viongozi ndani ya vijiji vyetu. Wakiingia pale vijiji, wenyewe wakishasema hii ni hifadhi, basi wamesema, wanaanza kutandika wananchi; na wakati mwengine inakera zaidi wanapochukua mali zao. Inasikitisha sana maana wakikuta hata ng'ombe wanabeba. Sasa tunajiuliza, hii *TFS*ni chombo kiko tofauti kabisa, kinajitegemea chenyewe kama chenyewe? Ina maana hakina suluhu na wananchi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mkurugenzi wa *TFS*, tumeendelea kumlalamikia kwa ajili ya Meneja wa Kanda, tunamshukuru sana kwani amechukua hatua ya kumhamisha. Tunamshukuru sana kwa sababu ilikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi, alikuwa hataki suluhu na viongozi wa Serikali ndani ya wilaya na ndani ya mkoa, na alikuwa hataki kuonana na sisi Wabunge, anasema sisi ni wanasiasa. Sasa kama ni wanasiasa, ni lazima tuwatetee wananchi wetu kwa sababu mali mazao wanayolima wakulima wale ndiyo inayoleta maendeleo ndani ya nchi yetu pamoja na kukuza uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri, ifike mahali sasa *TSF* ipite katika maeneo yote nchi nzima, waonyeshe mipaka yao na wananchi. Unakuta sasa hivi kama Kata yangu ya Ugala, wanasema yote ile ni hifadhi. Sasa unajiuliza, hii ni kata, ina vijiji, ina vitongoji; wanasema wananchi wote wahame kwenye Kata ya Ugala, waende wapi sasa? Wameshakaa zaidi ya miaka 50 mpaka 60, leo mnasema ni hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *Kijiji* cha Usense Kata ya Urwila, wameweka *beacon* katikati ya *Kijiji*, wanasema yote hiyo ni hifadhi. Sasa siku zote hizo milikuwa hamuoni, leo ndio mnakuja kuona kama ni hifadhi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana *TFS* wapite katika maeneo sasa tukubaliane, twende kuanza kuonyeshana mipaka ili tujue mipaka ya *TFS* iko wapi; na mipaka ya wananchi? Tujue wananchi waende wapi kwa ajili ya maendeleo mbalimbali ya kilimo na ufugaji. Kwa sababu tukienda namna hii tutaendelea kuwavuruga wananchi kwa sababu wanapigwa, wananyang'anya mali zao, hawana amani, wanaishi maisha magumu sana katika nchi yao na maeneo yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri kipindi hiki atoke, asikae ofisini pamoja na watendaji wake wote, twendeni tukaonyeshane mipaka ili wananchi tujue mipaka yetu iko wapi ili tusiweze kuwaingilia kazi zenu. Kwa hiyo, tunajua mnafanya kazi kubwa ya kuendelea kuhifadhi...

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mtoa taarifa yuko wapi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa *Engineer Manyanya*.

**MWENYEKITI:** Okay, Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*, karibu.

## TAARIFA

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Taarifa ninayotaka kumpa ni kwamba malalamiko hayo ya kuweka mipaka ya hifadhi yanafanana sana na kule jimboni kwangu Nyasa katika eneo la Lipalamba. Wananchi wanasema mpaka waliokuwa wanaujua, wanauona kabisa, lakini sehemu waliyoenda kuweka kama ndiyo mwisho wa eneo la kwao, wamepitiliza ndani huko kiasi kwamba hata wanavyoolezwa, wao hawaelewi. Wanasema kwa sababu kwanza kwa nini waende kuweka hiyo mipaka peke yao bila kuwashirikisha hao viongozi wa vijiji? Ndiyo taarifa yangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lupembe, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Ni tatizo kusema kweli. Hawataki maelewano kabisa *TFS*. Mkisema mkae pamoja mkaelezana jambo, hawakubali. Naomba nimuunge mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya jimbo langu, nina Hifadhi ya Katavi. Hifadhi hii bado haijatangazwa vizuri. Hifadhi ya Katavi ni nzuri, ina wanyama wakubwa, ina mambo mazuri sana, ina twiga mweupe, tembo wakubwa sana, lakini bado hatujaitanga vizuri na hatujajenga mahotel na mazingira yake siyo mazuri sana ya kuvutia watalii kuja katika Hifadhi ya Katavi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba basi Serikali, najua Waziri ana jitihada kubwa sana ya kufanya kazi na uhamasishaji, tunaona leo hii kuna mtu yupo Serengeti. Basi siku nyingine mlele Mbunga ya Katavi ili iweze kutangazika kwa sababu najua ikitangazika, sasa hivi tuna uwanja wa ndege, anatua Mpanda bila matatizo na kutoka pale mpaka kwenye hifadhi yetu, siyo mbali sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Katavi ambayo inasimamiwa na TANAPA, ule ujirani mwema bado haujawa mzuri sana. Ndani ya Kata ya Stalike nina mto pale. Ule mto una samaki pale...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwomba Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso wakati Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah wanajiandaa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Ulimtaja Mheshimiwa Kakunda. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, halafu atafuatia Mheshimiwa Joseph George Kakunda. *Sorry!* Halafu Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Mohammed Soud wajiandae. Karibu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naungana na Wabunge wenzangu kukupongeza kwa nafasi hiyo ya kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Hongera sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika mambo yafuatayo: kwanza, sote tunatambua umuhimu wa sekta ya utalii kama nchi, kwa sababu ni sehemu ya kutoa ajira, kuchangia pato la Taifa, kuiingizia nchi fedha za kigeni. Utalii wetu umejikita zaidi kwenye utalii wa wanyamapori. Hivyo basi, bado tuna fursa nyingine nyingi za kupanua zaidi utalii wetu ili uendelee kuwa na manufaa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina budi kuhakikisha utalii wetu unakuwa endelevu kwa kuendelea kutunza maeneo yetu ya utalii, kuvihifadhi, kuhakikisha haviharibiwi, kuhakikisha kile ambacho kinawavutia wageni kuja na kutupatia faida kama nchi, basi vinatunzwa kwa nguvu zote na kuhakikisha vinakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna athari za kutoweka hatuoni uendelevu wake kama bado upo ama utaweza kuendelea kuweko kwa miaka 10, 20 au 30 ijayo. Kwa sababu nydingi ambazo zinajitokeza, kwanza, mapito ya Wanyama, maarufu kama shoroba, nydingi zimevamiwa na wananchi. Zinavamiwa kwa sababu hatukuwa na mipango bora ya ardhi kwenye maeneo yetu. Pia kuna ongezeko la idadi ya watu na kuna ongezeko la matumizi ya ardhi. Siku zote napenda kusema ardhi haiongezeki, idadi ya watu inaongezeka, mahitaji na utumiaji wa ardhi unaongezeka kwa kasi kubwa kwa sababu ya idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ni lazima Serikali mwone namna gani ardhi yetu tunapangia matumizi bora na kuiwekea sheria; kama ambavyo tumetungia sheria maeneo yetu ya hifadhi, hivyo hivyo ukienda kwenye maeneo ya kilimo haina budi kuwa na sheria maalum ili wasilingiliane. Hivyo hivyo kwa wafugaji itatusaidia angalau kupunguza migogoro ambayo inajitokeza kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, Hifadhi ya Ngorongoro. Kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia, katika *speech* zake zilizopita ameweza kuonyesha kwamba tunahitaji kuendelea kuilinda Hifadhi ya Ngorongoro kwa nguvu zetu zote. Hifadhi ya Ngorongoro ni Kivutio cha Asili, na ni Hifadhi ya Urithi wa dunia toka mwaka 1979 na ni hifadhi ambayo inatambulika kama Hifadhi Mseto. Ni hifadhi ambayo ina wanyamapori na shughuli za binadamu na makazi ya binadamu humo ndani. Kwa hiyo, sioni Ngorongoro ya miaka 20 ijayo kwa sababu, matumizi mseto ilikuwa ina-*apply* miaka ya nyuma, lakini siyo leo. Leo shughuli za kibinadamu zikiongezeka, ule uhifadhi tunaotamani kuuona Ngorongoro utapotea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mhifadhi Mkuu wa Ngorongoro, wameanza kuonyesha mfano, kwa sababu Ngorongoro sasa hivi wamehama; Makao Makuu ya Hifadhi ya Ngorongoro imehama kutoka kule Ngorongoro iliko hifadhini na kuhamia Karatu. Ni nia ambayo ilikuwepo muda mrefu, haijawahi kutelezwa, lakini leo imetekelezwa. Nampongeza sana Mhifadhi wa Ngorongoro na timu yake nzima, na bodi yake kwa hatua hii muhimu ambayo sasa itatoa mwelekeo mzuri wa kuendelea kuifanya Serikali ipunguze matumizi ya watu na binadamu ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendelea kuilinda Ngorongoro ile ambayo tunaifahamu ilikuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ripoti ya *CAG*, ameonyesha mambo mengi kuhusiana na Hifadhi ya Ngorongoro. Kuna tatizo la magugu vamizi, ambayo yanahatarisha Wanyama. *CAG* kwenye ripoti yake ameieleza vizuri sana. Amesema kwamba *management* wamejitalidi kuondokana na hiyo, lakini bado kuna mkwamo. Kwa hiyo, Wizara muone namna gani ya kukabiliana na hayo magugu vamizi ili tuendelee kuona Ngorongoro inastawi na inaendelea kuwa urithi wa dunia kama ambavyo imetangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya tatu, kuna mgogoro wa muda mrefu kati ya wananchi wa Kata ya Buger na Hifadhi ya Msitu Mara ambao unalindwa na *TANAPA*. Niseme yafuatayo: mwaka 2013 mwananchi mmoja alipigwa risasi mguuni na Askari wa *TANAPA*; tarehe 25 Mei, 2015 mwananchi mmoja alipigwa risasi akafariki; tarehe 28 Oktobam 2020 siku ya kupiga kura wananchi wa *TANAPA* waliwapiga risasi ng'ombe kumi wa mama mmoja mjane kwenye ile kata. *TANAPA* waliahidi watamfidia yule mama, lakini mpaka leo yule mama hajapata fidia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Desemba, 2020, watu saba waliingia kwenye msitu ule wa hifadhi, walikuwa wanakwenda kuchimba madini. Sitetei watu wanaoingia na kuvamia hifadhi na kutaka kuharibu hifadhi zetu, nachukizwa

na utaratibu unaofuatwa baada ya hapo. Kama hao watu ni wahalifu, sheria zipo, tumezitunga ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao watu saba waliongia kwenye huo msitu, watu wanne mpaka leo hawajulikani walipo. Watu watatu walifanikiwa kutoroka, watu wanne inasemekana walichomwa mpaka kufa na Askari wa *TANAPA*. Haya ni mambo ambayo hayakubaliki. Sitetei uhalifu, lakini kuna sheria za kumchukulia hatua mhalifu yejote. Sheria ziko *very clear*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshakuwa ni utamaduni wa kudumu wa mgogoro kati ya wananchi hawa wa Buger na Askari wa *TANAPA*. Ni eneo pekee ambalo Askari wa *TANAPA* hajawahi kukwaruzwa na mwananchi yejote, ukilinganisha na maeneo mengine, labda inawezekana askari akauawa na wananchi kwa hasira; lakini kwa jinsi ambavyo wale wananchi walivyo, hakuna Askari aliyekwaruzwa wala kutolewa unyayo au kufanywa chochote kile, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, tuone namna bora ya kumaliza mgogoro huu. Leo ninapoongea hapa askari wale wako kule, nasikia wanarekebisha *beacon*, ambao ni mgogoro wa muda mrefu. Hatujapata suluhisho, lakini tunakwenda tena kuendelea ku-create matatizo ambayo yanaendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tuone namna bora ya kumaliza tatizo hili ili wananchi wale wakae kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, akiwemo Naibu

Waziri, kwa hotuba nzuri, fupi, ambayo inaeleweka; *brief to the point*. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Ndiyo maana nasimama hapa kuzungumzia suluhisho badala ya malalamiko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo nitakalolizungumzia ni la Jimbo langu la Sikunge. Jimbo la Sikunge au Wilaya ya Sikunge, ina eneo la kilometa za mraba 27,873. Eneo la Mkoa wa Kilimanjaro linaingia mara mbili na eneo la wilaya ni kubwa kuliko Mkoa wa Tanga. Kati ya kilometa hizo, eneo lililohifadhiwa ni kilometa za mraba 26,834, sawa sawa na asilimia 96.3 ya eneo lote la wilaya. Eneo ambalo wananchi wanaruhusiwa kuishi na kufanya shughuli zao za kiuchumi ni eneo la kilometa za mraba 1,039.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi takwimu hata kama mtu ye yeyote akiamua ku-google *Sikunge District*, atazikuta ziko hapo, Kimataifa, hata kama yuko Marekani. Hii ndiyo *concern* yangu kubwa na ni *concern* ya wakazi wa Sikunge kwa sababu moja kubwa. Wakati wa kupima eneo la kuhifadhi, mwaka 1954 mpaka 1956, wakazi wa Sikunge wakati huo ilikuwa kata tu, kwa ujumla wao hawakuvuka hata 30,000. Leo tuna wakazi wanaopindukia 350,000 katika eneo lile lile dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanapima eneo hilo lililohifadhiwa mwaka 1954 hadi 1956, wakazi wa Sikunge wakati ule hawakuwa wafugaji wa asili. Kwa hiyo, ng'ombe kule hawakuzidi 2,500 kwa eneo lote. Leo tuna ng'ombe zaidi ya 400,000 kwa eneo lile lile dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema wakati mwingine lazima ndugu zetu walioko Serikalini tutumie busara katika kutekeleza sheria. Kwa sababu eneo hilo sasa lime-*burst*, hakuna sehemu tena ya makazi, hakuna sehemu ya ng'ombe, mtu ye yeyote anayefuga ng'ombe ataingiza kwenye hifadhi. Asipoingiza kwenye hifadhi atalisha mashamba, kwa sababu hakuna eneo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababishwa na makosa mawili makubwa ambayo yalifanywa na Serikali. Kosa la kwanza, mwaka 1959 Gavana wa kikoloni baada ya kuwa amepata taarifa ya uharibifu wa mazingira katika eneo la wafugaji kule Usukumani hasa, akatoa *decree*, inaitwa *order*, kwamba sasa kila mfugaji kwenye maeneo yale anatakiwa apunguze mifugo ibaki 100 au chini ya hapo kwa ajili ya kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana kipindi kile hakukuwa na Maafisa wa Serikali wa kuweza kutekeleza hiyo *decree*. Kwa hiyo, ikabidi isubiri *decree* kutotekelezwa mpaka tulipopata Uhuru mwaka 1961. Tulipopata Uhuru mwaka 1961, Mwalimu Nyerere akasema hii *decree* hatuwezi kuitekeleza katika nchi huru kwa sababu nchi hii Tanzania ina maeneo mengi ambayo bado wananchi wanaweza wakahamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa ni kosa la kwanza, kwa sababu uhamiaji ule sasa wa kutoka maeneo yale ya wafugaji, kuja kwenye maeneo ya Wilaya ya Sikonge, haukuratibiwa na Serikali. Hilo lilikuwa ni kosa. Kwa hiyo, matokeo yake, wameingia watu wengi sana Sikonge na hatuna eneo la kulima wala kufugia na mifugo ni mungi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa la pili la Serikali; ilikuwa ni wakati wa operesheni vijiji, walikwenda kuanzisha Viji vya Ujamaa karibu kabisa na hifadhi ndani ya mita 500 unaingia hifadhi. Nina kata 16, nina vijiji 40 viko ndani ya mita 500 unaingia kwenye hifadhi; kosa kubwa la Serikali hilo. Unategemea mtu ambaye yuko ndani ya kijiji mita 500, asiingie kwenye hifadhi? Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni kosa. Ndiyo maana mimi niko hapa kwa sababu matokeo yake yamesababisha adha kubwa na usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono suluhisho ambalo linaletwa na Serikali la kuanzisha *nature reserve* kwenye maeneo yote haya. *Nature reserve* ambayo sasa itatoa nafuu kwa kupunguza eneo la hifadhi ili wananchi

wabaki na eneo kubwa zaidi la kulima. Wananchi hao kupitia Halmashauri tumeshaanza kuzungumza nao namna ambavyo watashiriki kulinda ile *nature reserve* mpya ambayo itaanizishwa ambapo itaacha maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndilo suluhisho ambalo kwa kweli naomba kulileta mbele ya Bunge lako Tukufu ili Mheshimiwa Waziri na timu yake yote waje Sikonge, tukae pamoja tuweze ku-determine kwamba sasa eneo ambalo ni la *nature reserve* lianzie wapi? Lazima tulinde miti yetu mizuri kabisa; Mininga na miti mingine ya thamani tulinde, lazima tulinde maeneo ya shoroba, lazima tulinde mbuga ambazo zina wanyama bado, tunazifahamu sisi. Kama hawafahamu wao, watuulize, sisi tunazifahamu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesimama hapa kuleta suluhisho la kudumu ambalo litaondoa malalamiko ya wananchi kutokana na yale makosa mawili makubwa ya Serikali ambayo yalifanyika ambayo yameifanya sasa Sikonge *ime-burst*, hakuna sehemu ya kuishi, hauna sehemu ya kulima wala kufanya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kuiwasilisha hoja hii hapa Bungeni na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri; na ninamwamini huyu bwana kwa sababu tuliajiriwa siku moja Serikallini, mambo haya niliyowasilisha atayatilia mkazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza nikupongeze kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti katika Bunge hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri; Katibu Mkuu, Dkt. Allan Kijazi; na watendaji wote wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Vile vile niwapongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuweza kusaini Mkataba wa *REGROW*. Pia tunawashukuru sisi Nyanda za Juu Kusini kwa kutupatia magari 12 kwa ajili ya operesheni za mbuga ambazo ziko Nyanda za Juu Kusini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri pia kwa kusaini *GN*. Najua huu ni mwanzo mzuri wa kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu kwa ajili ya kutangaza utalii Nyanda za Juu Kusini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua *REGROW Phase I* imechukua *Mikumi National Park*, *Nyerere National Park*, Udzungwa pamoja na Ruaha. Ni matumaini yangu kwamba *Phase II* mtachukua *Kitulo National Park* pamoja na hifadhi nyingine za Taifa zilizopo Nyanda za Juu Kusini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ni hifadhi nzuri sana; ina maua mazuri ya kila aina. Ni hifadhi ambayo hakuna ulimwenguni inayofanana na *Kitulo National Park*. Ina maua mazuri pamoja na ndege wa ajabu ambao wanakuja kila mwaka mara moja; wanatoka Australia moja kwa moja mpaka Kitulo, hawasimami sehemu yoyote. Kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba *Phase II* ya *REGROW*, *Kitulo National Park* ambayo iko Wilaya ya Makete ndani ya Mkoa wa Njombe inaingizwa kuwa sehemu ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo nilishawahi kuwaauliza watu wa Utalii, hivi kwa nini hawakuiingiza *Kitulo National Park* katika huu Mradi wa *REGROW*? Wakaniambia, unajua barabara kule haziko rafiki na nini; lakini nitumie nafasi hii kusema kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kushirikiana na Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kutengeneza ile barabara ya Njombe – Makete. Hivi sasa nina habari njema; Mheshimiwa Rais Samia ameshatuingizia pesa za kilometra 25 kutoka Makete kuitia

Hifadhi ya Kitulo kutokea Mbeya. Kwa hiyo, sitategemea tena kuwe na sababu ambazo zinahusiana na masuala ya miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi hapa Mheshimiwa Mrisho Gambo amejinasibu sana akasema kwamba asilimia 80 ya pesa zinazotokana na utalii zinatoka Kaskazini. Niwakumbushe basi Wizara, sasa hivi mwangalie maeneo mengine. Mje Nyanda za Juu Kusini, kuna vivutio vingi vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Nyanda za Juu Kusini mfanye ile mnaita *package tourism* (utalii wa vifurushi). Mtalii anatua Iringa, anaenda *Ruaha National Park*, anaenda kuangalia historia ya Mkwawa, anakwenda *Sao Hill* kufanya utalii wa picha, akitoka hapo anakwenda Njombe, anakwenda *Kitulo National Park*, anapita pale Kipengele, anatoka anaenda Songwe kuangalia kimondo pamoja na maji moto; anaweza akatoka hapo akaenda Mbeya kuangalia zile *waterfalls* na mambo mengine ambayo yanavutia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile anaweza akaamua kwenda kwa Mheshimiwa Waziri kule Ruvuma kuangalia historia ya wamisionari kwenye Jimbo la Mheshimiwa Jenista. Kuna njia ambayo wamepita watumwa zamani; na huo ndiyo mwanzo wa umisionari kule Ruvuma. Yote hayo mnawenza mkayaweka kwa pamoja mkafanya hiyo *package tourism*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia msisahau kule Njombe kuna mashamba mazuri ya chai, kuna mashamba mazuri ya miti, mnawenza mkafanya *farm tourism*. Hivyo vyote ni vivutio. Sisi hatujajaliwa wanyama wengi sana kule *Southern Highland*, lakini tuna utalii ambaao wanaita wa ikolojia, mnawenza mkafanya vizuri na tukaweza kuiingizia nchi yetu mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya vivutio ambavyo wananchi na Waheshimiwa Wabunge wa kutoka

Nyanda za Juu Kusini waliweza kuvainisha. Ni kazi sasa ya Wizara kuvifanyia kazi ili vithibitishwe rasmi. Kwa mfano, kuna Gereza hili la KiHesa Mgagao Iringa; Wabunge wa Iringa hapa miaka mitano wamezungumza. Lile gereza lina wafungwa 17 tu, yaani wafanyakazi ni wengi kuliko idadi ya wafungwa. Lile gereza, Nelson Mandela alipita pale akalala. Kile chumba ni historia nzuri, nayo ikaingia katika *package* ya utalii kwa Iringa na Nyanda za Juu Kusini kwa ujumla. (*Makofii*)

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Neema Mgaya, kuhusiana na hilo gereza. Ni kwamba aliwahi kuja Balozi wa *South Africa* hapa nchini, alipokuta kuwa ni gereza, akakataa kuingia pale kuona kile chumba ambacho mzee Mandela alilala pale. Kwa hiyo, unaweza kuona kwa namna gani tunapunguza watalii, maana yule angeweza pia kuwa balozi wetu wa utalii kule *South Africa*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili. Hapo sasa ndiyo Wizara iangalie namna gani tunapoteza mvuto katika suala hili la utalii kwa vitu vidogo vidogo lakini vyenye msingi na ambavyo vinaweza vikatuongezea pia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ogidivai, kule Wanging'ombe, kuna lile jiwe linaitwa Ogidivaa, lina ramani ya Afrika na jiwe lingine hapo hapo pembedi lina ramani ya *South America*. Vitu kama hivyo mvichukue. Pia kuna Msitu wa Nyumbanitu. Huo msitu uko Wanging'ombe, una kuku Weusi mbaao hawajawahi kufugwa na mtu na wanazidi

kuongezeka siku hadi siku. Ukienda pale unawakuta, hawafi, wapo tu. Kwa hiyo, vitu kama hivyo ni vya kuviungeza katika hiyo *package tourism*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema kule lyangweni na Matuhu, unajua majina ya huku Songea ni magumu magumu; hiyo nayo mnaweza mkaiingiza pia ikawa kwenye sehemu ya *package tourism*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nizungumzie suala la migogoro ya ardhi kati ya hifadhi za *TANAPA* pamoja na...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwende mkatatue mgogoro wa Hifadhi ya Mpanga Kipengele inayozungukwa na Vijihi vya Malangali, Mlangali, Mpanga, lyai, Igando na Ruduga. Migogoro ya ardhi kati ya hifadhi na wananchi imekuwa mingi. Mheshimiwa Waziri nendeni mkashughulikie mmalize migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Sasa wajiandae Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Ndumbaro pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Mary, pamoja na watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Dkt. Allan Kijazi, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo amekuwa akiifanya. Kwa kweli wameacha alama katika kipindi kifupi hiki ambacho wameikamata hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Maliasili na Utalii katika kipindi cha miaka mitano iliyopita wamefanya kazi kubwa sana. Nami ni shahidi, tumeweza kutembea katika baadhi ya hifadhi na tumeona mabadiliko makubwa ikiwa ni pamoja na kuona hivi sasa wanyama wameongezeka sana na wale tembo ambao ilikuwa hata ukienda kwenye hifadhi zetu kuwaona ni nadra, basi hivi sasa wamekuwa ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa hapa kwamba kabla ya kupata Uhuru tulikuwa na tembo waliokuwa wakifikia 200,000 lakini hivi sasa tembo wamepungua mpaka kufika 40,000. Hivi sasa wameongezeka mpaka wamefika karibu 60,000. Haya kwa kweli ni matokeo mazuri ya uhifadhi ambao unafanywa na wenzetu hawa wa Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, tumekwenda kwenye Hifadhi ya Ruaha, wenyeji wametueleza pale kwamba kwa miaka kumi iliyopita Mto Ruaha kilikuwa kinafika kipindi maji yanakata karibu miezi miwili au mitatu, lakini hivi sasa Mto Ruaha kwa mwaka uliopita haukukata maji hata mara moja, umeweza kutirisha maji kwa mwaka mzima. Haya ni matokeo ya juhudhi za uhifadhi ambazo wenzetu wamekuwa wakizifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wenzetu hawa wamefanya kazi nzuri hata katika masuala mazima ya uhifadhi wa maliasili, yaani miti. Kwa sababu wenzetu wa *TFS* hivi sasa ukiangalia mapato ambayo wameweza kuyapata katika kipindi kilichopita pamoja na maradhi ya *Covid*, lakini wamevunja rekodi katika vipindi vyote viliviyopita. Yaani wakati sekta nyingine zinahangaika kwa ukusanyaji haffu wa

mapato, wao wameweza kufanya kazi nzuri na kuweza kukusanya mapato kwa kiasi kikubwa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kidogo katika suala muhimu la usimamizi shirikishi wa maliasili zetu nchini. Kama tunavyoja, juzi na jana, nimesikiliza kwa makini wakati michango ikitolewa katika Wizara za Maji na Nishati, tumekuwa tukizungumzia sana kuhusu uhifadhi na uvunaji wa rasilimali zaidi, yaani vipi tutapata nishati, vipi tutaunganisha tupate umeme? Ila hatuangalii na tija: Je, haya maji *sustainability* yake itaendelea kuwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukizungumza masuala yote ya uhifadhi, ningependa tu kuwaomba wenzangu kwamba tuka-*adopt ile approach* ile *integrated natural resources management*, yaani usimamizi shirikishi. Tusiwaachie watu wa maliasili tu kwamba ndiyo wahifadhi rasilimali za misitu au rasilimali za wanyamapori. Kwa sababu tukizungumza maji wanategemea vilevile *sustainability* ya hifadhi ya misitu. Tukizungumza nishati wanazitegemea vilevile *sustainability*ya rasilimali za misitu, hata tukija kwenye masuala mazima ya *food security*, pia kama hatukuweza kupata kuni na makaa katika njia endelevu, basi hata usalama wa chakula nao hautakuwa mzuri. Kwa hiyo, lazima tuje na usimamizi shirikishi ambao utajumuisha sekta zote hizi muhimu ili tuweze kuhakikisha kwamba maliasili zetu zinahifadhika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakuja hapa tunazungumza kwamba tunataka kuifanya Tanzania kuwa ni nchi ya tembo. Hii siyo kauli nzuri sana kwa sababu, kama tunavyoja hivi sasa tuna tembo 60,000, huko nyuma tulikuwa tuna tembo zaidi ya 200,000 na tuliweza kuishi katika hali endelevu zaidi na wanyama hawa. Kwa hiyo, nafikiri ni pahala pa kujipanga kisekta tukashirikiana katika uhifadhi wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumza kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunategemea pale

tukapate *Megawatt* za umeme karibu 2100, lakini tunategemea kuanzia mwezi Aprili tuwe tumeatalijaza maji lile bwawa; na kuanzia mwezi Juni tunategemea tuanze kuchaji na kupata umeme. Wakati nazungumzia kuhusu kupata maji, hatuzungumzi kuhusu haya maji, *potential threat* yake ikoje kama maji hayataturika vizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuwa-*support* wenzetu wa maliasili ili wahifadhi vyanzo vya maji ili kuhakikisha kwamba bwawa letu la Mwalimu Nyerere linaweza kupata maji katika hali endelevu na kuweza kupata matunda ambayo tunakusudia. Kinyume na hivyo, tunaweza tukazungumza hapa bila kuangalia zile *threats* ambazo zinakabili suala hili zima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la taaluma kuanzia kwa Wabunge na wanajamlii. Kwa kweli kinachoonekana ni kwamba elimu ni hafifu. Kwa hiyo, naomba wenzetu wa maliasili tujipange vizuri kuweza kuelimisha kuanzia wanajamii hapa pamoja na Wabunge kuweza kupata taaluma muhimu kwa sababu michango tunayokuwa tunaitoa hapa wakati mwingine ni kutokuwa na taarifa za kutosha katika masuala mazima ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mfano mdogo tu; kule Zanzibar miaka ya 1970 tulikuwa na Chui zaidi ya 1,000 na kidogo hivi, lakini hivi ninavyokwambia Chui wale wamemaliza na hakuna tena hivi sasa. Chui wameisha. Pia tulikuwa na Paanunga zaidi ya 6,000 kipindi cha miaka ya 1970. Hivi sasa Paanunga wamebakia 300 tu Zanzibar nzima. Kwa hiyo, unaweza kuona athari ya viumbe kuweza kutoweka. Tukifanya masihara tutapoteza viumbe kwa kutokuzingatia uhifadhi sahihi na kutokuwapa nguvu wenzetu wa maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie suala la mifuko ya fedha. Kwa kweli mifuko ya fedha tumeamua kwamba fedha zikusanywe na watu wa *TRA* na ziende kwenye mifuko mkuu na baadaye ndizo zirejee tena kwa wenzetu hawa waweze kutumia. Vilevile naomba tu kutoa

indhari, wenzetu katika kipindi hiki cha fedha wamepokea asilimia 32 tu ya fedha. Kwa hiyo, kama tutaendelea na utaratibu huu, zile kazi ambazo tumezipanga hazitaweba kufanya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nakupongeza sana kwa wadhifa huo. Pia nawapongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri mliyoifanya hasa kudhibiti ujangili kwa asilimia 90. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia kwa kutuhakikishia kwamba mnaenda kuanzisha vituo vya askari wa kudumu katika maeneo hatarishi ya wanyama wakali na waharibu kwa maana ya tembo. Sasa hili nendeni mkalitekeleze, nasi tunawapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la wafugaji walioshinda kesi Mahakamani, lakini Serikali imekaidi kurudisha mifugo yao.

La kwanza, katika Pori la Maswa na WMA ya Makao, ng'ombe walikamatwa 1,739, walipoenda kwenye Mahakama Kuu Shinyanga wafugaji hawa walishinda, wakaenda kwenye Mahakama ya Rufaa Tabora, wakashinda. Ng'ombe jumla 1,739 mpaka leo hawajarejeshwa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Kanda Dodoma kwa kesi ya jinai ya 136 ya mwaka 2017 ng'ombe 466 zilikamatwa katika Pori la Akiba la Swagaswaga ambapo ni ng'ombe 113 tu walirudishwa, lakini wengine wote katika 400 na kitu hawajarudishwa mpaka sasa. Pori la Akiba la Moyowosi ambapo ng'ombe 216 walikamatwa mpaka leo hawajarudishwa na Serikali. Katika ile hesabu ya ng'ombe 6,000 hii ni mifano tu ya wafugaji wetu ambao wameshashinda kesi Mahakamani, lakini Serikali haijarudisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais hapa kwa uchungu mkubwa nikijua kwamba Serikali italichukulia hili maanani. Nimesoma hotuba ya Waziri, hakuna hata mstari mmoja alipozungumzia juu ya mifugo hii. Wewe unajua kwamba haki inatolewa na chombo gani? Nanukuu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara 107 (a) (1) Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama imeshaamua ng'ombe warudishwe, wahusika hawajarudisha mpaka leo hii hawa ng'ombe wa wafugaji. Waziri wa Maliasili na Utalii hajarudisha mifugo ya wananchi, Waziri wa Katiba na Sheria amekataa kurudisha mifugo ya wananchi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekataa kurudisha mifugo ya wananchi, Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali *DPP* amekataa kurudisha mifugo ya wananchi. Hawa wote wamevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo wao wameapa kuitetea na kuilinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Mawaziri wote wanen na hawa watendaji wengine wamevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo wao wameahidi kuilinda. Kwanza ni wasimamizi wa haki na sheria, inakuwa vipi waivunje sheria hiyo? Kama sheria imevunjwa, kama Katiba ya Jamhuri imevunjwa, Bunge hili ambalo limeapa kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba imevunjwa...

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, naomba tupokee taarifa.

### **TAARIFA**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kwamba mchangiaji wakati ule alikuwa Waziri wa Mifugo na hizi kesi zimetokea akiwa Waziri. Tunataka kujua ni kwa nini yeye hakurudisha? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Hilo ni swali au taarifa! Mheshimiwa Mpina endelea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, acha niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Mawaziri wamevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 107 (a). Kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano imevunjwa na Mawaziri hawa, Bunge lako lichukue nafasi. Hatuwezi kukubali wananchi wakadhulumiwa kwa namna hiyo inayoendelea sasa. Ng'ombe 6,000 wamekamatwa, wananchi hawa wameshinda kesi Mahakamani halafu mifugo hii inaendelea kushikiliwa...

**MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Musukuma.

### **TAARIFA**

**MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa tu mzungumzaji kwamba maneno anayoyazungumza yananikumbusha Bunge lililopita wakati tukichangia kuhusu suala la uvuvi, lakini alishindwa

kutusaidia kwa sababu alikuwa anatekeleza sheria. Sasa nadhani angejikita kushauri kama Bunge tubadilishe sheria kuliko kumu-*attack* Mheshimiwa Waziri. Akiendelea hivi, kuna watu tutalia humu, tumechomewa mitego, Mheshimiwa Mpina uliapiza humu. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, unaipokea taarifa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna taarifa pale ya kupokea, itanipotezea muda. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nitaomba *adjourning motion* nizungumze kidogo haya maeneo yanayochomekwa haya kwa sababu muda wote nilisimamia hiyo Sheria ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi hawa wameshinda kesi Mahakamani, Mahakama Kuu zimeamua mifugo irudishwe; Mahakama ya Rufaa imeamua mifugo irudishwe; nani tena mtoa haki mwingine ambaye anasubiriwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako liamue leo, azma ya mifugo ya wananchi hawa irudishwe kwa wananchi ambao wamepata mateso makubwa sana kwa muda mrefu na Serikali imeshindwa kurudisha mifugo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilzungumze hapa ni suala la utanuzi wa maeneo. Maeneo ya malisho yaliyo mengi mipaka ya hifadhi ilitanuliwa, ikachukua maeneo mengi sana ya malisho. Baada ya kutanuliwa, kwa mfano, ukienda kule Nsumba kule Ushetu; msitu ule wa Nsumba umeingizwa *GN*juu ya *GN*. Waziri wa Maliasili akatangaza *GN* wakati ule ni msitu wa wananchi wa eneo hilo na ulikuwa ukitumika kulishia mifugo. Huo ni mfano tu mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuje katika nchi yetu, tumeanzisha *WMA* zaidi ya 22, nadhani kwenye hotuba ya Waziri inaonyesha ni 38; na hiyo 38 imechukua hekta 3,062,300. Vile vile kuna shida kubwa sana katika hayo maeneo ya *WMA* ambapo vijiji 37 wameomba kujitoa, lakini hawasikilizwi. Bado kuna vijiji vingine walitoa eneo la *WMA* la zaidi ya asilimia 78 ya maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Vilima Vitatu kule Manyara, ukaenda Ipona kwenye Pori la Akiba la Mara, asilimia 75 imechukuliwa. Wananchi wale wanaomba muda wote kwamba maeneo yao yaweze kuangaliwa kufanyiwa tathmini, lakini hawaendi. Waziri wa Maliasili kuna shida gani kwenda kuwasikiliza wananchi wenyе malalamiko haya? Waziri wa Ardhi ambaye ndio refa wa ardhi nichini, unafanya nini kwenda kumaliza migogoro ya wananchi hawa tukaimaliza kabisa, mpaka mwishowe tuwe na malalamiko ya kudumu ya muda wote huo mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamechukua maeneo, kama ninavyozungumza hekta 3,062,300, yote haya tuje kabla ya *WMA* yalikuwa ni maeneo ya kulishia mifugo. Kwa nini leo hii maeneo haya wananchi wanaomba kwenda kufanya tathmini yasiende kufanyiwa tathmini ili sehemu nyingine ya ardhi ambayo inaweza ikapatikana wafugaji hawa wapewe? Sasa wananchi hekta zao 3,062,300 zimechukuliwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mpina. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Awali ya yote nakupongeza wewe kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, lakini pia umetosha kwenye kitinana kwamba ni mzoefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitoe shukrani kwa Wizara ya Maliasili. Pamoja na changamoto nyingi za Bonde la Kilombero, nimekuwa tukipishana nao mara nyingi tunagombana, lakini walau kwa kidogo tunashukuru kwamba wametoa idhini wananchi wetu waliolima kule waweze kuvuna kipindi hiki ambapo mpunga upo tayari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, niseme tu, natoa pongezi kwa Watendaji wa Jeshi USU la Uhifadhi, Kamishna wa Uhifadhi wa Ngorongoro Daktari Manongi; Kamishna wa TFS, Profesa Silayo Dos Santos, Kamishna Kijazi wa TANAPA, ambaye kwa sasa amepanda kuwa Katibu Mkuu wa Wizara. Nawapongeza kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote kwa yote, niseme utalii nchi hii unakumbana na changamoto kubwa mbili; ya kwanza, ni utegemezi wa alna moja ya utalii kwa maana ya utalii wa wanyamapori ndio sehemu ambayo tumelalia sana. Changamoto ya pili ni utangazaji wa utalii usiotosheleza. Kipande hicho hicho cha utangazaji wa utalii na chenyewe kina changamoto mbili; ya kwanza ni ufinyu wa bajeti; na ya pili ni ubunifu usiotosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika suala la kutegemea utalii wa aina moja, zaidi ya asilimia 80 au 90 ya watalii wanaokuja Tanzania wanaenda kwenye Hifadhi ya Taifa, kwenye Mapori ya Akiba na maeneo mengine mbalimbali ambayo tumejaliwa kuwa nayo. Ila ukiangalia takwimu za nchi ambazo zinafanya vizuri duniani na Afrika kiutalii kwenye kumi bora zote za Afrika, zimetajwa hapa asubuhi; *Morocco, South Africa* na maeneo mengine hawana vivutio vingi kwa maana ya wanyamapori, hawana hifadhi nyingi nzuri kama za kwetu, lakini wanafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili linatakiwa liifkirishe Wizara, Serikali na nchi kwa maana tunakoelekea utalii wa wanyamapori unaweza ukapotea na utalii mwininge mbadala ndio ambao unashika hatamu. Kwa hiyo, naomba Wizara ichukue hili kama changamoto. Tuna vivutio vyaa asili;

ukiangalia *beach* ya *Lake Tanganyika*, kule Kirando na Kipili Nkasi, ukiangalia tuna kimondo pale Mbozi, *Olduvai Gorge* kule Ngorongoro na maeneo mengine mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa kitamaduni ni vitu ambavyo vinapendwa sana na watalii wengi. Kwa hiyo, naishauri Serikali tujikite kwenye maeneo hayo. pamoja na kwamba tunafanya utalii wa wanyamapor, lakini utalii mbadala hasa wa kitamaduni uweze kuzingatiwa na kuangaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya utangazaji wa utalii, nilzungumza suala la kibajeti, ni kweli bajeti yetu ni finyu, Bodi ya Utalii ambayo ina dhamana ya kufanya matangazo, imekuwa ikitoa fedha ambazo siyo toshelezi kulinganisha na nchi shindani, lakini hata hicho hicho kidogo hatufanyi ubunifu kuweza kukitumia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu hata tufanye vyovyyote vile hatuwezi kuwa na fedha nyingi kama nchi nyingine ambazo zimetajwa saa zile, lakini ubunifu ndiyo kila kitu. Nitolee mfano, kufanya matangazo ya utalii kwenye *Media* kubwa kama *CNN* kwa dakika moja haipungui milioni 200, 300 na kuendelea. Ukweli ni kwamba tunaweza tusimudu sana, lakini ubunifu ni kwamba *television* zote kubwa; *CNN* na *Aljazeera* na wengine wana vipindi vya Makala kwa maana ya *documentaries*, wanaonyesha uhaba wa maji Afrika, Sudan, Tanzania na kwingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kufanya *lobbying* tukatumia *documentaries*, tukawaalika wakafanya kama *documentary* kuonesha vivutio vyetu, sisi tunakuwa tumepitia humo humo, tukaonwa na dunia nzima kwa bei rahisi ambayo pengine inaweza ikawa bure kabisa kuliko kutegemea kujaza bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bajeti ndogo ambayo imekuwa ikitolewa kwa ajili ya Bodi ya Utalii, maisha yangu yote ambayo nimekuwa Wizarani haikuwahi kutolewa hata kwa asilimia 90. Bajeti inatengwa, lakini fedha ambazo

zinatolewa kwa ajili ya utekelezaji kazi ni ndogo mno. Kwa hiyo, katika hali hii hatuwezi kushindana na mataifa mengine ambayo yametutangulia Afrika na dunia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuongezea kwenye ubunifu, nilikuwa naishauri Serikali, jambo hili Wizara ya Maliasili isaidiwe na Serikali kiujumla, kwa maana kwenye balozi zetu; watalii wengi tunawategemea wanatoka kwenye mataifa ya nje, tunawaagiza mara kadhaa mabalozi wafanye kazi kuleta watalii Tanzania, lakini unaweza ukakuta wenyewe hawana uelewa mkubwa juu ya suala la utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nishauri Wizara ya Maliasili na Mambo ya Nje wakashirikiana, tuwapeleke waambata wa utalii kwenye balozi zetu. Kuna waambata wa jeshi, kuna waambata wa idara, wapo kwenye balozi. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Mambo ya Nje na Maliasili zishirikiane tuwaweke Maafisa Utalii kwenye balozi zetu waweze kuwasaidia mabalozi kuweza kutangaza nchi yetu. Kinyume na hapo, tutaishia kuwalaamu mabalozi tu, lakini kazi haitaonekana kwenye sekta hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikihamza kwenye eneo hilo, kuna suala la vita dhidi ya ujangili. Mara nyangi kumekuwa na malalamiko na Jeshi *USU* la Hifadhi kutokana na kutotosheleza kwa *manpower*, kwa maana wapiganaji ni wachache. Mara kadhaa *TANAPA*, *Ngorongoro*, *TFS* na *TAWA* wamekuwa wakilalamika pengine na kuhitaji nguvu kazi kwa ajili ya ziada. Niseme, jambo hili tuli-*support* lakini ushirikiano uwe mkubwa kwa Serikali kiujumla wake. Tukimwachia Maliasili peke yake hataweza kulingana na *manpower* aliyonayo. Kwa hiyo, naomba tu, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Maliasili kuunganishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, wafanye ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wanamaliza *JKT*, wanakaa kwenye makambi yetu, wanajitolewa miaka miwili kumwagilia maua, kupanda bustani; wamekuwa *trained*, wale ni askari, wachukuliwe, wapate *short course* kidogo ya

uhifadhi, waripoti kwenye Jeshi *USU*la Uhifadhi, wakisimamiwa na Maafisa wa kule waweze kufanya *operation* ambazo zinapaswa hizo za kisheria. Kinyume chake tutalia suala la kuongeza askari, inaweza ikachukua miaka mingi tusiweze kumudu kupata idadi toshelezi, wakati tayari tuna nguvu kazi ya *JKT* au Jeshi la Wananchi Wapiganaji ambao wapo tu sasa hivi ambao ni ziada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili jambo lisiasihiwe Wizara ya Maliasili peke yake, askari wengine watumike, wapate *course* ya muda mfupi. Kule watalipwa tu posho kwenye *paramilitary*ile ya *conservation*, mishahara yao itaendelea kwenye majeshi yao ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano kwenye suala la *TFS* kwa maana Wakala wa Huduma ya Misitu, wamekutana na changamoto kubwa za kihifadhi. Doria zimekuwa ngumu, changamoto ni kubwa, askari wanalemewa hasa kwenye misitu yetu ambayo ipo karibu na mipaka. Kule Kigoma Misitu ya Makere Kusini na Kaskazini, majangili wamekuwa wakiingia kufanya uvunaji haramu wa misitu, *TFS* wanalemewa. Mara kadhaa kumekuwa na *incidents* wapiganaji wanazidiwa, wengine wanauliwa, mambo kama haya huwa hatutangazi, huwa hayasemwi, lakini yapo. Kwa hiyo, kuna haja ya Jeshi la wananchi au *JKT* kuongeza nguvu kwa *TFS* na Jeshi la Uhifadhi kwa ujumla wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuna suala la muundo mzima wa *conservation paramilitary*, Jeshi *USU* la Uhifadhi. Sasa kwa sababu masuala mengi ni ya kijeshi, siwezi kuyasema hapa, lakini nimeandika kitabu changu cha Maisha Yangu ya Uaskari kama Afisa wa Jeshi USU, humu kuna madini mengi. Naomba Wizara wakichukue, watapata vitu vingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa upendeleo, Jeshi la Uhifadhi kwa sasa lina-*operate differently* kwa maana ya kila...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana kwa kutupa mchango na kutukumbusha kwamba nchi yetu ina utajiri mwingi, lakini zaidi labda pengine kwa kuboresha ni kwamba nchi yetu ni ya pili kwa vivutio vyta utalii duniani baada ya Brazili. Tathmini ambayo inatakiwa tuifanye tujilize: Je, sisi ni wangapi kwa idadi ya watalii duniani? (*Makofii*)

Sasa namkaribisha Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nakupongeza kwa kupewa nafasi kubwa kama hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai siku ya leo. Pia nawashukuru wananchi wa Urambo wakiwemo ndugu zangu kwa ushirikiano wanaonipa. Nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Urambo kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote ndani ya Wizara yao. Hongereni kwa kazi kubwa mnayofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kwa niaba ya wananchi wa Urambo kuishukuru sana Serikali kwa kutupa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugala. Mwaka 2019 lilipitishwa azimio, kwa hiyo, sasa tuna Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugala. Hata hivyo, Serikali inapokuja na mambo mazuri kama haya ya Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugala, kuna umuhimu wa kuwapa elimu wananchi wanaohusika. Sasa tunajua wananchi wangapi wanajua faida ya kuwa na Hifadhi ya Msitu? Watanufaika vipi? Wataishije? Kwa hiyo, kuna umuhimu wa

Serikali inapochukua hatua kubwa kama hizi, kuwaelimisha wananchi wajue wataishije? Watanufaika nini? Kwa sababu, lengo kubwa ni kujenga mahusiano kat i Serikali na wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka pia niwaambie kwamba Kata nne za Nsenda, Ukondamoyo, Ugala na Kasisi, maeneo yao yalipunguzwa na mwaka 2014 kulitokea mgogoro. Wao wanaamini kwamba jiwe lao halali ni Namba 23 ambalo lilikuwepo kabla maliasili na utalii haijaweka mipaka yake. Kwa hiyo, wakawa wamerudishwa nyuma kilomita zipatazo 10. Kwa hiyo, likawapunguzia nafasi ya kulima, kufuga mifugo yao yaani ng'ombe na kadhalika na pia kuweka mizinga yao ya asali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa eneo kama hili ambalo liliababisha askari kuchoma nyumba zao na liliitetwa mpaka humu Bungeni, kwa kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati huo alikuwa Mheshimiwa Pinda na wakatoa pole kwa wananchi. Kwa hiyo, tayari kulikuwa na msuguano ambapo Serikali ingetafuta nafasi ya kuweka mahusiano mapya ili kuwe na ujirani mwema. Badala yake sasa hivi imekuja na hifadhi kabla haijaweka mahusiano mazuri na wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na shukurani kwa Serikali kutupa hifadhi, bado kuna haja ya kwenda kuwapa wananchi elimu, wataishije baada ya kuwa na Hifadhi ya Taifa? Maeneo yao yaliyopungua sasa, kwa sababu wamerudishwa nyuma kilomita 10, watapata wapi eneo lingine? Kwa hiyo, naomba niwasilishe maombi yao wananchi wa Urambo hasa katika Kata hizo nne ambazo zimeathirika kwa njia mojawapo ingawa wamepata faida ya kupata hifadhi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tulikuwa tunaomba wapewe elimu ya faida ya TANAPA na kadhalika na wataishije? La pili, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge walioomo humu, walioiomba Serikali kufikiria upya kwa kuwaongezea maeneo ya kulima, kufuga na kuweka

mizinga yao ya nyuki. Kwa hiyo, tunaomba kwa heshima na taadhima tupatiwe angalau kilomita tano kwa sababu, walirudishwa nyuma kilomita 10. Angalau tupate kilomita tano wananchi waweze kulima, kufuga na kuweka mizinga yao ya asali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tunaomba baada ya kuongezewa eneo, tupate mashine za kuchuja asali, nasi tupeleke Urambo asali, kwa sababu ndiyo maendeleo yenyewe hayo. Watu walikuja pale wanaita *Follow The Honey* kutoka *America*, lakini sasa tena ndio mmetufukuza, haturuhusiwi kuweka mizinga ndani ya eneo. Kwa hiyo, tunaomba kabisa kwamba tupewe mashine za kuchuja asali lakini wakati huo huo tuweze kuruhusiwa kuweka mizinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali imetupa ruhusa tarehe 6 mwezi huu wa Juni mpaka tarehe 6 mwezi wa Julai kuvuna asali, lakini baada ya hapo mizinga tunaweka wapi? Kwa hiyo, tunaomba tuongezewa eneo kama nilivyosema tulime, tufuge na tuweke mizinga yetu ya asali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala siyo la leo. Mheshimiwa Naibu Waziri na aliyekuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hasunga namwona pale. Alikuja, wazee wakamwonyesha mawe yao ya asili, alikuja Mheshimiwa Ramo akiwa Naibu Waziri, alikuja Mheshimiwa Naibu Waziri Angelina Mabula na yeye akawaweka wataalam, anajua. Kwa hiyo, suala hili siyo jipya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alikuja Mheshimiwa Kigwangala lakini bahati mbaya siku alikuja, mvua ikanyesha akashindwa kuingia. Maana yake nini? Nataka kusema hili tatizo au mgogoro huu wa mipaka siyo wa leo, ni wa siku nydingi na tulileta hapa Bungeni kwa barua hii hapa, kwamba Serikali katika ile Tume iliyokuwa inapitia migogoro, nasi tulileta. Kwa hiyo, nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi naye anasikiliza, naamini kabisa katika hili atatusaidia kwa

kushirikiana na Waziri mhusika wa sasa ili tupate maeneo yale kama yalivyokuwa yamekusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa heshima na taadhima kabisa, pamoja na kuipongeza Serikali kutupa hifadhi, bado tunahitaji waje wajenge mahusiano, watuongezee maeneo kama tulivyoomba, Serikali yetu ni Sikivu, inawapenda wananchi wake, tuongezewe eneo la kulima na kufuga na kuweka mizinga yetu. Tuna asali nydingi sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimiratajje Mheshimiwa Waziri maeneo ambayo atayakuta kule ambayo kweli yana changamoto katika hiso Kata nne. Atakuta Izengabatogilwe, Lunyeta, Mwagimagi, Msumbiji, Utewe, Mkola, Utenge, Mwengemoto na Holongo; katika hiso Kata nne ambazo nimezitaja hapo awali. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima, pamoja na kuunga mkono, nawapenda hawa Mawaziri kwa sababu ni wasikivu. Mheshimiwa Waziri mhusika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wote ni wahusika. Hayo matatu naomba nirudie kwa mara ya mwisho kabla kengele haijalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga mahusiano kwa kutupa elimu; pili, kuomba eneo, tuongezewe angalau kilomita tano, Serikali yetu ni nzuri; na tatu, tunaombwa mashine ili mizinga tutakayoweka, tuweze kuchuja asali yetu, Urambo tupeleke asali duniani. Waamerika wanasesma nzuri sana kwa ajili ya *chocolate*, kwa sababu ya kwetu ni nyeusi safii. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati mjadala unaendelea, naomba nitumie nafasi hii, kuwakaribisha baadhi ya wageni kwa sababu, wangehitaji kutoka.

Tuna wageni 23 wa Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge ambaao ni Timu ya Mpira ya Shirika la Utangazaji (TBC)

kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mkurugenzi, Ndugu Ayub Rioba. Kama mnavyofahamu, kesho kutakuwa na mechi kama siyo keshokutwa. Kwa hiyo, hawa wanajandaa kwa ajili ya kucheza. (*Makofi*)

Pia, tunao wageni 100 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Taifa cha Utalii Jijini Arusha, wakiongozwa na Ndugu Agnes Chuwa. Karibuni sana, sana wageni wetu kutoka Arusha. Ahsante. (*Makofi*)

Vile vile tunaye mgeni wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji ambaye ni ndugu yake kutoka Mafinga Mkoani Iringa, Ndugu Noel Nkana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge, ambaao ni Meneja Mwandamizi Benki ya NBC, Makao Makuu, Ndugu William Kallaghe, William Junior na Michael Nderumaki. Karibuni sana. (*Makofi*)

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimboni Itigi Mkoani Singida, Mchungaji Peter Sintoo. Karibu sana, Sintoo kutoka Singida. (*Makofi*)

Pia, tunaye mgeni kutoka Monduli Mkoani Arusha, ambaye amekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake, Ndugu Jubilate Obadia. Karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Namkaribisha Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba na wakati huo Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile pamoja na Francis Kumba Ndulane, wanajandaa.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nakupongeza wewe, Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonipelekea kuchangia kwenye Wizara hii ni kitu kimoja tu. Kuna sheria mpya hapa *ame-introduce* Mheshimiwa Waziri, ambayo inamtaka mtu atakayekuwa na gunia moja la mkaa, ni lazima akapate kibali kutoka Halmashauri ya Wilaya na awe na *EFD machine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda wenzetu wangejaribu kuangalia jiografia ya nchi, maisha ya wananchi wetu yalivyo unapotaka kutengeneza kitu kama hiki. Ina maana tatarajie ndani ya mwezi mmoja kutatokea *chaos* kubwa mno ya mkaa. Je, itawezekana? Yaani kwa kawaida itawezekana watu wasipike kweli na wasile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Wizarani labda wawe wanajaribu kuangalia yanayotutesa kule majimboni. Kuna majimbo mengine kutoka kwenye Makao Makuu ya Halmashauri kwenda kule kijijini ni zaldi ya kilomita 200. Mwananchi anataka gunia moja la mkaa kwenye mti wake mwenyewe, kweli aende mpaka wilayani apate na *EFD machine*! Anaipata wapi *EFD machine* mtu wa gunia moja? Ni kitu ambacho wala hakiwezekani wala hakiingii akilini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii vita ya mkaa na kuni toka tunapata uhuru, toka wametuachia Wakoloni: Je, watu milioni 60 wanaotumia mkaa na kuni itatokea wataacha kula? Nani ataibuka mshindi kwenye hii vita? Kwa nini Wizara isirasimishe hii biashara kama tulivyofanya kwenye madini? Dhahabu tulihangaika miaka 50, lakini ilivyorasimishwa, leo hatuna matatizo na biashara ya madini. Kwa nini mkaa na kuni usirasimishwe ukaenda halali, wao wakachukua ushuru wao kwenye gulio, wakapanga kabisa pale kwamba hii miti ya Serikali ikae hapa/mbao za Serikali zikae hapa, mkaa wa Serikali ukae hapa; mkaa wa mkulima mwenyewe mti ukae hapa ili biashara hii iwe halali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, ye ye *TFS* au ye ye Wizara ya Maliasili na Utalii, anao kweli askari wa kutosha kuwazuia watu milioni 60 wa Tanzania wasipike? Yeye mwenyewe hapa amekula chakula cha mkaa, sisi

tumekula chakula cha mkaa, anayekamata amekula chakula cha mkaa. Itawezekana? Ni kitu ambacho hakiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu ya kupigana vita usioshindia? Leo mkaa, kwa wenzetu Namibia na *South Africa* inaitwa dhahabu nyeusi, ni fedha. Sasa kama leo unasema kwamba huyu mwananchi tukamzuie kuchoma mkaa, nawe unatuambia tukamwambie apande mti, anapanda mti kwa ajili ya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake, sisi kwetu huko Kanda ya Ziwa ukimwambia mtu apande mti kwa ajili ya mvua, anakuona wewe ni mpuuzi. Maana tuna mafuriko miaka miwili. Atakuuliza: Je, unataka tupande miti ya kuzuia mvua? Maana yake ukiwaambia unataka miti ya mvua, wanakuuliza kuzidi hii illyopo leo? Hii mvua illyopo leo unataka izidi hapa? Ilitakiwa sisi tukawaambie panda miti ya kutengeneza fedha, ndiyo wananchi watapanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine mnasema labda tunawasakama wasomi, lakini jaribuni kufikiria maisha halali ya wananchi. Jiji la Dar es Salaam au Mji wangu wa Kahama, ukiuzuia mkaa kwa siku nne, unategemea nini? Maana yake yule mchoma mkaa hana ulazima wowote, ni mtu yuko porini, ataacha kuja kuchukua kibali. Sasa vipi hawa watu wa mijini, unataka gunia la mkaa lifike shilingi 300,000/=? Unao mkaa wewe wa *ku-supply*? Ni kitu ambacho lazima wenzetu wafikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania ni nchi ya nne kwa *ku-export* mkaa wa magendo na *TFS* hajawahi kutoa *export permit* ya mkaa, lakini kwenye *data za World Bank* inaonyesha ni ya nne. Sasa unakataaje kurasimisha ili upate hizo fedha na wale wanaonunua wa magendo waje wanunue pale kwenye soko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wenzetu wataalam lazima wafikirie sana. Haiwezekani baada ya miaka 60, kweli watoto wasome waende wakawe mgambo wa kukamata

wazazi wao, ni sawa kweli! Haiwezekani! Kazi ya elimu duniani ni kutatua matatizo. Leo, Wazungu wametengeneza mpaka mapapai ya miezi sita. Wazungu wametengeneza kuku wa kizungu baada ya kuona kuna tatizo la kuku wa kienyeji na mayai yapo ya kizungu. Kwa nini hawa wataalam wasipande miti, wasilete miti ya miezi sita ili watu wakawa wanapanda miti wanaauza kuni na mkaa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kurudi kwenye eneo la ugomvi, ugomvi, ugomvi, haiwezekani. Lazima twende kwenye pesa. Ina maana sasa hivi wao wanaenda kuanza *fine*, utawafunga watu milioni 60! Halafu mnataka hao watu tukawaombe kura. Unaweza? Unaweza ukaomba kura kwa watu uliowakatalia kula? (*Makofi*)

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Karibu.

## TAARIFA

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kesi zote zinazohusisha misitu ni kesi za uhujumu uchumi. Sasa na mkaa utaingia huko: Je, nchi hii itakuwa na nusura? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kishimba, unapokea taarifa?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono mitatu. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Haya, endelea.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua na wewe ni *graduate*. Tunataka wasomi mtuletee mabadiliko. hatutaki wasomi kuwa Polisi, tunakuwa na majeshi mangapi? Tuna Jeshi la Polisi, tuna Jeshi la Wananchi, tutakuwa na majeshi kutwa nzima, haiwezekani. Tunataka

mkaa ugeuzwe kama alivyofanya Mheshimiwa Dotto kwenye dhahabu. Sisi tumekaa gerezani miaka 20 kwa ajili ya dhahabu, lakini leo dhahabu si imekuwa halali? Ambayo ni sahihi. Kweli twende kuwaambia wazazi wetu kwamba tunakuja kukamatwa shauri ya miti. Sasa wanafanya nini? Haiwezekani tupeleke uhujumu wazazi wetu kwa ajili ya miti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana wenzetu wa maliasili, wajaribu kuangalia kabisa maisha ya watu. Tunapoongea, leo Jiji la Dar es Salaam ukiangalia matumizi ya mkaa ni makubwa mno. Kwa nini kusiwe na soko tu kesi hii ikaisha, wakachukua na ushuru wao pale pale; ili iwe ni kitu huru na kila mtu apende kupanda mti? Kupanda mti ni rahisi zaidi kuliko kulima mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kutoka kwenye Sheria za *TFF*. Maana yake *TFF*najua ndiyo yenye sheria ngumu sana, naye najua alikuwa kiongozi wa *TFF*. Ni kweli! Alikuwa *TFF* kwenye mpira, nafahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana wenzetu, kuna suala hili la mifugo. Kwa kuwa wewe mwenyewe ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Viwanda, Mazingira na Biashara...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Ni kengele ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wewe ndio Mwenyekiti wa Kamati yetu, najua hiki tunachoambiwa kwamba ng'ombe kwenye mapori yale ambayo hayana Wanyama, kwamba ng'ombe wanaharibu mazingira; unaonaje tukiteuliwa Wabunge watano na wataalamu watano, tuchukue ng'ombe 100 tukakae mle

porini siku nne tuchunge wale ng'ombe, tuone *physically* uharibifu unaosemwa? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Karibu Mheshimiwa, *Doctor.*

## T A A R I F A

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nimpe mzungumzaji taarifa kwamba kuna *model* za ufugaji wa mseto kati ya wanyamapori na mifugo ambayo imeshafanywa hapa Tanzania na hata Kenya. Tanzania kuna Ranchi inaitwa *Manyara Ranch* Mkoa wa Arusha, kuna mifugo maelfu pale na wanyamapori; ni njia ya wanyamapori na hatujaona madhara. Kule Kenya kuna Ranchi inaitwa Ol Pejeta ina hekta 95,000, kuna mifugo zaidi ya 5,000 na wanyama wa kila aina, hata faru weupe wapo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Unapokea hiyo taarifa Mheshimiwa Kishimba?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kupingana na elimu, lakini hao walimu wenu wanaowafundisha, waliwahi kuchukua ng'ombe 100 wakakaa porini ndiyo wakaandika huo uharibifu? Maana yake tunashinda tunazozana tu na wananchi mpaka wananchi wanaona kama hata na nyie Wabunge ni wapuuuzi tu. Hivi kweli, ng'ombe anafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna wanyama mle porini. Sawa, wananchi wako tayari kulipa, lakini watu wa maliasili wanachukua hela, wanaweka ng'ombe. Kwa nini tusiende nao tukaka humo siku tano tuone *physically* kwamba hasa huwa kinaharibika nini? Maana tukikalia tu makaratasi na kusomewa risala, uharibifu wa mazingira;

itakuja kuwa mpaka lini? Wenzetu wanatengeneza pesa, hatuwezi kukaa na mawazo ya makarasi kwa sababu tu mtu mmoja amesema, yeye amesoma; uharibifu wa mazingira alisomea London. Sasa wewe, tunataka kama ulisome London, utuletee mawazo ya kupata pesa, hatutaki mawazo ya London kuja kutukwamisha sisi, hapana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwininge huwa sipendi lugha ya Musukuma, lakini kuna wakati kwenye hili, inabidi niungane na Mheshimiwa Musukuma. Kweli inauma sana. Anakuja kijana kasoma, anasema hamruhusiwi kupikia mkaa, hamruhusiwi kuni, ni uharibifu wa mazingira. Kuni sisi tunachukua matawi. Leo ukitembea na gari usiku au mchana, wazee wamebeba matawi, hakuna mtu anakata gogo la mti. Sasa unawakatazaje? Hao unaowakataza, ndio wallkusomesha wewe na ndio wanaolipa kodi. Hiyo *degree* yako unaongea kiingereza, si ndio hao wanaotoa hela? Sasa unawakatazaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea wewe umesoma, uje ulete mawazo kama Wazungu wanavyofanya. Mimi nimetoka Ulaya, nimekuja na miti ya kisasa, inaota miezi mitatu, unakata mkaa, unauzu kwa pesa. Tunataka hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nashukuru sana, lakini namwomba sana Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kishimba. Haya, sasa ni Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi. (*Makofi*)

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze kwa kumpongeza

sana Rafiki yangu Waziri pamoja na Naibu wake; timu nzima ya Wizara pamoja na wadau wa utalii na maliasili kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye maeneo kama manne hivi. Kama muda hautaniruhusu, nitapeleka kwa maandishi. Nitachagia suala la *Half Mile*, wapigakura wangu wamenituma kule Moshi kwamba niombe kitu kuhusu *Half Mile*. Halafu nitatoa ombi la Wizara ikiwezekana wafungue *route* mpya za kupanda mlima Kilimanjaro kuititia Kata za Mpakani za Uru na za *Old Moshi*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda tutambue uwepo wa mti mrefu kuliko yote Barani Afrika wenye mita 81.5; na huu ndiyo mti mzee kuliko miti yote duniani, uko Kilimanjaro kwenye Kijiji cha Tema kwenye Kata ya Mbokomu. Pia nitazungumzia mgogoro uliopo wa kwenye hifadhi ya Ngorongoro kama muda utaruhusu kwa sababu watu wameongezeka kama alivyosema Mheshimiwa Paresto na kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa *half mile*. *Half mile* ni nini? *Half mile* ili ni eneo linalotenganisha Mlima Kilimanjaro eneo la hifadhi na makazi ya wananchi. Kwa hiyo, ni eneo lenye upana wa nusu maili ambalo linatengenisha watu na Mlima Kilimanjaro. Historia ya watu Kilimanjaro inaonesha kwamba tulianza kuishi pale karibia miaka 2,000 iliyopita. Kwa hiyo, tumeCAA pale muda mrefu tu. Pamoja na kukaa huko kwa muda mrefu, lakini tuna *experience* mbaya sana watu wa Kilimanjaro kuhusiana na umiliki wa ardhi kule kwetu na hizi hifadhi za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu tumevirithi, lakini niseme tu mwaka 1921 tulipata shida kidogo na Wakoloni, walipitisha sheria ya kusema kwamba watu wasiende kule Kilimanjaro kule mlimani, iliwekwa sheria kabisa kwamba mtu akienda kule ni kosa. Mwaka wa 22 Gavana aliyeokuwa

anatawala nchi yetu alisema ardhi yote ni yake; na mwaka 23 wakaanza *program* mbaya kabisa ya kuwanyang'anya watu ardhi yao na kujimilikisha na kuanza mashamba ya *masetla*. Mashamba hayo tuna bahati kwamba yalitaifishwa mwaka 1967 kupitia Azimio la Arusha, lakini bado hayajawa mikononi mwa wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wakoloni wametuletea matatizo makubwa sana kwa sheria kandamizi za umiliki wa ardhi pamoja na zile maliasili zetu. Pamoja na ukatili wa Wakoloni, niseme kwamba mwaka 1941 walianzisha kitu kinachoitwa *half mail*. Walituonea huruma wakasema ruksa sasa nusu maili wananchi mwingie mpate huduma za misitu kama kuni, mboga kama mnavu za kwenda kupika kitalolo, kuna chakula cha kienyeji kule nyumbani, mkajipatie mbao za kujenga na vitu vingine. Kwa hiyo, walituruhusu, walikuwa na huruma kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliendelea hivyo mpaka mwaka wa 2004. Matumizi yalikuwa mabaya kwenye hii *half mail*, Serikali yetu ya Tanzania ikasimamisha ule utaratibu ambao wakoloni walituonea huruma Serikali ikasema sasa basi kwa sababu mmeshaharibu sana; ni ukweli kulikuwa kuna uharibifu kwa sababu usimamizi haukuwa mzuri sana kwenye hii *half mail*, Serikali ikasimamisha, kwa hiyo, ikawa tena hakuna *half mail* na lile eneo likawa *declared* ni eneo la Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zuio hili la Serikali liliondoa ile huruma ya wakoloni ambao walituhurumia watu wa Kilimanjaro. Eneo hili sasa hivi linalindwa na maaskari wa *KINAPA (Kilimanjaro National Park)*. Jamani, hawa watu ni wakorofi, wapiga kura wangu wameniambia kwamba wakati naomba kura watu wamepigwa, wameuawa na akina mama wamebakwa. Kwa hiyo, kuna mambo yanaendelea kule ambayo siyo mazuri sana. Wakati Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein alipotembelea

Kilimanjaro mwaka 2008 kwenye safari ya kikazi, wananchi walimweleza hii kero na alikuwa na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe kwenye hiyo ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara ilikaa ikaelekeza *TANAPA* wachore ramani mpya. Kwa hiyo, Wizara ilipelekewa barua ambayo iliandikwa na Mheshimiwa Waziri Maghembe na Katibu Mkuu, Dkt. Ladislaus Komba kwamba wachore ramani ili eneo lirudishwe kwa wananchi. Bahati mbaya mpaka leo hakuna kitu ambacho kimeshafanyika na bado *half mail strip* hatujaipata. Kwa hiyo, tunamwomba Waziri achukulie pale walipoachia wenzake ili atusaidie. Hizi sheria ni kandamizi na zinafanya wananchi waichukie Serikali yao bila sababu. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa Muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, chonde chonde, nakuomba ulibebe hili na hii mtakapopeleka kwa Mheshimiwa Mama Samia tunamwomba sana alifanyie kazi mara moja, nasi tupate haki ya kumiliki na kutunza ule mlima ambao ni wa kwetu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Prof. Ndakideni sasa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa naomba Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile wakati huo Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Edward Olelekeita Kisau wanajiandaa.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami nikupongeze kwa kuwa Mwenyekiti. Nakutakia mema sana katika kazi hiyo. Pia nichukue fursa hii adimu sana kumpongeza Waziri, mtani wangu kwa kazi kubwa sana anayoifanya kwa jamii yetu hii ya Tanzania. Kipekee nampongeza Naibu Waziri kwa kazi

kubwa pia anayofanya na kweli ameonesha hekima kubwa sana hata leo asubuhi, ameonesha upendo wa dhati sana kwenye Wizara yake na hiyo ndiyo tumeona faida kubwa sana ya kuzaliwa usukumani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie mambo machache sana kwenye Wizara hii leo. Naishauri sasa Wizara, leo asubuhi hapa Mheshimiwa Mrisho Gambo amesema asilimia 80 ya mapato ya Wizara ya Utalii yanapatikana kule Kanda ya Kaskazini. Hata hivyo, tunaamini kabisa kwamba Kanda ya Ziwa pia tunaweza kuwa na mapato makubwa ya utalii mkitufanyia mambo ya msingi sana ikiwemo na kufungua geti la Ndabaka lililoko pale Lamadi na pia mtufungulie geti la pale Kijereshi. Mageti haya mawili yatakuwa mageti ya msingi sana kwenye pato la Taifa; vile vile yatakuza uchumi wa Kanda yetu ya Ziwa, yatakuza uchumi wa pale Jimbo langu la Busega, hasa pale Lamadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hoteli nzuri sana *Speke Bay*, tuna hoteli nzuri pale *Serenity* na pia tuna hoteli nzuri pale Ndabaka, zina uwezo kabisa wa kutunza watalii. Naomba mtufungulie yale mageti ili yaweze kupokea watalii mbalimbali. Watalii siyo lazima waende *KIA*, wanaweza kushukia pale *Mwanza Airport* na baadaye wakaenda Lamadi kwa ajili ya kufanya *tour* pale Serengeti.

Kwa hiyo, nawaomba sana, mkitufungulia haya mageti mawili yatafanya kazi kubwa sana ya kukaribisha wale watalii na hasa mkiyatangaza. Myatangaze ili watalii wetu sasa waweze kuititia pale kwenye geti la Ndabaga lililopo pale Lamadi na geti la Kijereshi lililoko kule Kata ya Mkura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nichangie ni uvamizi wa tembo kwenye makazi ya watu. Pale kwangu kuna Kijiji kinaitwa Kijereshi, kuna Kijiji kinaitwa Lukungu, kuna Kijiji kinaitwa Mwakiroba vijiji hivi vitatu vinaathirika sehemu kubwa sana na uvamizi wa tembo. Naomba sasa mchukulie hatua za dharula ili wananchi wetu

sasa waweze kutokutishwa na hawa tembo. Mwaka 2020 tulikuwa na vifo zaidi ya vinne viliviyotokana na uvamizi wa Tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, wewe ni msikivu, naomba sana kwa mara nyingine tuweze kuangalia namna ya kuleta askari wa kutosha tuweze kutengeneza Stesheni pale Kijereshi ili maaskari waweze kukaa pale. Ikipidi linapotokea tatizo, basi wapatikane kwa urahisi kwa sababu sasa hivi wanakaa Lamadi na Kijereshi ni mbali kidogo, tembo wanapoingia kule Kijereshi, wao mpaka waje wafike ni zaidi ya nusu saa muda mwingine, mpaka saa nzima au saa 1.30 ndiyo wanafika. Tembo tayari watakuwa wameharibu mazao, tayari watakuwa wamewadhuru wananchi.

Kwa hiyo, naomba sana, mtengeneze Stesheni pale Kijereshi kwa sababu ndiyo sehemu kubwa ya hifadhi. Pia muwape gari pale. Kuna shida ya gari kwa ajili ya usafiri wa kukabili hawa tembo. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie hili ili tuweze kupata gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililotaka kuzungumzia ni tatizo la *TFS*. Mheshimiwa Waziri, *TFS* ni pasua kichwa kwa baadhi ya watumishi; kuna baadhi ya watumishi sio waadilifu. Ukienda pale Magu, kuna *TFSambao* wanalinda Hifadhi ya pori la Sayaka. Pale ni pasua kichwa. Wanakamata wafugaji, ni sawa inawezekana wanasimamia sheria, lakini faini ni kubwa sana. Ni shilingi milioni sita, shilingi milioni nne au shilingi milioni nane. Ni tatizo kubwa. Naomba sana tuliangalie hili, mfugaji akiambiwa kulipa shilingi milioni sita leo, haiwezekani. Mfugaji akiambiwa kulipa shilingi milioni nne leo haiwezekani; yaani *how much is milioni nne?* Yaani ni fedha nyingi kweli kwa mfugaji mdogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hawa watumishi kidogo wanapokuwa wanalingalia hili, wawahurumie na wafugaji wetu, wawahurumie na wakulima wetu kwa sababu wanaumizwa sana na faini ambazo wanapigwa. Mheshimiwa Waziri, nimeshazungumza, nawe

umeshakubali kuja pale, uje ujionee namna wananchi walivyo na malalamiko juu ya hifadhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakuomba sana, wananchi wale walikuwa na shida ya eneo la mita 840. Naomba sana utakapofika pale uzungumze na wananchi, usikie kilio chao na kama uitaona inafaa Mheshimiwa Waziri, basi muweze kuwarejeshea eneo hilli ili watu wa Nyaruande pale Kata ya Nyaruande katika Jimbo langu la Busega na sehemu ya Jimbo la Magu waweze kunufaika pale Sayaka kwa sababu sasa hivi wanapata shida katika namna ya kupata sehemu za kuchungia ng'ombe, lakini pia sehemu kubwa ya kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri; wewe kule ni kwenu, wewe pale ndiyo umezaliwa, hilli tatizo unalifahamu, njooni militatue ili wananchi wetu sasa waweze kunufaika na hii sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nskushukuru sana, niseme nawapongeza, nawakaribisha Busega mje mtatue huu mgogoro. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji hapa ni ndefu sana. Kwa hiyo, tunafanya dakika tano tano. Ndiyo maana mtaona wachangia wawili waliopita ni kama muda wao umebanwa kidogo. Tunatazama muda wetu pale, halafu tunatazama na idadi ili yopo ili kila mtu apate fursa. Haya, sasa karibu Mheshimiwa Francis Komba Ndulane. (*Makofi*)

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyeiti, ahsante naitwa Francis Kumba Ndulane.

**MWENYEKITI:** Okay Sawa. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyeiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Utalii. Kwa kuwa muda ni mfupi, nitaongelea jambo moja tu, suala la kumbukumbu za Vita vya Majimaji. Naona nilipoongea Vita vya Majimaji, au kule kwetu Kilwa Kaskazini wanavitambua kama *Ngondo ya Machemache*, naona Mheshimiwa Jenista Mhagama ameshituka kidogo pamoja na Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita hivi vilianza tarehe 15 Julai, 1905 katika Kijiji cha Nandete Jimboni kwangu Kilwa Kaskazini, Tarafa ya Kipatimu. Ilihusisha; kama ilivyokuwa kule Songea, kulikuwa na Machifu 12, huku kwetu kulikuwa na viongozi wa koo tisa, ndio ambao waliongoza hivi vita. Naomba niwataje, alikuwepo kiongozi wa Kiroho aliyejulikana kwa jina la Kinjeketile Ngwale, alikuwepo ambaye alikuwa anaishi Kijiji kinaitwa Ngalamibilienga, alikuwepo Jemadari wa vita hivyo, alikuwa anaitwa Sikwako Mbonde, alikuwa anaishi Kijiji cha Nandete.

Pia alikuwepo Ngulumbari wa Mandai, alikuwa anaishi Nandete; Lindimio Machela, Mabiga Nandete, Bibi Ntabilwa Naupunda ndiye ambaye alibeba ile dawa ya maji, Nandete na vile vile alikuwepo Mpeliadunduli Kipengele; alikuwepo Libobo Mpanyu Kipengele; alikuwepo Mataka Nkwela Mwiru; alikuwepo Kilambo Mpetamuba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa miaka mingi wenzetu wa kule Songea Jimboni kwa Mheshimiwa Waziri, wamekuwa wakiadhimisha miaka karibu takriban 114 kuhusu Uwepo wa vita hivi au kumbukumbu za vita hivi, lakini kwa upande wa Kilwa Kasakazini hili jambo limekuwa halifanyiki. Hata miundombinu ya utalii imejengwa kule Songea. Kuna kumbukumbu; *National Museum* ipo, lakini kwa upande wa Kilwa Kaskazini haipo. Kwa hiyo, hata kumbukumbu za hawa wazee maarufu ambao walikuwa na uthubutu wa kupambana na Wakoloni wa Kijerumani mpaka sasa haipo. Kwa maana hiyo, hii historia imekuwa ikififia na hatimaye kutoleta tija katika sekta ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, siyo tu vita vya majimaji peke yake, bali kulikuwa na mazingira ambayo yaliambatana na hivyo vita. Kulikuwa na mapango; Pango kubwa la Nang'oma ambalo ni kubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara, Barani Afrika, lipo pia lile la Namaengo; lipo kaburi la mzungu ambaye alizikwa kutokana na vile vita vya majimaji. Kule tunaita *lisikolian nungu*, lipo katika Kijiji cha Kinywanyu, Kitongoji cha Mbongwe, Kata ya Chumo. Pia lipo boma la Mjerumani mahali ambako Wajerumani waliweka makazi yao kwa ajili ya kudumisha utawala katika eneo lile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hivi vivutio ni vivutio vizuri vya utalii, naomba tuvisimamie...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, hivi vivutio vya utalii ni vizuri. Naomba tuvisimamie, tuvitangaze, lakini tuviwekee miundombinu bora na kuhakikisha kwamba kunakuwa na makumbusho kwa ajili ya kudumisha kumbukumbu za vita vya majimaji na kuvutia watalii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau na wakati huo Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo wanajandaa.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwasababu ya muda nitatoa tu hongera ya jumla hivi, mnielewe. Nitawapongeza baadaye. (*Kicheko/ Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 113 unasema hivi, naomba sana wataalam wetu waisome sana: "Kuimarisha mahusiano kati ya maeneo ya hifadhi na wananchi." Mahusiano ya wananchi na hifadhi ni mabovu sana. Hilo moja. Ilani inaendelea kusema hivi, ili Sekta hii iwe endelevu, lazima mijali haki na maslahi ya wananchi. Hamwangalii sana maslahi ya wananchi wakati mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma vitu vingi tu hapa, nilichogundua ni kwamba, kama walivyosema wasemaji wengine, utalii tangu tumepata uhuru mambo yote bado yapo kikoloni zaidi; *ni boots and guns, fences, fines, mnaanza kuua watu, mnachukua ng'ombe wa watu; hiyo siyo sustainable*. Mwache! Uhifadhi ili uwe endelevu, ni lazima ushirikishe wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambia kwenye *data* hapa kwamba sasa tunaongelea asilimia 32 mpaka 40 ya nchi hii, iko kwenye hifadhi, *it may not be enough*, lakini lazima mfahamu tumeongezeka. Ni dhana ya kikoloni ambayo ni *exclusion, expansion, removable, nature, then people later*, haiwezi kuwa *sustainable*. Nchi nyingine zimeshabadilika, wameanzisha *model* ambazo zina-accommodate watu na uhifadhi. *WMA* ni *classic example*, inawezekana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kukaa na kuanza ku-characterize ardhi za watu, eti *corridor*, eti *buffer zone*, eti *wildlife or pastoral area*, *I mean!* Mheshimiwa Waziri, kuna tangazo laki hapa nililisoma asubuhi hapa. Umewaelekeza watu wako wachaji ng'ombe 100,000 kwa kichwa cha ng'ombe. Miaka miwili iliypita ilikuja sheria hapa ya kutaka kulishawishi Bunge lilete faini ya shilingi 100,000 kwa kichwa na Bunge lilikataa, hongereni sana. Sasa limeanza kurudi kwa mlango wa nyuma.

Mheshimiwa Waziri, *this is illegal*, haiendani na sheria zetu, nawe ni Mwanasheria, Wakili tena Dokta kabisa. Nakushauri sana, *please rethink kuhusu hili, it is illegal, it is unlawful.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana kuna wengine walikuwa wanasema hapa hatufuati sheria. Sheria haijasema *hai-punish* ng'ombe, *inam-punish* mwenye ng'ombe, ndiyo *logic* ya sheria. Sasa ninyi mkianza kuleta; na sheria iko hapa, haisemi hivyo. *Fine* kwa *group minimum* imetolewa na sheria na *maximum*. Kwa hiyo, mna-range pale. Hii *idea* ya kuleta sheria ya kichwa cha ng'ombe *it is illegal*, haipo! Kesho nataka nisikie hii inakuwa *supported* na sheria gani? Kama hamtasema, nitashika shilingi kwa mara ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache. Nchi hii sasa tusipofikiria kuleta *model* zinazotuchanganya Pamoja, huu uhifadhi utafeli. Suala la mifugo, mimi nina mwananchi wangu Kijji cha Warkyushi kuna pori linaitwa na Mkungunero. Pori la Mkungunero by GN iliko Kondoa, Dodoma; lakini wanatuambia eti *beacon* ziko Kiteto, how? Kwanza kisheria ukishakuwa na GNambayo ina-*conflict* na GPS points maana yake kisheria ni kwamba *you can't enforce*, lakini wewe unakamata ng'ombe kila wakati. Mheshimiwa Hayati Rais Magufuli...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante.

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, lakini nitumie fursa hii kukupongeza kwa nafasi uliyonayo. Hongera na naamini utakitendea haki kiti hicho. Naomba nianze kuchangia Wizara hii alipoishia Mheshimiwa Olelekaita kwenye migogoro ya hifadhi na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Mkoa wa Dodoma tuna mapori mawili ambayo yako Wilaya ya Chemba na Wilaya ya Kondoa. Pori la Mkungunero ambalo lipo Kondoa na Pori la Swagaswaga ambalo lipo Wilaya ya Chemba. Pori hili la Mkungunero limekuwa ni kichaka cha Maafisa wa Wanyamapori kutesa Watanzania wasiokuwa na hatia eti kwa sababu tu wana ng'ombe, eti kwa sababu tu ni wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2019 nilizungumza ndani ya Bunge hili nikaeleza mateso na manyanyaso wanayopata wananchi wa wilaya ya Kondoa kwa Kata ya Keikei, Kata ya Kinyasi pamoja na Kata ya Itasu. Mheshimiwa Waziri nimekuja kwako mara kadhaa nikiwa nakulalamikia suala hili na ninyi Wizara mnasema kuna shida gani? Pale tumemaliza kabisa Mkungunero. Ukweli ni kwamba mnafukia kombe mwanaharamu apite wakati Watanzania wanaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita kuna wananchi watatu ambao wamekamatiwa ng'ombe wao. Wawili wamelipa kwa makubaliano na Maafisa Pori wa Hifadhi ya Mkungunero. Mmoja akakataa akapelekwa Mahakamani, ng'ombe 50 kalipa shilingi milioni 10 faini. Hivi huyo mwananchi mkulima, mfugaji anayetegemea mifugo yake kwa ajili ya kuendesha maisha yake ya kila siku na kulichangia kodi Taifa hili, mnachomtafuta ni nini watu wa hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, katika hifadhi ile kuna akina mama ambao wanafanya shughuli zao mbalimbali za kujitafutia uchumi, wamekuwa wakibakwa kwenye Hifadhi ya Mkungunero, wamekuwa wakipata mateso ya kurushwa kichurachura, kupigwa na kila aina ya mateso kadha wa kadha wanayoyapata kwa ajili ya hilo pori. Mheshimiwa Waziri, kuna shida gani? Serikali ni moja, chama kimoja, Mawaziri mnakaa kwenye Baraza la Mawaziri, mnashindwaje kukaa chini na kuweza kutatua mgogoro wa pori hili? Serikali Sikivu, Serikali ya wanyonge mnaotamani kuwapigania Watanzania, hawa Watanzania hawana hatia, ardhi haiongezeki Mheshimiwa Waziri, watu tunaongezeka.

Pori lile Mheshimiwa Waziri kwa akili tu ya kawaida, Warangi sisi hatuna mahali pa kwenda. Lile ndiyo eneo letu tumezaliwa kule, twende wapi? Tunaomba Pori ya Mkungunero, kagaweni eneo, tuachieni na sisi watoto na wajukuu tuendelee kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Swagaswaga Wilaya ya Chemba Kata ya Lahoda, pale kuna wafugaji; na ninashukuru Mheshimiwa Mpina amelisema. Kuna wafugaji mwaka 2018/2019, Mheshimiwa Mpina ukiwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Ulega akiwa Naibu Waziri wako; Mheshimiwa Ulega alienda Wilaya ya Chemba Pori la Swagaswaga akakutana na wafugaji waliokamatiwa ng'ombe wao wasiokuwa na hatia wamewekwa pale, hawana chakula, hawana maji, hawana dawa, hawana chochote. Ng'ombe wamekufa zaidi ya 500. Tulisema humu ndani, hamkutaka kusikia eti tu kwa sababu mnalinda uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji uhifadhi lakini siyo kwa maisha ya mateso ya namna hii mnayotufanyia Watanzania. Mkitushirikisha wananchi, tutaulinda huo uhifadhi kwa sababu na sisi tunautaka na tunauhitaji sana. Ila kama mtaendelea kutunyanyasa, kututesa na kutuonea, hata hao wahifadhi wenu mnaowaleta kule, ipo siku hapatatosha. Tutachoka kunyanyaswa, tutaamua kuchukua hatua mkononi, kitu ambacho sitamani kitokee. Mheshimiwa Aida amesema, kwake imeshatokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mstaafu Mheshimiwa Mpina kasema. Zaidi ya ng'ombe 400 mpaka leo Wizara ya Maliasili hamtaki kurudisha ng'ombe wale, mnachotaka ni nini? Mmewapeleka wapi hao ng'ombe? Nani anao mpaka leo miaka miwili?

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni dakika kumi?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kunti, nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi niungane na wengine kukupongeza, Kiti kimekuenea. Napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ndumbaro na Makamu wake Mheshimiwa Mary Masanja. Nampongeza Katibu Mkuu Allan Kijazi na watendaji wote wa Serikali. Napenda pia kumpongeza Profesa Silayo kwa kazi nzuri alioifanya nchini kwa kulinda misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 17 ya pato la Tanzania linatokana na utalii na asilimia 25 ya pesa za kigeni zinatokana na utalii nchini kwetu Tanzania. Nichelee kusema kwamba barabara zinazokwenda kwenye hifadhi za Taifa za nchini kwetu hazifai. Sasa kama barabara haifai, hili pato la Taifa litapanda vipi? Tulikwenda *Ruaha National Park* barabara kutoka Iringa Mjini kwenda *Ruaha National Park*, ukimpeleka mgeni pale, *the moment anafika pale Ruaha National Park akirudi the business is finished there!* Hatarudi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Ujenzi waweze kujenga barabara zote zinazokwenda kwenye Hifadhi ili utalii uweze kukua nchini kwetu Tanzania. Kama tunavyojua, wageni wanapokuja wanataka kuona vitu mbalimbali. Hivyo basi, ninaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, isijikite kwenye utalii wa wanyamapor peke yake. Hebu fungukeni, nendeni kwenye utalii mwagine, nendeni kwenye utalii wa fukwe (*Marine tourism*); nendeni kwenye utalii wa nyuki (*Api-tourism*); nendeni kwenye utalii wa misitu (*forest tourism*); nendeni kwenye utalii wa malikale (*traditional tourism*); msijikite tu kung'ang'ania kuangalia tembo, faru na simba. Fungueni milango mingine ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niyaseme hayo kwa sababu nimeona kila kitu ni wanyamapor, wanyamapor. Utalii mwengine, hautangazwi. Naomba mtangaze na utalii mwengine ambao unapatikana nchini mwetu kama nilioutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze suala la uhifadhi wa malikale. Uhifadhi wa malikale nchini Tanzania haupo. Tunazo malikale nyngi nchini Tanzania, lakini hazijahifadhiwa vizuri na hatujaziweka kama ni kivutio cha watalii kuja nchini kwetu Tanzania. Labda kuzisema tu kwa uchache, tunayo mapango ya Amboni Tanga, tunayo *Laitoni footprint* ambayo iko kule Ngorongoro, tunayo magofu ya Kilwa, tunacho kimondo pale Mbozi, tunayo michoro iliyochorwa kule Kondoa Irangi; lakini pia UNESCO walizitambua hifadhi za Ngorongoro kama ni urithi wa dunia; walitambua pia magofu ya Kilwa kama ni urithi wa dunia; walitambua pia hifadhi ya Taifa ya Selous kama urithi wa dunia; walitambua pia hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro kama ni urithi wa dunia; walitambua Mji Mkongwe wa Jiji la Zanzibar kama urithi wa dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hivi vitu, Wizara ya Maliasili na Utalii ivizingatie na iviweke viwe kama ni vivutio vyaa utalii nchini kwetu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia hapa ni suala la wanyama wanaovunwa. Kuna mito ambayo ina mamba mengi na kuna maziwa ambayo yana mamba wengi kama Rukwa, lakini pia kule Mpanda kuna bwawa moja la Milala ambalo lina viboko wamejaa pale mpaka siku hizi hatutumii yale maji ambayo zamani tulikuwa tunatumia. Naomba Wizara hii ya Utalii iangalie wale wanyama waharibifu kama mamba wavunwe na kama viboko wavunwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja, maana yangu ni kwamba hatuwezi ku-compromise maisha ya binadamu na wanyama ambao tumepewa tuwatunze. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya. Namwita Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Nami niungane na wenzangu kuwapongeza viongozi wote wa Maliasili kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja ya msingi. Jimboni kwangu tunao wafugaji wa nyuki. Tunao wafugaji wa nyuki takriban 2,400 ambao wameundwa na Kata mbalimbali ikiwemo Bitale, Murungu, Kitahana, Lusohoko, Kimodo Mjini pamoja na Misezero. Wafugaji hawa wanaweka mizinga yao katika msitu wa Myowosi. Tunaishukuru Serikali ilitenga shilingi milioni 507 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki. Tumekwisha kupokea shilingi milioni 300 ambazo zimejenga jengo. Tunasubiri shilingi milioni 207 ambazo zinakwenda kununua vifaa kwa ajili ya kuchakata mazao ya nyuki. Tunaishukuru sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri hayo, bado tuna changamoto. Changamoto ya kwanza ni tozo. Wafugaji hawa wa nyuki walikuwa wakitozwa shilingi 5,000/= kwa mwezi kwa kwenda kurina asali au kuweka mizinga. Ni wiki tu iliyopita wametangaziwa kwa kupewa tahadhari kwamba ifikapo mwezi wa Saba mwaka mpya wa fedha watakwenda kutoa shilingi 15,000/= kwa mwezi kwa ajili ya kuingia msituni. Ni kubwa sana kwa mwananchi wa kawaida tena mfugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wameongezewa kodi ya baiskeli, shilingi 200/= kwa siku; hiyo inaleta shilingi

6,000/= kwa mwezi. Kwa hiyo, kwa mwezi mmoja huyu mrina asali atatoa shilingi 21,000/= ili aweze kufanya kazi zake kule msituni. Tunaiomba Wizara iangalie upya kabla haijaanza kutumika. Hii ni gharama kubwa sana kwa mfugaji wa nyuki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, mfugaji yule wa nyuki haruhusiwi kuingia na pikipiki. Angalia mfugaji wa nyuki mwenye ndoo 200 za asali, asombe kwa pikipiki na ana kibali cha mwezi mmoja, haitekelezeki. Tunaomba Wizara iangalie vizuri upya kuona jinsi gani huyu mfugaji atawenza kuyachukua haya mazao yake ya nyuki; asali kuweza kutoa kule msituni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya tatu ni eneo la kuweka ile mizinga. Wafugaji wale wameweke mizinga kilometa tano mpaka kumi. Mwanzo walikuwa wakienda mpaka kilometa 25, imekuja sheria warudi nyuma zaidi. Ombi lao, wafugaji wa nyuki wamenituma, wanaomba waendelee kuachwa pale pale kilometa 20 mpaka 25 kwa sababu hawataki wale nyuki wale haya mazao ambayo yanawekwa kemikali. Maana Jimbo langu la Muhamwe linaongoza kwa asali nzuri *organic*, hivyo nyuki wale wakila hizi kemikali asali ile itakuwa haifai. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa wakulima ambao wanalima karibu na hiyo hifadhi ya Myowosi. Wameshalima, wameshapalilia, umefika muda wa kuvuna, hawaruhusiwi kwenda kuvuna. Naomba hekima itumike, wakulima waweze kwenda kuvuna mazao yao, baadaye sheria itafuata mkondo wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo Kata ya Mrungu katika Kijiji cha Kumbanga. Hiki Kijiji kimeanza mwaka 1974 kikiwa na wakazi 800. Tukiwa tunafahamu kabisa *growth rate* ya 2.7 tunaweza tuka-*imagine* hiki Kijiji sasa hivi kina watu wangapi? Kijiji hiki kipo mpakanikabisa mwa Pori la Myowosi na mpaka uko chini ya kilometa moja. Wananchi hawa wamenituma, wanaomba wasogezewa mpaka kwa sababu ni dhahiri wameshaongezeka. Kama idadi ya watu

imeongezeka, basi na shughuli za kijamii zimeongezeka ikiwemo kilimo, ufugaji na ziada. Naomba Mheshimiwa Waziri ikikupendeza twende wote Murungu, pale Kumbaga...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niungane na wenzangu kukupongeza, kwa mara ya kwanza unatuongoza vema. Tunaamini tumpata Mwenyekiti sahihi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhaba wa muda nitaweza kuongelea mambo machache ambayo naamini Wizara ikiyafanya kazi watakuwa wametunusuru sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe, hususan Wilaya ya Songwe yenyeewe.

Mimi napenda kusema kwamba nilitamani sana niwapongeze watendaji wa Wizara hii kwamba wanafanya kazi vizuri, lakini nikikumbuka machungu ambayo tunayapata na watendaji wao wa chini kule, roho inakuwa inaniuma kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hii ndiyo Wizara pekee ambayo haina mahusiano mema nasi wananchi. Kimsingi tumekuwa tunalianao kila eneo. Tunaona kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ni watu wema, tunawaza ni kwa nini watu wao kule chini wanakuwa na roho za kiukatili namna hii kiasi kwamba inakuwa kama wao Kanisani hawakuui? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala la wavuvi ambao wanavua katika Ziwa Rukwa. Tunajua uvuvi ni kazi kama kazi nyingine na wale wavuvi wanafanya kazi zile kuweza kujipatia kipato *ku-sustain* maisha yao na watoto wao na ndugu zao wa karibu; lakini mambo yanayotendeka katika Hifadhi ya Katavi ni mambo magumu ambayo yanasiskitisha. Wavuvi wananyanyaswa sana. Sidhani kama taarifa hizi zingekuwa zinafika kwao viongozi wetu; Waziri na Naibu Waziri kama haya mambo yangekuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa kutoka kwa wavuvi ambao wanapatikana katika kambi za Kichangani, Malangali, Kasimanyenze, Kambang'ombe na nyinginezo, kule kuna kambi nyingi, wavuvi wale wanalamika kwamba, *ma-game*, sasa sijaelewa *ma-game* na uvuvi kwa nini wanawaingilia wavuvi kwenye kazi zao eti kisa tu hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ma-game* wanaolinda hifadhi ya Katavi wamejitengenezea mazingira ya kujipatia kipato kisicho halali. Wamekuwa ni watu ambao wanawatishia wavuvi kwamba wakiwakuta kando kando ya ziwa wanaendelea na shughuli zao, wanawatishia na kuweza kuwapora mali zao. Pia wamejitengenezea utaratibu wa kupata rushwa. Watu hawa wamejitengenezea utaratibu wa kupata shilingi 300,000 kila wiki kwa kigezo tu kwamba, wavuvi wanaofanya kazi kule, hawatakiwi kukanyaga ardhi ya hifadhi. Mwisho wa siku tunajiuliza kwamba, ile hifadhi imewekwa kwa ajili ya kututesa au imewekwa kwa ajili ya kutusaidia kama Taifa tuweze kupata kipato? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kisichoweza kuongeleva. imi naamini kabisa Wizara inaweza ikatafuta namna ya ku-*compromisen*a wavuvi ili mwisho wa siku Serikali ipate pesa yake. Badala ya hizi shilingi 300,000 kuendelea kuingia mifukoni mwa watu. Serikali ingeweza kutoa vibali halali, kama inavyotoa vya watu kuwinda na kadhalika; wavuvi wanapovua samaki wao waweze kuwaanika kandokando ya ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wavuvi wamekuwa wakiendelea kupata tabu hii. Pale wanapoonekana hawana pesa ya kuwapa, wanachomewa vitu vyao; wavuvi wanachomewa mitumbwi, wavuvi haohao wanachomewa ngalawa, lakini chumvi zao zinaloanishwa. Pia hata samaki wale ambao wameshakauka wanachomwa moto. Sasa hebu jiulize, mtu kawekeza pesa yake, ni mtaji, ndio inamfanya afanye maisha, vinachomwa halafu anaishije? Anaenda kuanza vipi maisha upya? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mambo haya ambayo yanakuwa yanaendelea, kwa sisi wanawake tunajua kabisa, imeshaelezwa hapa, ndio wanaofanya mazoezi ya kubaka wanawake. Sasa najuliza kwamba, kuwa mwanamke ni kosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba, kwa kweli sina amani na askari hawa. Napenda kuona kwamba Serikali inakuja na tamko au na neno ambalo kwa kweli litatufariji kuona kwamba wako kwa ajili yetu na siyo kwa ajili ya wanyama tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuunga mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanahamisi Said Kassim, wakati huo Mheshimiwa Mkenge na Mheshimiwa Mjika wanajandaa.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema Sebastian.

**MWENYEKITI:** *Okay*, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, sawa. Baada ya hapo, wanakuja wengine. Sawa.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waliofanikiwa duniani ni wenye jeuri ya kuthubutu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri

tusiache kuthubutu kuibua maeneo mengine mapya ya utalii kwa sababu waliofanikiwa duniani ni wenyewe jeuri ya kuthubutu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye eneo la sheria tunasema kama huna vielelezo, haujafanya utafiti, usiongee. Mwaka 1996/1997 nilikuwa Mombasa, Kenya, sehemu moja inaitwa Mtwapa katika hoteli moja ya Serena. Nilikutana na mtalii mmoja akaniambia maneno yafuatayo: amekuwa akiitembelea Kenya na Mombasa *for the last 15 years*, hana kitu kipywa cha kuona, anafikiria aende ama *South Africa* au kwingineko. Ujumbe anaouleta ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina hii ya watalii tunatakiwa ndani ya nchi yetu tuisiwapoteze kwa kuibua maeneo mengine mapya. Kama *this time around* alikuwa Kaskazini, *next time* aende Magharibi, *the other time around* aende Mashariki, hivyo. Kwa hiyo, huyo tuna uwezo wa kumhifadhi ndani ya nchi yetu, lakini kwa kuboresha maeneo mengine. Nilikuwa naliomba hilo sana na hiyo ndiyo tabia. Naomba niwapitisheni, mtalii ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tutajikita kutengeneza hoteli nzuri, mbuga nzuri, lakini tusipomtambua mtalii na tabia yake, hizo hoteli Wazungu wanasema zitakuwa ni *white elephant*. Kwanza mkumbuke mtalii ndio bosi wetu. Kama bosi wetu, ana tabia zifuatazo; tusipotii kiu yake hana nafasi ya kuja kwetu. Kwa hiyo, nilichokuwa nawaomba Waheshimiwa, lazima tujikite kwenye kujua mahitaji ya mtalii. Ni mtalii gani tunayemlenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu ukiorodhesha, nikiacha watalii wa ndani ambao ni Watanzania wenyewe, lakini hata hao watalii kuna kundi la watalii huko kwenye kada, wengine wanasema watalii vishuka. Kuna mtalii ambaye tunaweza tukabanananaye mtaani, tunakula wote muhogo wa kuchoma, anatembea pekuwa na vitu vingine kama hivyo, hatukatai, naye tunamhitaji. Ila kuna mtalii mmoja anakuja kwenye nchi yako, mtalii huyu akiridhika na kazi zetu na huduma zetu; leo tunauliza habari ya kwenda

kutangaza *CNN* na kwingineko, yeye mmoja ana uwezo wa kubeba dhamana hiyo akiridhika na huduma yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunaambishi kwenye *Hotel Industry*, kwenye utalii kwa ujumla wake ni *Hospitality Industry*. Kwa hiyo, tusipokuwa watu wa kutii kiu ya watalii, itabaki kuwa ni gumzo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana. Sasa ili tukawapate watalii wa daraja hilo, je, tumejikita katika mahitaji yake ya kimsingi? Leo kwa mfano, tuna hoteli kweli za viwango vile? Tuna hoteli ambazo zinaweza leo ukisema mtalii mmoja makini wa kutoka Marekani amekuja hapa tunaweza tukam-*accommodate*? Hayo ni mambo tuendelee kuyaangalia. Mtu anayehitaji labda huduma, bima, anahitaji *flying doctors*, hayo yote kweli tunayo? Ni vitu vya kimsingi sana kuviangalia. Maana mwinguine anasema, nakwenda Tanzania, nime-fall *sick*, nimeugua sasa hivi, huduma nazipata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nashukuru Marais wote ambao wameendelea kuboresha huduma zetu hapa nchini hata kama ni kwa maana ya *first aid* ataipata nchini kabla hata hajaruka kwenda kwenye nchi yake, ni jambo la msingi sana. Naomba tena tuendelee kuelewa leo tuna *trained personnel* kweli kweli jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda baadhi ya nchi za watu, ile tu umefika kwenye nchi yao, even *tax driver* wamekaa kistratejia. *Tax driver* tu ukiwanaye kwenye gari anaiuza nchi yake. Umwache huyo, ukikuta kama ni *air hostess* wanauza nchi zao. Ukimkuta kama labda ni *waiter* au *waitress*, umekaa hotelini, i dakika mbili za kukaa pale yuko *well trained*, anajua kwamba nifanye nini katika kuiuza nchi yangu. Huko tuendelee kwenda kwenye namna hiyo ya kufanya shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Ooh! Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanakhamis Said Cassim. Hayupo. Haya, Mheshimiwa Muhamari Shabani Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya, japo Wizara ina changamoto nyingi sana. Nami naomba tu niwaambie, wanayozungumza Wabunge hapa, hebu yachukueni kwa makini mkayafanyie kazi, msiyaache yakapita ikawa *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda zaidi kuzungumzia suala la utalii wa ndani. Utalii wa ndani naona umesuasua sana katika Taifa letu. Kila siku Wizara inapiga kelele, inahamasisha, inapiga debe kuhusu utalii wa ndani, lakini bado utalii wa ndani haujawa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ushauri. Sasa hivi duniani biashara huwa inamfuata mteja na siyo mteja anayeifuata biashara. Naomba niishauri Wizara, sasa hivi wabadilishe mfumo wa utalii wao wa ndani. Sasa hivi hakuna Watanzania walio wengi wenyewe uwezo wa kutembelea Ngorongoro, Manyara na Mikumi; na wana hamu ya kuona wanyama katika hizo mbaga na kutembelea mbaga hizo, lakini uwezo wao ni mdogo. Nawashauri kitu kimoja. Kama mnavyofanya Saba Saba katika maonesho, Banda la Maliasili linatembelewa na watu wengi sana kuliko mabanda yote katika maonesho ya Saba Saba. Hii ni kwa sababu gani? Watu wengi wanapenda kuona wanyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jaribuni sasa hivi kuweka utalii wa *mobile*. Mtafute viwanja katika miji kama Dar es Salaam na Dodoma, muweke mabanda ambayo wananchi watakwenda kutembelea wanyama na kulipia pesa.

Mtaingiza pesa nyingi za kutosha. Mikoa mingi sana haina mbuga za wanyama na hawawajui wanyama hawa wakoje, kwa hiyo, watu wengi sana wanapenda kuona simba, chui na wanyama mbalimbali, lakini wanakosa fursa za kwenda kuwaona. Sasa ifikie wakati mtengeneze hicho kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale Dar es Salaam, *Coco Beach* au pale kwangu Bagamoyo, kuna *beach* nzuri na maeneo mazuri. Mkiweka *zoo* pale ya Wanyama, watu waje kutembelea, watu wengi kutoka Zanzibar; Zanzibar inapokea watalii wengi sana, lakini wanaishia kule, hawana pa kwenda. Wakitoka Zanzibar wanaondoka zao kwenda Kenya. Hebu tuwape fursa watalii wengi wanaokwenda Zanzibar waje Bagamoyo. Nawashauri kitu kimoja, mjenge gati pale, mjenge gati ya kupaki *speed boat* ambapo mtalii anaweza akatoka Zanzibar akaja mpaka Bagamoyo, akatembelea Mbuga ya Wanyama ya Saadani, akatembelea vivutio vilivyo Bagamoyo na halafu akapanda boti akarudi Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana kuamsha uchumi wa utalii, lakini tukitegemea utalii wetu tuone watu wakitembelea mbuga za wanyama, hiyo itachukua muda mrefu sana na hamtatengeneza pesa. Kwa sababu, watu wengi sasa hivi wanapenda kuona Wanyama; vijana wa shule za msingi, vijana wa sekondari, vijana wa vyuo, wote wanapenda kitu hiki. Kwa hiyo, nawaomba sana, mbadilishe mfumo wa utalii wa ndani, mtengeneze *zoo* katika miji yetu...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MUHARAMI S. MKENG’E:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwomba Mheshimiwa Minza Simon Mjika, wakati huo Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Tabasam wanajiandaa kumalizia dakika tatu.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, lakini

kulingana na ufinyu wa muda nitaenda haraka sana na nitasema tu baadhi ya vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri iliyosheheni matumaini kwa Watanzania. Nimefurahi sana kwa mambo mengi ambayo wameweza kuyasema mle, kama yatatekelezeka hawatakuwa na ugomvi na wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaingia moja kwa moja katika Mkoa wangu wa Simiyu. Mkoa huu una wilaya tano, lakini wilaya nne ndizo zinazoshambuliwa na Wanyama. Kuna Wilaya ya Busega, Bariadi, Itilima na Meatu. Maswa tuko vizuri tunamshukuru Mungu. Nashukuru kwa upande wa Wilaya ya Busega, Mheshimiwa Songe ameweza kuongea kwa hiyo, sina haja ya kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika Wilaya ya Bariadi. Bariadi tunashambuliwa sana na wanyama, tembo hawa. Kwa mfano, Kijiji cha Nyawa, Gibeshi, Kindwabihe, Mwasenase pamoja na Ihusi, kule kuna mashambulizi makubwa sana ya tembo. Tunaomba Serikali iangalie sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niingie moja kwa moja tena kwenye Wilaya ya Itilima. Napenda tuishukuru kwanza Serikali yetu. Ninashukuru kwamba tuna gari la wanyamaporu katika Wilaya ya Itilima, tayari wameshaleta, tunashukuru. Kwa hiyo, msaada mkubwa umepatikana pale japokuwa kuna vijiji ambavyo vinahangaishwa sana na hawa wanyama; kuna Mwaswale, Nyantuguti, Nkuyu; hivyo ni baadhi ya vijiji tu ambavyo vinashambuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia katika Wilaya ya Meatu ninashukuru Mheshimiwa Mpina ameongea na baadhi ya vijiji amevitaja pamoja na changamoto zake. Tunaomba kupata msaada, katika hivyo vijiji tunahangaika sana. Vijiji ni vingi sana; tukiangalia kwa mfano katika Wilaya ya Meatu kuna Mwasengela, Mbuga ya Banya, kuna

Sakasaka, Nyanza, Igobe, Longaloniga; vijiji ni vingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia kwangu ninakotoka Meatu kuna Mwanyahina, Makao, Mwagwila, Mwajidalala, Busia, Mwanzagamba, Mwangudo, kote kule wanyamapori hawa tembo wamesambaa sana. Tunaomba msaada kutoka Serikalini.

Katika Wilaya ya Meatu hatuna hata gari la wanyamapori. Askari wapo, lakini hakuna usafiri. Hata tembo wakionekana wanafanya uhalifu sehemu, akipigwiwa hana usafiri, inakuwa ni shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iliangularie sana hili. Hatuna ugomvi na Serikali, lakini tunaomba watutendee ilivyo sahihi. Akina baba wengi katika Mkoa wa Simiyu, hususan hizo wilaya nne ambazi nimezitaja wameshakuwa doria, hawana *combat*, hawana silaha, hawana usafiri, lakini ni watu wa kulinda wanyamapor. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuomba tuone. Watu wengi sana wamepoteza maisha, akina baba, akina mama na watoto, hususan wanafunzi wanapoenda shule. Kwa mfano, mwaka juzi 2019 kuna mwanafunzi mmoja aliuawa katika Kijiji cha Mwangudo, mtoto wa Darasa la Pili anaenda shule. Alikutana na tembo, alimjeruhi vibaya sana yule mtoto, alimsaga na akaisha kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba vitu kama hivi tunavyoviongea tunaweza tukaona rahisi, lakini wananchi wanalia sana na wanateseka sana. Tunaomba basi Serikali ifanye hima itufanyie msaada huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nakupongeza kwa kukalia hicho kitii. Nilikuwa natafutatafuta hapa historia kwamba kuna mtu aliwahi kuwa mdogo zaidi wa kukalia hapo, nikajua ni wewe tu peke yako ambaye ni mdogo zaidi uliyewahi kukalia kiti hicho hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo wanasema nafasi inapata mtu au mtu kupata nafasi. Nadhani Wabunge wamejua kwamba, sasa hiyo nafasi imepata mtu. Kwa hiyo, ataishughulikia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa mimi huwa naangalia, yaani ukimwangalia Waziri wake aah, *super*, yuko vizuri sana yaani jamani. Ukimwangalia Naibu wake yuko vizuri sana, Katibu wake ndiyo usiseme, Mheshimiwa Kijazi. Wakae sasa ili tuiswabughudhi; maana inaonekana kama miaka yote tunawabughudhi. Ili tuiswabughudhi, waamue Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili, wako pamoja kwenye Kamati moja, wajiulize ni wapi ambapo sasa kuna shida ya Watanzania kwenye ardhi hii, waende watatue hayo matatizo ya Watanzania. Kwa sababu hatuwezi kuwa humu miaka nenda rudi, mwishoni Wabunge tutachokwa sasa. Nenda rudi, tunapigia akili kwamba Watanzania wananyanyaswa kwenye maeneo mengi. Watafute maeneo ambayo yapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi Na. 4 inaruhusu, kwa sababu ardhi yote ni ya Rais. Kwa hiyo, waangalie. Mimi huwa najiuliza, hivi ni kwa sababu hatukuandika *land reserve*, tumeandika game reserve? Ukiema land reserve, ni ardhi yote ya Watanzania; *general land, the village land*, yote hiyo na ya *game reserve* ni ya Rais. Kwa hiyo, tuangalie, ni wapi tunakosea jamani? Wapi tunakosea kila siku Wabunge tuko humu tunapiga kelele? Tuamue tulete migogoro yote. Marehemu Rais Magufuli aliunde Kamati, imeenda huko imefanya kazi, walete hiyo ripoti basi tuone wamebakiza wapi ili tumalize? Kwa nini tunapiga kelele kila siku humu ndani haiishi? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naipongeza Serikali kwa maana ya kuweka hali nzuri ya mambo ya mapori yalivyokaa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ila naomba Mheshimiwa Rais aingilie kati migogoro yote ambayo wananchi wanakerwa nayo na pia tumwombe Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu na wote, wale ng'ombe wote waliochukuliwa kwenda porini wakashinda kesi, warudishwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere ahasante.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Jamani warudishwe ng'ombe wa wananchi.

**MWENYEKITI:** Kwa dakika mbili zilizobakia namwita Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika mbili naona mchango wangu hautakuwa na maana kwa Taifa hili. Nakuomba tu uniongezee dakika kidogo kwa sababu kuna vitu nataka kuvizungumza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam!

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Kama utaweza kusema kwa dakika hizo mbili, tafadhali naomba utumie. Otherwise, upangwe kesho.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba iwe hivyo kwa manufaa ya nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, sasa sehemu kubwa ya wachangiaji wetu leo imeshakamilika. Naomba nimkaribishe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa ajili ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge. Karibu.

## **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, KAZI, AJIRA NA WENYEULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nikupongeze kwa kweli, kitimekuenea vizuri. Tunakutakia kila la heri kwenye hayo majukumu mapya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA, Mkutano wa Tatu wa Bunge ambao ullanza tarehe 30 Machi, 2021 umepangwa kumalizika tarehe 30 Juni, 2021;

NA KWA KUWA, kutohana na matakwa ya Kanuni ya 124 (4) na makubaliano ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bajeti ya Serikali itasomwa siku ya Alhamis, tarehe 10 Juni, 2021;

NA KWA KUWA, muda uliobaki kufika tarehe ya kusomwa kwa Bajeti ya Serikali ina takribani siku tano na bado Bunge halijakamilisha kazi ya kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

NA KWA KUWA, ili Bunge liweze kukamilisha kazi hizo zilizobaki, inabidi Kanuni ya 34 (2) (4) (15) ziweze kutenguliwa ili Bunge likutane kesho siku ya Jumamosi, yaani tarehe 5 Juni, 2021 kwa ajili ya kukamilisha shughuli za ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

HIVYO BASI, Bunge liazimie kwamba, Kanuni ya 34(2) ambayo inaelekeza Bunge likikutana saa 3.00 asubuhi liendelee hadi saa 7.00 mchana na likisitishwa saa 7.00

mchana lirejee saa 11.00 jioni hadi saa 1.45 usiku litakapoahirishwa na Kanuni ya 34(15) inayozuia Bunge lisikutane siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko, iweze kutenguliwa ili Bunge liweze kukutana siku ya kesho Jumamosi tarehe 5 Juni, 2021 saa 3.00 na liendelee kufanya kazi mpaka saa 8.00 mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa hiyo, Bunge litaendelea kesho.

Kuna tangazo hapa kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, anawajulisha Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote, *TWPG* kwamba Jumapili tarehe 6 Juni, 2021 kutakuwa na mafunzo yatakayofanyika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4.00 asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kikao chetu cha Bunge cha leo, tunawashukuru sana Wabunge waliochangia, uchangiaji ulikuwa wa kizalendo unaoakisi taswira kamili ya utajiri tulionao kwenye nchi yetu. Maliasili ni sekta nyeti sana kwa Taifa letu. Ziko raslimali zinazoweza kwisha, lakini huu ni utajiri ambao tukiulinda, upo na utakuwepo, utakuwepo na utakuwepo. Kwa hoja hiyo hiyo ambayo tumeizungumza muda ule kwamba kama Taifa letu ni la pili kwa vivutio, pengine sasa tuanze kujitafakari, tunakwendaje mbele zaidi?

Kwa hiyo, nawapongeza wenzetu wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge lillahirishwa mpaka siku ya Jumamosi,  
Tarehe 5 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*